SARUFI YA KINYANKORE NA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI: MFANO KUTOKA ASASI TEULE JIJINI MBARARA

NA

KUBAKURUNGI KYANGUNGU ABRAHAM

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA KWA AZMA YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA MOI

2025

UNGAMO

MTAHINIWA

Hii ripoti ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni yoyote katika Chuo Kingine. Hakuna mtu yeyote aliye na ruhusa wa kutoa nakala yoyote ya ripoti hii kwa namna iliyo ya dijitali au kurudufu bili kuruhusiwa na mwandishi au kupitia chuo kikuu cha moi.

Sahihi:____________________________________ Tahere:_______________________

Kubakurungi Kyangungu Abraham

PHD/KIS/6033/22

WALIOSIMAMIA

Hii ripoti iliwasilishwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa kibali chetu sisi walioisimamia wanaowakilisha Chuo kikuu cha Moi.

Sahihi:____________________________________ Tahere:_______________________

Prof. Mark M. Kandagor

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi:____________________________________ Tahere:_______________________

Prof. Samuel M. Obuchi

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa Mzee Amos Kyangungu na Mama Rosette Mirembe Kyangungu.

SHUKURANI

Naanza na kumshukuru Mwenyezi Mola Rabana kwa kunipa afya na nguvu ambazo zimeniongoza kufanya utafiti huu na kuandika ripoti yake. Kusema ukweli, imekuwa safari ngumu yenye shughuli nyingi, lakini mafanikio ya kazi hii ni matokeo ya mawazo na michango kutoka kwa watu wengi walioshiriki kwa njia moja au nyingine. Na Ingawa ni vigumu kuwataja wote, ninaona ni wajibu wangu kuwataja wachache wawakilishe wengine.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. Mark M. Kandagor na Prof. Samuel M. Obuchi kwa ushauri wao muhimu na wa kujenga na msaada wa mara kwa mara katika muda wangu wote wa kozi ya Uzamifu. Upendo wao uliufanya mchakato wa utafiti uonekane kuwa rahisi, ingawa kwa kweli ulikuwa na changamoto nyingi. Nimejifunza mambo mengi kutoka kwao, walinivumilia katika mapungufu yangu kama mwanafunzi ili niweze kuhitimu na kumaliza kwa haraka. Walikuwa tayari kunishauri kila wakati na kuniongoza kuhakikisha ninakamilisha kazi hii ndani ya muda uliopangwa. Kwa kweli, wamenifaa sana katika utafiti huu; Mungu awabariki sana.

Ninawashukuru kwa namna ya kipekee pia familia yetu kwa ujumla kwa kunitia moyo na kunivumilia sana katika kipindi cha masomo yangu. Baadhi yao, nashukuru mke wangu mpendwa, Bi. Jesca Katwesigye Kubakurungi, pamoja na watoto wetu Amos-Paul, Isaac-Levi, Matthew-Noah, na Omega-Steve, waliniunga mkono na kunituliza nilipokutana na changamoto, na walikuwa bega kwa bega nami kila wakati. Pia nachukua fursa hii kuwashukuru marafiki zangu, mkiwemo wazazi wangu na wanafamilia ya Kyangungu wote, familia ya Daktari Katebaka Raymond, familia ya Mha.Hilary Mugisha na Mha.Dkt.Aruho Apollo Tinka, dadangu Annah Kwarikunda Muhumuza, rafiki yangu wa zamani sana Mchungaji Eric Byakatonda, na wengine

ambao sitawataja hapa wote, ushauri wenu mzuri pamoja na maombi yenu yaliniwezesha kusonga mbele bila kuchoka wala kukata tamaa.

Nawashukuru viongozi wa shule ya Ntare, na Chuo kikuu cha Bishop Stuart kwa kunipa ruhusa, wakanivumilia nyakati zote nilipotoka kazini kushughulikia masomo yangu, kukusanya data nyanjani, na hasa wakati wa kuandika ripoti ya utafiti huu hadi mwisho wa kozi. Chuo Kikuu cha Bishop Stuart hasa kiliniwezesha kupata ufadhili kutoka mradi wa RUFORUM na mchango wao ulinisaidia pakubwa kumaliza masomo yangu ya uzamifu. Wengine ambao ningependa kushukuru ni wahojiwa wote walioshiriki na kuhusika katika utafiti huu. Data walizozitoa zilijenga ripoti kamili ya utafiti. Nawashukuru kwa dhati wanafunzi wangu katika shule ya Ntare pamoja na wala wa Chuo kikuu cha Bishop Stuart, na hata walimu wa Kiswahili katika shule zote nilikokusanyia data. Nilifurahia ushirikiano na upendo wenu wa somo la Kiswahili na michango yenu katika utafiti huu. Ninashukuru tena viongozi wa Chuo Kikuu cha Moi hasa Mama Daktari Magdalene Wafula, Dkt.Harriet Ibara, Marehemu Dkt. Allan Opija (Pumzika kwa amani) na Prof.Oduori, waliokuwa Wahadhiri waandamizi na Wakuu wa Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika, wote walijitoa kunipa huduma nilizozihitaji pamoja na kunishauri hatua kwa hatua. Mungu azidi kuwabariki kwa upendo mlionionyesha. Siwezi kumsahau ndugu yangu Paul Meltus, rafiki aliyenisaidia kwa hali na mali na hasa katika pilka pilka za kugotoa shughuli za maandalizi ya tasnifu hii. Bila wewe Paul, juhudi zangu kuhitimu zingeligonga mwamba! Nakuombea baraka za Bwana! Namalizia kwa kushukuru wanafunzi wenzangu wa shahada ya Uzamifu katika Kiswahili – 2021-2024, hawa walinisaidia tangu mwanzoni katika mijadala ya darasani, mawasilisho ya kutahiniwa na hasa kunitia moyo kusonga mbele. Mbarikiwe nyote sana!

IKISIRI

Wataalam waliohusika na utafiti wa lugha wanabaini kwamba lugha ya kwanza inaathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, na hivyo kumletea mjifunzaji wa lugha ya pili changamoto mbalimbali. Huu utafiti ulichunguza namna sarufi ya lugha ya Kinyankore inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, ulilenga kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi wa Kinyankore wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili, na mwisho, kutoa mapendekezo ya jinsi ya kushughulikia changamoto hizo. Huu utafiti ulikuwa na malengo maalum matatu: Kwanza, kubaini athari za Kinyankore na vile zinavyojitokeza wakati wa kusoma somo la Kiswahili ikiwa ni lugha nyingine. Pili, kuchunguza kwa nini athari hizo zinajitokeza kwa wanafunzi hao wa Kinyankore wakati wanapojifunza lugha hiyo nyingine ya Kiswahili. Lengo la tatu lilikuwa kutambua mbinu mbalimbali zinazotumika kukabiliana na changamoto hizo na kusaidia wanafunzi waathiriwa wa Kinyankore katika mchakato wa kujifunza Kiswahili. Mahali ambapo utafiti huu ulifanyika ni jijini Mbarara katika asasi za elimu zilizochaguliwa, na mtafiti alilenga asasi teule za shule za sekondari na Vyuo vikuu. Takwimu za utafiti zilipatikana baada ya kuhusisha njia mbalimbali za ukusanyaji wa data, kama vile mahojiano, majadiliano, mazungumzo, hojaji, pamoja na dodoso. Njia ya usampulishaji maalum na nasibu zilitumika kuteua washiriki waliochaguliwa. Jumla ya washiriki katika utafiti huu ilikuwa mia mbili (200). Utafiti huu ulilenga kutumia idadi hii ya washiriki ili kupata maoni yanayowakilisha kundi kubwa zaidi mkoani. Utafiti huu ulichochewa na nadharia mseto, ambayo inajumuisha nadharia kadhaa hasa ile ya Uchanganuzi Makosa, Nadharia ya Uchanganuzi-Linganuzi, pamoja na ile ya Mawasiliano. Aidha, utafiti ulifanikiwa kubainisha mbinu zinazotumika kuwasaidia wanafunzi wanaokabiliwa na taathira za sarufi ya Kinyankore wakijifunza Kiswahili. Utafiti ulibainisha kwamba wanafunzi wa Kinyankore wanakabiliwa na changamoto za kisarufi katika ujifunzaji wao wa Kiswahili katika nyanja za kimsamiati, kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki na kimuundo. Utafiti ulionyesha kwamba wanafunzi wanakabiliwa na matatizo kadhaa ya kiisimu, mkiwemo matatizo ya kisarufi, kimaandishi, kuchanganya ndimi pamoja na changamoto katika kutafsiri vipengele vya Kiswahili kulingana na lugha ya Kinyankore. Kuhusu lengo la pili, utafiti ulitambua sababu za sarufi ya kinyankore kuathiri namna Kiswahili kinavyosomwa kwa kuzingatia vigezo vyote vya sarufi ya lugha ya kwanza, matumizi ya ala za sauti za kaa kaa, kukosekana kwa baadhi ya fonimu katika kinyankore, kufundisha vibaya kwa somo la Swahili, mazingira yasiyofaa kujifunzia somo la Kiswahili, nakadhalika. Kulingana na lengo la tatu, utafiti ulionyesha mbinu zinazotumika kukabiliana na changamoto za wanafunzi wenye asili ya Kinyankore wanapokuwa katika mafunzo ya Kiswahili. Na hizo mbinu ni pamoja na; kufundisha Kiswahili tangu utotoni, wanafunzi wa kinyankore wapewe nafasi za matumizi na mazungumzo ya Kiswahili, kuhamasisha wazazi, walimu na wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili, kuongeza vipindi na muda wa kufundisha Kiswahili kwenye ratiba za shule, kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia Kiswahili na kadhalika. Utafiti ulihitimisha kwamba, ijapo Kinyankore kinaathiri kujifunza somo la Kiswahili kwenye ngazi zote za kisarufi kisarufi kama vile kimatamshi, kisemantiki, kimsamiati, kimuundo na kimofolojia, athari hizo haziwezi kuzuia mafunzo ya somo la Kiswahili kuendelea. Kwa maana, Kinyankore jinsi inavyotambulika kuwa Kibantu huenda ikasaidia wanafunzi kutumia uwezo wao kuelewa jinsi matumizi na uundaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili yanavyojitokeza. Utafiti ulihitimisha kwa kupendekeza kwa tafiti zijazo kutumia nadharia nyingine kuchunguza athari zinazojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya pili, pamoja na kutumia muda mwingi zaidi kuzibainisha sababu na suluhisho za kila moja.

ABSTRACT

Many language researchers explain that there are effects of the first language in the learning of the second language where there are challenges that the second language learner faces. This study aimed to investigate the impact of Kinyankore language grammar on Kiswahili language learning. It also aimed at identifying problems encountered by Kinyankore students learning Kiswahili when it is their other language, and finally to provide suggestions for solutions to these challenges. This study was guided by three specific objectives; First, to establish the implications on students of Kinyankore language while studying Kiswahili language for students who speak Kinyankore as their first language. Second, to explore reasons for those effects on Kinyankore speakers who learn Kiswahili like any other language. Third, to suggest various methods to help students who are affected by Kinyankore when learning the Kiswahili language. This study was conducted in the city of Mbarara in selected educational institutions such as high schools and colleges. Research data were collected using the following methods; reading texts, discussions, interviews, questionnaires and questionnaires. Participants were selected through purposive and random sampling. The sample which was considered in the research involved two hundred (200) participants. The research aimed to use this size of the sample to get a representative opinion of all others in the region. This study was guided by hybrid theories such as Error Analysis Theory, Contrastive analysis theory and Communication Satisfaction Theory. The research was able to identify methods which could be handy in helping students who are affected by the original language when they learn the Kiswahili language. The data was organized, analyzed in regard to research objectives and the results were presented descriptively. Regarding the first objective, the study found that the implication of the Kinyankore language while studying Kiswahili are semantic (meanings), vocabulary, and pronunciation. The study found that there are several linguistic problems faced by students such as spelling, grammar, mixing of languages and problems translating Kiswahili concepts associated with the Kinyankore language. Regarding the second objective, the research identified the reasons for the grammar of Kinyankore affecting the process of studying Kiswahili language at all levels of grammar as the effect of the mother tongue, the use of palatal sound instruments, some phonemes being non-existent in Kinyankore, bad teaching of the subject of Kiswahili, a poor environment for learning Kiswahili, and so on. Basing on the third objective, the study showed methods to help Kinyankore students learning Kiswahili when it is an additional language for them including; to teach Kiswahili, and also to find the correct structures and phonology of the Kiswahili language, students should also be given opportunities to practice speaking the Kiswahili language, Students should be given the opportunity to practice a lot in the language, especially those of composing sentences, vocabulary, structures writing essays and pronouncing words and sentences with tongue twisters. The study suggested that there should be debates about the Kiswahili language in schools, students should compete and those who win should be given positive incentives. The study concluded that, although Kinyankore has affected Kiswahili while regarding to the nouns and verbs, at the morphological level, in phonology and structurally, the research study coud not find any effects to prevent the teaching of Kiswahili as a second language. Finally, the study provided recommendations by showing aspects which could be more investigated, especially the semantic aspect which can be investigated using other theories to determine these effects in more detail.

YALIYOMO

UNGAMO....ii
TABARUKU iii
SHUKURANI iv
IKISIRI vi
ABSTRACT....vii
YALIYOMO viii
ORODHA YA MAJEDWALI xiv
ORODHA YA VIELELEZO xvi
UFAFANUZI WA ISTILAHI xvii
ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA xviii
SURA YA KWANZA 1
MISINGI YA UTAFITI 1
1.0 Utangulizi....1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti 1
1.2 Suala la Utafiti 11
1.3 Malengo ya Utafiti 12
1.4 Maswali ya Utafiti....12
1.5 Sababu za Kuchagua Mada 13
1.6 Upeo wa Utafiti....14
1.6.1 Upeo wa kiufundi 14
1.6.2 Upeo wa Kijiografia 14
1.6.3 Upeo wa kiwakati....14
1.7 Umuhimu wa Utafiti 15
1.8 Muhtasari wa Sura 16
SURA YA PILI....18
MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA....18
2.0 Utangulizi....18
2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi 18
2.1.1 Maelezo ya dhana mbalimbali za lugha 21
2.1.2 Maelezo kuhusu uamilisi na mafunzo ya lugha nyingine 22
2.1.3 Lugha ya Kinyankore nchini Uganda....29
2.1.4 Taarifa kuhusu Swahili....33

2.1.5 Hali na hadhi ya Kiswahili tangu ukoloni 34
2.1.6 Historia fupi juu ya Swahili 35
2.1.7 Jinsi Kiswahili kinavyofundishwa 39
2.1.8 Dhima ya Lugha tangulizi 41
2.2 Mwingiliano uliopo kati ya lugha tangulizi na lugha nyingine 43
2.2.1 Mwingiliano uliopo wa lugha tangulizi katika kujifunza lugha nyingine 44
2.2.2 Kufundishwa kwa lugha nyingine 50
2.2.3 Ushirikiano wa Kinyankore na Kiswahili 54
2.3 Zana zinazotumika katika utamkaji wa sauti 56
2.3.1 Matamshi ya Sauti Mbalimbali 56
2.3.2 Matumizi ya fonimu na sifa zake kwa Kiswahili 57
2.3.2.1 Maana ya fonimu 57
2.3.2.2 Aina za fonimu 57
2.3.2.2.1 Vipashio vya sauti vinavyojulikana kama fonimu 58
2.3.2.2.2 Viyeyusho/ Nusu irabu za Kiswahili 61
2.3.2.2.3 Konsonanti za Kiswahili 63
2.4 Mbinu za Kuwasaidia Wanafunzi wakiwa wanajifunza lugha nyingine 69
2.4.1 Muundo 70
2.4.2 Ufundishaji wa Maelekezo 71
2.4.3 Mbinu ya kutatua makosa 72
2.4.4 Ufundishaji wa udadisi 74
2.4.5 Mafundisho yanayodhibiti Maudhui 76
2.4.6 Mafundisho ya kushiriki 77
2.4.7 Mafunzo ya kuimarisha zamu 79
2.4.8 Mbinu ya mafundisho ya kufanya vitendo 82
2.5 Mitazamo ya kisera katika nchi ya Uganda 86
2.5.1 Maana ya sera 86
2.5.2 Utekelezaji wa mifumo ya lugha 88
2.5.3 Mfumo wa kisera nchini Uganda 89
2.6 Misingi ya Nadharia 92
2.6.1 Uchanganuzi Makosa 93
2.6.2 Mfumo wa Kuchanganua-Linganuzi 96
2.6.3 Mfumo wa kimawasiliano 102
2.7 Namna ya kutumia Nadharia 107

2.8 Pengo la Utafiti 109
2.9 Hitimisho........ 112
SURA YA TATU 115
MBINU ZA UTAFITI........ 115
3.0 Utangulizi........ 115
3.1 Sehemu ya Utafiti 115
3.2 Taarifa kuhusu Wahojiwa 118
3.2.1 Taarifa kuhusu kabila la washiriki 118
3.2.2 Taarifa kuhusu jinsia ya wahojiwa 119
3.2.3 Kuhusu Umri wa wahojiwa 120
3.2.4 Elimu ya wahojiwa 123
3.3 Usanifu wa Utafiti 125
3.4 Sampuli 126
3.4.1 Sampuli ya wahojiwa 126
3.5 Usampulishaji 129
3.5.1 Mbinu za Usampulishaji........ 129
3.5.1.1 Usampulishaji lengwa 129
3.5.1.2 Usampulishaji wa nasibu 130
3.6 Mbinu za ukusanyaji wa data........ 131
3.6.1 Njia za majadiliano katika utafiti 131
3.6.2 Matumizi ya dodoso 132
3.6.3 Mbinu ya mahojiano........ 136
3.7 Data za Utafiti 137
3.7.1 Data za msingi........ 138
3.7.2 Data za upili 139
3.8 Vifaa vya data 140
3.8.1 Unakilishaji wa data 140
3.8.2 Tarakilishi........ 141
3.8.3 Rununu 142
3.9 Uchanganuzi wa Data 143
3.10 Uthabiti na Kuaminika kwa Mbinu za Utafiti........ 145
3.10.1 Uthabiti wa mbinu za kukusanya data........ 146
3.10.2 Uaminifu wa data 146
3.11 Maadili ya Utafiti 147

3.12 Mpango wa Ushiriki wa Jamii 148
3.13 Muhtasari 148
SURA YA NNE 150
ATHARI ZA SARUFI YA KINYANKORE NA MAFUNZO YA KISWAHILI KAMA L2 150
4.0 Utangulizi 150
4.1 Aina za Fonimu za Kinyankore 150
4.1.1 Vokali fupi za Kinyankore 151
4.1.2 Irabu ndefu 152
4.1.3 Konsonanti za Kinyankore na Kiswahili 154
4.2 Jinsi Kiswahili kinavyoathiriwa na L1 ya Kinyankore 156
4.2.1 Athari za kisemantiki (maana) 156
4.2.2 Athari za kimsamiati 160
4.2.3 Athari za Kifonolojia 161
4.2.3.1 Kubadilisha fonimu 162
4.2.3.2 Athari ya matumizi ya /θ/ 165
4.2.3.3 Athari katika matumizi ya /ð/ 168
4.2.3.4 Athari za matumizi ya / γ/ 169
4.2.3.5 Uchopekaji 170
4.2.3.6 Kudondosha fonimu 178
4.3 Athari za Kimofolojia 179
4.3.1 Namna ya kuchambua vivumishi vya sifa 180
4.3.2 Vivumishi vimilikishi 181
4.3.3 Vivumishi vya idadi 182
4.3.4 Vivumishi vionyeshi 184
4.4 Athari za Kisintaksia (Kimuundo) 185
4.5 Muhtasari 187
SURA YA TANO 188
ASILI YA ATHARI ZA SARUFI YA L1 KATIKA MAFUNZO YA L2 188
5.0 Utangulizi 188
5.1 Sababu za Kutokea kwa Taathira za L1 Iliyo Kinyankore katika Kujifunza L2 iliyo Swahili 188
5.1.1 Mwingiliano wa L1 188
5.1.2 Matumizi ya ala sauti za kaakaa 192

5.1.3 Fonimu za /θ/ na / ð / hazipo katika Kinyankore 194
5.2 Mafundisho Yasiyofaa ya Kiswahili...194
5.3 Kiswahili Haipewi Kipaumbele...197
5.4 Mtagusano wa Kinyankore na Kiswahili...199
5.5 Thamani ya desturi za Wanyankore...200
5.6 Ukosefu wa Mazingira Rafiki ya Kufunzia Kiswahili.......................................201
5.7 Kinyankore kuwa Kitambulisho cha Jamii..202
5.8 Upungufu wa Wataalam wa Swahili..203
5.9 Mafunzo Yasiyokidhi Kiwango Sanifu 204
5.10 Ujuzi na Tajriba ya Wafundishao Swahili..205
5.11 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili...206
5.12 Wazazi Kutoheshimu Kiswahili 207
5.13 Mbinu Zisizofaa za Ufundishaji..209
5.14 Muhtasari 211
SURA YA SITA...212
MBINU ZA KUFUNZA KISWAHILI KAMA L2 212
6.0 Utangulizi...212
6.1 Namna ya Kukabili Changamoto Zinazokumba Usomaji wa L2 212
6.1.1 Haja ya Kiswahili kufundishwa tangu Utotoni 212
6.1.2 Haja ya Mijadala ya L2 ipewe Kipaumbele..213
6.2 Haja ya Uhamasishaji wa L2 214
6.3 Haja ya Ajira ya wanaofundisha L2..216
6.3.1 Mchango wa tamaduni za Kinyankore..217
6.4 Haja ya Umahiri wa Walimu 219
6.5 Haja ya Mazingira Yafaayo ya Kufundishia Kiswahili 221
6.6 Uhamasishaji wa Wazazi na Watoto kuhusu L2...222
6.7 Muhtasari wa Sura 223
SURA YA SABA 224
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 224
7.0 Utangulizi...224
7.1 Muhtasari wa Utafiti 224
7.2 Matokeo ya Utafiti 227
7.2.1 Jinsi umilisi L1 unavyoathiri usomaji wa L2 231
7.2.1.1 Kimsamiati...231

7.2.1.2 Kifonolojia 232

7.2.1.3 Kisemantiki 233

7.2.1.4 Athari za kisintaksia (kimuundo) 234

7.2.2 Sababu zinazosababisha athari za Kisarufi 234

7.2.2.1 Mchango wa L1 234

7.2.2.2 Kutumia L2 shuleni tu 235

7.2.2.3 Ukosefu wa sauti /θ/ na /ð/ katika Kinyankore 235

7.2.2.4 Ufundishaji usiofaa wa Kiswahili 235

7.2.2.5 L2 kutothaminiwa kama lugha muhimu 236

7.2.2.6 Kuimarisha desturi za wanyankore 236

7.2.2.7 Mazingira duni ya kufundishia Kiswahili 236

7.2.2.8 Lugha ya Kinyankore hutumika kama utambulisho 237

7.2.2.9 Vipindi vinavyotumika kufundisha L2. 237

7.2.2.10 Mafundisho yasiyofaa kwa wanafunzi 238

7.2.2.11 Tajriba ya wahadhiri kuhusu Swahili 239

7.2.2.12 Matumizi yasiyofaa ya Stadi za kufunzia 240

7.2.2.13 Ukosefu wa baadhi ya msamiati wa Kiswahili 241

7.2.3 Mbinu bora za kufunzia L2 ya Swahili 242

7.3 Hitimisho 246

7.4 Mapendekezo ya Utafiti 246

7.5 Mchango wa Utafiti 249

MAREJELEO 251

VIAMBATISHO 256

Kiambatisho 1: Hojaji lililojazwa na wanafunzi 256

Kiambatisho 2: Hojaji lililojazwa na walimu 261

Kiambatisho 3: Wamilisi wanaoelewa Kinyankore Wanavyozungumza L2 ya swahili 264

Kiambatisho 4: Wanafunzi wa L1 ya Kinyankore katika Ngazi Tofauti wazungumzaji wa Kiswahili. 267

Kiambatisho 5: Idhini ya REC 269

Kiambatisho 6: Matokeo kutoka uwanjani 270

Kiambatisho 7: Cheti cha Plagiarisim 286

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Tofauti iliyopo kati ya Uamiliaji lugha na Ujifunzaji lugha 27
Jedwali 2.2: Kufanana kwa Kileksia kwa lahaja nne za Kirunyakitara......................30
Jedwali 2.3 Sifa bainifu za Irabu za Kiswahili 60
Jedwali 2.4 Sifa za Konsonanti za Kiswahili...66
Jedwali 3.1 Umri wa Wahojiwa...121
Jedwali 3.2 Elimu ya washiriki..123
Jedwali 3.3: Sampuli ya wahojiwa...127
Jedwali 4.1: Matumizi ya irabu tano fupi 151
Jedwali 4.2: Matumizi ya irabu ndefu...152
Jedwali 4.3: Matriki ya irabu za Kinyankore..153
Jedwali 4.4: Konsonanti na Nusu Irabu za Kinyankore...155
Jedwali 4.5 Athari za Kisemantiki...158
Jedwali 4.6 Makosa ya Kileksika...160
Jedwali 4.7 Jinsi fonimu zinavyobadilishana...163
Jedwali 4.8: Ubadilishanaji wa Fonimu wa /l/ na /r/ 164
Jedwali 4.9: Ubadilishanaji wa /ki/ na /chi/...164
Jedwali 4.10: Makosa yaliyojitokeza katika matumizi ya /Ɵ/ 166
Jedwali 4.11 Matumizi ya /ð/...168
Jedwali 4.12 Matumizi ya / γ / 170
Jedwali 4.13 Matumizi ya uchopekaji wa /e/ na /i/...171
Jedwali 4.14: Uchopekaji wa /e/ mwanzoni mwa neno..172
Jedwali 4.15 Uchopekaji wa /i/...173
Jedwali 4.16 Matumizi ya /o/ na /u...175
Jedwali 4.17: Maneno kadhaa ya uchopekaji 176
Jedwali 4.18: Athari ya Udondoshaji wa sauti /h/ 178
Jedwali 4.19: Vivumishi vya sifa...180
Jedwali 4:20: Matumizi ya vivumishi vimilikishi 182
Jedwali 4:21: Matumizi ya vivumishi vya Idadi...183
Jedwali 4:22: Matumizi ya vivumishi vionyeshi 184
Jedwali 4.23: Jinsi sarufi ya Kinyankore inaathiri miundo ya sentensi za Kiswahili 186
Jedwali 5.1: Wanavyotumia lugha nyumbani..189
Jedwali 5.2: Watafitiwa - Walioshiriki 190

Jedwali 5.3: Watafitiwa 191
Jedwali 5.4: Athari za kimsamiati 191
Jedwali 5.5: Sauti zinazotamkwa kwa Kaa kaa laini 193
Jedwali 5.6 Uchopekaji wa /θ/, /ð/ 194
Jedwali 5.7: Makosa ya walimu 195
Jedwali 5.8: Ubadilishanaji wa /l/ na /r/; /th/ na /s/ 195
Jedwali 5.9: Wanaopendelea Kinyankore kuliko Kiswahili 197
Jedwali 5.10: Wanaoathiriwa na mazingira 201
Jedwali 5.11 Washiriki walimu wa Kiswahili 204
Jedwali 5.12: Umilisi wa Walimu 206
Jedwali 6.1: Wahusika walipoulizwa juu ya kufundisha Kiswahili tangu utotoni 213
Jedwali 6.2: Wahusika walipoulizwa Kuhusu nafasi za kuzungumza Kiswahili 214
Jedwali 6.3: Wahusika walipoulizwa kuhusu umuhimu wa kujifunza Kiswahili 215
Jedwali 6.4: Walipoulizwa kuhusu Kuajiri Walimu wengi wa Kiswahili 216
Jedwali 6.5: Wahusika kuhusu lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele 218
Jedwali 6.6: Wahusika kuhusu Walimu wenye umahiri wa kufundisha Kiswahili 220
Jedwali 6.7: Wahusika walipoulizwa juu ya mazingira ya kufundishia Lugha ya Kiswahili 221

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Vokali 59
Kielelezo 2.2: Matumizi ya Uchanganuzi Makosa 95
Kielelezo 2.3: Kielelezo cha Matumizi ya Mfumo wa Kinadharia wa Changanuzi-Linganishi 99
Kielelezo 2.4: Matumizi ya mfumo wa mtazamo wa kinadhariakidhi ya kimawasiliano 103
Kielelezo 3.1: Ramani ya Jiji la Mbarara kama sehemu utafiti ulikotokea 116
Kielelezo 3.2: Kuhusu jinsia ya washiriki 119
Kielelezo 3.3: Umri wa Wahojiwa 121
Kielelezo 4.1: Sauti za Vokali Fupi za Kinyankore 151
Kielelezo 4.2: Jinsi Uchopekaji wa /i/ unavyojitokeza 174

UFAFANUZI WA ISTILAHI

Mirudio	- Urudufu wa Visa
Mizani ya Likati	- Mizani ya kupima mielekeo ya lugha.
Mwelekeo chanya wa lugha	-Hali ya kuipenda lugha
Mwelekeo hasi wa lugha	- Hali ya kutoipenda lugha

ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

FY	Fasili yangu
GWP	Government White Paper
IPA	International Phonetic Alphabet
KN	kundi nomino
KT	Kundi Tenzi
L1 -	Lugha Mama
L2 –	Lugha ya Pili
N	Nomino
NCDC	National Curriculum Development Centre
NKM	Nadharia Kidhi ya Mawasiliano
NUL	Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi
NUM	Nadharia ya Uchanganuzi Makosa
REC	Research Ethics Committee
SPSS	Statistical Package for the Social Sciences.
T	Kitenzi
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Utafiti wa Kiswahili ambayo kwa sasa ni TATAKI
UNEB	Uganda National Examination Board
UNESCO	United Nations Education Scientific and Cultural Organization.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii inahusu utangulizi unaojumlisha maswala yenye kujadili hata kubainisha vipengele vinavyohusiana juu ya mambo muhimu ya jumla katika utafiti mzima. Baadhi ya vigezo vinavyoshughulikiwa katika sehemu hii ni kama vile, utangulizi kuhusu utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, yale maswali yanayotokana na shabaha za utafiti, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti na hata ufafanuzi juu ya lugha zilizofanyiwa utafiti za Kinyankore na Kiswahili.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujadili taathira zinazotokana na mwingiliano wa sarufi ya Kinyankore zinazokabili wanafunzi wa Kinyankore kwenye shughuli zinazozingatiwa kusoma funzo lililo la swahili walio katika asasi za elimu wilayani Mbarara. Mwingiliano wa lugha ni dhana inayorejelewa kama matumizi ya lugha nyingi katika mazingira na wakati mmoja[1]. Pia, Thomason, Sarah Grey na Kaufman wanasema kwamba lugha zinazoweza kuleta taathira za kiisimu ni zile zilizoko katika mawasiliano yanayokuwa yanakaribiana kupitia muda mrefu sana kama miaka inayozidi mia moja au hata mia mbili. Alieleza kategoria mbalimbali zinazoweza kuathiri na kujitokeza kwenye mwingiliano huo hata kufafanua kwamba taathira hizo hazijitokezi tu katika maneno, bali pia katika vipengele vyote vya kimuktadha kwa kutegemea mifumo ya matamshi, miundo inayoongoza maumbo, jinsi ya kutunga tungo na sentensi kamili, maana inayojitokeza kwenye tungo hizo, halafu leksimu zenyewe kama msamiati unaoangaziwa. Kazi za Sarah Grey Thomason na Terrence Kaufman zinazoonyeshwa katika chapisho la Language Contact ambalo linajadili mwingiliano wa lugha pamoja

---

[1] Thomason, Sarah Grey, and Terrence Kaufman. *Language Contact*. Citeseer, 2001.

na mchango wake katika mifumo ya kisarufi, kimsamiati, na semantiki. Kazi hiyo imeangazia njia mbalimbali ambazo lugha zinavyoathiriana zinapokutana kwenye mikutadha mbalimbali, ambayo inahusisha mifano kama vile athari za kihistoria na za kijamii. Wakati wa uchambuzi, waandishi wanaangazia mifano ya mwingiliano wa lugha, mila za lugha, na mabadiliko ya lugha yanayotokea kutokana na mwingiliano huo, wakitoa mitazamo ya kitaaluma na tafiti mbalimbali zinazohusiana.

Hali ambayo inayofafanuliwa zaidi ni kuwa yale maneno ambayo wanafunzi waliyokosea wakati wanapokuwa wanasoma lugha ni dalili kwamba kuna changamoto kuelewa hasa vigezo kadhaa katika lugha hiyo[2]. Katika kazi hii, Lado anachambua changamoto ambazo walimu wa lugha wanakabiliwa nazo wakati wa kufundisha wanafunzi kutoka tamaduni mbalimbali. Anapitisha nadharia za isimu zinazoweza kuimarisha njia zinazotumika katika kufundisha na kuelezea njia za kuboresha matumizi hasa ya kuwasiliana na wenye lugha tofauti.

Kitabu hiki kinafaa sana hasa kuhusu nyanja ya isimu inayotumika wakati wa kuchunguza mwongozo wa jinsi ya kutumia njia bora kadhaa za kufundisha kwa ajili inayolenga kukabili shida zinazohusiana na kutumia lugha vibaya na kusaidia wanafunzi na haja zao au wasikilizaji kutoka tamaduni tofauti. Lado pia anasisitiza umuhimu wa uelewa wa kimaadili na hisabati wakati lugha hiyo nyingine inapofundishwa.

Watafiti walioshughulikia uwanja wa kiisimu wanadai kuwa lugha asili inaathiri mkakati wa kufundisha lugha nyingine ambapo inasisitizwa kwamba kuna changamoto zinazoikabili mtu anayeshughulikia masomo ya lugha nyingine. Changamoto hizi

[2] Katika kazi ya Lado, R. (1957) inayoitwa *Linguistics across Cultures: Applied Linguistics and Language Teachers,* anatoa mtazamo wa pekee juu ya uhusiano kati ya isimu na tamaduni. Lado anajadili jinsi isimu inavyoweza kutumika katika mazingira ya kufundisha lugha, akisisitiza umuhimu wa kuelewa tofauti za kisimu na tamaduni zinazohusiana na lugha tofauti.

zinatokana na uhamishaji wa kanuni zinazotawala vigezo vya kisarufi kuanzia L1 mpaka kuathiri L2. Inadaiwa pia kuwa kila muundo la lugha unajitokeza kwa namna ya kipekee ikitofautiana na nyingine, kwani kuhamasisha hizo kanuni za sifa zinazojitokeza katika lugha ya asili kwenye lugha nyingine kunasababisha utokeaji wa kukosea wakati wa kutumia lugha nyingine[3].

Pia, tofauti za kisarufi zinaweza kutokana na jinsi lugha ya asili inavyoundwa. Jambo hili linasababishwa na kuwepo kwa kategoria ya muundo ulio na sentensi kama unavyojitokeza kulingana na lugha ya asili unaweza kumwathirisha mtu anapozungumza lugha nyingine. Kuingiliana kwa lugha popote kunapojitokeza kunatoa fursa kubwa pale ambapo zinaathiriana kwa vigezo mbalimbali. Kwa kurejelea jamii kadhaa za kiafrika Kiswahili kinadhaniwa kuingilia lugha nyingine ambazo zinakaribiana, na taathira hiyo ya lugha ya asilia inajitokeza sana sana katika matamshi[4]. Katika kazi hii, maelezo ya kina yanatolewa juu ya nadharia za lugha na jinsi zinavyohusiana na Kiswahili, pamoja na mifano na mazoezi yanayosaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi dhana hizo. Pia shughuli za kujifunza ambazo zinawasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao zinajumuishwa ili kukuza mazingira yaliyo tofauti kulingana na namna ya kutumia maumbo hayo ya L2.

Taathira kutokana na lugha ya asili zinahusu mchakato wa kusoma lugha nyingine ambazo zimechunguzwa na kufafanuliwa, zikionyesha kuwa lugha nyingine inapokuwa inafunzwa, mwanafunzi anaathiriwa na jinsi lugha inavyoundwa aliyoijua

---

[3] Otiende, M.A (2013). *Athari za Kimofofonolojia za kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama Lugha ya pili.* Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

[4] Kitabu cha Masebo, J. A na Nyangwine, N. (2008) kinachoitwa Nadharia ya lugha, Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6 ni mwongozo wa kujifunza lugha kwa wanafunzi wa shule za sekondari hasa kwa ngazi ya kidato cha 5 na 6. Kitabu hiki kinaangazia dhana na misingi ya isimu, likijumuisha vipengele mbalimbali vya lugha kama vile sarufi, fonetiki, semantiki, na muktadha wa lugha.

tayari kulingana na lugha ya asilia[5]. L2 ya Swahili inaathirika na zile lugha zenye ushirikiano na ukaribu wa kuwa za kibantu kwa ngazi za kisemantiki, kileksika, na kisarufi. Mitazamo mbalimbali inajadiliwa kuhusu uhusiano wa lugha mbili na jinsi namna lugha inavyofahamika inavyoweza kuathiri maendeleo ya watoto. Mifano ya maendeleo yanayohusu sayansi ya utafiti inatolewa kuhusu lugha, ikijielekezwa katika athari za kijamii na kisaikolojia zinazohusiana wakati wa kusoma lugha kadhaa.

Pia umuhimu wa mazingira ya kijamii na kabila kulingana na mfumo wa kufundisha masomo ya kilugha unaangaziwa, ukionesha jinsi lugha mbili zinavyoweza kufanana na kutofautiana katika vipengele tofauti mkiwemo sarufi, fonetiki, na msamiati.

Sarufi inaelezwa kama mfumo wa kanuni ambazo katika lugha hiyo hiyo zinadhihirisha uwezekano wa kutumika kwa lugha husika.[6]. Sarufi pia ni dhana inayojumuisha vipengele vya fonetiki, matamshi, maumbo, miundo na Semantiki[7]. Sarufi kwingineko inafafanuliwa kama dhana inayoeleweka kuwa inatumia kanuni za kijumla zinazoongoza kuongea na kuandika lugha sahihi[8].

Uchambuzi wa kisarufi ulilenga kufuatilia jinsi vipengele vya kimatamshi, kimaumbo, kimuundo, na kimaana vinavyoshirikiana kulingana na vile lugha ilivyoundwa[9]. Aidha, Sarufi huweza kufafanuliwa kama maneno ya kiisimu yanayorejelea makundi yote

---

[5] Katika kazi yake Hagége, C. (1999) ya *The Child Between Two Languages*, anachunguza jinsi watoto wanavyoshughulikia na kujifunza lugha mbili kwa wakati mmoja. Hagége anasema kwamba kujifunza lugha mbili kunaweza kuwa na manufaa makubwa kwa watoto, lakini pia kuna changamoto ambazo wanakutana nazo.

[6] Katika kitabu chake Mdee, anaangazia maendeleo ya kamusi za Kiswahili na athari za teknolojia katika uandishi wa kamusi. Anaonyesha pia umuhimu wa kamusi katika kujifunza na kuhifadhi lugha. Pia, anachangia katika utafiti wa lugha na inatoa mwanga juu ya mabadiliko yanayoweza kufanyika katika nyanja hiyo.

[7]. Tasnifu hii inatoa mwanga kuhusu athari za lugha ya kwanza katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya pili, ikichangia katika maarifa ya kiisimu na elimu ya lugha.

[8] TUKI (2013). *Kamusi ya Isimu na Lugha,* Dar-es-salaam: Education Publishers and Distributors.

[9] Collins, G (2015). *Language to Motivate Learning: The Power of Inspirational Quotes.*

yanayohusiana na misingi ya kiisimu na jinsi yanavyotumika katika lugha fulani.[10]. Hii inamaanisha kwamba dhana kama namna lugha inavyoendelea, athari za mazingira ya kijamii kwenye mfumo wa kusoma lugha huwa ni tofauti kwa kurejelea lugha kama ya Watoto, pengine na ile lugha inayotumika na watu wazima yanahusishwa. Pia, uchambuzi wa mifumo tofauti ya isimu zinazohusiana na kujifunzia lugha unatolewa kwa kuhusisha utafiti wa kisayansi na mifano halisi kutoka kwa wanafunzi.

Hivyo, mtagusano wa kisarufi ni hali ambapo muundo wa namna ya kutumia lugha kutokana na lugha ya asilia na lugha nyingine unashirikisha vipengele vya kisarufi kama vile matamshi, maumbo, miundo, hata maana, na unategemea athari kubwa za uhusiano, ukaribu, hata mlingano wa muundo au kitipolojia. Kwa hivyo, mtafiti alitumia sarufi kama usahihi wa sentensi na tungo nyinginezo za lugha. Sentensi sahihi ya kisarufi lazima izingatiwe na upatanishi wa ngeli, vivumishi, virejeshi, vibaini, vitenzi, udogo, na ukubwa nakadharika ikilinganishwa kwenye kiwango cha mikutadha inayotumika.

Lugha zinapokuwa na mwingiliano huwa na athari zinazojitokeza upande zote mbili. Athari hizi hazitokei tu kutofautisha lugha mbalimbali, bali pia ndani ya lugha zinazotokana na kundi moja. Massamba (2006) anasema kwamba ufahamu juu ya lugha asilia unachangia pakubwa katika uelewa wa lugha nyingine. Kuingiliana huku kunatoa athari ambazo zinakuwa tatizo Zaidi katika ufahamu wa wale wanafunzi wanaojifunza Kiswahili nyingine ya ziada kwa kuzingatia uwezo wa ufahamu wa lugha moja tu. Lusesa (2013) anasisitiza kwamba kufahamu lugha asilia ni msingi muhimu wa kusoma lugha nyingine. Anazidi kueleza kuwa tajriba ya kutumia lugha hiyo asilia huathiri

[10] Kazi ya Crystal, David (1980) iitwayo *Child Language Learning and Linguistics* inachunguza mchakato wa kujifunza lugha kwa watoto na uhusiano wake na isimu. Kitabu hiki kinatoa mtazamo wa kina kuhusu jinsi watoto wanavyopata lugha, kuanzia hatua za awali za kutamka maneno hadi kuelewa na kutumia sarufi na msamiati wa lugha.

mchakato wa kusoma lugha inayotakiwa kuongezeka. Wakati wa uhamishaji huu, makosa yanajitokeza kwa kuwa mabadiliko ya kilugha yanajitokeza katika uwanja wa kimatamshi na kimaumbo kuzilinganisha hizo lugha mbili au zaidi. Kwa hivyo, kusoma lugha nyingine kutaweza kuwa kugumu na kuleta athari kubwa ikiwa kuna jinsi muundo unavyotofautiana katika sauti baina ya lugha iliyo asilia na lugha nyingine. Kadhalika, ikiwakunatokea tofauti zinazojitokeza kati ya miundo hiyo ya lugha mbili, changamoto za kusoma lugha nyingine tena zitakuwa kubwa. Ili kubaini matatizo yanayojitokeza kwenye mkakati wa kusoma lugha nyingine, ni muhimu kuelewa tofauti zilizopo baina ya hizo lugha kadhaa. Njia ya kutatua matatizo hayo ya athari ni kuelewa jinsi matatizo hayo yanavyoweza kujitokeza katika sauti, namna maneno yalivyoundwa, au hata sarufi.

Kulingana na mtaalam Rocha (2011) anaeleza ya kuwa L1 inayotangulia hufasiliwa kama lugha inayotumika na msemaji kwa ajili ya mawasiliano ya kwanza kabisa katika Maisha yake wakati ambapo jajifunza lugha yoyote nyingine ile. Kwa kuzingatia lugha nyingine ni ile ya pili inayojifunzwa na mtu akishamaliza kuelewa na kusoma lugha asilia. Mtumiaji wa lugha huenda akajifunza lugha katika mazingira mbalimbali; kwa mfano, anaweza kujifunza akitumia mbinu kadhaa ambazo si za rasmi kwa kusikiliza wenzake au kwa njia rasmi katika darasa. Aidha, mwingine huenda akajifunzia lugha nyingine ya pili akizingatia jinsi lugha inavyotumika katika nchi au eneo fulani inapotumika.

Aidha, watu wenye ujuzi katika lugha mama wanategemea ujuzi huo wanapojifunza stadi za lugha nyingine. Kulingana na Lusesa (2013) uzoefu anaotumia mwanafunzi kufahamu na kutumia stadi za lugha inayotangulia huhamishwa kwenye matumizi ya lugha ile inayofunzwa ili kuwezesha ujifunzaji. Uhamishaji huu unaweza kusababisha makosa mbalimbali, hasa pale ambapo mikakati ya lugha husika inapotofautiana. Yeye

Lusesa (keshatajwa) anabainisha kwamba lugha hii inayojifunzwa ya Kiswahili inavyopata athari kutokana na hasa ile lugha inayofundishwa, wakisema, "Hiyo lugha inayokuwa yap li wakati wa masomo ni ya watu wanaoishi katika ukingo wa bara kubwa. Hivyo, watumiaji waliotangulia hawawezi kuepuka namna inavyoathiriwa au ikaathiri watumiaji wanaoisema." Walidhihirisha pia jinsi lugha kama ya Kiarabu ilivyoingilia Swahili na ikaiathiri. Pia, inajulikana wazi kwamba lugha moja huweza kuingilia nyingine wakati zinapotagusana.

Swahili inazidi kusonga mbele kama lugha inayopiga hatua kubwa, kikipanuka kwa kuendelezwa na kutumika katika maeneo mbalimbali kikiwa na majukumu mengi. Lengo lake ni kuhakikisha inafanya kazi katika shughuli za kuwasiliana kwa nyakati hizi kufuatia tanzu zote zinazoshughulikiwa kitaaluma. Wakati wa maendeleo haya na kutekeleza majukumu yake, Kiswahili kimeathiriwa na kuzingatia sifa na matumizi ya lugha mbalimbali za Kiafrika na zisizo za Kiafrika. Hivyo, licha ya kupanuka kwa lugha hii, inaendelea kuwa na athari humu Afrika Mashariki na Afrika Kati, ambapo lugha hii imeingiliana na lugha nyingine na kuleta athari.

Mukuthuria (2004), alipokuwa anatafiti miundo ya jinsi lugha zinavyoathiriana hasa ya Kiswahili na ile ya Kitigania, alieleza kwamba utafiti wa athari hauhusishi tu kutambua sababu za kuathiriana, bali pia kusaidia kubaini shida za kisarufi zinazosumbua wanafunzi na zinazoelekea kusababisha taathira hizo, ili kuthibitisha kwamba yanatafutiwa suluhisho na kuyakamilisha. Ingawa utafiti unaohusu taathira kutoka ile lugha ya asili kwenda kwa lugha inayojifunzwa kama ya pili au ya tatu umewavutia wataalamu wengi, na kuna mahitaji zaidi ya kuendelea na utafiti wa kutosha ili kubaini chanzo cha athari hizo na kutuwezesha kutatua matatizo yanayohusiana na masomo ya Kiswahili.

Kiswahili kinakisiwa kuzungumzwa na watu kati ya milioni 120 hadi 150 (Kihore na wenzake, 2001 ananukuu Malcolm Guthrie (1948) kuwa aliainisha Swahili kwenye kategoria ya zile lugha zinazotumika kwenye eneo la maziwa makuu za wenyeji wa Kibantu katika ukanda wa G, kundi la 40, na kile cha pili. Lugha hii ina nambari G42 kama mmoja wapo ya baadhi ya lugha zinazozungumzwa barani Afrika. Kulingana na data hizo, Kiswahili huenda kikawa na wazungumzaji zaidiya Mia mbili (200) mwakani 2024.

Kulingana na mkakati wa Katiba ya jamhuri ya Uganda ya 1995 hii lugha inayojulikana kama Kiswahili iliidhiinishwa kama lingua franka ili itumike katika taifa zima kadri na maamuzi ya bunge. Uganda ina wazungumzaji takribani 313,000 ambao huzungumza lugha hiyo ikitumika kwa kiwango cha uasilia wake, na watu zaidi ya milioni kumi na tatu na laki nane (13,800,000) ambao huzungumza lugha yenyewe kwa mfumo wa kiwango cha lugha ile inayofunzwa shuleni. Kulingana na sensa ya 2024 inaeleza kuwa wazungumzaji wengi wanatoka katika eneo la Magharibi, Mashariki, Kaskazini na baadhi ya wasomi na wafanyi biashara katika eneo la kati na kusini mwa nchi. Kiswahili kiliingia nchini Uganda kabla ya kuja kwa wakoloni mnamo mwaka 1844 (Masereka 2020).

Masereka alisisitiza kuwa Kiswahili kilikuwa na mwanzo mzuri nchini Uganda kabla mifumo ya utawala wa kikoloni. Kilitumiwa katika shughuli za kibiashara na mawasiliano yalikamilishwa kuwezesha watu wenye asili mbalimbali kutangamana wa kikabila kutoka maeneo mbalimbali. Kiswahili kilitagusana na lugha za makabila mengi ya kiafrika katika maeneo ya kati na magharibi ya Uganda, ambapo watu walifanya biashara na kuhamasisha utamaduni wao hasa lugha zao. Hii ilichangia katika kuimarisha uelewa wa lugha ya kibiashara iliyotumika katika baadhi ya jamii husika zinazozungumza lugha za Bantu. Katika kipindi hicho, Kiswahili kilitumika

kuwezesha hasa mawasiliano kati ya wanajamii, wasiokuwa na lugha sawa. Hii ilifanyika hasa kuwezesha shughuli hizo za kibiashara, ambapo watu walihitaji kuelewana ili kufanikisha shughuli zao.

Masereka (2020) anatoa picha ya wazi kuhusu nafasi ya lugha hii iliyoteuliwa katika nchi ya Uganda nyakati za watawala wa kikoloni walipokuwa bado hawajadunisha lugha za kienyeji, ikionyesha jinsi lugha hiyo ilivyokuwa msingi wa mawasiliano, biashara, na mabadiliko ya utamaduni. Utafiti huu hauwezi kupuuzia kwani unaleta mwanga kuhusu mambo yanayohusiana na Kiswahili yakionyesha umuhimu wake na jinsi ilivyosambazwa kote katika jamii nchini Uganda, ambao unaweza kusaidia kuelewa muktadha wa lugha hiyo katika siku za kisasa.

Wakati wa kufanya huu utafiti, malengo yake yalikuwa kufafanua athari za mtagusano wa sarufi ya Kinyankore na jinsi Kiswahili fasaha kinavyotumika, ukijumuisha vipengele vinavyohusu jinsi maneno yanavyotumika hasa aina yake, matamshi, viwakilishi nafsi, vikanushi, vivumishi, mifumo ya kisintaksia, maumbo ya kimofolojia, maana inayojitokeza na vile inavyotumiwa na wenyeji wake. Hata ingawa kuna tafiti zilizofanywa kuhusu athari na mwingiliano kuhusu lugha zinazoingiliana zenye utamaduni wa kibantu zikilinganishwa na Kiswahili, jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoathiri wanafunzi wanapokuwa wakisoma lugha hiyo nyingine ya Kiswahili fasaha hazijaanishwa ipasavyo ili kuonyesha upungufu unaodaiwa na wanaisimu wakirejelea mazingira ya wanyankore wa nchi ya Uganda.

Huu utafiti wa kuangazia athari za sarufi ya Kinyankore kwa wanaofundishwa masomo ya Kiswahili fasaha unalenga kubaini jinsi sifa za sarufi kutoka Kinyankore zinavyoathiri namna ya kutumia lugha inayokuwa ya Kiswahili, hususan katika vipengele mbalimbali vya sarufi.

Kwenye ngazi ya sarufi inayohusiana na matamshi, Utafiti huu unachunguza jinsi matamshi na lafudhi za Kinyankore zinaweza kuathiri matamshi ya Kiswahili. Wanafunzi wanaotoka katika mazingira ya Kinyankore wanaweza kuleta tofauti za kipekee zinazolingana na vile wanavyotamka Kiswahili.

Ngeli za majina zilipozingatiwa, Kiswahili kina ngeli tofauti zinazotumika kwa nomino, wakati Kinyankore kina namna yake ya kupanga ngeli hizo. Utafiti huu unachunguza jinsi wanafunzi wa Kinyankore wanavyoweza kuhamisha matumizi ya ngeli za Kinyankore kwa Kiswahili, labda kwa kuchanganya ama kufikia makosa katika uorodheshaji wa ngeli. Halafu, viwakilishi vya nafsi vilipochunguzwa, Utafiti unaangazia jinsi viwakilishi vinavyoonyesha nafsi (kama vile mimi, wewe, yeye) vinavyotumiwa kwa kuelezea Kiswahili kwenye matumizi yao yanaweza kuathiriwa na muundo wa viwakilishi katika Kinyankore. Aidha katika utafiti wa aina hiyo, tunabaini jinsi vikanushi (kama vile si, hapana) vinavyotumika kwenye lugha iliyo ya Kiswahili hasa ikiwa kuna tofauti yoyote katika matumizi kutokana baadhi ya mitazamo ya vikanushi katika Kinyankore. Vivumishi katika Kiswahili vinaweza kuathiriwa na mifumo ya vivumishi ya Kinyankore. Utafiti ulichunguza matumizi ya vivumishi, kama vile namna ya kuunda vivumishi, aina za vivumishi, jinsi vivumishi vinavyojitokeza katika maumbo ya Kiswahili, na kadhalika. Pengine, huo utafiti uliangazia jinsi miundo ya kutunga sentensi za Kiswahili zinavyokuwa kwenye uwiano wake na vile namna sentensi za Kinyankore zinavyowekwa. Hii inajumuisha jinsi sentensi zinavyoundwa, matumizi ya viunganishi, na ushirkiano uliopo kwa sentensi hizo. Utafiti huu unaweza kuchambua jinsi milingano ya sarufi kati ya Kinyankore na Kiswahili inaweza kuathiri tafsiri na maana inayojitokeza. Ingawa Kiswahili kina mfumo wake wa maana, namna wanavyotumia maandishi na maongezi ya Kinyankore yanaweza kuleta tafsiri tofauti au makosa ya kisarufi yasiyokusudiwa.

Kwa hivyo, kuelewa jinsi lugha mbili zinavyoingiliana na kuweza kusaidia kuweka mikakati bora kuuinua viwango vya namna wanavyofundisha lugha ambayo inalengwa kuhusisha watu wanaozungumza Kinyankore, Utafiti huu unatoa rasilimali kulenga wafundishao lugha lengwa ya Kiswahili ili waweze kutambua maeneo ambayo wanafunzi wanapata ugumu kwa sababu ya matokeo ya mtagusano ulioathiriwa na sarufi. Utafiti huu unaweza kuleta mwangaza wa kina kuhusu changamoto na fursa zinazowakumbana wajifunzao wale wanaozungumza Kinyankore, hivyo kusaidia kuifanya ziwe nzuri njia ya kuwafundisha wanafunzi wanaolengwa kumiliki lugha nyingine.

Utafiti wa utafiti huu ulizingatia vipengele vya kisarufi ili kutambua jinsi Kinyankore kinavyoingiliana na lugha zinazokuwa zinalengwa kufundishwa kama za pili (L2) katika maandiko na mazungumzo, kama yanavyotumika na wanafunzi walio na Kinyankore wakimiliki uwezo wake wa kiasili.

1.2 Suala la Utafiti

Uganda inaendelea kufanya maendeleo katika kueneza na kukuza somo la Swahili kwenye asasi za elimu mkiwemo shule zilizoko chini kama za msingi, za upili, na hata Vyuo na Vyuo Vikuu. Wataalamu mbalimbali kama Lusesa (2013), Nyanda (2015), Munyua (2002) walikwishafanya utafiti unaohusu mtagusano unaotokea kufuatia hiyo lugha inayokuwa inatumika kama ya asili na vile inavyoathiri ile inayofunzwa baadaye kama ya pili. Ingawa tafiti hizi zimefanyika hasa nchini Kenya na Tanzania, hakuna utafiti uliofanywa nchini Uganda ambao unalenga kuchunguza kwa namna gani lugha tangulizi huenda ikaathiri usomaji wa ile lugha inayofuata, hasa mwingiliano wa sarufi ya Kinyankore kwa mchakato wa kujifunzia ile lugha inapokuwa Kiswahili. Kwa sababu ya kwamba utafiti wa aina hii unakosekana, kumesababisha kutokuelewa changamoto zinazowakabili wanafunzi wanyankore wanapojifunza lugha inayolengwa

kufunzwa kukitokea shida za kimasomo. Hivyo, utafiti huu ulichanganua zile taathira zinazojitokeza wakati lugha lengwa inapokuwa inafundishwa kwa wanafunzi walio na uasili wa lugha tangulizi ili kubaini changamoto zinazohusika katika hatua zote ili hatimaye kutoa maelezo ya kiufundi wa elimu kuimarisha mafunzo ya somo la Kiswahili.

Sababu za kufanya huu utafiti ni kueleza, kutathmini, na kufafanua mwingiliano wa sarufi ya Kinyankore kwa wanafunzi wanajaribu kusoma sarufi ya lugha lengwa ikiwa ni ya Kiswahili kwenye mawanda ya mazungumzo, maumbo, miundo ya kisintaksia (virai, vishazi, na sentensi), Kimofolojia na kifonolojia. Mtafiti pia alinuia kuchunguza na kuangazia vile ulionyesha miradi ya kufundishia huenda ikaboreshwa ili iweze kuwasaidia wanafunzi wanaoathiriwa na Kinyankore wakati wakijifunza Kiswahili.

1.3 Malengo ya Utafiti

i) Kupambanua athari za sarufi ya Kinyankore kwa mafunzo ya lugha ya pili ikiwa ni Kiswahili.
ii) Kubainisha mchango unaosababisha taathira kwa wanafunzi Wanyankore wanaosoma mafunzo ya sarufi ya Kiswahili.
iii) Kutathmini mbinu za kuboresha ufunzaji wa sarufi ya L2 ya Kiswahili.

1.4 Maswali ya Utafiti

i) Je, sarufi ya Kinyankore inaathiri mchakato wa kusoma lugha nyingine ikiwa ni ya pili?
ii) Je, kuna sababu zinazochangia taathira kutokana na lugha ya Kinyankore wakati wa mafunzo ya lugha nyingine ikiwa ni Kiswahili?
iii) Je, kuna mbinu bora zinazoweza kuwasaidia wanafunzi Wanyankore wanapojifunza somo la lugha nyingine ikiwa ni ya Kiswahili?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mtafiti alichagua uwanja huu kuufanyia utafiti ili kuangazia athari za sarufi ya Kinyankore wakati wa kuendesha masomo ya Kiswahili kwa kurejelea manufaa kadhaa yanayofaa. Kwanza, kujenga Msingi unaolenga kupambanua uhusiano kati ya Kinyankore na Kiswahili. Kinyankore kama ilivyo Kiswahili ni baadhi ya lugha za Kiafrika na hasa za Kibantu, na zina mifumo ya sarufi inayofanana. Kuchunguza jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoathiri mafunzo ya somo la Kiswahili kunasaidia kuelewa masuala ya muktadha juu ya lugha fulani ili kuleta mwangaza kuhusu jinsi wafunzwaji wanavyobeba ufahamu wa kilugha ya kiasili wakatiinapofunzwa kama lugha nyingine. Pili, Kuhifadhi na Kuendeleza Utamaduni. Utafiti huu unasaidia kutoa mwangaza kuhusu jinsi mawasiliano ya lugha mbili yanavyoweza kuathiri uelewa wa tamaduni tofauti. Hii inaweza kuchangia katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Kinyankore na Kiswahili, kwa kuzingatia jinsi wageni wanavyoweza kujifunza kutoka kwa lugha hizo. Tatu, Kuboresha Mbinu za Ufunzaji. Kwa kuelewa athari za sarufi ya Kinyankore wakati wanaposomeshwa mafunzo ya lugha nyingine ya Kiswahili, wazazi, walimu, na watafiti wanaweza kuhusisha njia za kutumia miradi bora ya kufunzia ambazo zinazingatia tofauti za sarufi. Hii inaweza kusaidia kuongeza ufanisi unaorejelewa kufundisha Kiswahili kwa wasomaji wanyankore wenye msingi asili wa Kinyankore. Nne, Kuhakikisha Usanifishaji wa Mafunzo. Shabaha ya utafiti huu ni kuangazia matatizo ambayo wanafunzi wa Kinyankore wanaweza kukutana nayo katika kujifunza Kiswahili. Kuelewa vizuri changamoto hizi inasaidia katika kuboresha mpango wa mafunzo kwa kusisitiza ufanisi wa haja za wanafunzi katika mazingira ya kimasomo.

Hivyo, kuchambua mwingiliano wa sarufi ya Kinyankore wakati Kiswahili kinapokuwa kinasomeshwa kunaweza kutoa uelewa mzuri kuhusu kuingiliana na

mtagusano kati ya lugha husika, utamaduni, na elimu, na hivyo kuchangia katika ukuzaji na usomeshaji unaojitokeza katika mchakato mzima.

1.6 Upeo wa Utafiti

1.6.1 Upeo wa kiufundi

Juhudi zote katika utafiti zilinuia kuchunguza uchambuzi wa mtagusano wa lugha mbili zenye asili ya Kibantu hasa ile ya Kinyankore na vile inavyoathiri jitihada za kusoma sarufi ya Kiswahili. Ili kufanikisha lengo hili, mtafiti alizingatia vipengele vikuu vitatu: kutambua taathira za sarufi ya Kinyankore wakati wa kusoma lugha nyinie ya pili, na kuchanganua kinachosababisha uathirishaji huo kwenye wanafunzi Wanyankore wanaojifunza Kiswahili, na kutoa jinsi mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi wanaathiriwa na Kinyankore wakati wakijifunza mifumo ya sarufi ya lugha nyingine iliyo Kiswahili. Hata hivyo, wazungumzaji wa lugha nyingine isipokuwa Kinyankore hawakuhusishwa wakati wa kushughulikia huu utafiti.

1.6.2 Upeo wa Kijiografia

Utafiti huu ulishughulisha asasi teule mkiwemo shule na Vyuo vikuu vilivyochaguliwa jijini Mbarara nchini Uganda. Jiji la Mbarara lilichaguliwa kwa sababu ndiko chimbuko la wazungumzaji Kinyankore na pia wanaojifunza Kiswahili shuleni na vyuoni.

1.6.3 Upeo wa kiwakati

Fata za huu utafiti zilikusanyika ndani ya miezi mitatu kulingana na muhula wa shule. Utafiti ulitendeka kuanzia mwezi wa Septemba 2023 hadi mwezi wa Disemba 2023 ambapo ulikuwa muda wa wanafunzi kuwa shuleni. Halafu data za uwanjani zilichanganuliwa hapo baadaye na uandishi wa ripoti ulifuatia kuchukua miezi minne hadi mwezi wa Machi 2024.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Shabaha ya utafiti ilikuwa kutoa mchango wa maana kwa kurejelea viwango kadhaa vya kitaaluma, kinadharia, na kiutamaduni kadri na vile itakavyojadiliwa hapo baadaye;

Kwanza kabisa, katika eneo la kitaaluma, utafiti huu unasaidia kufunga pengo katika tafiti kuhusu athari za Kinyankore, haswa kwa wanafunzi wanaosoma lugha nyingine iliyo Kiswahili. Pili, huu utafiti unawafaa wapenzi wanaoelekeza na wengine wanaoendeleza elimu hasa wadau wa kisarufi hasa kwa L2 ya Swahili, wasomaji, wafundishao na maaofisa wa elimu kuelewa athari zinazoweza kutokea kwa kurejelea lugha iliyotangulia, hasa Kinyankore, katika wakati wa kusoma na kuelimishwa lugha nyingine. Hii itawasaidia kukumbana na matatizo yanayoweza kusumbua wasomaji wa lugha nyingine. Tatu, mtafiti anatarajia kwamba utafiti huu utaibua mawazo mapya kuhusu taathira kuhusu vile lugha ya asili inavyoweza kuleta ugumu fulani wakati sarufi ya lugha nyingine inavyofundishwa, ambayo yanaweza kutumika kuunda nadharia mpya au kuboresha nadharia zilizopo katika kuchambua masuala yanayohusu taathira kutoka kwa kuingiliana kwa lugha ya asili kwa mafunzo ya lugha nyingine ikiwa ni Kiswahili.

Utafiti huu unatoa matokeo ambayo yatakuwa ya umuhimu yakilenga walimu na wasomaji wanaoyatumia ili kutabiri uwezekano wa makosa katika harakati zao za kufundisha wanafunzi wenye asili ya kinyankore na wale wa lugha nyingine za Kibantu. Hivyo, wataweza kusaidia wasomaji namna ya kutatua matatizo hayo kwa njia sahihi.

Baadhi ya malengo mengine ya utafiti ni kutoa msingi mzuri kwa tafiti zijazo katika eneo la miundo wa umilisi wa hali ya juu wa kutumia lugha sanifu ya Kiswahili ikijitokeza katika nafasi ya pili. Kiswahili kimepewa kipaumbele na sekta ya elimu

katika kukikuza na kukiendeleza nchini nzima kutokana na umuhimu wake jinsi ilivyo lugha yenye dhima nyingi za mawasiliano, lingua franka, na urasmi katika mikutadha inayoteuliwa na bunge. Kufundisha lugha nyingine ya Kiswahili katika asasi teule kama zilivyochaguliwa kwa ajili ya utafiti unatokana na vile mkakati unaoongoza sera na sharia ya nchi ulivyo ili iweze kuwa ya lazima katika shule hizo[11]. Hivyo, juhudi za kuchunguza utafiti kama huu ulilenga kuendeleza na kutimiza sera ya serikali, kwa kuhamasisha wale wanaohusika katika utungaji wa mitaala ya asasi hizo kuanzisha njia anuai ya kufundishialugha zinazojitokeza katika nafasi ya pili kama ya Kiswahili.

1.8 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii, mambo nyeti yameelezwa. Sura inatoa utangulizi kuhusu shughuli la utafiti ikijadili jinsi habari zilipochimbuka kama usuli, tatizo lenyewe, shabaha za utafiti, yaliyoulizwa kama maswali muhimu, dhima ya utafiti, Nyanja zote za upeo na maeneo ya utafiti kiufundi, kijiografia, na kiwakati.

Hii sura hasa imetuelezea kwa undani kuhusu mambo muhimu ya utafiti inayohusu taathira ya sarufi ya Kinyankore hasa katika usomaji wa Kiswahil katika mazingira ya kusomeka ikiwa katika nafasi nyingine. Tumebainisha suala hili kwa kutenga na kujadili sarufi inayotumika kama lugha asili inavyoathiri miradi ya kufunzia lugha nyingine katika nafasi ya pili, hasa kwa kuangalia mazingira ya wanafunzi wanaozungumza Kinyankore. Pia, tumeona kuwa Kinyankore, kama lugha ya Kibantu, iliyo na mfumo wa sarufi unaofanana na wa Kiswahili, jambo ambalo linaweza kuhifadhiwa kama rasilimali muhimu katika kujifunza. Aidha, kupitia utafiti huu, tunalenga kuangazia changamoto na fursa ambazo zinashughulikiwa kufunzia

[11] *Government White Paper ya Uganda ya mwaka 1992* ilikuwa ni nyaraka muhimu iliyotolewa na serikali ikilenga reformu katika sekta ya elimu. Iliwasilishwa kama majibu kwa ripoti ya Tume ya Elimu, ambayo ilipendekeza maboresho mbalimbali ili kuboresha mfumo wa elimu nchini Uganda baada ya kipindi cha machafuko.

Kiswahili na mtindo wa sarufi kutoka Kinyankore unavyoweza kuathiri jinsi hiyo lugha inavyotumika kama mpya.

Katika sura inayofuata, tunaendeleza uchambuzi huu na kuangazia mapitio ya maandishi, matokeo yaliyopatikana kulingana na wataalam mbalimbali, dhima ya matokeo haya wakati wa kukuza na kuendeleza viwango vya elimu kuhusu lugha asilia (Kinyankore) na lugha nyingine iliyo katika nafasi ya pili (Kiswahili). Pia, sura inayofuata inaangazia muundo wa nadharia na nadharia zilizoongoza utafiti wa sasa.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Mjadala katika hii sehemu kuhusu yale yaliyoandikwa hapo awali na mifumo ya nadharia itaangaziwa katika sehemu hii ambapo utatoa mwongozo wa lengo la utafiti. Sura hii pia inajadili kujadili vile vigezo vinavyoonyesha kuingiliana kwa lugha zinazotagusana hasa katika mchakato wa kuelimishwa, zinajadiliwa mkiwemo ile inayochanganua makosa, Nadharia ya Uchanganuzi-Linganuzi, bila kusahau ile Mawasiliano, na jinsi zinavyojifunza kuelezea mada ya utafiti inayohusu taathira zinazokumbwa wasomaji wa lugha asilia ya Kinyankore wakati wa kusoma lugha nyingine ikiwa ni Kiswahili

2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Lugha Mama inaelezwa na wataalamu na watafiti mbalimbali kama ile namna ya kutumia lugha kwa mtu anapojaribu kusoma hata kuitumia kwa mara ianayotangulia katika Maisha ya mtumiaji akiwa hajajifunza L2 yoyote ile ile. Mapitio ya tafiti za awali yanatoa mwongozo na ufafanuzi kwa mtafiti kwa kutathmini kama kuna pengo linalohitaji kuzibwa katika tafiti zilizofanywa hapo awali[12]. Lugha mama pia inaelezewa kama lugha anayojifunza mtoto baada ya kuzaliwa[13]. Kulingana na vile lugha mama hutumiwa katika mawasiliano kwa binadamu wa kawaida, ambayo yanawezesha mawasiliano na kuelewana bila shida yoyote kurahisisha kufahamiana.

---

[12] "Kisilu na wenzake (2006). Desturi na Mila Zetu" ni kitabu kinachozungumzia desturi na mila za jamii za Afrika, ambapo wataalamu wanasisitiza kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kudumisha desturi za jadi, huku wakipitia changamoto zinazokabiliwa na mila hizo katika ulimwengu wa kisasa. Kwa ujumla, kitabu hiki kinatoa mwanga kuhusu utamaduni wa Kiafrika, kikisisitiza umuhimu wa mila na desturi katika kujenga utambulisho wa jamii, na pia kutoa nakala muhimu kwa wanafunzi na watafiti wanaovutiwa na masuala ya utamaduni na jamii za Kiafrika.

[13] Kazi ya Msanjila na wenzake, iliyochapishwa mwaka 2009 na kutajwa kama "Isimu Jamii," inahusisha utafiti na uchambuzi wa lugha katika muktadha wa kijamii. Kitabu hiki kinachunguza jinsi lugha inavyotumika, inavyofanyika, na jinsi inavyoathiri jamii mbalimbali, ikitilia mkazo umuhimu wa isimu katika kuelewa mienendo ya kijamii na kiutamaduni.

Ilitambulika pia kuwa inakuwa kazi ngumu kwa watumiaji kutegemea lugha moja tu wakiwa wanawasiliana. Tukirejelea yale yaliyoandikwa hapo awali, makala zote zinazofafanua kwa kifupi tafiti zilizofanywa katika eneo fulani[14]. Mashaka (2015) anabainisha kuwa kunahitaji kuwepo hiyo lugha iliyo ya kipekee inayowaletea watu wanaohusika kuunganishwa.

Hivyo, ile habari ambayo imepitiwa mwanzoni ilinuia kuchunguza mambo yaliyopo kabla katika eneo fulani la elimu. Kazi zinazopitiwa katika mapitio haya zinaweza kuwa kazi za kitaaluma zilizoandikwa, tasnifu, au majarida. Kazi hizi zinaonyesha kwamba katika ulimwengu wa sasa unaozungumzia lugha nyingi, ujifunzaji wa lugha ya pili umekuwa jambo muhimu, hasa katika nchi ambazo kuna mwingiliano wa tamaduni na lugha tofauti.

Katika muktadha huu, hiyo lugha nyingine ikiwa ni Kiswahili inachukua nafasi muhimu inavyotumika ikiwa lugha nyingine inawafaa wahusika wengi, hususan wale wanaozungumza baadhi ya lugha hizo za Kibantu kama ile ya Kinyankore. Kinyankore kama tunavyoeleza kwa kurejelea matokeo ya utafiti huu huonyesha lugha inayozungumzwa katika sehemu za Uganda, na ina sifa zake za kipekee za kimuktadha na kisarufi.

Habwe na Karanja (2004) wanafafanua kuwa lugha hutumika kama chombo muhimu cha mawasiliano, lakini pia ina umuhimu katika kutengeneza na kudumisha utamaduni. Sarufi, inayohusisha sheria na vile lugha ilivyoundwa, inachukua jukumu muhimu katika mchakato unaolenga kusomesha lugha nyingine mpya. Tukiangalia pia matokea

[14] Kazi ya Cosy P. na Bates, iliyochapishwa mwaka 2012 na kutajwa kama "Method in Behavioral Science," inajishughulisha na mbinu za kisayansi zinazotumika katika utafiti wa tabia za binadamu. Kitabu hiki kinatoa mwanga kuhusu njia tofauti za kuchunguza, kuelewa, na kufanyia utafiti tabia za watu katika mazingira mbalimbali.

ya utafiti wa sasa, tunalenga kuchunguza jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoathiri masomo ya kufunza Kiswahili inayosomwa kama lugha ya baadaye, na kutafiti muktadha ambao unachangia mahusiano haya.

Wakati wa kusoma hiyo lugha ya baadaye, wanafunzi kutoka katika mazingira ya Kinyankore mara nyingi wanaweza kutumia maarifa ya kanuni za sarufi ya hiyo lugha iliyotangulia ili kuelewa wanapofundishwa lugha nyingine mpya. Hiyo picha inayodhihirishwa huweza kuleta faida, lakini pia kuna changamoto zinazoweza kuwakabili wanafunzi hao, hususan katika maeneo kama matumizi ya viambishi, muktadha wa maneno, na tofauti katika sarufi.

Utafiti huu unachangia kwenye uelewa wa jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoathiri mafunzo ya lugha husika ya Kiswahili hasa kusaidia washiriki mkiwemo wanafunzi na wahadhiri wao kuweza kuzifanya bora njia ya kusomesha lugha ya baadaye. Kwa kuzingatia uhusiano wa zamani wa lugha hizo mbili, utafiti huu unaangazia mifano halisi inayoshughulikia jinsi ya kutumia sarufi ya kwa mazingira ya kusoma Kiswahili, kutoa picha kamili ya jinsi maarifa ya awali yanavyoathiri ufahamu kuhusu hizo lugha nyinginezo zinazofanana.

Kwa mtazamo huu, tunatazamia kwamba yaliyotokea kwa utafiti uliofanyika yanatoa mwanga kuhusu mahusiano baina ya zile lugha husika mbili, halafu baadaye unakuwa wa manufaa zaidi kuboresha jinsi ya kufundisha wanafunzi wanyankore kuelewa hiyo ya Kiswahili. Masuala haya yanaweza kuleta mabadiliko chanya katika mbinu za kufunzia Kiswahili ili ziweze kujenga uelewa wa kitaifa na kikanda kuhusiana na lugha na utamaduni.

Malengo ya kufanya hizi kazi ambazo zilipitiwa yalikuwa kupata uchanganuzi wa kitaaluma kuelewa utafiti mwingine uliotangulia kwa ajili ya kutambua yale mapengo

ya kitafiti yanayojitokeza, hivyo kumwezesha mtafiti kukabiliana na shida hiyo kwa njia bora ama kutia bidi ya kutatua shida hiyo kwa kiwango fulani. Namna ya kupitia shughuli tofauti unahusisha sharia haza zile za uhakiki, majadiliano, utoaji wa hoja zinazowezesha uboreshaji wa utafiti unaoendelea. Katika hayo yote, huu utafiti umepitia kazi zilizopita kadhaa.

2.1.1 Maelezo ya dhana mbalimbali za lugha

Kabla ya kujadili lugha fulani, ni muhimu kwanza kuelewa maana ya lugha. Wataalamu kadha wa kadha wameifasili lugha kwa njia tofauti, lakini tofauti hizo ni ndogo. Kwa mfano, Habwe na Karanja (2004), wakinukuu TUKI (2013)[15], wanaeleza kwamba lugha hufasiliwa kama mkakati unaotumia sauti za nasibu zinazoonekana miongoni mwa watumiaji wa kundi husika iliyoshikana kwenye desturi za kukamilisha mawasiliano.

Zaidi ya hayo, tunaonyesha kwamba ile lugha inayotangulia kwfunzwa na mtu anaisoma katika utoto wake kabla ya kujifunza lugha nyingine. Hiyo ndiyo lugha ya asilia inayotumika na mwanafunzi anayejifunza akitumia njia ya kusikia watu waliomkaribia wanapozungumza maneno hayo hayo husika. Mwanafunzi kwa kiwango hiki huiga mazungumzo hadi anapofikia uelewa kamili unaohusisha kumiliki lugha tangulizi ya mama. Masebo na Nyangwine (2008) wanasisitiza kwamba pale ambapo mtu anajifunza lugha nyingine inahusu ile ambapo mtu hujifunza akiwa amejifunza ile lugha inayotangulia. Na wanatoa kielelezo cha zile lugha kama ya kiswahili ilivyo kwa kujulikana kama lugha nyingine inayotumika na wengi wa Watanzania, ambayo watanzaniaa hujifunza baada ya kufahamu baadhi ya lugha zingine za kienyeji kama

[15] Kamusi hii ni muhimu kwa sababu inatoa misemo sahihi wa maneno, maana zake, matumizi katika sentensi, na mifano ya matumizi ya kisarufi. TUKI imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kudumisha Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha ya kimataifa.

Kinyakyusa, Kichaga, kisukuma nakadhalika. Pia inasema kuwa matumizi ya kusoma lugha hufuata unasibu katika matumizi yake na vile lugha zilivyoundwa na jamii kulingana na kuwasiliana baina yao.

Ufafanuzi unaotolewa na wataalam hawa, unadhihirisha kuwa unasibu wa kimfumo unatumika kujifunzia lugha kwa wahusika wa mazingira fulani yenye utamaduni unaoshabihiana kwa mawasiliano. Msanjila na wenzake (2009) wanasisitiza kwamba L1 inayotangulia ni ile lugha inayotumika na wakaazi wa mahali husika penye tamaduni, tabia, desturi na mienendo iliyo sawa sawa. L1 inajitokeza kutoa maelezo ya kina kuhusu mambo yanayohusiana na jamii hizo. Hivyo, Kinyankore ni lugha ambayo huenda ikawa imeenea kote katika maeneo yaliyomo jimboni Ankole, ambapo Wanyankore ni wenyeji wa maeneo hayo wazungumzapo hiyo.

Msanjila na wenzake pia wanasema kwamba ile lugha inayotangulia kufunzwa na mtu mara hivi anapozaliwa ndiyo lugha asilia anayojifunza mtoto baada ya kuzaliwa. Wanasisitiza kwamba baadhi ya zile lugha zinazofunzwa baadaye ni kama ile inayojifunzwa na mtu akiwa hajajifunza lugha yoyote nyingine. Tukirejelea wasemaji waliohusika, matumizi ya lugha tangulizi huifanya kujitokeza kama ya pili ikiwa inatumika sana katika shughuli za elimu na shughuli mbali mbali za kiserikali au kwa mawasiliano mapana. Kwa hivyo shabaha ya utafiti huu ni kulenga wanyankore ambao wengi wao wanasoma lugha nyingine ikiwa ni Kiswahili.

2.1.2 Maelezo kuhusu uamilisi na mafunzo ya lugha nyingine

Mtoto akizaliwa, huenda akawa na hazina ya sauti mbalimbali ambazo hazina maana. Hata hivyo, akianza kukaa kwenye eneo hilo, anaanza kutunga matamshi hayo akiwa hana kusudi hilo hata kujaribu kuzielewa kimaana. Wataalamu wametaja dhana ya Uamiliaji lugha, ambayo ni mchakato unaotokea ndani ya akili ya mtu, unayomsaidia

kuongea au kuandika kwa urahisi[16]. Wanakubaliana kwamba uamiliaji huwajia watu kwa hali ya ung'amuzi wa wazi bila mhusika kujitambua.

Kazi ya Krashen na Tracy (1983) inazungumzia mbinu mpya inayohusu kufundisha hiyo lugha ambayo inategemea nadharia zao kuhusu jinsi watu wanavyopata lugha. Kuhusu nadharia ya Kupata Lugha, Krashen anasema kuwa watu wanajifunza lugha kwa njia ya asili wanapokuwa katika mazingira yanayowapa fursa ya kuwasiliana kwa njia ya maana, badala ya kupitia mazoezi ya sarufi. Pia, mazungumzo ya Asili yanaonyeshwa katika kitabu hicho ambapo kinashawishi kuunda hali zisizo na msongo wa mawazo, ambapo wanafunzi wanahimizwa kuzungumza na kuelewa lugha katika muktadha wa mazungumzo ya kila siku. Badala ya kusisitiza kanuni za sarufi, mbinu hiyo ilihakikishia zile dhima za mawasiliano ya maana ambapo wanafunzi husoma baadhi ya lugha kupitia kujihusisha na maudhui yanayowavutia. Krashen anafafanua tofauti kati ya kujifunza (conscious learning) ili kuweza kumiliki lugha (subconscious acquisition), akisisitiza kuwa kupata lugha ndicho kinachohitajika kwa ajili ya kuwa na ufahamu unaotosha katika lugha.

Yeye Matinde (2012), anabainisha kuwa wakati wa kumiliki lugha tangulizi unahusiana na mikakati ya kusoma hata na lugha ile inayofuata[17]. Kazi ya Matinde mwaka 2012 inaashiria kuchapishwa kwa makala muhimu kuhusu umilisi wa lugha ya baadaye. Tafiti zake zilihusisha hasa njia za kusoma na kumiliki ile lugha fuatizi na jinsi inavyofanyika ikitegemea mikutadha mbalimbali. Matinde alichambua tofauti kati ya kusoma lugha moja kwa njia ya kienyeji kuliko ile inayoelekezwa kidokezo, akichunguza jinsi mazingira na mbinu zinavyoweza kuleta athari za umulisi wa kusoma

[16] Krashen, S. D., & Terrell, T. D. (1983). *The natural approach: Language acquisition in the classroom.* Alemany Press.

[17] Ellis, R. (1996). *The study of second language acquisition*. Oxford University Press. Kazi ya Ellis ni mojawapo ya machapisho makubwa katika utafiti wa upataji wa lugha ya pili na inachunguza nadharia, mbinu, na matokeo ya tafiti mbalimbali zinazohusiana na jinsi watu wanavyojifunza lugha ya pili.

lugha nyingine. Katika kazi yake, Matinde alitumia mifano ili kuonyesha jinsi watu wanavyoweza kupata uwezo wa lugha nyingine kupitia matumizi yanayomwezesha msemaji wa mawasiliano ya kutumika kama lugha ya kawaida. Matinde alijadili pia umuhimu wa muktadha wa kijamii na kitamaduni wakati wanaposoma mafunzo ya lugha nyingine, akionyesha kuwa inaathiri pakubwa kuhusu jinsi na wakati mtu anavyoweza kujifunza lugha mpya. Matinde alitoa mapendekezo kuhusu njia zilizo nzuri zaidi kufundishia ile lugha nyingine, akisisitiza namna ya kutumia lugha kwa mazingira yaliyo halisi zaidi kuliko kwenye mazingira ya kiserikali.

Kazi ya Matinde ina manufaa mengi sana kwenye eneo la umilisi wa kusoma lugha nyingine ili kuchukuliwa kama sehemu ya msingi ya nadharia kwa ajili ya uchanganuzi uliopo jinsi watu wanavyopata mafunzo ya lugha kama hiyo mpya. Tafiti zake zinatoa mwanga kuonyesha maofisa wa elimu hasa watafiti katika kufahamu mifumo yote ya kufundishia lugha nyingine ikiwa ni hatua muhimu katika maendeleo ya nadharia za kisasa kuhusu lugha. Utafiti huu unazingatia mtazamo wa Matinde katika kuchambua mtagusano wa sarufi ya Kinyankore kwenye wakati wanapojifunza somo la Kiswahili likiwa ni la pili jijini Mbarara.

Katika mchakato wa uamiliaji lugha, watoto wachanga wanahusika kwa umakini na lugha kuanzia walipozaliwa. Hao wanaweza kuanza kusema maumbo yanayofahamika kati ya muda wa miezi kumi na miwili mpaka miezi karibu kumi na mitano ili kuweza kuunganisha hayo maumbo kuanza na miezi kumi na minane. Anasema kwamba mtoto yeyote ambaye asipokuwa na shida zozote za kimaumbo ya kuzaliwa, pamoja na baadhi ya waliwo na changamoto za kuelewa, huanza kuzungumza wanapokuwa wakiweza kusikia lugha wakiitumia kwenye maeneo yao.

Massamba (2004) anadai kwamba kulingana na vile wale wanafunzi ambao hawana kasoro za kimwili huenda wakamiliki lugha hiyo wakiweza kusikia lugha ikizungumzwa katika mazingira yao.

Massamba (2004) anasisitiza kwamba kusoma mifumo ya lugha unazingatia mikakati inayosababisha kuwepo kwa bidi zinazojulikana kirasmi kuendeleza na kukuza lugha husika. Msemaji anaweza kumiliki uwezo wa stadi za lugha akiwa ana uelewa wa mawazo timamu na ufahamu wa msingi unaohusiana na kusoma stadi hizo za lugha. Anakubali kuwa sarufi ni muhimu katika mafunzo ya kufahamu lugha nyingine, kwa sababu maarifa ambayo mwanafunzi anayesoma lugha iliyotangulia anatumia nayo hufanana kama yale anayoyaweka katika ile lugha inayofuatilia. Waamiliaji wanaojifunza lugha tangulizi wanakuwa na maarifa ya asili ambayo yanawasaidia kuiamili lugha hiyo hiyo ikitumika kwa uelewa huo. Sifa za mwanafunzi wa lugha tangulizi ndizo hizo hizo anazokuwa nazo yule anayesoma lugha inayofuata ya pili. Kielelezo hapa chini kinadhihirisha zile tofauti zinazokuwepo kutofautisha umilisi wa lugha na ufundishaji wake.

Mawazo ya Gleason na Massamba yanaonyesha kwamba wanajadili hatua mbalimbali za maendeleo ya lugha kwa watoto, kuanzia hatua za awali za sauti na matamshi hadi kutunga sentensi na kuelewa muundo wa zana za lugha. Gleason pia anatumia njia tofauti za kufanya utafiti na hata ikihusisha ufuatiliaji wa watoto wachanga na majaribio yaliyorejelewa ili kuchambua kile watoto wanachoweza kujifunza katika umri tofauti. Gleason anasisitiza umuhimu wa mazingira ya kijamii na kitamaduni wakati wa mikakati ya kufundisha lugha hiyo. Anapoteza umuhimu wa mawasiliano, mitindo ya familia, na ushirikiano kuhusu umilisi wa lugha husika. Anachambua jinsi watoto wanavyoweza kujifunza mifumo ya sarufi kadri wanavyoendelea kuzungumza. Mifano

mbalimbali inatolewa ili kuonyesha jinsi watoto wanavyoweza kufanikiwa katika kuunda na kuelewa sentensi zisizo za kawaida.

Kazi ya Gleason inaangazia pia masuala ya mabadiliko kuhusu zile lugha zinazohitaji ufahamu wa kisasa na kueneza namna ya kufundisha lugha, ikijumuisha muktadha wa lugha nyingi na jinsi watoto wanavyoweza kuhusika katika mafunzo ya hiyo lugha ya ziada kwa wakati mmoja. Mtaalam Gleason anachangia katika uelewa wa jinsi watoto wanavyokua kielimu kuhusu zile njia za kuweza kuwafunza lugha wanafunzi ili kuendelea kutoa sauti chanya wakati wa kufanya utafiti unaoshughulikia lugha katika elimu.

Katika mikakati ya kuendeleza utafiti wa sasa, rasilimali muhimu kwa wataalamu wa lugha, walimu, na wazazi wanaotaka kuelewa njia za kujenga uelewa wa lugha inayojumuisha watoto. Mchango wa Gleason unatuelezea dhima ya matokeo yanayotia mwanga juu ya uhusiano wa lugha.

Jedwali 2.1: Tofauti iliyopo kuhusu umilisi wa lugha na namna ya kufundisha

Namba	Uamiliaji Lugha	Ujifunzaji Lugha
i.	Uamiliaji lugha hutangulia kisha kufuatiwa wakati wa kufundisha hiyo lugha. Hii inamaanisha kwamba mtu anaanza kuongea bila kutambua sheria zinazohitajika kuunda miundo na tamaduni zinazohusiana na lugha hiyo.	Ujifunzaji lugha hufuata baada umilisi wa kilugha. Baada ya mtoto kujifunza kuzungumza, ndipo anapoanza kufundishwa sheria mbalimbali zinazohusiana na lugha hiyo.
ii.	Inajitokeza kwenye ngazi ya kung'amua kwa asili, ambapo mtoto anaweza kuzungumza kwa ufasaha bila kuwa na ufahamu wa kiakili wa sababu zinazomfanya azungumze hivyo.	Hujitokeza pale ambapo mtu anatambua na kujua anapoisoma lugha hiyo.
iii.	Katika hali hii, mtaalamu wa lugha au mazingira maalumu kama hayo si muhimu.	Inabidi kuwapo kwa mazingira na tajriba ya mwalimu wa lugha ili usomaji uweze kufanikiwa kiurahisi.
iv.	Haifai kufuata sheria zinazotumika ili kuzingatiwa na vigezo husika.	Ni muhimu kwa mtu kuelewa vipengele vyote vya lugha.
v.	Desturi na mila za matumizi ya lugha haufai kuzingatiwa sana.	Ni muhimu anayejifunza lugha kufahamu mila na desturi za jamii Fulani aweze kukabiliana na changamoto zinazosababisha mahusiano mabaya kwa wahusika katika jamii.

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Kielelezo kinachoonyeshwa juu katika 2.1 kinanuia kusisitiza jinsi mazingira ya kufunzwa kwa Kiswahili kwa wanafunzi wanyankore, yanayojitokeza katika utafiti kama huu ambao unaangalia wataalam wengi waliowahi kuchunguza suala hili. Lusesa (keshatajwa) aliangazia taathira zinazohusiana na lugha tangulizi kwenye mchakato wa kusoma lugha hiyo inayofuata baadaye na alisisitiza umuhimu wa kuelewa namna lugha zinavyoathiriana. Kazi yake Massamba (2006) pia ilichunguza jinsi lugha zinavyoweza kuathiriana kwa kurejelea mazingira yanayohusisha kufunza Swahili jinsi kulivyo hatari kwa kuleta makosa yanayotokana na kuhamisha mifumo ya sarufi kutoka lugha husika kwenda kwa lugha inayofuata. Rocha (keshatajwa) aliangazia uchambuzi wa

mabadiliko ya kisarufi na kifonolojia yanayotokea wakati wazungumzaji wanapojaribu kuhusisha namna lugha ile nyingine inavyotumika ikizingatiwa msingi halisi wenyewe wa lugha asilia. Rocha (keshatajwa) alijikita katika kuangalia uhusiano wa kimapokeo juu ya kilugha maendeleo ikizingatiwa kudhihirisha umilisi wake kwenye jamii, akisisitiza ushirikiano unashughulikia baadhi ya lugha za kienyeji barani Afrika.

Rocha (keshatajwa) alichangia katika kujadili uhusiano wa lugha akirejelea mikutadha inayotumika kisasa, wakitilia maanani mawasiliano baina ya watoto wenye makabila mbalimbali na athari zinazoibuka. Massamba (1986) Alikazia dhima za utafiti wa kuvuka mipaka katika shughuli za ile lugha na jinsi lugha zinavyoweza kuathiriana kimwili na kihisia. Kazi yake Massamba ilichangia katika kuelewa jinsi lugha tofauti zinavyoweza kushirikiana na kutoa mifano dhabiti ya mabadiliko ya kiakademia na kimatendo. Lusesa (keshatajwa) alifanya utafiti kuhusu lugha nyingi na uhamasishaji uliohusu masomo ya Kiswahili yakiwa kwenye mandhari ya hiyo lugha yenye mila za kijamii.

Kwa hivyo, shabaha ya utafiti wa sasa ulikuwa kuchunguza jinsi Kinyankore, inayochukuliwa kama lugha tangulizi inavyoathiri mafunzo ya Kiswahili inapokuwa inafunzwa kama lugha ambayo inajotokeza katika nafasi ya pili ili kueleza mwingiliano unaoletwa katika lugha kwa ajili ya kuchambua jinsi muundo wa kisarufi, maneno, na lafudhi za Kinyankore zinaweza kuingiliana wakati wa kutumia Kiswahili kwa sababu ya kuleta changamoto kwa wanafunzi. Pia kufafanua mafunzo ya wanafunzi ambapo uchambuzi huu unajaribu kueleza changamoto zinazowakabili wanafunzi ambao walio na ile lugha tangulizi inahusisha vigezo mbalimbali vinavyotumika kisarufi na kifonolojia na Kiswahili.

Utafiti pia unatoa mapendekezo juu ya njia zinazofikiriwa kuleta manufaa Zaidi katika mafunzo ya lugha hiyo nyinginezo kwaa wanyankore na kubaini maeneo ambayo wanafunzi wanahitaji msaada zaidi ili kupunguza makosa yanayotokana na kuhamasisha lugha. Utafiti wa kuathiriana kwa lugha, hasa kwa kuzingatia ile inayojulikana kuwa lugha tangulizi kama Kinyankore wakati wa juhudi za kusomesha Kiswahili na kuleta jitihada za kuboresha uelewa unaokuwa kama mikakati wa kusoma lugha yoyote ili kuimarisha zile njia za kufunzia. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuboresha mawasiliano katika mazingira ya lugha nyingi, hivyo kusaidia wanafunzi kusoma lugha fuatizi ukiwa na ufanisi zaidi.

2.1.3 Lugha ya Kinyankore nchini Uganda

Runyankore-Rukiga hujitokeza kama baadhi ya Kibantu inayoitwa kundi la Niger-Kongo. Ni moja ya lugha kuu za asili za Uganda zinazozungumzwa Kusini-Magharibi katika Kigezi (Rukiga) na Mikoa ya Ankore (Runyankore) yenye takriban wazungumzaji milioni 4 kulingana na mwaka wa 2002 ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi Uganda. Lahaja hizi mbili zinaeleweka kwa pande zote kiwango cha takriban 94% ya ulinganifu wa kileksimu kwa mujibu wa Ladefoged na wenzake kama Lewis 1972. Runyankore-Rukiga ina uhusiano wa karibu na nguzo nyingine inayohusiana na lugha zilizo za Kibantu, Runyoro-Rutooro, pia inayozungumzwa katika upande wa kusini magharibi nchini Uganda. Lahaja nne: Runyankore (JE13), Rukiga (JE14), Runyoro (JE11) na Rutooro (JE12) wanaunda Runyakitara18 [JE10A], ambalo huwa inaonyesha kuwa ni ‘lugha’ sanifu Lusesa (keshatajwa) inayofundishwa katika baadhi ya vyuo vikuu nchini Uganda. Kuna mbili vyanzo vinavyojadili mfanano wa kileksia kati ya lahaja hizi nne, yaani, kama inavyofafanuliwa na Ladefoged na wenzake (keshatajwa). Lahaja nne zinaeleweka sana kama asilimia katika onyesho la jedwali hili chini.

Jedwali 2.2: Kufanana kwa Kileksia kwa lahaja nne za Kirunyakitara

	Runyankore na Rukiga	**Runyankore na Runyoro**	**Rukiga na Rutooro**	**Rutooro na Runyoro**	**Rukiga na Runyoro**
Ladefoged (1972)	94%		85%	93%	87%
Lewis (2013)	84-94%	68%		78-93%	77%

Lahaja hizo nne zilijumuishwa katika lugha mbili mnamo 1952 (Runyoro-Rutooro) na 1954 (Runyankore-Rukiga), na wamekuwa na maandishi mawili tofauti kutokea enzi hizo (Rubongoya, 1999). Kuna lugha zingine zinazozungumzwa nje ya Uganda ambazo zinaeleweka kwa usawa na Runyankore-Rukiga. Hizi ni Nyambo (JE21), Haya (JE22), Zinza (JE23) na Kerewe (Kerebe) [JE24] yote yanayozungumzwa nchini Tanzania.

Masomo ya kiisimu kuhusu Runyankore-Rukiga ni machache. Sarufi mbili za kimapokeo elekezi juu ya lugha ilionekana, yaani, Morris na Kirwan (1957) na toleo lililorekebishwa la 1972 na Taylor (1985). Kazi nyingi zinazopatikana ni za utamaduni na yale mawasiliano ya kidrama, tafsiri tafiti katika nadharia ambazo hazijachapishwa, ambazo kwa hivyo hazipatikani kwa utafiti mpana jumuiya. Tukirejelea shabaha ya huu utafiti, mtafiti alitumia msamiati wa sarufi za kimapokeo zinazopatikana.

Lugha ya Kinyankore inajulikana kama Runyankore-Rukiga, ambayo inatambulika mara nyingi kama RR, tunazungumzia baadhi ya lugha za Afrika Mashariki zinazozungumzwa katika sehemu ya Kusini-Magharibi mwa nchi kama vile Mbarara, Kabale, Bushenyi, Ntungamo, Rukungiri, Kisoro na Kanungu. Wilaya hizo zinazozungumza Kinyankore hasa ni za jimbo la kusini magharibi zikiwa na wakaazi wengi wanyankore. Wanaokizungumza ni sehemu ya jamii ya Wanyankore, ambao ni mojawapo ya makabila makubwa nchini Uganda.

Kulingana na Ethnolojia, Kinyankore kinazungumzwa na watu 5,649,800, huku Kikiga kinazungumzwa na watu 3,764,800. Hii inathibitishwa zaidi na Sensa ya Kitaifa

iliyohesabu watu mwakani 2024 ilifanywa na Ofisi ya Kitaifa ya Takwimu ya Uganda (http://www.ubos.org/).

Matini iliyopo kuhusu Kinyankore inazichukulia Runyankore na Rukiga kama lugha moja. La kushangaza ni jinsi utumiaji wa hizi lugha husika zimeunganishwa na kuunda lugha moja[18]. Kabla ya 1950, lugha hizi mbili zilikuwa familia moja kubwa ya lugha iitwayo Runyoro ambayo ilizungumzwa kwenye sehemu za Bunyoro-Kitara. Familia ya lugha kubwa ilijumuisha lugha nne zinazohusiana, ambazo ni, Runyankore, Rukiga, Runyoro na Rutooro.

Hata hivyo, miongoni mwa wenyeji hawakufurahishwa na kikundi hiki, kwa kuwa kazi nyingi, hata Biblia, ziliandikwa zikitumia Kinyoro. Ndiposa watalaamu mashuhuri Ladefoged na Rubongoya walifanya mikutano miwili mwaka 1952 na 1954 ili kujadili jambo hili chini ya mwongozo wa wamisionari. Wakati wa mkutano wa pili (1954), Runyoro iligawanywa katika lugha mbili, Runyankore-Rukiga na Runyoro Rutooro. Miongoni mwa sababu zilizochangia mkutano huo kugawanya lugha hizi nne katika vikundi viwili ambavyo vinahusisha kueleweka kwa kiwango kikubwa ambacho mfanano wa kileksika baina ya zile lugha husika zilizounda vikundi vidogo viwili. Runyankore na Rukiga zina uhusiano wa karibu sana na zinashiriki zaidi ya 84% ya leksimu huku mfanano wa kileksia kati ya Runyoro na Rutooro ni kati ya 78% na 93% (Ethnologue).

Ladefoged (1971), alichambua jinsi sauti zinavyopatikana na zinakuwa na uwezo wa kushughulisha zile lugha za Kiafrika, pamoja na uhusiano wao kimatamshi, kimasikizi hata kiakustiki. Katika tafiti zao, waliweka msisitizo kwenye ukusanyaji wa habari za sauti kutokana na watumiaji waliotangulia, kuonyesha umuhimu wa mtazamo

[18] Kazi za Taylor (1985), Morris, na Kirwan (1972) zinahusiana kwa kiasi fulani na utafiti wa lugha na fonetiki.

unaotumia lugha kiutafiti kwa kiwango cha fonetiki. Kazi hii ilichangia sana katika kuelewa tofauti na ufanisi ulihusisha lugha zote za kienyeji hata kuandika mwanga zaidi kwenye changamoto na faida za utafiti unaoshughulikia lugha ngeni za baadaye. Kazi ya Ladefoged na wenzake mwaka (keshatajwa) inabaki kuwa muhimu katika nyanja ya fonetiki ukihusisha uchanganuzi wa baadhi ya lugha, hasa katika kuchangia kwenye maarifa ya mahusiano ya utofauti wa lugha zile za Kiafrika. Inaonyesha umuhimu wa tafiti zinazojitokeza kuleta fonimu asili na jinsi zinavyoweza kusaidia kuelewa mifumo tofauti ya lugha.

Kinyankore ina muundo wa sarufi ambao unajulikana kwa matumizi ya viambishi, ambavyo vinaweza kusababisha ubadilishanaji wa matokea ya maneno na maana yake au kuunda maneno mapya. Mifano ni viambishi vinavyohusiana na nafsi, wakati wa, na hali. Kinyankore ina sauti mbalimbali ikihusisha hata toni, ambapo sauti tofauti zinaweza kubadilisha maana ya maneno. Hii inafanya lugha kuwa na changamoto kwa watu wasiokuwa na uzoefu nayo.

Kinyankore ina dhima kubwa kadhaa kwa tamaduni za Wanyankore. Ni lugha inayotumiwa katika sherehe, nyimbo, na hadithi za jadi, na inachangia katika uhifadhi wa utamaduni wa eneo hilo. Katika zama za sasa, kuna juhudi za kuhifadhi na kukuza Kinyankore kutokana na mvuto wa lugha nyingine, hasa tukirejelea lugha ya kingereza n ahata ile ya Kiswahili, ambavyo vinaendelea kutumiwa sana katika maeneo ya elimu na biashara. Katika elimu, kuna juhudi za kufundisha Kinyankore kwenye asasi za elimu mkiwemo mashule ya upili na vyuo, lakini changamoto za rasilimali na mabadiliko ya yanayohusiana na zile lugha zinazokopwa na kuigizwa kutoka nje ya bara la Afrika bado zinakabiliwa. Kinyankore ina mfumo wa uandishi, ambapo alfabeti ya Kilatini inatumika.

Hata hivyo, maandiko mengi ya Kinyankore yameandikwa na kusambazwa yakitumia mbinu ya habari katika muktadha wa muktadha wa kijamii badala ya maandiko rasmi. Kinyankore huainishwa kama ile lugha iliyo na utajiri wa tamaduni na historia, ambayo inachangia katika utambulisho wa jamii ya Wanyankore nchini Uganda. Utafiti na juhudi zinazoelekezwa katika kuendeleza Kinyankore huwa na jukumu la sababu inasaidia katika kuhifadhi urithi kwa desturi na mila za eneo hilo, kwa muda ule ule kwa kukabili matatizo ya lugha zinazoibuka na ukuaji wa lugha nyingine.

Katika utafiti huu, Mtafiti alizingatia lahaja ya Kinyankore peke yake bila kuhusisha lahaja ya Kikiga wala Runyoro – Rutooro. Alilenga Kinyankore kinachozungumzwa kwa wanyankore kama badhi ya zile lugha zinazozungumzwa nchini Uganda.

2.1.4 Taarifa kuhusu Swahili.

Ni jambo lililo wazi kwamba Swahili ni miongoni mwa lugha zinazoainishwa kama za kibantu, iliyo na mifumo yenye upekee wake ikilinganishwa kuleta utofauti kati ya lugha zenye uasilia wa kiafrika nyingine. Upekee huu unasababishwa na hadhi yake kuwa linguafranka ya nchi kadhaa za Afrika na kimataifa. Kwa sasa, baadhi ya asasi nyingi katika nchi ya Uganda zimeanza kufundisha Kiswahili wenye mitaala yao. Hii inaonyesha kwamba hiyo lugha inayofundishwa kwenye zile asasi zinazotangulia hadi kwenye zile asasi za ngazi ya juu ina uwezo fulani. Kikatiba, iliidhinishwa hata kuchaguliwa ikidhihirishwa kuwa lugha ya kiofisi na kutumika katika shughuli zilizorasmi kunakohitajika. Hadhi hii husababisha matumizi mapana kwa ajili ya kukuza na kueneza lugha hiyo yanakumbwa na athari kuingiliana kwa vipashio vya kiisimu vya hiyo lugha tangulizi. Kwa hiyo azma inayochunguzwa katika kazi hii huwa ni kuchanganua mtagusano wa sarufi ya Kinyankore wakati kazi ya kusoma namna ya kutumia Kiswahili inaendeleza kwa ufasaha kwa wajifunzaji wanyankore wakati wanajifunzapo lugha iliyo Kiswahili jijini Mbarara nchini Uganda. Utafiti ulichanganua

kanuni na vile sarufi inavyoundwa ili kubaini taathira ya Kinyankore wasomapo Kiswahili kiufasaha. Hali hii inasababishwa na madai kwamba namna lugha tangulizi inavyoingilia ile inayofuatia huenda ikasababisha kukosea kisarufi katika ujifunzaji jambo linakwamisha usomaji wa lugha inayofuatia haswa lugha hizo zinavyotofautiana kimuundo.

2.1.5 Hali na hadhi ya Kiswahili tangu ukoloni

Baadhi ya lugha zinazozungumzwa nchini Uganda kuna Kiswahili ambayo inatumika kwa ajili ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali. Kiswahili kilianza kuenezwa Uganda nyakati za, kwa sababu ilianzishwa ikisambazwa na shughuli za biashara kati ya nchi za mashariki mwa Afrika. Ilikuwa lugha ya iliyotumiwa na wakazi wa maeneo mbalimbali, hasa kutokana na ushawishi uliolenga kukamilisha biashara katika jamii za wanaohusika katika uwanja wa usafiri.

Katika katiba ya Uganda ya mwaka 1995, Kiswahili ilitambuliwa kurasmishwa pamoja na Kiingereza. Hii ilionyesha dhamira ya kuimarisha umoja na jinsi ya kuwasiliana baina ya makabila tofauti nchini Uganda. Katika katiba ya Uganda, Kiswahili kina nafasi maalum kwa urasmi wake. Kifungu cha sita (6) cha Katiba ya Uganda kinaeleza kwamba Swahili inajulikana kuwa na urasmi wake nchini pamoja na Kiingereza. Hali hiyo hudhihirisha kuwa Kiswahili kinatambuliwa rasmi serikalini na hutumika kwenye ngazi zote zilizo rasmi na za utawala, elimu, na mawasiliano rasmi. Hata hivyo, matumizi yake katika vitendo vya kila siku na katika sekta zingine zinaweza kutofautiana kulingana na eneo na muktadha. Pamoja na kuwa na urasmi huo kwa sasa, jinsi lugha hii inavyotumika huweza kutofautiana katika maeneo tofauti ya Uganda. Kiswahili hutumika Zaidi katika maeneo ya kibiashara na ya umma, hasa kutimiza kazi za kiserikali na mawasiliano rasmi. Ingawa kiwango cha vile lugha hiyo inavyotumika

kinatofautiana, serikali imechukua hatua kuongeza uwezo na upana wake kwa maeneo mbalimbali ya nchi.

Kiswahili hutumika katika mfumo wa elimu hasa kwa asasi za elimu kama zile shule na vyuo vikuu. Hata hivyo, kiwango cha ufundishaji na matumizi kinaweza kutofautiana kutoka eneo hadi eneo. Kiswahili kinatumika kwa baadhi ya wanahabari wanaofanyia vyombo kadhaa vya mawasiliano na habari, vikihusisha runinga, redio, vile vya kielektroniki na kidigitali. Vyombo vya habari vya Kiswahili vinatoa nafasi kwa jamii kuweza kujadili masuala ya kijamii, siasa, na utamaduni. Kiswahili huwa na ubora wake kimawasiliano kwa watumiaji wake wa kawaida, hasa katika mazingira ya mijini ambako watu wa makabila tofauti wanakutana. Hii inachangia katika kuimarisha umoja wa kitaifa.

Tukirejelea namna lugha hiyo inavyotumika katika nchi nzima, itagunduliwa kwamba Kiswahili huwa lugha iliyo na uwezo na dhima ya kukuza umoja wa kitaifa, urahisi wa mawasiliano, na maendeleo ya kijamii. Ingawa inakumbwa na changamoto kadhaa, Kiswahili ina nafasi yake katika ujenzi wa jamii inayohusiana na lugha na tamaduni tofauti. Juhudi za kuwezesha mafunzo ya Kiswahili kuendelea na matumizi yake kwa shughuli tofauti zinaweza kusaidia katika kuimarisha hadhi yake nchini Uganda.

2.1.6 Historia fupi juu ya Swahili

Mnamo enzi za utawala wa wakoloni mwakani 1927, viongozi waliokuwa wanaongozwa na Mkubwa wao aitwaye Frederick Gowers akiwa na aliyesimamia mambo ya masomo aitwaye Eric Hussey, walitoa amri kwamba Kiswahili kifundishwe wakilenga kuimarisha utawala wao na kuunganisha jamii, kwa matumizi ya kufundishia kwa tasisi za elimu ili iweze kutumika ofisini[19]. Hali hii yaonyesha kwamba Kiswahili

[19] Kazi ya Karoro, E.A. (2001) inatoa uchambuzi wa maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda, ikizingatia jinsi lugha hii ilivyoanza kutumika katika nchi hiyo na changamoto zinazokabili maendeleo yake.

hakikuwa kikitumiwa katika masuala ya kijamii, ndiyo sababu wakoloni walipendekeza mafunzo ya lugha hiyo yaanzishwe katika jamii walizozitawala. Walipotumia harakati hizo, Kiswahili hakikutumika katika shughuli za kijamii, na hivyo kubaki ikiangaliwa kama ya kigeni[20].

Kulingana Karoro (2001), kwa wanauganda, Kiswahili inachukuliwa kama lugha iliyotolewa mahali pengine ili kufanikisha mawasiliano ya kijamii na kutatua changamoto ya mawasiliano yoliyosumbua wananchi ni kuwepo makabila mengi. Kazi yake Karoro inaelezea historia inayoeleza lugha hiyo kwa mazingira ya kikoloni, ikionyesha jinsi serikali ya kikoloni ilivyolazimisha kusomesha hiyo lugha kwa makusudi ya kuboresha namna wanavyowasiliana kwa makabila tofauti.

Karoro pia anachunguza jukumu la walimu katika kufundisha Kiswahili, na anabainisha kwamba licha ya juhudi za serikali, lugha hiyo bado haijawa jambo muhimu linalochukuliwa kuwa na dhima kubwa katika jamii husika. Kwa ujumla, kazi ya Karoro inaonyesha upungufu wa vile inavyotumika kukamilisha shughuli za jamii, kwa kuongezea uwezo wa kutumika kulingana na mkakati wa kimasomo. Hii ni hatua muhimu inayoweza kutumikwa kufahamu matatizo hasa matarajio kuelewa upana wa mazingira yake ya Uganda.

Zaidi ya hayo, viongozi katika nyakati za enzi za ukoloni, walisisitiza kulazimisha mafunzo ya lugha hiyo kwani walitaka kutatua haja ya kimawasiliano iliyokuwepo kati ya makundi ya kikabila ya kibantu na Kinailotiki kwa urahisi. Ingawa waliiona Kiswahili kuwa lugha iliyokuwa ngeni, serikali iliweka msisitizo kwamba ifundishwe. Vyuo kama Makerere viliteuliwa na Gavana ili viweze kufundisha na kuendeleza somo

[20] Makala ya Aleidine, J. M. na Theresa, C. (2015) inazingatia ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za kigeni katika Chuo Kikuu cha Nebraska-Lincoln. Katika tafiti zao, waandishi wanachambua mbinu tofauti za ufundishaji wa lugha, changamoto zinazokabiliwa na wanafunzi na walimu, na umuhimu wa lugha za kigeni katika muktadha wa elimu ya juu.

la lugha hiyo kwa ajili ya kupata walimu ambao wangeweza kusambaza lugha hiyo kote nchini[21].

Juu ya ulazimishaji wa lugha, wataalamu kama Matinde (keshatajwa) anaeleza kwamba lugha za kigeni mara nyingine zinaweza kulazimishwa. Kwa kurejelea mazingira hayo, serikali ya kikoloni ilitarajia kwamba Kiswahili kingekuwa kifaa chenye kusaidia katika namna ya kuwasiliana baina ya makabila mawili makubwa nchini. Sababu hizo zenyewe zilitolewa tena mwaka 1995 wakati serikali ya Uganda ilipoingiza Kiswahili katika Katiba yake na kutambulika kuwa lugha nyingine. Pengine, katika miaka iliyopita wana mitalaa na maofisa wa wizara ya elimu walitoa sababu kama hizo ili kuweza kulazimisha ufunzaji wa somo hilo, ingawa kuna miongoni mwa maaofisa waliokataa kwa kusema kwamba si lugha ya wenyeji wa Uganda. Miongoni mwa watu wenye fikra kama hizo, wanaendelea kufikiria kwamba Kiswahili ni lugha iliyo ngeni kwa wanauganda. Yeye Masereka (2020) anasema kuwa juhudi za kuendeleza Kiswahili zilipamba moto wakati ambapo mmoja wa viongozi wa elimu alipounda kamati ya kukuza masomo ya kiafrika na kuiongeza lugha ya Kiswahili kwenye mtalaa wa mafunzo muhimu ya kufundishwa.

Viongozi wa Kanisa mkiwemo Maaskofu pamoja na wamishonari, hata waliomwakilisha Kabaka walihudhuria (Karoro, 2001). Halmashauri ilishauri kuwepo kwa mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na: kwanza, Swahili ianzishwe ikiwa moja ya masomo; pili, wanafunzi wote wafundishwe Kiswahili kwenye asasi za ngazi ya juu hasa zile zinazofunza wahadhiri mkiwemo Kyambogo, Bishop Stuart, Makerere na nyinginezo; tatu, katika maeneo yaliyo na baadhi ya lugha za makabila tofauti

---

[21] Ssekamwa, J. C. (2000). *History and Development of Education in Uganda.* Kampala: Fountain Publishers.

zikizungumzwa, Kiswahili kifundishwe kwenye tasiisi za elimu za kawaida (*vernacular schools*) ambapo walimu waliohitimu wangjifunza Kiswahili na kingewafaa vya kutosha; nne, Kiswahili kifundishwe kwenye asasi za kiufundi za kiserikali zilizokuwa jijini Kampala, ambacho kilikuwa kimejengwa ili kusaidia wavulana.

Maoni haya yanadhihirisha kwamba wakati huo Kiswahili kilikuwa kipya nchini Uganda. Hadi siku ya leo, juhudi za kuanzisha Kiswahili zilikuwa zinaendelea. Kwa kurejelea mawazo ya aina hiyo ambayo yanatolewa, ambayo ni uthibitisho kuwa Kiswahili inchukuliwa kuwa ilitoka kwingineko kwa watu wengi. Miaka ya mwanzoni mwa 1930, hii lugha ilipewa hadhi kubwa kwani waliofuzu kama walimu ambao walikuwa wamejifunza Kiswahili chuoni Makerere. Jukumu la kufundisha Kiswahili lilikuwa linasisitizwa kwenye asasi hizo za wahadhiri kuanzia asasi za chini, likiwa limetengwa wakiliona kuwa geni kwao kinachotarajiwa kutumika kwa manufaa ya kuwezesha mawasiliano ya jamii yao. Kiswahili kilipendwa sana na wanafunzi waliomaliza shule hapo kati kati kwa wale waliokosa kujifunza kimombo. Nyakasura, wilayani Kabarole, sasa Canon Apolo Core PTC, ilikuwa moja ya vyuo ambapo walimu walihisi kujipongeza kwa kujieleza kwa L2 ya Swahili. Mmoja wa wanafunzi waliojifunza Kiswahili, alikuwa anaitwa Bw. Yowasi Kagumire ambaye ananukuliwa na Karoro (2001) akieleza kwamba:

> "Tulipenda Kiswahili kwa sababu ilikuwa lugha mpya iliyofanana na lugha zetu za huku kwetu kusini magharibi. Licha ya hayo kwa kukizungumza ilikuwa wazi kwamba wewe umesoma. Iwapo mtu yeyote angezungumza Kiswahili, kila mtu angejua kwamba msomi amekuja. Ilitarajiwa kwamba mtoto akiwa ana ufahamu wa lugha hiyo ingekuwezesha kufundisha mahali popote katika bara la Afrika."

Mawazo ya Kagumire yanadhihirisha kinagaubaga kwamba hiyo lugha huenda ikawa mpya nchini Uganda, na hadi sasa, kwa kipindi kirefu mafunzo yake katika asasi mbalimbali, bado linafikiriwa kufuatiliwa na mawazo potofu likiwa linafunzwa

wanafunzi. Wengi wao wanakutana na Kiswahili kama wanavyokutana na masomo mengine mapya kwa kwanza[22].

Hii inathibitisha kuwa hiyo lugha husika ikiwa ya kigeni nchini Uganda, wanafunzi wanakutana nayo darasani pekee na hawaitumii wakiwa wanagotoa kazi zao kila siku. Ili kuhakikisha wataalamu wa lugha wanamiliki ufahamu unaowatosha, hasa katika matamshi, miongoni mwa maofisa wa elimu kutoka Chuo cha Walimu cha Makerere walipelekwa Pwani nchini Kenya kwa miezi minne, kwani Kiswahili kilikuwa kinatumika katika shughuli za kijamii huko, tofauti na hali ilivyo nchini Uganda (Karoro, 2001). Ingawa siku hizi walimu hawapelekwi Pwani, bado Kiswahili kinafundishwa, lakini hakitumiki kufanyisha kazi za kikawaida.

2.1.7 Jinsi Kiswahili kinavyofundishwa

Ilipofika mwakani 1986, halmashauri ya kimapinduzi ya Taifa ijulikanayo kama National Resistance Council (NRC) ilishauri ya kuwa Kiswahili na Kiingereza zitumike kirasmi kuwa lugha ya taifa iliyo rasmi kutumika kugotoa majukumu ya kiofisi na ya kimazingira ya kawaida. Hiyo Halmashauri yenyewe ilichagua tume iliyokuwa na jukumu la kuchunguza na kutathmini hali na kiwango cha elimu nchini Uganda na kutoa mapendekezo. Mnamo mwaka wa 1987, tume iliyoitwa *Ssenteza-Kajubi Education Commission* iliundwa, ikipendekeza somo la Kiswahili lifundishwe katika shule zote nchini Uganda kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi kuelewa na kuiendeleza katika jamii. Hii ilikuwa muhimu kwani Kiswahili hakikufundishwa nchini Uganda hapo awali, na watu wengi walikiona kama lugha ya Wakenya au Watanzania. Katika mwaka huo huo wa 1992, serikali ilichapisha *Waraka wa Serikali (GWPE)* ambapo

---

[22] Mtesigwa, C. K.P. (2009). Utayarishaji wa vitabu vya kufundishia Kiswahili kama lugha ya Kigeni: Haja ya kuzingatia mkabala wa mawasiliano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Kiswahili.* 72, 52- 67.

lilitolewa mapendekezo kuhusu Kiswahili, kama itakavyoelezwa hapa chini baadaye. Wakati tume hiyo ilikuwa ikifanya kazi, Chuo cha Kitaifa cha Kakoba, chini ya uongozi wa Karoro Emmanuel, kilianza mafunzo ya lugha hiyo katika kiwango cha stashahada mwaka wa 1991 (Karoro, 2001).

Kwa upande mwingine, baraza la mitihani la *Uganda National Examinations Board* (UNEB)[23], kwa kurejelea silabasi iliyorithiwa kutoka *East African Examination Council* (EAEC)[24], lilianza kuandaa namna ya kutahini wanafunzi wa darasa la nne na la sita, ingawa idadi ya wanafunzi waliowahi kufanya mitihani hiyo ilikuwa ndogo, kutokana na mtazamo kwamba lugha yenyewe ni ngeni. Chuo cha Kakoba na nchi nzima kwa ujumla hawakuwa na silabasi kufundisha Kiswahili kwa maana hiyo haikufundishwa wala kuwahimiza wanajamii kuendelea kuitumia nchini Uganda. Aliyekuwa akikizungumza Kiswahili wakati huo angeweza kuwa askari jeshi au mgeni kutoka Tanzania, Kenya, au Rwanda (Karoro, 2001). Hadi leo, Kiswahili kilikuwa kinatumika na askari jeshi na wasomi waliokuwa wamejifunza lugha hiyo. Katika jamii nyingi za Uganda, mtu anayesema swahili, akiwa kama amesomea nchini Uganda, mara nyingi huchukuliwa kuwa Mwanatanzania au Mwanakenya. Kulingana na Karoro (keshatajwa) hali hii inaonyesha jinsi watu wanavyofikiria kuwa Kiswahili huwa lugha ya kutoka nje ya nchini Uganda.

[23] Shirika la kutunga mitihani nchini Uganda (UNEB) ni chombo cha serikali kinachohusika na kuandaa, kuratibu, na kutunga mitihani kwa ajili ya elimu ya msingi na sekondari nchini Uganda. Wanajukumu kama vile kupanga ratiba ya mitihani, kuhakikisha kwamba mitihani inafanywa kwa uadilifu, na kutangaza matokeo.

[24] Shirika la EAEC lilikuwa chombo cha kikandakilichohusika na kupanga na kusimamia mitihani katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. EAEC ilianzishwa ili kuboresha kiwango cha elimu na mitihani katika kanda ya Afrika Mashariki, lakini baadaye majukumu yalianzishwa kwa kila nchi kivyake. EAEC ilikoma kufanya kazi na majukumu haya yakachukuliwa na mashirika ya mitihani ya kitaifa ya kila nchi. Kwa mfano, Nchini Uganda, majukumu haya yanashikiliwa na UNEB.

Baada ya Kipindi hiki, kwa kurejelea hilo waraka la serikali GWPE [25], wanafunzi wanaosoma kwenye asasi za mkoa wa Magharibi mwa Uganda walianza kufundishwa Kiswahili, kwani ni pale ambapo chuo pekee kilikuwa kinafundisha wengi wao wa maofisa wa elimu wenye umilisi wa Kiswahili (Karoro, keshatajwa).

2.1.8 Dhima ya Lugha tangulizi

Lugha tangulizi ni lugha inayofunzwa mwanzoni kama Kinyankore kilivyo kwa wanyankore na inakuwa na umuhimu mkubwa kwa watumiaji wake popote ilipo. Hii ni kwa sababu inakuwa na manufaa kadhaa. Kwanza, inamsaidia mtu kuelewa desturi na tamaduni zake juu ya mazingira yanayomhusu[26]. Pili, inamwezesha mwanajamii kujiona kuwa mmilisi wa tabia za wanajamii wenzake na kufahamu chimbuko lake. Tatu, inamsaidia mtumiaji kumwongezea uelewa anaposoma lugha zianzofuata baadaye, na tayari anaelewa misingi ya kutumia lugha husika. Nne, inawasilisha elimu kwa ufanisi zaidi ikilinganishwa kwingineko, kwani inamfanya mwanafunzi aweze kuwasiliana na kujieleza kiurahisi.

Aidha, lugha za kwanza zina majukumu muhimu katika jamii[27]. Kwanza, zinampa mtoto uzoefu wa kipekee kuhusu mazingira anamoishi, na pili, zinahifadhi utamaduni wa jamii na kusaidia kuhamasisha utamaduni kuanzia kwenye watu wa rika moja kwenda kwa wengineo wakitumia ngano, methali, vitendawili, na kadhalika. Tatu, zinamwezesha mtoto kuelewa maadili yanayotarajiwa kuzingatiwa na wanajamii hao. Nne, zinampa yeyote anayejihusisha kutambulika kwa namna ya kipekee katika bahari ya jamii nyingi duniani.

---

[25] Mnamo mwaka wa 1992, Tume ya Kupitia Sera ya Elimu iliwasilisha kwa Wizara ya Elimu na Michezo sera mpya ya kusimamia elimu nchini Uganda. Waraka lililowasilishwa ndilo linaitwa GWPE. Waraka hilo lilitoa mapendekezo mengi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda.

[26] Ruhlen, M. (1996). A personal perspective on language and the brain. In R. E. Asher (Ed.), *The Encyclopedia of Language and Linguistics* (Vol. 4, pp. 1986-1989). Oxford: Pergamon Press.

[27] Vigdis, S. (2003). Language and Gender: A New Approach. In *The Cambridge Handbook of Language and Gender* (pp. 1-46). Cambridge University Press.

Tsunoda (2006) anasema kwamba "lugha za mama zina manufaa makubwa katika jamii, kwani zinakuwa ishara ya kujitambulisha kwenye wanajamii wanohusika, zinachochea mienendo ya kuwa wazalendo kuungana, hata pia ni mali inayomilikiwa na wanaohifadhi tabia za jamii hiyo zinazoenezwa kwa kuhusisha vizazi kadhaa kama vinapojitokeza na kufuatana."

Katika wakati ambapo Jamii inakosa lugha yao ya mama, inakosa pia chombo muhimu cha kuelezea na kuhifadhi utamaduni wao, na hivyo wanahitaji kujieleza kupitia lugha na kumbukumbu za wageni[28]. Kwa hivyo, mtu akipoteza namna ya kutumia lugha tangulizi huwa anafanana kama akiupoteza utamaduni wake. Ingawa lugha za mama ni muhimu, bado zinapuuziliwa mbali na kutazamwa kiuduni na kudharauliwa kwa watu wengi

Kulingana na Vigdis (2003), sababu kubwa ya kupuuziliwa mbali na lugha hizi tangulizi za mama ni pamoja na mifumo ya elimu, masuala ya kisayansi, wanahabari, fursa za kazi, na siasa. Nyanja hizi katika jamii nyingi zinahimiza namna ya kutumia lugha hiyo maarufu kama zinazojulikana sana kutoka ngambo huku lugha za mama kama Kinyankore zikiachwa nyuma. Kama anavyosema Matinde (keshatajwa) "kadri utandawazi unavyoshamiri kutoka mazingira ya dunia nzima, ili lugha zinazoweza kutumika kama linguafranka zinavyopata kutambulika halafu L1 zikikosa kuthibitishwa na zingine zikikaribia kuangamia."

Kazi hii inachunguza mwingiliano wa lugha, hasa kwa kuangazia lugha tangulizi kama Kinyankore wakati wa kusoma lugha hiyo huwa na masharti kuboresha uelewa juu ya mikakati inayosababisha njia bora za kufundishia, na hivyo utafiti ukanuia kuboresha

[28] Ngugi, W. T. (2004). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi, Bosha (East African Educational Publishers.

mawasiliano katika mazingira mbalimbali, hivyo kusaidia wanafunzi wanaosoma lugha hiyo katika njia yenye ufanisi zaidi.

2.2 Mwingiliano uliopo kati ya lugha tangulizi na lugha nyingine

Wataalamu wengi wamevutiwa na suala la mtagusano unaohusisha lugha mbili hasa ile inayotangulia na ile inayofuata. Wataalamu kama Ontieri (2010) wanasisitiza kuwa mwingiliano unaotokana na lugha tangulizi huwa unajitokeza wakati kusoma na kutumia lugha inayofuata. Kazi hizi, Zaidi ya zile nyingine zilizotangulia, zinajaribu kuchunguza suala la jinsi lugha moja huweza kuingilia usomaji wa lugha nyingine, ambayo ni Kinyankore wakati usomaji wa lugha nyingine unapoanza.

Nyanda, (2015), akitafiti juu ya athari za kinyamwezi na vile kinavyoathiri usomaji wa swahili, anaeleza kwamba mtagusano huenda ukatokea kati ya ile lugha tangulizi wakati mtu anaposoma hiyo lugha nyingine husababisha athari za kimsamiati kutoka lugha hiyo na kuathiri ile inayoigwa. Anazidi kuelezea kuwa kuathiriana huku kwa lugha hutokana na vile zile lugha zinavyoingiliana kwa wanajamii amabo wanazitumia lugha zikikaribiana. Kilichotokea kuotka kwa utafiti wake Nyanda kilifafanua ya kwamba watu wakiwa wanatumia ligha mbili kwa ukaribu sana wanavifanya vipengele vya sarufi ya lugha kwenye ngazi ya sauti maumbo, miundo na kisemantiki kuingiliana na kuathiriana.

Huu utafiti uliweka bayana pengo la kutathmini taathira ya mtagusano wa sarufi kwa kuwa muundo wa Kinyankore ukiwa unafuatiliwa katika kusoma lugha nyingine kuchunguza kanuni na vigezo vya muundo wa lugha kama ya Swahili fasaha baadhi ya wajifunzaji wa Kinyankore wakisoma Swahili wanaliziba pengo husika kwa kuegemea vipashio vya kisarufi vya mofolojia vya ngeli, uundaji maneno, Njeo, unyambuzi, Viwakilishi nafsi, vikanushi, vivumishi, dhamira katika tungo.

Mwingiliano unaojitokeza wakati ambapo usomaji wa lugha ile nyingine kama ya Kiswahili unavyoeleweka na jinsi wanafunzi wanavyopata uwelewa unaofunua upya mawazo mapya tofauti na walivyokuwa mwanzoni. Kuelewa mchakato huu kunaweza kusaidia watumiaji wa lugha wawe wanafunzi na wanaowafundisha kujifunza na kufikia matokeo bora zaidi wanaposoma masomo ya Swahili.

Wanafunzi kwa kawaida huwa wanaleta muundo na sarufi za lugha zao kwanza katika kujifunza Kiswahili. Hii inasaidia au kuzuia ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa mfano, ikiwa pale ambapo lugha tangulizi ina mifumo ya kisarufi tofauti, mwanafunzi anaweza kukumbwa na matata ya kuelewa kanuni za Kiswahili. Wanafunzi wanaweza kutumia neno au dhana zinazofanana kwa kuanzia zile lugha zinazotangulia ili kufanikisha ufahamu wa maneno mapya ya Kiswahili. Hii inaweza kuwa njia nzuri ya kujifunza, ingawa inaweza pia kuletea kuwepo kwa kasoro za kizamani wakati wa kutafakari maneno.

2.2.1 Mwingiliano uliopo wa lugha tangulizi katika kujifunza lugha nyingine

Massamba (1986) alifanya utafiti juu ya taathira zinazotokana na vile lugha tangulizi inavyoingilia lugha nyingine huko maeneo ya Mara nchini Tanzania, na akabaini ya kuwa zile lugha zinazofunzwa kwanza zinaingiliana na Kiswahili. Katika uchanganuzi wake, alifanyia kazi kwa vile hizo lugha tangulizi zilivyoathiri Kiswahili katika maeneo tofauti, akieleza kuwa mabadiliko haya yalijitokeza katika fonolojia, msamiati, na sarufi. Kwenye fonolojia, Massamba anaeleza jinsi baadhi ya sauti zilizoongezwa au kuondolewa kwenye mfumo wa silabi za lugha ya Swahili ni kwa vile inavyoshawishi kusoma lugha iliyotangulia. Matokeo yake, kulikuwepo na makosa katika namna baadhi ya silabi zinavyotamkwa ambapo maneno kadhaa ya lugha hizo zinazotangulia zilipenyezwa halafu zikatumika kwenye ile lugha ya Swahili na kwa usanifu hivyo kuathiri namna ya kutumia Swahili sahihi ambayo tayari ilikuwa na msamiati kamili.

Tukizingatia njia nyingine ya kisarufi, viambishi vilivyotolewa kuanzia lugha za mwanzoni hadi lugha nyingine ndipo kukatokea kasoro za kimaumbo, kasoro za kimuundo, ambayo yalisababisha kukiuka kanuni ambazo zingeonyesha kwamba ni mfumo wa Swahili ulio sahihi, hivyo kuhatarisha uwasilishaji wa ujumbe. Ingawaje, Massamba (2006) alifanya utafiti kuhusu namna lugha tangulizi zilizo katika maeneo ya Mara, hakufanya utafiti kuhusu lugha zote za kibantu, zikiwemo lugha kama Kinyankore. Akichunguza kazi zake barabara, mtafiti alielekeza nguvu zake katika kuangalia athari za Kinyankore hasa kwa mchakato wa kuelewa na kusoma lugha nyingine ya Swahili.

Yeye Hagége (1999) alichunguza vile lugha za mwanzoni zinavyoathiri mifumo ya kusoma lugha zinazofunzwa baadaye, akionyesha kuwa athari hizi zinajitokeza bila kubagua ni nani anayejifunza awe mtoto hata mtu mzima. Alisisitiza kwamba athari hizi huwa kubwa zaidi zikiwasumbua hasa watu wenye umri wa juu zaidi, kwani kuelewa mfumo wa lugha inayotangulia kunakuwa thabiti kadri umri unavyoongezeka. Aidha, Hagége alieleza kwamba katika watoto, athari hizi hupungua wakianza kusoma mafunzo ya lugha nyingine zinaweza kutoweka kabisa. Utafiti ulivyofanywa, ulionyesha kazi ya Hagége haikueleza ni lugha zipi maalum alizoziangazia, basi akishughulikia utafiti wake, mtafiti alijikita kuchunguza vile taathira za kinyankore zinavyoingilia usomaji wa lugha ya Swahili ikiwa ndiyo ya pili.

Naye Mukuthuria (2004) alifanyia utafiti hili jambo juu ya mtagusano unaohusu lugha mbili katika eneo la Kitigania, akabaini kwamba wanafunzi wanaotumia Kitigania wanakumbwa na matatizo mbalimbali ya kiisimu wanapojifunza Kiswahili. Matatizo haya ni kama yale ya kisarufi, kitahajia, kuchanganya lugha, pamoja na vile walivyotafsiri istilahi za Kiswahili wakizingatia mfumo wa kitigania. Baadaye, utafiti

wake ulibaini kuwa matatizo haya yanatokana na muundo wa namna wanavyotamka maneno na hata maumbo ya lugha husika.

Kwa kuzingatia utafiti huu, tunasisitiza mtagusano wa vile hizo lugha mbili zinapokaribiana kwa wanyankore wanaofunzwa Swahili na ukaribu huo wa lugha hizi unawaathiri. Kulingana na Hymes pamoja na kina Fromkin na Rodman (2009), wakirejelewa na watalaam kama Ontieri (2010) kwenye matini aliyochapisha kuhusu taathira za lugha tangulizi, wanaonyesha kwamba kusom lugha zile za pili unategemea muundo wa sarufi ya lugha hiyo hiyo iliyotangulia. Wakati wahusika wanaelekezwa katika kusoma hiyo lugha inayofuata, mara nyingi wanakumbwa na makosa yanayotokana na kuhamasisha kanuni za kisarufi kutoka ile lugha ya asilia inayojitokeza mwanzoni awali. Wanasimu hawa wanaongeza wakisema kwamba taathira zinazokumba lugha iliyotangulia wakati wa kuelewa lugha nyingine zinaonekana hasa katika fonolojia, sintaksia, na mofolojia.

Mudhune (2008), kama alivyotajwa na Ontieri (2010) katika makala kuhusu athari zinazohusu matamshi ya maneno ya lugha asilia ikiwa Kiswahili, alifanya utafiti akiwarejelea wanafunzi wajaluo wajifunzao Swahili kama lugha nyingine. Alieleza kuwa mifumo ya kimatamshi inavyotofautiana kati ya Swahili na Luo ilisababisha makosa katika sehemu inayohusika. Alieleza kwamba wakati Watoto wajaluo wanapojifunza Swahili ikiwa lugha nyingine, mara nyingi wanaingiza miundo ya matumizi ya maneno ya lugha asilia ikiingilia hiyo lugha inayofunzwa. Mtaalam huyu aliibaini kuwa shida inayosumbua ya kimatamshi ilikuwa inahusisha sauti zinazopatikana wakati wa kusoma lugha nyingine hata kama zisizokuwapo kwenye lugha asilia.

Kulingana na fikra zilizoelezwa na wanaisimu hao, inadhahirishwa kwamba wakati kuna mwingiliano wa lugha inayozidi Moja, lazima kutakuwa na taathira zinazohusiana na kisarufi. Lugha Mama za Kiafrika zinajitokeza kuathiri hiyo lugha inayokuwa inajifunzwa katika jamii nyingi, hali ambayo inasababisha makosa mbalimbali. Kwa hivyo, mtafiti alishughulikia utafiti wa ndani kuhusu taathira za Kinyankore katika mafundisho yanayohusu mfumo wa lugha iliyo swahili.

Wanaisimu kama Komunte (2001) wanaelezea kuwa kuna zile taathira zijitokezazo wakati lugha mbili zikikaribiana, athari zenyewe huenda zikawa za kimatamshi; kwa mfano, utafiti ulionyesha kuwa wanafunzi wanapojifunza Kiingereza wanashindwa kutamka baadhi ya sauti vilivyo kwamfano tofauti kati ya "right" na "light" kwa sababu "l" haipo katika kinyankore. Vivyo hivyo, mtu anayejifunza lugha nyingine anaweza kushindwa kutambua tofauti zilizopo kulinganisha namna ya kutamka konsonanti za kipekee na jinsi zilivyo kwa wanafunzi wanaojifunza italiano ambao wanaweza kushindwa kugundua konsonanti hizo zinazotumiwa katika kulinganisha semantiki maelezo katika lugha husika. Aidha, wanaisimu hawa walizingatia lugha za barani Ulaya. Mtafiti akichunguza mapitio ya maandishi alimakinika katika kuangalia lugha mbili za Kibantu, Kinyankore na Kiswahili.

Mudhune (2008) alifanyia utafiti masomo ya mofolojia na sintaksia kaika matumizi ya Swahili kwa wanafunzi wazaliwa wakijaluo kuzingatia uchanganuzi wa lugha. Aligundua kuwa makosa kadhaa yanayojitokeza yakiwasumbua wajifunzao yanatokana kwa kutegemea sana miundo ya lugha zao asilia. Baadaye, alibainisha kwamba kulitokea kasoro nyingine zisizo na chanzo wala uhusiano wowote na wahusika. Tukizingatia misimamo hii, Mudhune alipendekeza kufanywe utafiti wa kutosha kubaini kwa nini kasoro hizo zinajitokeza na nini kinachozisababisha na sababu tofauti na zile zinazotokana kwa lugha asilia.

Naye Komunte (2001) alishughulikia vile ufundishaji wa kingereza unavyngiliwa na lugha za Kiafrika katika shule za sekondari hasa za kitanzania. Alisema kwamba pale ambapo walifundishia kulikuwa na hali iliyosababisha kuwepo kwa lugha nyingi na ililetea wajifunzao hao kusaidiwa na matumizi ya maneno ya lugha za kienyeji. Utafiti wake ulionyesha kuwa hali hii ilichangia pakubwa ugumu wakati wa kusoma lugha ya kimombo kwa wajifunzaji hao. Aliendelea kutambua pia asilimia Zaidi ya themanini wa wajifunzao walikubali kwamba wanawaza kwa kurejelea lugha zao asilia kabla ya kuwasilisha mawazo yao katika Kiingereza. Komunte (2001) alionyesha kuwa wengi wa wanafunzi walikosa uelewa na ujuzi wa kimombo, na wengine walitamka sauti za kimombo wakifuatilia maandishi, akimuelezea vile lugha asilia inavyoathiri jinsi wanavyotamka ambako kuna kasoro fulani. Kwa kurejelea utafiti wa sasa, mtafiti aliangazia hasa mwingiliano wa L1 iliyo Kinyankore wakati wa L2 iliyo ya Swahili inapofunzwa.

Wataalam wengine mkiwemo Munyua (keshatajwa) walichunguza dhana ya kuibuka kwa Viswahili wakionyesha vinavyoingilia masomo ya Swahili. Ilibainishwa kwamba kuna taathira za lugha asilia wakati wa mafunzo yanayosomwa katika lugha nyingine na huleta makosa kadhaa ya matumizi, akiwa na lengo la kueleza matumizi yasiyo sahihi kuhusu somo la Swahili likipata maneno ya mkopo kwa zile lugha za kienyeji kama vile Kibukusu, Kikibii, Kikikuyu, Kimeru, Kikalenjini, na Kiluo. Munyua aligundua ya kwamba taathira hizi huonekana ukirejelea sehemu zote za kiisimu kama matamshi, maumbo, muundo na kimaana.

Mtaalamu Munyua alishikilia pia ya kwamba kama kasoro zikizidi kuwa nyingi, maelezo huwa magumu kueleweka. Ndiposa akapendekeza kufanyike utafiti Zaidi kuhusu "viswahili" ukilenga kutoa mwongozo kwa wanaotunga mingozo ya mafundisho ya Swahili ili kuanzisha njia bora za kusomesha Swahili sahihi. Basi

tukiyazingatia hayo yote yanaleta mwangaza katika utafiti unaohusisha Kinyankore kwa wasomaji wa swahili, kwani hakuna utafiti mwingine kama huo uliowahi kufanyika.

Mangwa (2005) naye alifanya utafiti kuhusu vile lugha tangulizi ya Kikisii inavoingilia usomaji wa swahili nchini Kenya. Aliona kuwa kasoro zilizopo kwa swahili yalihusiana na chanzo kinachoanzia ile lugha ya asilia ambayo ilikuwa Kikisii. Mangwa alionyesha kwamba kasoro hizo ziliathiri matokeo ya wanafunzi walifanya mitihani ya Swahili wilayani nzima yakijitokezakwa kurejelea kiwango cha kifonolojia na kitahajia na kimsamiati. Alipoeleza makosa hayo, Mangwa alieleza ujuzi wake na njia ya kupata data.

Kwa hivyo, kutokana na haya yote, mtafiti anadhihirisha kuwa kiutafiti kunahitajika utafiti wa kutosha, kwani Mangwa (keshatajwa) hakuzingatia taathira zinazotokana na Kinyankore katika kujifunza hiyo L2 ya swahili. Kwa mjibu wa Mtaalamu kama Ngugi (2007), wanaeleza kuwa umilisi wa lugha tangulizi unaathiri usomaji wa lugha nyingine kimatamshi. Alipofanya utafiti kuhusu jinsi lugha ya Kikuyu inavyoathiri usomaji wa lugha nyingine hata iwe ya swahili, Huyu mtafiti aligundua kwamba taathira hizo zinapatikana sana katika kiwango cha kifonolojia na tahajia. Ngugi alisisitiza kuwa kasoro nyingi ziligunduliwa wakati masomo ya lugha za wasomaji kwa shule za sekondari waliokuwa wakichunguzwa yalisababisha taathira za kuchopeka au kudondosha au uzalishaji wa maneno ya Swahili. Alibaini kwamba mifano ya kimatamshi ilikuwa dhahiri kwa wale wanaojaribu kuitumia wanafunzi, huku makosa yakitokana na zile taathira zinazoonyeshwa kwa lugha zote zinazoingiliana. Mwishowe, Ngugi alishauri ya kwamba kufanyike tafiti ili kasoro za kimaumbo na kifonolojia na jinsi masomo ya lugha asilia zinavyoathiri kusoma kwa lugha nyingine.

Kwa hivyo, mtafiti wa kazi hii alilenga kueleza jinsi lugha ya Kinyankore inavyoathiri usomaji wa Swahili kwa wale wanaoisoma ikiwa kugha nyingine

2.2.2 Kufundishwa kwa lugha nyingine

Mtaalam Corder (1967) anabainisha kwamba matatizo yanayojitokeza wakati mtu anapojifunza masomo kuhusu lugha Zaidi ya moja huwa ni jambo linalotokeana sana sana kabla ya mtumiaji kuzoea mifumo inayotawala matumizi ya lugha nyingine. Kuna mifano kadhaa inayotambulika kisaikolojia iliyo ya maana ya uchambuzi wa shida zinazojitokeza wakati wa kutumia lugha[29]. Baadhi ya mifano iliyotolewa ni Ujumlishaji mno kiholela, Uhamishaji Lugha ambapo mifumo inayotawala matumizi ya lugha asilia zinatumika na hivyo kuvunja mikakati ya kuendeleza lugha nyingine. Aidha, kuna mifumo inayotumika kuwasiliana kwa lugha nyinginezo, namna ya kusomesha iliyo sahihi, hata namna ya kuhamisha ufundishaji ambapo makosa yanatokana na kuokuwa na ujuzi wa kutosha kwa wanaofundisha. Haya matatizo yote huonekana kupitia njia hizo zilizoorodheshwa na Selinker (1969). Kulingana naye, makosa haya yanasababisha hali nyingine ya kutumia na kukamilisha dhima ya mawasiliano inayoitwa Lugha ya kati ambayo hujitokeza msemaji anapojitahidi kusoma L2, kwa kuwa msemaji wa lugha ya kati kati anahamisha sheria zinazotumika kwa lugha asilia kwenda lugha nyingine anayoelekeza.

Wataalamu wengine mkiwemo Richard na Selinker (1969) katika miaka ya Sabini wamebainisha kategoria za kasoro zinazojitokeza tungoni. Mfano wa aina hizo ni:

a) Kuhamisha Maneno. Hii ni njia mojawapo ya kuhamasisha viambajengo vya muundo wa lugha unaotumika katika lugha fuatizi. Wanafunzi wengi huenda wanadhani kuwa viwango vinavyotumika katika lugha zote vinafanana. Aidha,

[29] Selinker, L. (1969). *Studies in Second Language Acquisition,* 3, (2), Spring 1981, pp.201-220

wanafunzi wanaweza kuamini kwamba mikakati inayotawala matumizi ya lugha hizo mbili ni sawa, hivyo wanaweza kuzitumia kwenye lugha zote kwa kubadilishana.

b) Mafundisho mabaya kwa lugha inayosomwa. Ukosefu wa kufahamu ile lugha inayofunzwa hupelekea ufundishaji usiofaa na matarajio yasiyokamilishwa. Wakati mwingine, walimu hupungukiwa na elimu sahihi katika jinsi hiyo lugha inavyofunzwa. Pia, kuna wale wafundishao wanapokosa tajriba ifaayo, mara nyingi wakitumia mbinu zisizofaa, kama vile matumizi yasiyofaa kutumika katumika kama kanuni za lugha husika.

c) Mikabala inayotumika kuwasiliana wakati wa mafunzo ya lugha nyingine. Mawasiliano haya yanahusu lugha inayofunzwa kutegemea lugha maalum inayotumika kufundishia watu waweze kuelewana na watu wanaoongea nao kama wamilisi wa lugha. Wakati mwingine watu hujibidiisha kadri anavyoweza ili aweze kukabiliana na mapungufu yake kwa ile lugha inayofundishwa. Ili kufikia mawasiliano bora, mwanafunzi huyo hujikita katika juhudi.

d) Kujumlisha kighafla. Hii ni namna ya kutoa hitimisho ya jumla sana hadi kufikia mipaka ya juu. Kwa kawaida, Watoto wanaojifunza lugha hiyo wanatumia kanuni ovyo ovyo, hata pale ambapo haifai. Kutokana na kutenda hivyo, wanafunzi hujenga dhana inayoeleweka kwa lugha inayofundishwa kwa kutumia mikakati ya ufunzaji wa lugha asilia ili kusoma lugha nyingine, hali hii ikisababisha kasoro nyingi zinazopatikana wakati wa kusoma lugha nyingine.

Kwa mujibu wa mtaalam Selinker, kuna walimu ambao hufundisha lugha nyingine kwa mfano Swahili wakitumia mbinu ambazo hazifai katika mchakato wa ufundishaji wanalaumiwa ya kwamba hawastahili kuwa walimu. Masebo na Nyangwine (waliotajwa hapo awali) wanafafanua kwamba somo la lugha inayofunzwa mtoto

akishajifunza lugha inayotangulia. Mpango wa kusoma lugha nyingine unategemea mambo kadhaa kama walimu, uelewa wa wanafunzi, mbinu za kufundishia, na mandhari na mkutadha wa kijamii yanayoizunguka mtu anayejifunza. Kwa mfano, yeyote ajifunzaye Swahili nchini Tanzania atakuwa na maarifa ya kina zaidi kuliko yule ajifunzaye swahili nchini Malawi, Nigeria, ama Ujerumani. Tofauti katika muundo unaotumika wa lugha zinaonekana wazi wakati mtu anapojifunza zile lugha nyingine akishasoma ile L1 inayotangulia. Katika hatua hiyo, tunaangalia mfumo unaofuata silabi zinazotamkwa katika lugha hiyo ya kwanza umeshakuzwa, na anapojifunza hiyo lugha nyingine, mara nyingi anatafsiri silabi za maneno hayo mapya kwa kutumia mikakati ya kimatamshi iliyoko katika lugha tangulizi ya kwanza. Pengine, hiyo lugha nyingine hutumika kwa mawasiliano katika jamii ambazo si za hiyo lugha asilia ya kwanza, hivyo kusoma hiyo lugha kunakuwa muhimu ili mawasiliano na kuungana na jamii hiyo.

Kulingana na Chomsky [30], kama alivyotajwa na Ellis (1996), Mikondo ya matawi ya kisarufi hufuata mikakati iliyojengwa kwenye matumizi ya lugha hizo za kibinadamu. Msimamo wa madai hayo unaamini kuwa mtu akizaliwa ana maarifa asilia yanayomsaidia wakati wanaposoma hiyo lugha. Haya maarifa hujitokeza tu wakati wa kuzaliwa, kwani huja yakiwa na maumbile yenye umilisi wa lugha ambazo zinazobadilika, zinazokutana na uzoefu unaopatikana katika kabila fulani hivyo kuwezesha kuelewa kwa lugha husika.

Flyn (1984-1987), akinukuliwa na Mtaalam mwingine Ellis (1996), anasema kwamba chombo cha kumiliki uwezo wa lugha asilia kinahusika katika mchakato wa kusoma

[30] Noam Chomsky alitoa nadharia ya Language Acquisition device (LAD) kuwajibika kwa kasi ya haraka ambayo watoto wanaonekana kujifunza lugha na sheria zake. Kifaa cha kupata lugha ni chombo cha dhahania katika ubongo ambacho huwasaidia watoto kujifunza na kuelewa lugha haraka. LAD baadaye ilibadilika kuwa nadharia kuu ya Chomsky ya sarufi ya ulimwengu wote.

hiyo lugha inayofuata. Anakubaliana na dhana ya kwamba mikondo ya sarufi huwa na dhima katika uelewa na usomaji wa lugha nyingine, akisisitiza kuwa maarifa ambayo mwanafunzi aliye na umilisi wa lugha asilia anayatumia kama yale anayoyatumia mwanafunzi anayesoma lugha nyingine. Wanaokuwa na umilisi wa lugha tangulizi wana uelewa halisi unaowasaidia kujifunza baadhi ya mawaidha katika lugha zao na hivyo sifa za mwanafunzi anayesoma lugha asilia pia ni sifa za mwanafunzi akijifunza lugha nyingine.

Mchakato wa kusoma lugha nyingine huenda ukafanyika kulingana na hali ya muktadha. Wengine hujifunza kwa urahisi kutokana na jinsi lugha nyingine inavyoweza kutumiwa kuongeza kwa ile iliyotangulia nyumbani au katika michezo na wenzao. Katika hali nyingine, kuna pale ambapo lugha nyingi zinafundishwa katika asasi za elimu, hii inasaidia watu wengi kujifunza Kiswahili kama somo la lugha nyingine, ikiwa inaenda sambamba na usomaji wa Kinyankore kwa baadhi ya Wanyankore.

Kulingana na Gardiner (1985)[31], pamoja na wataalam wanaoamini nadharia ya saikolojia ya kijamii, mambo yanayochangia masomo ya lugha nyingine huwa mengi kama vile uelewa wa wanafunzi, umri wao, mbinu za kuwafunza, muktadha, mazingira yenyewe, na hata uwezo wa Mwalimu awafundishaye.

Gardner (1985), anaeleza kwamba uwezo wa kupendelea kusoma na kutumia lugha nyingine unategemea vigezo kadhaa vinavyohusisha misimamo na kuvutwa kwa wasomao.

[31] Gardner, R. C. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation.* London: Edward Arnold

Katika utangulizi wa kitabu chake Gardner (1985), Giles anaeleza kwamba,

> "Inawezekana ya kwamba tabia ya kutumia lugha inategemea vile wanaoitumia wanaonyesha mila za jamii zao na hata wanavyoelezea hali yaliyo mkabala nao kwa njia binafsi wakizingatia kanuni zao ..." Gardner (ix).

Krashen na wenzake (1983)[32] wanafafanua ya kwamba mfano mzuri wa kusoma lugha nyingine unafaa. Aidha wameongeza kwamba anayefundisha astahili kuwa mfano mzuri katika kutumia lugha nyingine hasa mbele ya wanafunzi wake ili waweze kumwiga. Kwa hivyo, anayefundisha anastahili kuwa na uwezo mzuri katika matumizi ya lugha ili aweze kuigwa na wanafunzi wake.

Inasisitizwa kwamba Mwalimu hastahili kudhihirisha kuwa aliathirika na matamshi ya lugha asilia wakati anapotamka silabi za lugha nyingine[33]. Pia inapendekezwa na wataalam kuwa shida za walimu zisisitizwe kwa sababu wanastaahili kuwa mfano mzuri kwa wanafunzi wanaowafundisha.

Yeye Ellis (1996) anasema kwamba shida za wanafunzi ambao wanasoma lugha nyingine huwa kwamba hawawezi kutambua miundo ya mikakati ya kutumia lugha inayohusika na wengine wanakosa tajriba ya kutambua makosa na kutumia hiyo lugha nyingine.

2.2.3 Ushirikiano wa Kinyankore na Kiswahili

Lugha inasemekana kubadilika kutokana na kulingana na vile wanajamii wanaitumia, jinsi wanavyoitumia katika maisha yao na kiwango ambacho wanathiriwa na zile lugha nyingine kila siku. Wazungumzao wa zile lugha ambazo ni tofauti kikabila nchini, kama Wanyankore, mara nyingi huathiriwa na kuingiliwa kwa lugha asili

[32] Krashen, S. D., & Terrell, T. D. (1983). *The natural approach: Language acquisition in the classroom*. Alemany Press.

[33] Curtain, FL, & Martinez, L S. (1990). Elementary school content-based foreign language instruction. In A. Padilla, H. Fairchild, C. Valadez (Eds), *Foreign language education: Issues and strategies*. (pp. 202-222). Newbury Park, CA. Sage.

wanapojifunza Kiswahili, ambapo wanaweza kuingiza kanuni zinazounda uelewa wa lugha zao. Muktadha huu unasababisha kuathiri jinsi wakati wanapokizungumza, na inawezekana pia kupotosha ujumbe waliokusudia kufikisha kwa wasikilizaji. Wanaisimu wamekuwa wakifanya tafiti ili kubaini vyanzo vya makosa mbalimbali na pia kubuni namna nyingine ya kusuluhisha matatizo hayo.

Kiswahili kikiwa kinafundishwa kama lugha nyingine kwenye jamii nyingi za kikabila, inamaanisha kwamba kinaathiri lugha zinazotangulia na zinaonekana wazi katika matamshi. Pia, imebainika kwamba watumiaji wawili wenye lugha zinazotofautiana katika kuwasiliana huwa ni wa zamani sana hata wanapoathiriwa lugha zenyewe. Hizi lugha ambazo ni zina chimbuko la kibantu pia zimechangia katika muktadha wa L2 ya Swahili; Masebo na Nyangwine (2003) wanasema kwamba lugha hizo zimeleta asilimia 64 kuhusu msamiati wa Kiswahili.

Wataalamu kadhaa, kama Masebo na Nyangwine (2008), wamesisitiza kuwa Kiswahili kimeingiliana kwa karibu na lugha nyingine za Kibantu. Athari hizi zinadhihirika katika namna ya kutamka sauti, kimaana, leksika, hata isimu nzima. Watumiaji kadhaa wanakumbana na shida ambazo zina asili ya lugha zenyewe za kikabila wanapozungumza Kiswahili sanifu. Swali muhimu tunalolishughulikia katika kazi hii ni jinsi Kinyankore kinavyoathiri mafunzo ya lugha nyingine mkiwemo Swahili. Tafiti nyingi zimefanyika kuhusu vile lugha zenye asili ya ubantu zinavyoweza kuingilia Swahili. Licha ya jitihada zinazolenga kukuza na kuendeleza kuboresha Swahili, utafiti uliotangulia ulionyesha kwamba wanafunzi wanaojifunza lugha hiyo wanakosea wakiwa wanazungumza, ambayo yanajitokeza kwenye ngazi za kimaumbo, kimatamshi, kimuundo hata kimaana. Wataalam wa isimu wanaendelea kufanya juhudi za kubaini chanzo cha makosa haya na kutafuta njia bora za kuyatatua.

Wataalamu wengi wamejadili suala hili, kama ilivyoelezwa na Masebo na Nyangwine (2008), ambao wanasema kuwa Kiswahili kimeingiliana kikiwa na haraka sana na hata lugha tofauti za Kibantu. Tunaona pia kwamba Kiswahili ni lugha nyongeza kwa jamii nyingi za Kibantu, Ikiingilia kati yake huonekana kwa uwazi katika matamshi. Mara nyingi tunaposikia mtu akizungumza Kiswahili, tunaweza kubaini haraka kuwa ni mgeni wa lugha husika; moja ya sababu inaweza kuwa ni kwamba anakosa kuzingatia tofauti za kifonimu au kialofoni zinazohitajika, au anaweka taratibu za fonolojia za lugha asili hizo ambazo hazipo katika Kiswahili. Hata lugha zinazoshirikiana kwa karibu zinaweza kuwa zinajenga utofauti Fulani wa kifonetiki na kifonolojia. Swali kuu la utafiti huu ni jinsi Kinyankore kinavyoathiri namna ya kufunza somo la Swahili.

2.3 Zana zinazotumika katika utamkaji wa sauti

2.3.1 Matamshi ya Sauti Mbalimbali

Matamshi ya sauti fulani hutegemea lugha tu ambazo zinaweza kutolewa na viungo vya sauti vya wanadamu. Hata kama lugha hizi mbili zinazotumia sauti zifananazo, hasa zenye sifa zile zile za kifonolojia, huweza kuwa tofauti kulingana na vile sauti hizo zilivyotumika. Hivyo, ni kawaida kutarajia kwamba lugha huwa na miundo mbalimbali za kimatamshi.

Yeye Mgullu (2012) anasema kwamba, ala za matamshi ni viungo vilivyopo katika maumbile ya binadamu vinavyohusika na utamkaji. Wakati mtu anapozungumza, hutumia viungo mbalimbali, ambayo pia huenda yakawa na uwezo wa kushawishi tofauti katika uzungumzaji; wengine wana jukumu kuu, wengine wastani, na wengine ni wachache. Ala za matamshi zinagawanywa kwa kutegemea kategoria kuu mbili zifuatazo:

i. Ala sogezi, na
ii. Ala tuli.

Hizo ala zinazojulikana kuwa sogezi zinazosogea wakati wa kuzungumza, kama vile jinsi tunavyotumia ulimi mdomoni kutamka sauti. Pengine, zile ala zinazojulikana kuwa tuli huwa aina ambazo haziwezi kusogoa, kwa mfano, ufizi.

Matinde (2012) anabaini kwamba hizo sauti binadamu anazotumia kujenga lugha yake hutamkwa wakati viungo mbalimbali vya mwili vinapozuia hewa inayoingia na kutoka mapafuni hadi mdomoni ikipitia puani. Viungo hivi vinaitwa zana za sauti.

Ala muhimu za matamshi huhusisha mifano kama vile, midomo, meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini, kimio, sehemu ya mbele kwenye ulimi, bapa la ulimi, shina la ulimi, kidakatonge, nyuzi sauti, koo, pua, mdomoni na koromeo.

2.3.2 Matumizi ya fonimu na sifa zake kwa Kiswahili

2.3.2.1 Maana ya fonimu

Kulingana na Mgullu (2012) anafafanua kwamba katika lugha kunakuwepo kijisehemu kidogo sana kilicho na uamilifu wa kutofautisha maana katika maneno.

2.3.2.2 Aina za fonimu

Mgullu (2001), akiwa na wataalam wengine kama Iribe Mwangi (2010) wamejitokeza kuwa baadhi ya wale wataalamu wa lugha ambao wamechambua mfumo wa jinsi sauti kama fonimu zilivyo. Wamebaini fonimu kuwa zinainishwa katika makundi matatu kama vile sauti za vokali, fonimu za nusu irabu, na zile zinazokuwa za kikonsonanti. Katika uchambuzi unaofuatia mikakati ya matamshi ya lugha tofauti, mfanano wa kifonetiki kati ya sauti ni muhimu sana, ikiwa ni pamoja na uhusiano wote wa kifonolojia, kanuni, na minyumbuo yote ile.

Katika mchakato wa kuziweka katika kategoria kadhaa, ziweze kutambulika vizuri kama foniimu katika lugha Fulani zikiwa na alofoni hizo, kuna umuhimu wa kuzingatia namna fonimu hizo zinavyohusiana kulingana na maeneo ya utamkaji na mbinu za utamkaji. Katika kielelezo cha jedwali la IPA, fonimu zenyewe zimegawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na namna zinavyotumika kipekee[34].

Kulingana na jinsi zinavyotamkwa, zile fonimu katika lugha ambazo zinawekwa katika kategoria mbili kuu kama irabu na konsonanti.

2.3.2.2.1 Vipashio vya sauti vinavyojulikana kama fonimu

Habwe na Karanja (2004) wanafafanua kwamba vokali zinatamkwa na zile zana zinazotumika kutoa sauti zikiwa huru, bila ya kutokea mkwaruzo wazi kama ilivyo kwa konsonanti.

Mgullu (2012) anaelezea kwamba, mtu akiwa anatamka vokali, hewa haizuiwi wala kubanwa sehemu yoyote.

Kuna aina nyingi za irabu, na idadi yake inategemea lugha husika, kwani katika lugha yoyote ile inachagua nambari fulani ya vokali kutoka kwenye akiba ya sauti. Kiswahili kina vokali tano: / a /, /ɛ /, / i /, / ɔ /, na / u /. Vokali hizi zinaungana na konsonanti ili kuwa na silabi kamili.

Vokali zinaainishwa kwa kuzingatia vigezo kadhaa, ambavyo ni:

i. **Sehemu ya ulimi:**

Sehemu hii inaweza kuwa ya mbele, kati, au nyuma. Katika Kiswahili, hizo vokali zinazokuwa mbele ya kinywa huwa / i / na /ɛ /, huku za nyuma zikiwa / ɔ / na / u /. vokali ya kati ni / a /.

[34] Habwe na Karanja 2004. *On the foundation of Swahili grammar*

ii. Kuinua ala ya ulimi

Ulimi unaweza kuinuliwa juu kuwa sambamba na sehemu ya juu ya kinywa, kulazwa chini, au kuwa katikati.

a. Vokali ambayo hutamkwa na ulimi ukiwa umeinuliwa juu ni zile zinazotamkwa zikiwa juu, mfano ni: / i / na / u /.
b. Vokali zinazotamkwa na ulimi ukiwa katikati ni /ɛ / na / ɔ /.
c. Vokali inayotamkwa kwenye sehemu inayokuwa chini kinywani ni / a /.
d. Vokali /ɛ / na / ɔ / huwa na namna yake kama katika [-kaze], hivyo mwanzo wa kutamka hulegezwa, tofauti na / a /, / i /, na / u / ambazo hutamkwa ukiwa na ulimi mkazi, na hivyo huwa na vile zinavyotambulika [+ kaze].

iii. Jinsi mdomo unavyokuwa

Katika mchakato wa utamkaji wa vokali za Kiswahili, midomo huenda ikawa mviringo au mtanda. Vokali zinazotamkwa na mdomo ukiwa mviringo ni / u / na / ɔ /. Irabu zinazotamkwa na mdomo ukiwa mtanda ni / a /, /ɛ /, na / i /. Ni muhimu kutambua kwamba jinsi mdomo unavyokuwa mviringo au kutanda kinatofautiana kulingana na irabu inayohusika katika matamshi, kama vile, mdomo hutanda zaidi wakati wa kutamka / a / kuliko /ɛ / na / i /.

Mchoro ufuatao unaonyesha irabu zitamkwavyo:



Kielelezo 2.1: Vokali

Jedwali 2.3 Sifa bainifu za vokali

	/a/	/e/	/i/	/o/	/u/
Juu	-	+	+	-	+
Chini	+	-	-	-	-
Nyuma	-	-	-	+	+
Mbele	-	-	+	-	-
Mviringo	-	-	-	+	+
Kaze	+	-	+	-	+
Kati	+	-	-	-	-

Katika jedwali 2.3, Vokali za Kiswahili zinadhihirisha sifa bainifu kadhaa ambazo zinaweza kuainishwa kama ifuatavyo:

Mahali pa kutamkia kwenye ulimi:

- Irabu zinaweza kuainishwa kulingana na mahali ambapo panatumika kutamka vokali. Hizi zinaweza kuwa:
- Vokali zinazokuwa mbelembele: Kama vile / i / na /ɛ /.
- Vokali zinazokuwa Katikati: Kama vile / a /.
- Vokali zinazokuwa nyumanyuma: Kama vile / ɔ / na / u /.

Kuinuka kwa ulimi:

- Irabu pia zinaweza kuainishwa kwa kutegemea vile ulimi unavyoinuliwa au kushuka wakati wa kutamka:
- Vokali zinazokuwa juu (+ juu): / i / na / u / hutamkwa huku ulimi ukiinuliwa.
- Vokali zinazokuwa Kati: /ɛ / na / ɔ / hutamkwa huku ulimi ukiwa katikati.
- Vokali zinazokuwa chinichini (- juu): / a / hutamkwa huku ulimi ukiwa umelegea chini.
- Irabu /ɛ / na / ɔ / hutambulika kwa [-kaze] ambapo ulimi hulegezwa, wakati / a /, / i /, na / u / hutambulika kwa [+ kaze] ambapo ulimi hukazwa.

Jinsi mdomo unavyokuwa:

- Jinsi mdomo unavyokaa katika utamkaji huwa sifa nyingine muhimu ya irabu:

- Mkao wa Mviringo: Irabu kama / u / na / ɔ / hutamkwa na mdomo ukiwa mviringo.
- Mkao wa Mtandazo: Irabu kama / a /, /ɛ /, na / i / hutamkwa na mdomo ukiwa mtando.
- Kiwango cha mviringo au kutandazwa kinaweza kutofautiana kulingana na irabu inayotamkwa. Kwa mfano, mdomo hutanda zaidi wakati wa kutamka / a / kuliko /ɛ / na / i /.

Kukuzwa na Kukazwa:

- Irabu zinaweza kuwa na sifa ya kukazwa au kukuzwa. Hili linategemea uwezo wa hewa kutoka kwa koo katika mchakato wa utamkaji. Vokali zilizokazwa zinaweza kuhusishwa na kuongezeka kwa shinikizo la hewa katika hali ya kutamka tofauti na zile zisizo na mkazo.

Kwa ujumla, sifa hizi za irabu hutoa muundo wa msingi wa kutambulika na kuziwezesha kuunganishwa na konsonanti katika lugha ya Kiswahili ili kuunda silabi na maneno.

2.3.2.2.2 Viyeyusho/ Nusu irabu za Kiswahili

Nusu irabu, kwa upande mwingine ni sauti zinazojulikana pia kama viyeyusho ambavyo huwa vokali ambazo zinatamkwa kwa namna ya nusu ya irabu kamili. Nusu irabu katika baadhi ya lugha hutumika kuleta utofauti katika matamshi ya maneno. Viyeyusho kwa kawaida huwa na sauti za nusu za irabu ambazo husisitiza sauti ya maneno. Katika hali ya kutoa sauti, mtu hukosa nguvu ya utamkaji inayopatikana kwenye irabu kamili, hivyo hutambulika kama sauti ngumu au dhaifu.

Sifa za Viyeyusho:

- Nusu ya Irabu: Kama ilivyobainika hapo awali kwamba nusu irabu huitwa viyeyusho pia, haviwezi kusimama na kujitegemea bila kutoa sauti inayolingana na ile ya irabu kamili. Katika hali kadhaa zinasemwa kwa kasi zaidi kuliko irabu kamili.
- Matumizi Katika Maneno: Viyeyusho katika Kiswahili ni mara nyingi /y/ na /w/. Mfano mzuri unaweza kuwa katika sauti "mya" (/mya/), /y/ hutamkwa kama ni nusu irabu inayonyesha mwinuko wa sauti.

Mwonekano wa Kihurufu:

Viyeyusho vinaweza kuonyeshwa kwenye maandiko kwa kutumia sauti ya kipekee kama zinajulikana ‘y’ au ‘w’. Kwa mfano:

- Katika neno “tuwa” (/tuwa/), ‘u’ na ‘a’ ni irabu kamili, lakini ‘w’ inawakilisha nusu irabu.
- “mwana” (/mwana/), nusu irabu ‘w’ inatambulika, ikionyesha mpito wa sauti.

Viyeyusho hutumika katika sarufi kutoa matamshi sahihi kuhusu zile sauti ili kufanya wazi uhusiano wa sauti ndani ya neno. Vinaweza kuathiri maana kwa kubadilisha mfumo unaojenga sentensi. Chini hapa ni vielelezi vya silabi zilizoundwa na nusu irabu;

- W… (wimbo – naimba)
- Y… (yanakuja – natarajia)

Katika ujumla, viyeyusho ni sehemu muhimu inayotumika kuunda muundo wa lugha, kwani vinasaidia katika kuboresha uelewano wa sauti na uharaka wa matamshi.

Nusu irabu, kulingana na Iribe Mwangi (2010), inahusisha mbinu za kuunda sauti za kisarufi kwa kutumia silabi mbili. Hii mara nyingi inamaanisha kutoa maana zaidi zinazotumia silabi za kisarufi ambazo zinajumuisha sehemu za neno au maneno mapya. Katika muktadha wa lugha, nusu irabu inaweza kueleweka kama matumizi kuhusu silabi zinazoweza kuchukuliwa kuwa kipashio cha neno wala utungo ili kuleta maana na umuhimu katika kuelewa muundo wa kisarufi.

Hii inamaanisha kwamba, zile sauti zinazojulikana kama viyeyusho hukosa uwezo wa kujenga silabi zikijitegemea kuwa vokali ama konsonanti bila kutambulika kivyake. Jambo linguine linahusu viyeyusho ambavyo haviwezi kuwa silabi kama vokali. Viyeyusho pia huwa na kazi ya kuwa sauti inayotangulia silabi.

2.3.2.2.3 Konsonanti za Kiswahili

Wataalam mkiwemo Habwe na Karanja (2004), wanafafanua kwamba konsonanti ni zile fonimu zinazotamkwa wakati hewa inakabiliwa na kizuizi kamili au kidogo, hivyo nafasi ya hewa inakuwa ndogo sana kiasi kwamba hupita kwa mkwaruzo. Kwa hiyo, konsonanti zinaweza kupita kupitia mkwaruzo wa aina fulani. Kuna sifa maalum zinazotumiwa kubaini konsonanti, ambazo ni:

i) mahala pa kutamkwa

ii) Vile sauti inavyotamkwa

Idadi ya konsonanti katika Kiswahili sanifu inatajwa kwa namna tofauti kulingana na wanaisimu kadhaa. Kwa mfano, Mgullu (2012) na Polome (1967) wameorodhesha konsonanti tofauti, huku kina Massamba (keshatajwa) wakiziainisha kuwa 23, na Iribe Mwangi (2010) akitaja 25. Tukirejelea kazi hii, tutatumia idadi ya konsonanti 25, zilizogawanyw kwenye kategoria kuu sita kama zilizotajwa hapo chini.

Maelezo ya jumla kuhusu konsonanti za Kiswahili yanaonyesha Konsonanti mbalimbali kama vile;

Konsonanti za Kawaida:

Mfano wa sauti na neno
sauti ya "b" kama katika neno "beba"
sauti ya "d" kama katika neno "dodo"
sauti ya "f" kama katika neno "fika"
sauti ya "g" kama katika neno "goma"
sauti ya "h" kama katika neno "haba"
sauti ya "j" kama katika neno "jana"
sauti ya "k" kama katika neno "kera"
sauti ya "l" kama katika neno "leta"
sauti ya "m" kama katika neno "moja"
sauti ya "n" kama katika neno "nini"
sauti ya "p" kama katika neno "pata"
sauti ya "r" kama katika neno "roga"
sauti ya "s" kama katika neno "sera"
sauti ya "t" kama katika neno "teka"
sauti ya "v" kama katika neno "vaa"
sauti ya "w" kama katika neno "wewe"
sauti ya "y" kama katika neno "yote"
sauti ya "z" kama katika neno "zamu"

Konsonanti za Kichanganyiko:

Mfano wa sauti na neno
sauti ya "ch" kama katika neno "chakula"
sauti ya "dh" kama katika neno "dhambi"
sauti ya "kh" kama katika neno "kheri"
sauti ya "ng'" kama katika neno "ng'amua"
sauti ya "sh" kama katika neno "shati"
sauti ya "th" kama katika neno "thamini"

Kwa hivyo, Konsonanti za Kiswahili huwa fonimu zinazozalishwa wakati hewa inakatizwa au kuzuiwa kwa namna fulani. Konsonanti hizi huchanganya na irabu kuunda maneno na kuharakisha mawasiliano ndani katika lugha hiyo mahsusi. Kila kundi la konsonanti lina nafasi maalum kwenye sentensi, na ufahamu unaotumika huwa dhima kwa uandishi na mawasiliano ya lugha husika. Jedwali lililo chini 2.4 linaelezea Zaidi.

Jedwali 2.4 Sifa za Konsonanti za Kiswahili

NAMNA YA KUTAMKA	MAHALI PA KUTAMKIA								HALI YA GLOTA
Vipasuo/ Vizuiwa	Midomo	Midomo meno	Meno	Ufizi	Kaaka gumu na ufizi	Kaaka gumu	Kaaka laini	Koromeo	
	b			d			g		Ghuna
	p			t			k		Hafifu
Vizuiwa kwamizwa						/ ɟ /			Ghuna
						/ ʧ /			Hafifu
Vikwamizwa		v	Ð	z			γ	h	Ghuna
		f	Ө	s	ʃ		x		Hafifu
Nazali	m			n		ɲ	ŋ		Ghuna
Kitambaza				l					Ghuna
Kimadende				r					Ghuna
Nusu Irabu	w					y			Ghuna

Kulingana na jedwali 2.4 la konsonanti za Kiswahili linaelezea makundi kama Vizuiwa mkiwemo /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/, Vikwamizwa (/s/, /z/, /f/, /v/, /Ө/, /ð/, /ʃ/, /x/, /γ/, /h/), Vizuiwa Kwamizwa (/ts/, /ɟ/), Nazali (/m/, /ɱ/, /n/, /ŋ/, /ɲ/), Kitambaza (/l/), na Kimadende (/r/).

Hizi ndizo sauti za konsonanti zinazopatikana tukirejelea abjadi ya Kiswahili. Konsonanti hizi zinajumuisha sauti ambazo zinatumika kujenga sentensi za Kiswahili. Hizi zinahusisha mifano ya konsonanti za Kiswahili pamoja na maelezo ambayo yanazielezea:

Vizuiwa

Hizi ni konsonanti ambazo hewa inakatizwa isitamkwe vizuri. Hapa chini kumeonyeshwa mfano:

- /p/: Sauti hii inatamkwa kwa kuzuia hewa na vidole vya mdomo.

- /b/: Sauti hii ni kama /p/ lakini ina mkazo wa sauti (voiced).
- /t/: Hewa inakatizwa kwenye sehemu ya juu ya ulimi.
- /d/: ingekuwa kama /t/ lakini ina mkazo wa sauti.
- /k/: Inatokana na kizuizi cha hewa kilichopo nyuma ya kinywa.
- /g/: Ingetamkika kama /k/ lakini ina mkazo wa sauti.

Vikwamizwa

Vikwamizwa ni konsonanti ambazo zinakabiliwa na upepo wa hewa. Mifano ni:

- /s/: Sauti hii inatengenezwa na hewa inayopita kupitia nafasi ndogo iliyopo chini ya mahali juu ya kinywa na ulimi.
- /z/: Ni kama /s/ lakini ina mkazo wa sauti.
- /f/: Inazungumzwa na hewa ikikatizwa na jino la chini na labi.
- /v/: Ni sawa na /f/ lakini ina mkazo wa sauti.
- /Ɵ/ na /ð/: Sauti hizi hazitambuliki sana katika Kiswahili lakini zinapatikana kwenye lugha zingine.
- /ʃ/: Hii ndiyo inayotamkika kama “sh” inayoonekana kwenye neno "shuka".
- /x/: Inatamkwa kwa kuzuia hewa kwenye eneo la katikati ya kinywa.
- /γ/: Mara nyingi inatumiwa haswa kwa wajuzi wa lugha iliyo sanifu.
- /h/: Sauti hii hutamkwa kwa deribahi sauti, bila kuweka nguvu kwenye kizuizi cha hewa.

Vizuiwa Kwamizwa

Konsonanti hizi ni zile zilizo na muingiliano wa vizuiwa na vikwamizwa. Mifano ni:

- /ts/ Hii ni sauti inayoweza kuonekana katika maneno kama "tsunami".
- /ɟ/: Sauti hii inayotamkwa kwa mkanganyiko wa kizuizi na hewa ikikatizwa kidogo.

Nazali

- Hizi ni konsonanti zinazohusisha uzito wa hewa kupitia pua. Mifano ni:
- /m/: Sauti hii inazalishwa kwa kufunga mdomo kabisa halafu kutoa pumzi kupita kupitia pua.
- /ɱ/: Huwa ingetamkika kama /m/ lakini hutokea katika kutamka sauti nyingi kwa kupita hewa kupitia pua na fuvu.
- /n/: Hii inaleta uzito wa hewa kupitia pua na hulindwa na ulimi.
- /ŋ/: Inaweza kuonekana katika maneno kama "singa", na inazalishwa kwa kufunga pua.
- /ɲ/: Sauti hii pia inatokana na upande wa pua na hutumika katika majina mengi kwa wanaotumia Swahili.

Konsonanti ya Kitambaza

- Konsonanti za kitambaza ni zile zisizo na kiwango cha kuvuka kwa hewa. Mfano ni:
- /l/: konsonanti hii inatokea wakati ncha ya ulimi inavyogusa sehemu ya juu ya kinywa.

Kimadende

- Hizi ni konsonanti za sauti ya "r". Mfano ni:
- /r/: Inajulikana kama "r" ambayo inatamkwa kwa kushika ulimi sehemu ya juu ya mdomo.

Konsonanti hizi huchanganya na irabu kuunda maneno na kuharakisha mawasiliano ndani katika lugha mahsusi ya Swahili. Kila kundi la konsonanti lina nafasi maalum kwenye sentensi, na ufahamu unaotumika katika uandishi na mawasiliano yanayohusisha swahili.

Konsonanti za Kiswahili zinaweza kuunganishwa na vokali kuunda silabi. Kila konsonanti ina sauti yake maalum na inachangia kujenga msamiati wenye umuhimu wa kueleweka wa Kiswahili.

2.4 Mbinu za Kuwasaidia Wanafunzi wakiwa wanajifunza lugha nyingine

Kufundisha ni mchakato ulioandaliwa na shughuli zinazokusudiwa kwa lengo la kuboresha matokeo yanayotarajiwa ya mwanafunzi [35]. Mafunzo huwa yanahitaji mpangilio ulio na mantiki ili kuwezesha ujifunzaji, ambapo inategemea mkusanyiko wenye ujuzi wa wanafunzi kwa ajili ya kufikia viwango vya ujifunzaji vilivyopangwa. Aidha, ufundishaji unaweza kueleweka kama vitendo vinavyofanywa na mwalimu ili kuunda mazingira ya kushawishi. Mwalimu anawapa wanafunzi ushauri nasaha na vifaa sahihi vinavyotumika katika kufunza wanafunzi ili kutekeleza shughuli zitakazohamasisha ujifunzaji. Pia, ana jukumu la kukuza tabia zinazofaa kwa manufaa ya wanafunzi.

Mwalimu anapaswa kuunda mandhari ya kimasomo yanayowezesha mawasiliano na ushirikiano kati ya wanafunzi. Anatumia mbinu za kufundisha zinazowezesha wanafunzi kushiriki na kujifunza kwa pamoja. Mbinu zinazotumika kusomesha huwa njia zinazomwelekeza mwalimu anatumia katika darasa ili kuimarisha uwezo na hata adabu kwa wanafunzi. Njia zilizo sahihi kutumia kufundisha zinamsaidia mwanafunzi kupata ufahamu, ujuzi, mitazamo, na maadili yanayotarajiwa kulingana na malengo ya mtaala. Njia zinazotumika nyakati hizi nimiundo inayoelekeza ufundishaji zinaonyesha kudhihirisha kuwa shabaha zakusomesha huwa ngumu na zinahitaji mtazamo wa kina. Wahitimu wa mafunzo wanapaswa kutumia mbinu tofauti za ufundishaji zinazozingatia

---

[35] Candy, R.L. & Retting, M. (1996). *Teaching in the block: Strategies for engaging active learners*. Princeton, NJ: Eye on Education.

mahitaji ya kielimu ya kila mwanafunzi kutoka kwa mazingira mbalimbali ili kufikia malengo yao. Hivyo basi, Yeye Williams (2004) anasisitiza kwamba wale wanaotoa mafunzo wanahitaji kuchagua mbinu sahihi kati ya zile zilizopo waweze kuwaelezea wanafunzi.

Kuna njia kadhaa zinazoweza kutumika katika ufundishaji kuboresha elimu. Utafiti ambao umefanywa na wataalam umeonyesha njia hizo za kufunza wanafunzi, zikionyesha mchango uliyomo na falsafa yake kwa ujumla. Njia zenyewe huhitaji uwezo wa kipekee na tajriba kwa walimu na pia vifaa vya kutosha. Ili kuchagua mbinu sahihi, mwalimu anapaswa kuzingatia stadi zinazofanywa, mtaala, umri wa wanafunzi, rasilimali zilizopo na mazingira yenyewe. Mbinu hizi ni kama vile:

2.4.1 Muundo

Huu ni mpango wa kujifunza ambapo wanafunzi wanapata ujuzi kupitia mwingiliano kati ya maarifa mapya na yale wanayojua tayari (Harel & Papet 1991). Katika mpango huu, wanafunzi wanajenga ujuzi na kuelewa kwa kuungananisha yale wanayojifunza na tajiriba zao zilizopo. Wanafunzi wanapaswa kuelewa sarufi inayohusu lugha tangulizi, kwani hii itawasaidia kuelewa mfumo unaozingatiwa katika lugha nyingine. Wanapaswa pia kukuza msamiati unaohusu lugha tangulizi kuwezesesha wanafunzi kuwa na msingi mzuri wa kuelewa maneno na dhana zinazopatikana katika lugha nyingine.

Umuhimu wa mkakati wa uundaji wa mfumo ulio katika elimu na ufundishaji, hasa tukizingatia masomo ya hesabu na sayansi[36]. Mkakati huu unahusisha matumizi ya

[36] Hii ni mbinu ya ufundishaji ambapo wanafunzi hujifunza ujuzi kwa njia ya mwingiliano kati ya maarifa wanayopata na yale waliyonayo awali (Harel & Papet 1991). Katika mbinu hii, wanafunzi wanaunda ujuzi na maana kwa kuchanganya kile wanachofunzwa na kile wanachokijua au wanachokikutana nacho.

mbinu na zana mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi kuelewa dhana za kisayansi na za kimaendeleo kwa njia inayoeleweka na kujiamini. Katika tafiti zao, walitaja mambo kadhaa muhimu yanayohusiana na mkakati wa uundaji. Kwanza, kushirikisha wanafunzi ambapo wanafunzi wanapaswa kuwa washiriki kwa kuhusishwa kupitia shughuli kama vile miradi, majaribio, na majadiliano. Pili, muktadha wa ijamii ambapo utafiti unasisitiza umuhimu wa mazingira ya kijamii ili kuwepo njia ya kufunza ambapo wanafunzi wanaweza kujifunza wakisaidiana wao kwa wao. Tatu, uundaji unaohusisha majibu ya mwanafunzi ambapo mkakati huu unasisitiza kwamba wanafunzi wanapaswa kuunda uelewa wao wenyewe kuhusu dhana badala ya kukariri. Nne, matumizi ya ana za kujifunzia. Harel na Papert (1991) walisisitiza matumizi ya teknolojia na zana maalum, kama vile kompyuta, kusaidia katika uundaji wa maarifa na uelewa. Kwa hivyo, Mkakati wa uundaji husaidia kuboresha uzoefu unaotumiwa kufanikisha lengo la elimu ya kina.

2.4.2 Ufundishaji wa Maelekezo

Hii ni njia mojawapo ya kufundishia ambapo anayefundisha anatumia njia za kuchochea, kuwafanya wanafunzi kutafakuri, kujibu maswali, kuwauliza waeleze maswala na kuigiza mawazo ya yanayojadiliwa ili kusababisha uwajibikaji wao katika kutekeleza majukumu. Wakati wa kutumia njia hiyo, anayefundisha anakuwa kama mwezeshaji pekee, badala ya kuwa mjuzi kuhusu masomo yote.

Fisher na Frey (2010) walifafanua mkakati wa ujifunzaji kupitia muktadha unaohusisha mafunzo ya kiushirikiano na mbinu kadhaa ya kufunzia ambayo inaweza kuongeza ushirikiano kati ya wanafunzi. Katika kazi yao, walijitahidi kuimarisha mbinu za ajira na mawasiliano ili kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi.

Baadhi ya mapendekezo yao muhimu ni, kwanza, kujifunza kwa ushirikiano ambapo wanafunzi wanapaswa kujifunza wakionyesha namna ya kushiriki kazini pamoja katika vikundi. Hii inawasaidia kubadilishana mawazo na kujenga maarifa kwa pamoja. Pili, mifumo ya kujifundisha. Fisher na Frey (keshatajwa) walisisitiza matumizi ya mifumo inayowezesha wanafunzi kushiriki katika masomo wakiwa pamoja ili waweze kuelewa, kwa mfano majadiliano ya kikundi na mradi wa pamoja. Tatu, ushirikiano wa walimu, ambapo walimu wanapaswa kuhusika kama nguzo kuu katika mikakati ya mafunzo, wakitoa mwongozo na msaada kuelekea wanafunzi kuhakikisha wanaelewa vizuri yaliyomo. Nne, kudhibiti mbinu za kimasomo. Hapa, walifafanua umuhimu wa wanafunzi kuelewa jinsi ya kudhibiti mchakato wao wa kujifunza kwa kutathmini na kutafakari juu ya maendeleo yao. Tano, kutumia njia zilizo tofauti za kutoa maelezo, ambapo Mbinu kama vile kutumia michoro, mifano, na teknolojia yanaweza kuboresha uelewa wa wanafunzi na kuongeza hamasa yao katika kujifunza.

Kwa ujumla, Fisher na Frey wanasisitiza kwamba ujifunzaji unapaswa kuwa mchakato wa pamoja ambapo wanafunzi wanashirikiana kuunda maarifa mpya kwa msaada wa walimu.

2.4.3 Mbinu ya kutatua makosa

Mbinu ya kutatua makosa inahusu hatua za kufundishia zinazingatia changamoto zinazotumika kusaidia kusuluhisha shida za kibinadamu za kawaida. Wakati hutumiwa kuchambua na kutatua matatizo yanayobainishwa kupitia utafiti na kufikiria suluhu za matatizo hayo.

Wakati lugha nyingine inapofundishwa, mbinu tatuzi ni njia muhimu ambazo zinaweza kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi. Mbinu hizi zinahusisha zile njia za kufuatilia nyenzo kadhaa kujifunza ili kuongeza ufanisi wa mchakato wa kujifunza. Kwa mfano,

Ufundishaji wa Kihisia ambapo Mbinu hiyo huonyesha dhima ya mawasiliano ya kipekee wakati mazingira ya kufunza somo hilo. Kichocheo kikuu ni kwamba wanafunzi wanapaswa kujiingiza katika hali halisi za mawasiliano. Wanafunzi wanajifunza kupitia majadiliano, shughuli za kikundi zenye shughuli juu ya kuwasiliana ambayo yanajumuisha kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma. Hii inawezesha wanafunzi kuimarisha ujuzi wao kuhusu somo linalofundishwa katika maisha halisi, na hivyo kuwapa ujasiri wa kutoshakulingana na mazingira tofauti. Pili, Mbinu ya kujifunza kote ambapo wakitumia njia hiyo, wanafunzi wenyewe wanafanya zoezi kwenye majukumu au miradi ambayo yana lengo la kukuza ujuzi wa lugha. Kila jukumu linahusisha jinsi ya kutumia miundo ya lugha kimawasiliano asili, kuwatia nguvu wanafunzi kushughulikia changamoto mbalimbali. Hii inawezesha wanafunzi kuzingatia namna wanavyotumia lugha kwa mazingira ya matumizi halisi, na kuwawezesha kujifunza kutoka kwa makosa na uzoefu wao. Sababu iliyo nyingine huhusu Ushirikiano wa Kijamii na Utamaduni ambapo umuhimu wa muktadha wa kijamii na utamaduni unaotumika wakati masomo ya lugha nyingine yanasisitizwa. Wanafunzi husoma lugha sio tu kupitia sarufi na leksimu, bali pia wanajifunza kuhusu tamaduni zinazohusiana na lugha hiyo. Mbinu hii inajumuisha matumizi yenye zana zakufundishia kwa mfano filamu, muziki, na fasihi ya utamaduni wa lugha inayojifunzwa ili kuongeza uelewa ulio kwa wanafunzi na wakati wanapojifunza chumbani. Hii inawasaidia wanafunzi kuelewa si tu lugha, bali pia mifumo ya kimasomo ambayo yanahusiana na lugha hiyo. Kwa kutumia mbinu hizi tatuzi, ili wanafunzi wanaweza kupata tajriba ya lugha nyingine inayowafanya wajisikie kuwa na nguvu, wenye uelewa na kufurahia muundo wa kimasomo.

2.4.4 Ufundishaji wa udadisi

Mifumo hii ya kielimu unahusishwa na kujifunza kupitia kutatua matatizo. Wanafunzi wanajifunza kwa kuangazia masuala au matukio. Wakiuliza namna ya kutoa jawabu kivyao na peke yao, na/au wakizingatia msaada wa wenzao kwa ajili ya kufikia maamuzi kuhusu mambo mahsusi au matukio wanayokabiliana nayo.[37].

Ujifunzaji wa kudadisi ni mbinu inayosisitiza umuhimu wa wanafunzi kuchunguza, kufikiri kwa kina, na kutafuta maarifa mapya kupitia maswali na majaribio. Katika muktadha wa kusoma masomo ya lugha mengine, hivyo hii inachangia pakubwa katika kuimarisha uwezo wa kutumia lugha kiufundi na kimantiki. Ujifunzaji wa kudadisi

Ujifunzaji wa kudadisi unasisitiza kuwa wanafunzi wanapaswa kuwa na kazi muhimu ya kusoma. Badala ya walimu kutoa habari zote, wanafunzi wanatumia maswali, tafiti, na shughuli za kudadisi kupata maarifa. Wanafunzi wanajifunza kwa kurejelea njia za zkudadisi ambamo wanachunguza maswali yao wenyewe kuhusu lugha, utamaduni, na hali halisi zinazowazunguka. Katika namna hiyo haswa, Wanafunzi huanza kwa kuchagua maswali ya kudadisi ambayo yanawavutia, yanayohusiana na lugha wanayojifunza au muktadha wake.

Wanafunzi hufanya masomo ya kiundani kupitia kazi kadhaa mkiwemo machapisho, vijitabu, majarida, filamu, na mahojiano. Hapa, wanatumia lugha wanayojifunza kwa kusoma, kuandika, na kuzungumza. Wanafunzi wanajenga uelewa mpya na wanashiriki katika majadiliano ya kikundi ili kubadilishana mawazo na kuimarisha maarifa yao. Aidha, Wanafunzi wanatathmini matokeo ya kudadisi yao na kufanyakazi kurekebisha

---

[37] Hakverdi-Can M na Sönmez D katika tafiti zao zilizochapishwa mwaka 2012, walichunguza jinsi ya kubuni mazingira ya ujifunzaji yanayosaidiwa na teknolojia katika muktadha wa kujifunza kupitia utafiti. Hacettepe University, College of Education, *Turkey Science Education International* 23, (4), 338-352

uelewa wao. Ujifunzaji wa kudadisi wakati wa kusomesha lugha inayofuata na umuhimu wake hasa kujenga uelewa unaoongoza mazungumzo. Kwa kujishughulisha na maswali, wanafunzi wanajifunza kuweza kuonyesha namna wanavyotumia lugha nyingine katika mawasiliano yanayojitokeza kiasili ili yaeleweke, halafu ikajitoa kusisitiza uelewa kisarufi na kileksimu.

Pia, Mbinu hii inawapa wanafunzi uwezo wa kuchagua mada wanazopenda, hivyo kuwafanya wajihusishe zaidi katika mazingira ya kusoma hasa kuongeza motisha yao. Wanafunzi wanaweza kufikiri kwa kina na kuunda ushirikiano kuhusu maarifa mapya pamoja na yaliyotokea enzi za kale, kwa hivyo kuimarisha uwezo wao wa kujifunza kwa njia ya muktadha. Wanafunzi wanashirikiana katika vikundi kusoma kwa kusaidiwa na wenzawo, ambao huwasaidia kuboresha lugha yao kupitia mazungumzo na ushirikiano.

Kutekeleza ujifunzaji wa kudadisi hutumia mbinu kadhaa mkiwemo, miradi ya kielimu ambapo wanafunzi wanaweza kufanya miradi inayohusishwa katika mambo yanayohusika kijamii, utamaduni wa lugha inayojifunzwa, au saikolojia ya lugha. Inaweza pia kutumia majadiliano na mazungumzo. Majadiliano ya kikundi au majadiliano ya darasani yanaweza kutekelezwa ili kuruhusu wanafunzi kubadilishana mawazo na kusaidiana. Mifano Halisi pia hueza kutumika. Kutumia mifano halisi yanayoonyesha umilisi wa lugha kwenye mazingira yanayotofautiana mkiwemo filamu, nyimbo, au vitabu, ili kuimarisha uelewa wa muktadha.

Ujifunzaji wa kudadisi wakati wa usomaji wa lugha inayofuata ili kuleta uzito wa kazi nzima ya kufundisha kwani inawapa wanafunzi uhuru wa kujifunza kwa njia inayowafaa na yenye maana.

2.4.5 Mafundisho yanayodhibiti Maudhui

Hii ni namna inayohusu mafunzo ya kupitia mbinu tatuzi, ambapo hapa mwanafunzi anapata msimamo na dhana inayoweza kuchanganuliwa. Misimamo hii inatumika kulingana na kigezo kinachohusisha kazi yote. Wanafunzi wanatambua, wanafasiri, na kuchunguza matatizo huku wakichambua mada husika wakitumia mifumo mbalimbali.[38].

Kwa kurejelea Mtaalam Duran *na* Kariuki, kazi inatoa mwanga kuhusu mfumo wa kusomesha ambao unaongozwa na maudhui hasa katika muktadha wa kusoma lugha inayofuata. Katika makala yao, *"Identifying Instructional Moves During Guided Learning,"* wanazungumzia jinsi walimu wanavyoweza kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji ili kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi zaidi. Mkakati huu unaelezea kuhusu maudhui ya ujifunzaji uliofadhiliwa kwa kudhibiti mfumo unaotumika kusomesha. Mkakati huu unahusisha walimu kutoa mwongozo ulio mfululilizo kusaidia wanafunzi, hivyo kuwawezesha kuelewa dhana ngumu zinazotumia lugha nyingine kupitia kiwango kwenda kingine. Walimu hujishughulisha na wanafunzi akiwauliza maswali na wakajibu vilivyo, halafu mfumo wa mazungumzo yanayohusishwa wakiwa pamoja, ili kuhakikisha wanaelewa yaliyomo. Pia mkakati unajenga Uelewa wa Maudhui. Walimu wanatumia mbinu za kufundisha ambazo zinawasaidia wanafunzi kuunganisha maarifa mapya na yale ya zamani. Hii inajumuisha matumizi ya mifano, picha, na shughuli ambazo zinaweza kusaidia katika kueleweka kwa dhana mbalimbali za lugha.

---

[38] Kariuki M. na Duran M. (2004) katika tafiti zao waliangazia matumizi ya Mwalimu wa Msingi wa Mbinu za Kifungamano (Anchored Instruction) ili kuwasaidia walimu wanaojiandaa kuingiza teknolojia katika mtaala.), ISSN 1059-7069 Publisher: Society for Information Technology & Teacher Education, Waynesville, NC USA

Kariuki na Duran wanashughulikia mbinu kadhaa ambazo walimu wanaweza kutumia katika ujifunzaji uliodhibitiwa, kwa kutoa mifano mbalimbali ili kuonyesha matumizi yanayotofautisha misingi ya lugha haswa maswali yanayohamasisha wanafunzi kufikiri kiundani na maudhui wanayojifunza, Walimu wanachukua jukumu la kuongoza mazungumzo ili kusaidia wanafunzi kuelewa maudhui na kuwasilisha mawazo yao wenyewe. Aidha, Mkakati huu unajumuisha ushirikiano na ushirikishwaji kwa wanafunzi wakati masomo yanapoendelea. Wanafunzi wanapaswa kushiriki katika majadiliano kuwaelekeza kushirikiana pamoja katika vikundi vidogo ili kubadilishana mawazo na kujifunza kutoka kwa wenzako. Hii itasaidia katika kujenga hali inayoweza kuwapa nafasi kusoma pamoja na kuimarisha ujuzi wa mawasiliano.

Mkakati huu una manufaa kadhaa hasa kudhibiti mifumo ya kusoma ili kuwapa wanafunzi mwongozo, walimu wanaweza kusaidia wanafunzi kuelewa maudhui vizuri zaidi. Pia, Wanafunzi wanaposhirikiana kimasomo, wanasaidia kuhifadhi maarifa wakifunzana na kubadilishana mawazo kijamii. Hii inasaidia wanafunzi kuandika vizuri wakifanikiwa kuelewa hata mazungumzo zaidi kwa kuwa wanajifunza namna inayolenga umilisi wa lugha kwenye muktadha unaofaa.

Mifumo ya kufunzia ambayo ilidhibiti wema wa maudhui kama ilivyoelezwa na Kariuki na Duran (2004) unaleta manufaa makubwa katika utafiti na kufundisha hiyo lugha fuatizi. Kwa kurejelea namna tofauti ya kufundisha ambayo inaweza kuimarisha uelewa wa wanafunzi, walimu wana uwezo wa kusaidia wanafunzi kufikia lengo lao la kufunzia matumizi ya lugha kiufanisi.

2.4.6 Mafundisho ya kushiriki

Hii inatoa mwelekeo wa elimu unaohimiza wanafunzi kushirikiana na wenzao ili kufikia malengo maalum ya kujifunza, Nyanda (keshatajwa). Kutumia mbinu hii

kunahitaji wanafunzi hufanya mazoezi yenye shughuli za somo katika vikundi au kwa kushirikiana kama darasa lote. Kufundisha kiushirika ni mbinu inayowezesha wanafunzi kujifunza kupitia muktadha halisi na mifano halisi, na kusaidia katika kuelewa dhana ngumu kwa njia ya kushirikisha na kuhakikisha kuna uhusiano kati ya mawazo na hali halisi. Kwa kuzingatia kufundisha lugha nyingine, namna hii inaweza kunufaisha pakubwa kwa kuwasaidia wanafunzi kupata uwezo wa kutosha juu ya lugha hasa namna ya kutumia teknolojia.

Ujifunzaji wa kiushirika unahitaji wanafunzi kujifunza katika muktadha halisi. Hapa, wanajifunza kwa kutumia hali ambazo ziko karibu na maisha yao, hivyo kufanya maudhui kuwa ya maana na rahisi kueleweka. Wanafunzi wanatumia mifano zaidi, iliyo na uwezo wa kueleweka kama masimulizi, picha, au hadithi, ili kuunganisha maarifa wanayojifunza na hali halisi. Hii inasaidia kujenga mwelekeo wa mawazo na uelewa ambao unakuza uelewa kupita somo la lugha hiyo. Wakati lugha inapofunzwa, mafunzo ya pamoja yanaweza kuhusisha matumizi ya teknolojia. Hapa, wanafunzi huenda wakavitumia vifaa kama kompyuta, vidio, na programu za kujifunzia ili kuimarisha mchakato wa kujifunza. Ujifunzaji wa kiushirika unawahimiza wanafunzi kutafuta na kutumia rasilimali mtandaoni, kurasa za wavuti, Mitandao ya tovuti, na hata mifumo ya kielektroniki katika mchakato wao wa kujifunza.

Hii mbinu ya Kiushirika ina faida muhimu wakati wa matumizi yanayokuwa yanatumika sambaba wakati wa kuongeza uelewa wa maudhui. Wanafunzi wanapata fursa ya kuelewa kwa kina dhana ngumu ili zitumike kwenye muktadha halisi, hivyo kuimarisha uelewa wao wa lugha. Pia, wanafunzi wakishirikishwa kwenye mambo yanayohusiana na maisha yao halisi, wanapata motisha zaidi kujifunza na kutumia lugha mpya. Ujifunzaji wa kiushirika pia unawasaidia wanafunzi kuimarisha ujuzi wao kuweza kutamka na kuongea hata kuandika, kwani wanajifunza kutumia lugha

kulingana na mazingira yanayofaa. Wanafunzi wanajifunza kuwa makini kwa kutegemea hali ya kujifunza, huku wakihitaji kufikiria kwa kina na kutathmini hali mbalimbali na mifano.

Kwa kurejelea mkondo ulio kwenye utafiti uliofanywa juu ya kutumia teknolojia za kuhudumia kazi ya ufunzaji, wanafunzi wa ualimu wanaweza kupewa ufundisho unaosomeshwa kwa lugha fuatizi wakitumia vifaa vya kiteknolojia mkiwemo programu za kujifunza lugha za mtandaoni. Kulingana na mifumo hii, wanaweza kuchagua Mifano halisi kama vile kuangalia machapisho ya mitandaoni yanayotumia ile lugha ya kutoa ripoti, au kuandika insha yenye uwezo wa kilugha katika hali zao. Pia, Wanaweza kuunda vikundi vya kujadili na kubadilishana mawazo yanayolenga kutumia teknolojia katika kujifunza lugha, ambapo kila mwanafunzi anatoa mchango wake. Kila mwanafunzi anaweza kuunda mfano wa kipekee wenye kutumia mbinu za teknolojia kwa kusomesha zile lugha kuwasilisha kwa wenzao.

Kwa ujumla, ujifunzaji wa kiushirika una hatua muhimu kwa kuimarisha ujuzi unaochukuliwa na wanafunzi kusoma hiyo lugha nyingine, hasa kwa kutumia teknolojia na muktadha halisi.

2.4.7 Mafunzo ya kuimarisha zamu

Hii huwasilisha njia ya kusoma kwa ushirikiano ambapo wanafunzi wanachukua majukumu kutoka kwa anayewafundisha kwa zamu. Hiyo ni mbinu inayotumika kuimarisha masomo ikielekezwa kulingana na matarajio ya sekta inayoshughulikia mambo ya elimu kuendeleza sifa za ushirikiano (makundi), uongozi, mikakati ya kuwasiliana kwao wenyewe na hata kuifanya kuwa bora mambo yote yanayohusika kwenye mtaala wa masomo.[39] Njia hizo zinazotumika katika ufundishaji zinaimarisha

---

[39] Enamul Hoque (2017). *An Introduction to the Second Language Acquisition.* (pp.1-23). EDRC, Dhaka, Bangladesh

uelewa wa lugha fuatizi hata zinakubaliana na maelekezo ya kimtaala unaosisitiza umilisi.

Ujifunzaji marika kwa zamu *(Alternating Instruction)* hutumia mfumo wa kufundisha unaoelekeza katika kubadilisha namna ya kufundisha kwa kiambatanisho cha kujifunza, ili kuboresha uelewa unaotakikana kwa wanafunzi. Wakati wa kusoma lugha fuatizi, njia hii inaweza kusaidia katika kukuza mahusiano ya kisarufi, ujuzi wa kuzungumza, kuongea, kutumiwa na wanafunzi.

Katika ujifunzaji marika kwa zamu, namna ya kufundisha inabadilishwa baadaya ya kipindi Fulani kwa sababu ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata mtazamo tofauti juu ya maudhui wanayojifunza. Jambo hili husababisha mchanganyiko wa masomo ya ndani, kujifunza kwa ushirikiano, unaohusisha kutumia teknolojia.

Mbinu hii inasaidia Wanafunzi Kujifunza kwa Ufanisi. Wanaweza kupokea maelekezo tofauti kuhusu lugha kupitia mbinu kadhaa ambazo huweza kuwa zikawa kazi za pamoja, maswali ya wazi, au shughuli za vitendo. Pia, mbinu hii inawasaidia wanafunzi kuunganishwa kwa kutumia mawasiliano katika muktadha tofauti, ili kuwezesha msisitizo wa kujua lugha vizuri. Kwa kuzingatia mbinu hii wanafunzi wanapewa nafasi ya kufanya mazoezi wakishirikiana, kubadilishana mawazo na kujifunza kutoka kwa wenzako. Usanidi huu wa ushirika unaongeza msisimko wa kujifunza na ushirikishwaji wa wanafunzi.

Ujifunzaji marika umepata ushawishi kutoka kwa waasisi mbalimbali katika elimu, ingawa haupewi kuhifadhiwa kwa kitaifa tu kutumika na mwanafunzi wa kipekee au kundi. Baadhi ya waasisi muhimu na dhana zao ni kama vile Jean Piaget aliyejulikana kwa nadharia yake iliyohusu mkondo wa kisaikolojia, akisisitiza umuhimu wa hatua za

maendeleo ya kibinafsi kwa mazingira ya kufundisha. Piaget anasisitiza kwamba wanafunzi wanajifunza kupitia kuchanganya habari mpya na maarifa waliyokuwa nayo tayari. Mwingine alikuwa Ellis (keshatajwa) ambaye alisisitiza umuhimu wa mikutadha iliyo ya wanajamii katika kujifunza. Kazi yake ya *"Zone of Proximal Development"* inachangia kwenye wazo la ujifunzaji marika, kwani wanafunzi wanaweza kuunganishwa na wenzao wakubwa katika kuelewa dhana ngumu.

David Kolb alitengeneza mhemko wa kujifunza wa kinadharia ambao unadhihirisha mfumo unaotumika kufundisha kama mzunguko wa hatua nne: mazoezi ya mfululizo, kutafakari, dhana na majaribio. Mbinu hii inatumika katika ujifunzaji marika kuwasaidia wanafunzi wanaohimiza kujifunza kupitia hatua zilizobadilishwa.

Mtaalamu mwingine alikuwa Howard Gardner aliyeendeleza nadharia ya *intelligences* nyingi, akisema kwamba wanafunzi wana mitindo tofauti ya kujifunza. Mbinu ya kujifunza marika inachangia hii kwa kutoa njia tofauti za kujifunza.

Ujifunzaji marika kwa zamu katika mafunzo yanayoshirikisha lugha fuatizi hudhihirisha dhima ya kukuza uelewa wa wanafunzi. Wanafunzi wanapobadili mbinu za kujifunza, inawasaidia kujenga uelewa zaidi jinsi wanavyostahili kutumia lugha kwa hadhira mbalimbali. Wanafunzi pia wakishirikishwa kwenye mazoezi ya kitaaluma, wanajifunza kuzungumza na kuandika kwa ufanisi zaidi, huku wakijenga ujasiri katika kutumia lugha hiyo. Mbinu hii inawasaidia wanafunzi kugotoa shida wanazokutana nazo kwa kutafuta mbinu tofauti za kujifunza zinazoendana nao.

Ujifunzaji marika kwa zamu unatoa mbinu zinazofaa kwa kufanya mafunzo ya lugha fuatizi vizuri kutoa mchanganyiko unaotumia njia kadhaa kufunzia. Hii inawasaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi, kuongeza ujuzi katika mazungumzo ili kujenga mazingira yenye kujenga ushirikiano.

2.4.8 Mbinu ya mafundisho ya kufanya vitendo

Kuna mbinu ya ufundishaji nyingine ambayo huwa ya kufunzia kimfululizoikijulikana kama ufunzaji wa vitendo (UV). Ufunzaji wa UV una muundo maalum unaokusudia kuwezesha ujifunzaji wa haraka na kuwafanya wanafunzi kuelewa lugha vizuri katika somo na kuboresha stadi za kimsingi. Mbinu ya UV ni muhimu hasa katika muktadha ambapo wanafunzi hawana tajriba ya kutosha kuchambua Makala na hawatumii lugha inayotumika darasani katika hali nyingine. Mbinu hii ilianzishwa katika makala ya Rosenshine[40]. Kazi hii ilitafitiwa kwa sababu ya kudhihirisha ufanisi na umuhimu wa mbinu hii kwa mafunzo ya wale watoto wanaosoma lugha hiyo wailinganishe wenyewe kuliko wenzao ambao hawakufundishwa kupitia mbinu hizo. Walimu walipatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutumia njia hii, na baadaye, mbinu hizi zilichambuliwa ili kupima ufanisi wake. Hatimaye, mbinu ya UV ilionesha ufanisi mkubwa. Hiyo njia inayozungumziwa inayotumia vitendo (UV) inazingatia mambo kadhaa:

a) Ujifunzaji katika hatua fupi, zikijumuisha kazi zinazofanywa na wanafunzi kulingana na hali zao.
b) Kuwaelekeza wanafunzi katika kushiriki katika shughuli za kikazi za mwanzo.
c) Kusisitiza kila mwanafunzi anapata kazi zinazomfaa kwa kiwango cha juu. Wakati wa kusomesha mkondo huu wa mafunzo, anayefundisha anapaswa kuzingatia mambo kadhaa kama yanavyoelezwa hapa chini:

i. Kueleza dhima ya ustadi.
ii. Kuonyesha kinagaubaga vile ustadi huweza kufunzwa.

[40] Rosenshine, B. (2007) katika kitabu chake "Systematic Instructions," kilichohaririwa na T. L. Good katika "21st Century Education: A Reference Handbook," anatoa mwanga juu ya mbinu za ufundishaji zinazotumia mipango madhubuti ili kuboresha ufanisi wa kujifunza. Rosenshine anajadili jinsi mbinu zilizopangwa zinaweza kusaidia wanafunzi kwa kutoa muundo wa kimahesabu wa ujifunzaji, kuanza na maelezo ya wazi na hatua zinazoweza kufuatwa.

iii. Kutoa mazoezi ya mwongozo unaohusu ustadi ili wanafunzi wawe makini.

iv. Kuchunguza kiwango cha uelewa na kutoa marekebisho ya kujenga.

v. Kutoa mazoezi mengine zaidi.

vi. Kutathmini namna ya kufundisha mwisho wenyewe.

Namna hii inayotumika kufundisha kwa kufanya vitendo (UV) inahusisha kukuza ustadi kupitia yale maelekezo ya anayefundisha. Kwa kuzingatia makundi madogo yanayoelekeza moja kwa moja kusisitiza malengo ya mwalimu[41] aliyeandaa vikao vinavyofaa kuhakikisha kila mada inafundishwa kimpangilio, kikamilifu, kitaratibu hadi mwisho kwa ukamilifu. Kwa kurejelea mkondo huu wa UV, yale maneno yaliyofafanuliwa yalikuwa yakieleweka yenye mantiki, yakilenga stadi muhimu mbalimbali ambazo zinapangwa na kuwasilishwa kwa ufanisi ili kusiwe na stadi muhimu zinazopuuziliwa mbali. Ploti ya ufafanuzi huwa inapaswa kueleweka vizuri halafu kuongozwa na mafunzo yaliyotokana na kazi za kiutafiti zilizofanywa. Mbinu zinazotumiwa na mwalimu zinapaswa kuendelezwakwa uzoefu moja kwa moja kwa kuanza na hizo zilizo ngumu na nyingine zinazoeleweka. Kwa hivyo, kwa kuzingatia njia hiyo, ni bora anayefundisha kuwapa wanafunzi fursa ya kutumia shughuli za uzoefu wake walizojifunza, pamoja na kutoa marekebisho ya kujenga.

Amri zinazotawala matumizi wa njia za kufundishia ni ile ya kufanya vitendo (UV) kama inavyosemwa na Naik (2013) ni:

i. Zile tungo zinazojitokeza kwenye mifumo inayozungumziwa kawaida zinapaswa kufundishwa kwanza, wakati inapoonyesha kanuni za lugha zinazotawala usomaji na hufundishwa baadaye.

---

[41] Carnine, D (2000). *Why Education Experts Resist Effective Practices (And What It Would Take To Make Education More Like Medicine).* University of Oregon, January 2000

ii. Ile tajriba ya kusikia halafu ya kuzungumza zinakuza matumizi ya kuuliza swali kwa jibu mbele ya mwanafunzi.
iii. Sarufi inafundishwa kwa muktadha.
iv. Msamiati ambao haueleweki kwa wanafunzi kwa wakati huo huwasilishwa kwa kutajwa.
v. Maneno ya kijina yanayofundishwa yakitumia njia za kuonyesha, vifaa halisi, na picha, huku maneno yaliyo ya bandia ukihusishwa na dhana tofauti.
vi. Uzoefu unaozingatia maongezi haswa unakua.
vii. Matamshi sahihi na sarufi yanasisitizwa.
viii. Wanafunzi wanapaswa kushiriki kwenye mawasiliano ya kiwango cha 80 katika wakati uliotengwa kwa ajili ya kikao hicho.
ix. Wanafunzi wanapewa mazoezi ya kuhusika katika uulizaji wa maneno magumu na hata majibu yao.

Wakati wa kufunza umegawanyika kwenye kategoria kadhaa:

a) Kifunguzi
b) Kiwiliwili
c) Mwisho

Sehemu hiyo ya kwanza ni ufunguzi ambao anayefundisha wanafunzi huandaa mikutadha inayofaa kwa ajili ya masomo. Katika sehemu ya kiwiliwili, anayefundisha aanajaribu kuonyesha mambo yaliyo muhimu katika kikao hicho pamoja na kutoa ufafanuzi wa kutosha na hata vielelezi vinavyofaa. Katika sehemu ya mwisho, wakati unaisha kwa kutoaa ufupisho wa yale yote yaliyofundishwa. Kisha, wanafunzi hupewa kazi mbalimbali kudhihirisha matumizi ya tajriba inayofundishwa kwa wanafunzi na

wakizielewa vilivyo bila kusaidiwa na kiongozi wao. Kuchanganua kunasaidia kutambua nguvu zao za kujifunza, kama inavyolingana na Carnine, (2000).

Mkakati wa Carnine (keshatajwa) unaangazia changamoto zinazokabiliwa na wataalamu wanaoshughulikia masomo ya kielimu kwa kuzingatia njia mwafaka zinazoendeleza kufundisha, hasa wakizingatia mazingira ya kufunza hiyo lugha fuatizi. Katika makala yake yaliyozungumzia kwa nini wataalam wa elimu wanapinga mazoea Madhubuti na hatua zipi zinazoweza kuchukuliwa ili kufanya elimu kuwa kama taaluma za tiba. Carnine anabainisha sababu kadhaa za upinzani katika kuingiza mbinu zinazothibitishwa kuwa na ufanisi katika elimu. Carnine anataja kuwa wataalamu wa elimu mara nyingi wanakataa mbinu ambazo zimejaribiwa na kudhihirishwa kuwa na ufanisi katika kufundisha. Hii inatoka kwenye mitazamo ya kiutamaduni, imani za kibinafsi, maendeleo yanayodhihirika kisiasa na mwisho wake yakaathiri hali ya elimu. Wataalamu wengi wa elimu hawana uhusiano unaoeleweka wazi wazi kielimu, jambo ambalo linapelekea kutokuangalia maelezo ya kisayansi yanayoonyesha ufanisi wa mbinu fulani za ufundishaji. Carnine anashauri kwamba wanataaluma wanahitaji kuunganisha utafiti unaotumia sayansi ili kuboresha mazoea yao ya kufundisha. Akiangazia historia ya elimu, Carnine anasema kuna mifano mingi ambapo mazoea yasiyo na ufanisi yameendelezwa katika wakati mwingi licha ya kudahiliwa kuwa sio bora. Jambo lenyewe linadhihirisha kwamba hata kama kuna ushahidi wa kimataifa, ushawishi wa zamani bado unaweza kutawala. Utekelezaji wa mbinu bora unahitaji sera na mwelekeo thabiti ukitolewa walio na majukumu ya kuongoza elimu. Carnine anasisitiza dhima ya kuwepo kwa sera zinazojenga mbinu zilizo na ufanisi na kuondoa vikwazo vinavyoweza kuzuia mabadiliko.

Kwa hivyo, Carnine anashauri kuwa elimu inapaswa kufuata mifano ya sayansi ya afya ambayo inategemea utafiti na ushahidi. Kila mabadiliko ya mbinu ya ufundishaji

yanapaswa kuungwa mkono na utafiti wa kisayansi ili kuwa na maana. Anasisitiza pia kutoa mafunzo, rasilimali, na msaada kwa walimu ili waweze kutekeleza mbinu bora za ufundishaji. Hii inajumuisha kuongozwa na wataalamu wa elimu walio na ujuzi katika mbinu zitumikazo. Carnine anaelekeza kuunda mazingira ya shule ambayo yanahimiza uvumbuzi na kufikiri kiundani juu ya namna ya kufundisha, na kuchochea mabadiliko endelevu katika mazoea ya kitaaluma.

Aidha, anapendekeza ushirikiano kati ya wataalamu wa elimu na wanachama wa jamii, kwa sababu ya kwamba muungano thabiti wa kufanikisha kubadilisha mifumo inayotumika kielimu ni ya kuhakikisha kwamba yale mambo yanayohitajika na wanafunzi yanatimizwa. Mkakati wa Carnine (keshatajwa) unasisitiza umuhimu wa kutafakari upya jinsi elimu inafundishwa na kuimarisha mazoea ya ufanisi wakati wa kufunza somo la lugha fuatizi. Kwa kuzingatia mazingira ya ufunzaji wa somo la lugha hiyo, inakuwa muhimu kutoa mbinu zinazoendana na utafiti wa kisayansi ili kuboresha matokeo ya wanafunzi. Utekelezaji wa maoni haya unahitaji ushirikiano kutoka kwa walimu, waamuzi wa sera, na jamii kwa ujumla.

Utafiti huu ulifafanua, kubainisha, na kujadili jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoingiliana katika mafunzo ya lugha husika ya Swahili kupitia miundo ya kifonolojia, kimofolojia, na kisintaksia (virai, vishazi, na sentensi). Hata hivyo, utafiti huo ulileta mbinu mbalimbali zilizotumiwa kusaidia wanafunzi wanaoathiriwa na Kinyankore wakati masomo ya lugha husika inapokuwa inafunzwa.

2.5 Mitazamo ya kisera katika nchi ya Uganda

2.5.1 Maana ya sera

Neno "sera" linatazamwa kama sheria, udhibiti, utaratibu, hatua ya utawala, motisha, au mazoezi ya hiari ya serikali na asasi. Wasomi wengine wanaona sera kama dhana

inayotumika ambayo inaweza kubadilisha shughuli za usimamizi zinazoendelea. Wengine wanaielezea kama njia au njia mahususi ya utekelezaji inayoegemezwa hasa na busara kwa ajili ya ustawi wa kimwili. Fasili ya "sera" inatofautiana kwa kurejelea mabingwa wa taaluma kadhaa, lakini kwa ujumla inahusisha mpango au mwelekeo wa hatua zinazochukuliwa na asasi, serikali, au mashirika katika kukabiliana na masuala maalum, Masereka (2020).

Masereka (keshatajwa) kwamba sera ni "yoyote ya hatua ambayo inafanya taarifa za serikali kuhusu shughuli za umma". Jambo hili hudhihirisha kwamba sera ni njia ambayo serikali inatekeleza majukumu yake. Masereka (keshatajwa) anasema "sera ya umma huwa na mtazamo unaosaidia kuunda, kutekeleza, na kutathmini maamuzi rasmi yaliyowekwa na serikali". Hii inatoa mtazamo wa mchakato mzima wa sera. Nyanda (keshatajwa) Katika mtazamo wake, anafafanua kuwa sera inategemea "mchanganyiko wa matatizo, suluhisho, na fursa za kisiasa". Hii inaonyesha umuhimu wa mazingira yanayojitokeza kukiwepo sera inayofaa.

Nyanda (keshatajwa) anabainisha kwamba sera ni "mwelekeo wa kawaida wa hatua au uamuzi uliofanywa ili kutatua tatizo fulani". Pia, hili linathibitisha kuwa kuna sababu ya kukumbana na shida zinazokabili jamii.

Kila mtazamo huu unatoa uelewa tofauti na vile unavyofasili sera, lakini wote wanakubaliana juu ya umuhimu wa sera katika uamuzi wa kisiasa na usimamizi wa kijamii.

Kwa hivyo, fasili ya sera huweza kuwa mitazamo inayochujwa na kukubakiwa ikachukuliwa kama msimamo rasmi ulio na uwezo wa kutumika kama sharia. Sera inakuwa kama uamuzi ulio rasmi wenye nguvu na ushabiki wa serikali kuthibitisha kwamba umetekelezwa na afisi zote husika kwa hata mtumiaji wa kibinafsi. Huo

ulikuwa mfano mzuri wa kuongoza kirasmi namna ya kuzingatia matendo ya shabaha yaliyokubaliwa.

2.5.2 Utekelezaji wa mifumo ya lugha

Mabingwa wa lugha wanafasili Sera inayoshughulikia lugha kuwa kipengele muhimu katika masuala yanayohusu mtindo wa mafunzo ya lugha pamoja na utamaduni, na inafafanuliwa na wataalam mbalimbali kufuatia njia zisizofanana kama wanavyonukuliwa hapa chini.

Kulingana na Masereka (keshatajwa) anasisitiza kwamba "sera ya lugha ni mchakato wa kutambua itakuwa lugha gani inayopaswa kutumika katika maeneo mbalimbali katika elimu, serikali, shughuli za mawasiliano nakadhalika". Hii inaonyesha nafasi inayotakikana kudhihirisha hali ya lugha kwenye sekta mbalimbali za kijamii.

Naye Ellis (keshatajwa) anafafanua dhana ya sera inayohusu lugha kuhusisha ushirikiano kati ya siasa na lugha, na mara nyingi ina mwelekeo wa kuimarisha nguvu za kisiasa au kiuchumi za makundi fulani". Hii inaonyesha jinsi mfumo wa lugha unavyoweza kuathiri uhusiano wa nguvu katika jamii.

Kulingana na watalaamu waliotajwa hapo juu wanasema kwamba mfumo wa kisera unaoshughulikia lugha huwa na mipango rasmi na isiyo rasmi inayohusiana na matumizi na udhibiti wenye mamlaka ya kuchunga matumizi ya lugha za jamii". Hii inaonyesha kuwa mifumo hiyo ya kisera inayohusisha lugha inajumuisha mbinu zote za utawala wa lugha.

Watalaamu wengine kama Rettig na Canady (1996) wanafafanua mfumo wa kisera unaohusu lugha kama "maamuzi juu ya matumizi, maendeleo, na ulinzi wa lugha katika jamii fulani, ikijumuisha zile lugha katika bara la Afrika na za kikabila". Anaangazia dhima ya hizo lugha ili kufikia malengo ya utamaduni na jamii.

Yeye Cozy (2012) anabaini kuwa mifumo ya kisera inayoshughulikia lugha inahusisha mbinu za kulinda na kukuza lugha za asili na za wachache wakati wa mikutadha inayohusisha mataifa yanayoleta changamoto za lugha". Jambo hili linadhihirisha dhima ya kulinda lugha ambazo zinaweza kuwa katika hatari.

Fasili hizi zinaonyesha kwamba mifumo ya kisera hiyo inayoshughulikia lugha huwa na mchakato mzito unaohusisha maamuzi, mipango, hasa mazingira ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Inahitaji kuzingatia mambo yanayojitokeza katika maeneo husika pamoja na masuala ya utamaduni na utawala.

2.5.3 Mfumo wa kisera nchini Uganda

Uganda ni taifa lenye lugha nyingi kama nchi nyingi za Kiafrika. Mfumo huu wa kisera katika elimu nchini Uganda umeundwa kulingana na mtazamo mmoja, (Karoro 2001). Kwa kuzingatia shule zilizo chini kama za kimsingi huko vijijini, sera inashauri matumizi ya lugha tangulizi kuwa ndiyo lugha ya kimasomo kwa miaka minne inayotangulia ya kielimu. Muda wa miaka kama minne ilipopita kunaingizwa lugha ya kingereza inayoanzishwa hapo kuwa namna ya kufundishia. Kuna njia nyingine katika maeneo ya mijini, mfumo wa kisera unapendekeza shule zitumie lugha ya kimombo kutokana na wingi wa lugha katika maeneo hayo. Katika hali zote sera inalenga Kingereza kuwa lugha inayotumika kufunzia wanafunzi na hata kutunga na kufanyia mitihani. Ukiritimba huu wa Kingereza unahusiana na uanuwai wa hali zinazokuwa kadhaa kama vile; urithi wa ukoloni wa nchi, thamani inayoambatanishwa na lugha za kikanda na za kienyeji ndani katika sehemu za umma, na umilisi wa Kingereza ndani ya maswala ya mwingiliano ya kimataifa. Baadhi ya watendaji huchukulia lugha nyingi nchini Uganda kama kipindi kipya cha lugha; juu ya kuongezeka kwa athari za kina na pana, zinazoendelea katika mazingira yanayofaa uthabiti kwa utandawazi na kipengele cha asili cha jamii ya binadamu ambacho kina dhima teule katika utendaji wa vipengele

vikuu vya muundo wa kijamii (Karoro 2001, keshatajwa). Waigizaji wa "kijadi" katika hali kadhalika, wanakuza Kingereza nchini Uganda kwa sababu wanadai Kingereza ni ufunguo wa elimu bora, lugha ya mitihani ambayo inadhibiti kuingia katika viwango vya mfululizo vya mtazamo unaoongoza mafunzo ya kielimu nchini Uganda wenye ushindani mkubwa na huwa na umuhimu wa kutokea fursa tele za kikazi. Wote waliotajwa hapo juu wanawakilisha Kingereza kama "mtaji wa lugha" nchini Uganda. Mtaalam Karoro anathibitisha kwamba uchaguzi wa lugha hufanywa ili kutoa uwezekano wa siku zijazo.

Kulingana na nchi nyingine za Afrika hasa zile za upande wa mashariki na kote duniani, Kiingereza, nchini Uganda huhusisha mambo yanayoelekeza sayansi na teknolojia, ya nafasi za kazi, ya kuvuka mipaka na mawasiliano ya kimataifa na biashara ya serikali.

Sawa na Waafrika wengi, Waganda pia wanahamahama na hawabaki kwenye sehemu za "kabila" au mahali pa kuzaliwa (Masereka 2020). Kwa hivyo ingawa makabila yanatawala katika maeneo fulani, yanapatikana pia katika maeneo mengine. Zaidi ya hayo, wingi wa lugha badala ya lugha moja ndio utawala unaotawala, kama ilivyoonyeshwa kwa sehemu nyingine za Afrika (Masereka 2020)[42]. Tangu enzi za ukoloni Kiingereza imekuwa lugha ya uhamaji wa kijamii na kiuchumi. Hata leo, ambapo ni zaidi ya miaka hamsini nyakati zilizofuatia kupata uhuru wa Uganda, ujuzi wa Kiingereza bado ni hitaji la kupata ajira kwenye asasi za umma (Karoro 2001). Basi, ikitakiwa kwamba mtu aendelee maishani lazima aweze kuwa na uelewa wa kimombo ili kufanya kazi wa yoyote ile. Hata hivyo, Waganda wanatakiwa kushindana na angalau zile teule kama tatu zilihifadhiwa nafasi ya urasmi kwa taifa zima. Kiswahili

[42] Masereka, (2020) Keshatajwa

ikiwa ni lingua franka ikijulikana kuwa lugha inayokamilisha mazungumzo mapana katika mataifa yote ya Afrika mashariki huwa lugha moja ya ndani[43].

Ssekamwa (2000) anafafanua kuwa wingi wa lugha hauleti tofauti bali hurahisisha utangamano kwenye ujenzi wa kuimarisha matumizi ya lugha nyingi na tamaduni nyingi ili mradi kanuni za demokrasia, uvumilivu na kuishi pamoja kitamaduni zikubaliwe kama miongozo.

Mfumo wa kisera unaoshughulikia maswala ya lugha yalizungumziwa katika mkakati rasmi wa Uganda mwakani 1992 kuhusu elimu. Kwa kuzingatia sera hiyo ya elimu ya Uganda, chanzo cha mafunzo ya kielimu huanzia ngazi ya kwanza mpaka ngazi ya saba. Ni wazi kutoka kwa Waraka wa Serikali ya Uganda wa 1992 kuhusu Elimu (UGWPE)[44] kwamba lugha inayounganisha na kusababisha ukuaji wa kitaifa ni Kiingereza. Lugha mama zinapendekezwa kutumika katika elimu, si kuwa namna inayotambua utofauti wa lugha nyingi bali kama nyenzo ya kutayarisha ufundishaji bora kupitia hiyo lugha iliyo ya kimombo. Katika mapendekezo yote katika UGWPE, Lugha mama zitatumika zikiwa namna iliyo ya maelekezo hadi darasa la nne na elimu nyingine nchini Uganda inapaswa kutolewa kupitia Kingereza. Kiswahili kilipewa hadhi maalum kama moja wapo ya lugha teule nchini. Ibara ya 6 (2) ya Katiba ya Uganda inasema "Kiswahili itakuwa lugha ambayo ni rasmi katika nchi nzima ili iweze kutumika katika mazingira ambayo Bunge linaweza kuamuru na sheria".

[43] Waraka wa Serikali ya Uganda wa 1992, uliopewa jina rasmi "The White Paper on the Education Policy Review Commission," ulikuwa waraka muhimu unaoelezea dira na mageuzi ya serikali kwa sekta ya elimu nchini Uganda. Mada hiyo ilikuwa ni jibu la mapitio ya kina ya sera ya elimu yaliyofanywa na serikali ya Uganda, ambayo yalilenga kutatua changamoto na udhaifu katika mfumo wa elimu uliojitokeza kwa miaka mingi, hasa kufuatia misukosuko ya miaka ya 1970 na 1980.

[44] Waraka wa Serikali ya Uganda kuhusu Elimu wa 1992 ulikuwa muhimu katika kuunda mazingira ya elimu ya Uganda na uliweka msingi wa sera na mageuzi ya elimu yaliyofuata, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Elimu ya Msingi kwa Wote mwaka 1997. Ulionyesha mabadiliko makubwa kuelekea mfumo wa elimu jumuishi zaidi na sikivu unaolenga kukuza. maendeleo ya taifa.

2.6 Misingi ya Nadharia

Wataalam wengi mkiwemo Massamba (2004) anavyonukuliwa na Msanjila (2006), wameelezea dhana ya nadharia kama utaratibu, kanuni, na misingi zilizoundwa katika muundo wa kimawazo, zikiwa na madhumuni ya kutumika kama kielelezo cha kuelezea jambo fulani.

TUKI (2013) wanasema mifumo huweza kufasiliwa kuwa wazo, fikra, ufafanuzi, miongozo iliyowekwa kuboresha maelezo na kusuluhisha utekelezaji wa mambo husika. Mdee (2011) alisisitiza kuwa mkakati wa kinadharia kuwa muundo unaotumia maumbo ulioandikwa kwani kutoa mwongozo kuhusu namna ya kutekeleza jambo.

Utafiti huu unatumia mfumo wa kinadharia kama muundo wa kimitazamo, dhana, au kanuni ambazo zinaongoza mtafiti kuhusu namna mazingira ya uchambuzi na utambuzi unavyokuwa. Kwa kurejelea umuhimu wake kwa sababu husaidia katika kuelewa, kuchambua, na kuelezea matukio au tatizo linalochunguzwa. Huo mfumo wenyewe unajumuisha wazo au modeli inayoweza kuwasilisha na kueleza ushirikiano uliopo kwenye vipengele mbalimbali katika tafiti tofauti. Nadharia inaweza kuwa ya kimaandiko au inaweza kujengwa kutoka kwa yale yaliyotokea kwenye utafiti uliokuwepo hapo awali. Mifano ya nadharia huhusisha ilie mikakati ya mitazamo ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi, na saikolojia. Kila moja ina msisitizo wake tofauti kutoka tofauti na inachangia katika kuelewa matatizo mbalimbali. Nadharia ya kijamii inahusisha kuelewa jinsi mambo ya kijamii yanavyoweza kuleta athari kwenye mienendo ya binadamu na uhusiano wao. Nadharia ya mfumo inatazama jinsi vipengele tofauti vinavyofanya kazi pamoja katika mfumo fulani. Nadharia ya mabadiliko ya tabia inachambua jinsi watu wanavyoweza kubadilisha tabia zao kwa kuegemea hali inayokuwepo kwao.

Kiunzi cha nadharia kinasaidia mtafiti kupanga na kuongoza mchakato wa utafiti, kuamua maelezo kuhusu utafiti ili kuchagua namna iliyotumika kukusanya data.

Mfumo wa mtazamo wa kinadharia unatoa msingi wa kueleza yaliyotokea kwenye utafiti ili kuwezesha ufahamu wa sababu na mwelekeo. Mfumo wa mtazamo wa kinadharia pia hutoa njia ya kuthibitisha nadharia au dhana zilizowekwa kabla ya utafiti.

Kwa ujumla, mfumo wa mtazamo wa kinadharia ni chombo ambacho kina manufaa Zaidi kukuza hatua zote za utafiti, kwani kinabainisha na kuratibu mbinu, maswali, na mbinu za kuchambua matokeo yaliyopatikana kutoka utafiti wowote.

Kwa hivyo, utafiti huo ulielekezwa na nadharia mseto ili kuweza kuoanisha maswala kadhaa ambayo yanadhihirika kwenye namna ya kutumia lugha ile hasa kusoma lugha fuatizi. Miongoni mwa nadharia hizo ni ile ya kuchanganua makosa na nyingine inayochanganua na kulinganisha ya Uchanganuzi-linganuzi na hata nadharia kidhi ya mawasiliano ndizo ziliongozwa.

2.6.1 Uchanganuzi Makosa

Mfumo huu wa kinadharia ujulikanao kama Uchanganuzi wa makosa ulianzishwa na mtaalam aitwaye Corder miaka ya 1967. Mtazamo huu uliibuka kukidhi upungufu uliotambulika kwenyenadharia nyingine iliyokuwa ya uchanganuzi-linganuzi ambayo uliotumiwa na wanaisimu kutofautisha kinachojulikana kama lugha inayotangulia kwenda nyingine inayotumika na mwanafunzi kwa kudhihirishia kasoro zinazojitokeza. Kuchunguza zile kasoro huonyesha njia iliyotumika ingethibitisha hasa zile kasoro zinazopatika kufuatia lugha iliyotangulia kwa mwanafunzi. Watu ambao wanajaribu kusoma lugha inayofuata hukumbana na kasoro nyingi zikiwemo matamshi mabaya ya maneno. Kwa kuzingatia mtazamo huo, mabingwa wa lugha wamejitokeza

kubainisha namna ya kuanzisha pale kasoro zinapoanzia, halafu wapendekeza njia za kurekebisha kasoro hizo. Wahadhiri wanaotia moyo kuwafikirira Watoto wakiwa wanatumia lugha hiyo wanawaelewa wakikosea. Walimu wa lugha wanaowasikiliza wanafunzi wao wakizungumza hutambua makosa. Linalojulikana kiukweli huonyesha kwamba watu wanafanya kasoro mbalimbali wakati wa kuzungumza mkiwemo na walimu wenyewe ambao pia ni wazaliwa wasemaji wa lugha hiyo hiyo. Wenyeji wenyewe wanaotumia lugha wanapuuza matumizi ya kanuni zinazoelekeza matumizi ya lugha hata zikiwa zimeandikwa kwenye kitabu au Makala. Uchanganuzi makosa, inachunguza zile kasoro zinazosababisha kasoro hizo hizo. Tukichagua kurejelea Mwanaisimu Corder, mtafiti alifuata mambo kadhaa kuchanganua kasoro hizo:

i) Kukamilisha mkusanyiko w sampuli zifaazo kudhihirisha wasomao wa L2. Kupatikana kwa kasoro za kikanuni katika matokeo ya wanafunzi yalikusanywa kutoka kwa hojaji zao na kulingana na vile walivyotumia lugha.
ii) Kutambua makosa. Zile kasoro ambazo ziliweza kutambuliwa kwa kupigiwa mstari.
iii) Kufafanua kasoro. Kasoro hizo zinapelekwa kutunga tungo halafu akazieleza kiisimu. Zile kasoro zenyewe ndizo zinatumiwa katika kutunga kategoria kwa sarufi.
iv) Kueleza pale ambapo kasoro zilianzia.
v) Kuzingatia kasoro hizi ili kuweza kutambu namna ya kuzitatua. Wakati wanafunzi wanaposikilizwa wanaongea wakitufahamisha zile kasoro wanazozifanya. Na hivyo basi huwa ni vizuri kuwa na maswali kuhusu wanaozungumza wakilenga kutaja yote wanayoyapenda kuwa ni yapi. Ukitaka kurekebisha kasoro hizo, haiwezi kuwa kazi inayowezekana kwani ni namna mojawapo ya kukosoa maongezi hayo.



Kielelezo 2.2: Matumizi ya Uchanganuzi Makosa

Kielelezo hapo juu kinaonyesha kwamba kuna haja ya kufikiria juu ya kile kilichozungumzwa na mnenaji ili kizingatiwe zaidi kuweza kusahihisha kasoro zinazopatikana katika mazungumzo. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba kuna njia nyingi zinazoweza kutumiwa kukosoa hizo kasoro. Kwa mfano, mkosoaji hana uwezo wa kuhakikisha kile mwanafunzi alicholenga kukisema. Kwa hivyo ni jukumu lake kuachiwa huru kueleza alichokilenga kukisema. Inafaa pia kutambua ni sababu zipi zilizoleta makossa hayo kufanywa. Kuingiliwa kwa lugha nyinginezo pia huenda kukasababisha kanuni za lugha moja ambapo zinahama na kuathiri lugha nyingine inayotumika. Pia kuna maandishi mengine katika baadhi ya vitabu ambayo huweza pia yakaletea mwanafunzi kupotoshwa na akajifunza makosa badala ya yale yaliyo sahihi. Pengine mwanafunzi huenda akawa na mifumo ya kuwasiliana isiyo sahihi na ndiyo inamletea kufanya hayo makosa ingawa ajuapo kanuni zilizo sahihi.

Corder (1967) alipojadili uhusiano kati ya mwingiliano uliopo kwenye lugha ya upokeaji kutoka kwa lugha nyinginezo, alielezea kwamba zile kasoro zinazojitokeza kwenye lugha nyingine zinaashiria matatizo fulani ambayo mzungumzaji anapata kwa kuzingatia uhamishaji wa kanuni zilizopo katika lugha moja na vile inavyoathiri lugha fuatizi. Ili kuelewa makosa haya, ni muhimu kufahamu sababu zake. Makosa huweza kutokea kwa vile mtumiaji anavyobadilishana sifa na mitindo ya lugha tangulizi hadi ile lugha nyingine.

Vilevile, anayefundisha wanafunzi huenda akawa ndiye shida kama chanzo cha kasoro kwa vile anavyoelezea kanuni fulani. Kwa msingi huu, utafiti wenyewe ulielekezwa na mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kuchanganua kasoro (N.U.M) uliozinduliwa na Corder mwaka 1967, ambaye alidhihirisha kwamba kasoro ni njia muhimu ya kufundishia lugha fuatizi. Basi, kukitokea kosa lolote kwa upande wa wanafunzi, hawafai kuadhibiwa bali ni muhimu kubaini pale kasoro ilipoanzia.

2.6.2 Mfumo wa Kuchanganua-Linganuzi

Nadharia ya uchanganuzi-linganuzi ni eneo la isimu linganishi ambalo hujishughulisha na ulinganishaji wa lugha mbili au zaidi kwa sababu ya kuonyesha namna zinavyotofautiana au mfanano baina yao, ama kwa madhumuni ya kinadharia au madhumuni ya nje ya uchanganuzi wenyewe.

Nadharia ya Uchanganuzi-linganuzi ilianzishwa katika enzi za kale ili kuwa namna moja wapo wa kufundisha lugha, yenye msingi katika isimu miundo. Mwanzoni ilifanya kazi ya kulinganisha maendeleo mbalimbali juu ya hizo lugha husika, na pia kuangalia tofauti na ulinganifu baina ya lugha hizo zenyewe. Waasisi walizindua mfumo huo wa kinadharia mlikuwemo Fries, Weinrich, Haugen, na Lado (Njoroge, 1987). Kulingana na Njoroge, kazi ya Lado (1957) ndiyo iliyokuwa ya kwanza

kutekeleza matumizi ya kisasa ya nadharia hii, ikisisitiza kwamba mifumo miwili ya lugha huweza kufanyiwa ulinganisho na matokeo yake yanaweza kutumika na waalimu kuboresha ufundishaji juu ya lugha hiyo fuatizi. Mchakato wa kuchanganua lugha unahusisha kazi ya kufanya ulinganisho na kulinganua vipashio vya lugha ili kuonyesha jinsi vinavyofanana na kutofautiana. Kulingana na mfumo wa mtazamo huu wa kinadharia, ufanano unaokuwepo kutofautisha hizi lugha zote huweka rahisi mafunzo ya lugha inayofuatilia na kuthibitisha mlinganuo uliopo kwenye hizo lugha ambao huweza kuleta changamoto wa kusoma na kuelewa hiyo lugha lengwa[45]. Katika mwelekeo huu, ilionyesha kuwa Uchanganuzi-linganuzi ukihusisha Kinyankore na Kiswahili unaweza kusaidia kuelewa athari za mwingiliano kwa mawasiliano na hivyo kuendeleza masomo ya swahili katika muktadha huo.

Uimarishaji unasisitiza mfumo wa mtazamo wa kinadharia huu ulifanyika zaidi kupitia kazi ya James (1980) katika kitabu chake "Contrastive Analysis." Katika kazi hiyo, James anaonyesha jinsi nadharia hii inavyoweza kuchanganua lugha katika vipashio vinavyotofautiana hasa vya fonetiki, fonolojia, vya kimaumbo, kimuundo, na vya kimaana. Pia, anashauri kuwa wataalamu wa isimu wanapaswa kujaribu nadharia hii katika vipashio vikubwa zaidi ya sintaksia, kama vile matini. Anapoweka wazi jinsi Uchanganuzi-linganuzi unavyopaswa kutekelezwa, anashauri hatua mbili muhimu: Kwanza, kutoa maelezo ya lugha zinazohusika katika vigezo vinavyochanganuliwa; pili, kulinganisha maelezo yanayohusisha hizo lugha zote. Kutumia mbinu hizi, James

---

[45] Lado, R. (1957) anaelezea umuhimu wa Uchanganuzi-linganuzi katika ufundishaji wa lugha. Katika "Linguistics across Cultures: Applied Linguistics and Language Teachers," Lado anachunguza jinsi tofauti na ufanano wa lugha mbalimbali zinavyoweza kufanywa ili kuboresha ufundishaji wa lugha ya pili.

anatoa mfano wa Uchanganuzi-linganuzi kati ya sentensi za Kireno na Kiingereza, ukionyesha jinsi kimombo kilivyo lugha inayofuata, imeingiliwa na Kireno.

Nadharia hii inatatiza vipengele vilivyoelezwa hapa chini:

a. Kwamba changamoto katika mafunzo yanayohusu lugha fuatizi zinatokana na ushawishi unaochimbuka kwenye lugha tangulizi.
b. Kwamba changamoto hizi zinaweza kutabiriwa kupitia Nadharia ya Uchanganuzi-linganuzi.
c. Kwamba zana zinazotumika kufundisha zinaweza kusaidiwa na mfumo huo wa Uchanganuzi-linganuzi ili kupunguza kiwango cha kuathiriwa na lugha tangulizi.



Kielelezo 2.3: Kielelezo cha Matumizi ya Mfumo wa Kinadharia wa Changanuzi-Linganishi

Kulingana na kielelezo hapo juu, mfumo wa mtazamo wa kinadharia wakuchanganua-linganishi ni mbinu inayotumika katika utafiti wa lugha, hasa katika uelewa wa masomo yanayohusu lugha fuatizi. Mfumo huo wa kinadharia unaeleza kwamba tatizo au changamoto zinazokumbana na wanafunzi wanapojifunza somo la lugha nyingine zinaweza kueleweka kupitia tofauti zinazopatikana kwenye masomo ya lugha tangulizi (L1) na lugha wanayojifunza (L2). Matumizi ya nadharia hii wakati wa mafunzo ya lugha fuatizi huwa ya aina nyingi. Nadharia hii inabainisha kwamba tofauti katika mifumo ya kisarufi, leksikali, na fonetiki inayohusisha lugha hizo zote zinaweza kuathiri ujifunzaji. Kwa mfano, kama kuna tofauti kubwa iliyo wazi kuhusu lugha zote mbili, ya mama na ile nyingine, wanafunzi wanaweza kusuluhisha shida zote za kujifunza. Wanafunzi wanaweza kusoma hizo lugha zote akilinganisha kanuni na matumizi ya lugha hizo zenye uasili wa lugha inayojifunzwa. Hii inasaidia kubaini maeneo ambayo wanafunzi wanaweza kuwa na ugumu. Mfumo huu wa mtazamo wa

kinadharia pia inaelekeza wanaofundisha na wale wanaosoma kuelewa mifumo tofauti ya sarufi kuhusu lugha zote mbili, ambayo inaweza kusaidia wanafunzi kubaini makosa yanayoibuka katika vipindi vya kusoma L2. Kwa kuelewa tofauti na ufanano unaohusisha lugha, wanafunzi wanaweza kujenga mikakati ya kujifunza inayoendana na changamoto walizokutana nazo. Hii inaweza kujumuisha mbinu kama vile matumizi yanayoonyesha miundo ya kisarufi ya L1 kufundisha L2. Uchambuzi linganishi unaweza kusaidia wanafunzi kuelewa jinsi tamaduni na mazingira ya kijamii yanavyoathiri yale mawasiliano, jambo linalosababisha kusoma kwa urahisi na kutumia lugha zote kamili.

Mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kuchanganua- Linganishi inasaidia kubaini aina ya makosa ambayo wanafunzi huenda wakafanya, hivyo kuwapa walimu na wasomao ufahamu wa maeneo yanayohitaji umakini zaidi. Mifano ya mazungumzo inayohusisha zile lugha husika na inaweza kutumika kwa sababu ya kuwezesha wanafunzi kuelewa vizuri muktadha wa namna ya kutumia lugha. Mfumo wa mtazamo wa kinadharia unachangia katika kujenga uelewa wa tofauti za kitamaduni ambazo zinahusiana kutegemea jinsi lugha inavyotumika kusababisha jinsi inavyoimarishwa na kuelewa kwa jamii ya wanafunzi.

Hata hivyo wakati mwingine, nadharia hii inaweza kuwa na makosa, kwani si kila unapotofautisha lugha zote husababisha makosa. Wanafunzi wanaweza kusoma hiyo lugha nyingine na wakafanikiwa bila matatizo. Aidha, kusoma hayo masomo ya lugha huwa mchakato mgumu unaohusisha mambo kadhaa, kutoa mifano kama motisha, hisia, hali halisi ya kufundishia, ambayo hayawezi kufanywa kwa urahisi kupitia uchanganuzi wa kulinganisha pekee.

Kimuhtasari, mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kuchanganua- linganishi inatoa mwanga wakati wa masomo ya lugha nyingine kwa kutoa msingi wa kuelewa changamoto zinazozuka, huku pia ikitoa mbinu za kuboresha uzoefu wa ujifunzaji. Aidha, kama ilivyoelezwa hapo juu, inatakiwa kutambua kuwa inapaswa kutumika kwa njia ambayo huchukulia muktadha wote kwenye nafasi ya kusoma lugha husika.

Wakati wa enzi zile za miaka ya sitini (1960) Di Pietro alifafanua zaidi nadharia hii kwa kuingiza ndani yake mtazamo wa Sarufi Geuza-umbo-zalishi[46]. Kulingana na mtaalamu huyu, si rahisi kulinganisha lugha mbili zinazozingatia muundo sawa ambazo hazina ufanano wowote. Hivyo, alieleza kuwa tofauti za mitazamo ya uafafanuzi wa kiundani na wa kijuujuu ambayo inapewa umuhimu na sarufi geuza-umbo-zalishi, huhitaji kufuatwa katika utekelezaji wa Uchanganuzi-linganuzi wa lugha yoyote.

Kwa kufuatia mtazamo wa Di Pietro, nadharia hii ilisaidia kutafakari athari za umbo la ndani za lugha zinazojidhihirisha wakati ambapo lugha mbili zinapoingiliana. Hii ni kutokana na ule mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa Uchanganuzi-linganuzi huvitafiti vipengele vinavyopatikana kwenye lugha nyingine ambavyo hutofautisha sawa na vipengele vinavyohusu lugha tangulizi ya kwanza[47].

Utafiti huu ulishughulika na masomo juu ya lugha mbili, ya Swahili na ya Kinyankore, zinazotumiwa katika mawasiliano kuhusu washiriki wa kawaida waliojumuika katika utafiti. Kutokana na hili, nadharia hii ilichaguliwa ili kuchunguza jinsi lugha hizi zinavyoathiriana. Chanzo cha ujumbe unaopatikana katika lugha zinazohusika huwa ni ubongo wa watumiaji, na ujumbe unaosababisha athari zinazodhihirika katika mazungumzo, maneno ya maandiko, au muziki. Kuingiliana kwa lugha kupitia

---

[46] Stern, H.H. (1983) *Fundamental Concepts of Language Teaching*. O.U.P, New York.
[47] James, C. (1980) *Contrastive Analysis*. Longman, Burnt Mill Harlow.

mazungumzo na maandiko ndivyo vilivyoshughulikiwa. Kulingana na utafiti huu, kienezi kinaweza kuwasilishwa na mfumo-sauti, ambao huleta sauti zinazotumika katika namna ya kuwasiliana kwa lugha fulani. Kulingana na vile watu wanapozungumza, hewa inakuwa mfumo-enezi wa ujumbe. Kwa maandiko, karatasi inatekeleza jukumu hili. Kama alivyosema Weaver, mfumo-enezi una uwezo kutoa maelezo kwa kiwango fulani.

2.6.3 Mfumo wa kimawasiliano

Mtafiti aliongozwa pia na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) kama ki msingi cha utafiti wake ili kufikia malengo aliyokusudia kuchunguza. Nadharia hii, iliyozinduliwa na Howard Giles mwaka 1973, ilijaribu kueleza sababu za mabadiliko ya matamshi, kuweza kutoa namna ya kutumia msamiati mpya na wazungumzaji wanaohusika katika matumizi ya lugha ya kijamii. NKM inasisitiza kwamba wanadamu hujaribu kuzungumza kwa njia au kuiga mtindo fulani wa matamshi na msamiati mpya kutoka kwa wanapozungumza nao ili kukidhi namna wanavyotaka haja zao za mawasiliano. Hii inaweza kufanyika bila kujua au kwa kujua, kwa fikra au bila kufikiri. Hivyo, watu huiga msamiati au vigezo vinavyopatikana katika matumizi ya lugha kutoka kwa wale wanaozungumza nao.

Wakati wa kutumia mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kimawasiliano, kuna hatua ambayo mtu anajitahidi kujichanganya na mwingine katika mawasiliano. Urekebishaji huenda ukawa wa kiuchumi (kuelekea hatua za kupandisha za ushirikiano) au kinyume (kukataa au kuonyesha tofauti).

Pengine watu wanaweza kuchagua kubadilisha mtindo wao wa mawasiliano ili kujikurubisha na mwingine (kurekebisha kuelekea) au kuonesha tofauti zao

(kurekebisha kinyume). Mabadiliko haya yanategemea ushirikiano wa watumiaji wa lugha na hali za mawasiliano.

Wakati wanapozungumza, watu hujenga utambulisho wao kupitia mawasiliano. Kielelezo kinachofaa ni mtumiaji lugha kujitambulisha na mazingira yake ya kijamii au kitamaduni kupitia namna ya kujieleza kilugha, lafudhi, au mbinu nyingine za mawasiliano.

Nadharia hii inatoa ufafanuzi wa jinsi mtu anavyoweza kupata faida au kuhatarisha sehemu yoyote kwa kurejelea mabadiliko ya mawasiliano, ambayo yamelenga masuala kama hisia, mtazamo, na uhusiano wa kimwili kati ya wale wanaoshiriki mazungumzo.



Kielelezo 2.4: Matumizi ya mfumo wa mtazamo wa kinadhariakidhi ya kimawasiliano

Kielelezo hapo juu kinaonyesha kwamba Nadharia hii inajieleza katika namna ambavyo watu wanavyobadilisha mitindo yao ya mawasiliano ili kuendana na wenzako katika mazungumzo. Inachunguza jinsi watu wanavyoweza kuwa wanashirikiana wakihusisha wengine kupitia njia kadhaa zinazosaidia katika mawasiliano, kama lafudhi, kiimbo, matamshi, umbo na maana ya lugha.

Nadharia hii inajikita kwenye wazo la "kurekebisha" ambapo mtu anabadilisha mitindo yake ya mawasiliano yanayosababisha kuambatana kwenye yule anayezungumza naye. Jambo hili hujitokeza kwa kujifunza lafudhi, muundo wa sentensi, au hata kutumia silabi na maumbo maalum ili kuwa mwaminifu kwa mazungumzo. Katika nadharia hii, kisima muhimu ni kwamba watu wanapowasiliana, mara nyingi wanatafuta kuungana na wale wanaozungumza nao. Hii inaweza kujitokeza wakati wenye ushawishi mkubwa wa wenyeji katika jamii moja kama Kijiji, kazi, ya kibiashara, au hata mikutadha yoyote ile.

Nadharia inatambua kwamba mabadiliko haya yanategemea makundi yanayohusisha makundi tofauti ya kitamaduni ambamo mtu anajikita, kwenye hali fulani hasa jinsia, na hadha ya kijamii. Watu wanaweza kubadilisha mitindo yao ya mawasiliano kwa kuzingatia ule ushirikiano wa wahusika kwa wale wanaozungumza nao.

Nadharia hii inaeleza kwamba mawasiliano au mtagusano wa kiisimu yanaweza kutazamwa kama njia inayotumiwa na watu kufikia kukubalika katika jamii. Tukichagua kutoa mfano wa mwanafunzi anayeweza kuigiza mikondo husika ya kimatamshi akifuatilia matamshi ya wengine ili kudumisha lafudhi ya lugha inayohusika na hivyo kufikia malengo yake. Giles anabainisha kwamba kusudi iliyoletea ubadilishanaji wa mitindo ya kifonolojia kuweza kuboresha sauti ni

kuonyesha makubaliano yanayohusu wengine, jambo ambalo linawafanya wafanyakazi wenye kutoa mahusiano na lugha nyingine.

Kwa kurejelea mfumo wa mtazamo wa kinadharia huo, mawasiliano ya kiisimu yamegawanywa katika makundi mawili: mawasiliano wima na yasiyo wima. Mawasiliano wima yanatokea wakati mtu anapozungumza na mjuzi mwingine anayejaribu kujilazimisha kuzungumza kwa lugha hiyo ili kumfikia. Mawasiliano yasiyo wima yanatokea pale mtu anapozungumza na vijana, kwa mfano, akijaribu kurahisisha lugha ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano.

Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) inajikita katika mihimili mitatu muhimu. Kwanza, watu huwasilisha historia ya uzoefu wao kupitia matamshi na tabia zao, kuonyesha uhusiano wa mfanano wa matamshi na tabia katika mazungumzo. Pili, mawasiliano hubadilika kulingana na kanuni zinazopatikana kulingana na miktadha inayofaa. Tatu, mawasiliano yanayotokea kwa wajua lugha huathiriwa na mazungumzo na jinsi watu wanavyopokea na kutafasiri kile walichosikia katika mazungumzo hayo.

Nadharia hii inasisitiza kuwa mikakati ya kuwasiliana ndiyo msingi wa lugha. Nobert Wiener baadaye aliongeza mtazamo wa matokeo kwenye mfumo wa mtazamo wa kinadharia huu, akisisitiza kwamba kila ujumbe una mtoa na kuwa wa kinasibu. Vipengele vingine muhimu vinavyopatikana hapa huwa kienezi (ambacho hueneza ujumbe), mfumoenezaji (mbinu ya kueneza ujumbe), kipokezi (mpokeaji), kiishio (kilichokusudiwa ujumbe), nakadhalika. Kipengele cha kelele, kilichotolewa na Cozy (2012), kinamaanisha hali zinazoweza kuingilia mawasiliano, kama vile vizuizi vinavyojitokeza kwenye lugha zote husika.

Wakati wa hatua zinazohusisha kuhakikisha kwamba masiliano yasitatazike, Shannon na Weaver walipendekeza kwamba ni muhimu kuwepo hali ya entropi na uradidi,

ambapo hali hizi zinapaswa kuwa katika usawa ili kuimarisha mawasiliano. Usawa huu unaleta kutabirika na kutotabirika katika ujumbe. Kiwango hiki kinaegemea sana muda na wakati, na hivyo kuafikiana na mwingiliano unahusu hizo lugha, ambapo wakati mwingi unaosababisha kuingiliana huleta athari nyingi.

Katika uchambuzi huu, matokeo yanachukuliwa kama kiashiria muhimu kinachoonyesha kwamba mawasiliano yamefanikiwa. Katika muktadha huu, mchanganyiko wenye maneno yenye kuathiri mawasiliano kuhusu mawasiliano haya yote ni uthibitisho wa ufanisi wa mawasiliano. Neno "mawasiliano" kwenye mfumo wa mtazamo wa kinadharia linatumika kueleza dhana kubwa sana, likihusisha mbinu zote ambazo zinazuia ubongo mmoja kuathiri mwingine. Kifungo hiki kinachukuliwa pia kama hatua ya kuathiri kiishio. Hivyo, dhana ya kimawasiliano inaweza kutumika kutatua mahusiano yaliyo ya kategoria tofauti na matokeo yake. Tukirejelea sehemu nyingine, ujumbe kulingana na mfumo wa mtazamo wa kinadharia huu hauwezi kutabirika, hali inayofanya nadharia hii yakatoa umuhimu katika kuelezea mwingiliano wa lugha, kwani lugha haina mfumo maalum inapoathiri nyingine. Hii inamaanisha kwamba ngazi yoyote ile huenda ikaathirika.

Hata hivyo, nadharia hii inaonya kwamba ujumbe haupaswi kuchukuliwa kama ulivyo maelezo sawa, kwa sababu kila mtu anatoa uwezo anaouonyesha kiujumbe anaoupokea. Kwa hivyo, nadharia hii inampa mtu yeyote uwezo unaomletea kutafuta wajibu wa ujumbe. Pia, inasisitiza kwamba inapokuwa ujumbe umeandikwa vizuri, hali ya kutotabirika inapungua. Katika hali hiyo, ujumbe unakuwa wa kidogo. Ikiwa kuna vipengele fulani vya ujumbe ambavyo havipo, kuna uwezekano mkubwa kwamba mpokeaji atajaza mapengo hayo, hali ambayo inaweza kuathiri kiishio. Hili linadhihirisha kuwa kwa mfano, ikiwa lugha fulani haina uwezo ulio na mawasiliano, kuingiliana kwa hizo lugha husika na kunaweza kupelekea kuongezeka kwa msamiati

au muundo. Ikiwa hii itatendeka, lugha hiyo itaanza kuathiriwa. Nadharia hii ilisaidia pakubwa kufafanulia mtafiti matokeo yanayoathiriwa na hizo kugha zinazochukuliwa kuwa hazitoki kwenye lugha tangulizi; yaani, chanzo chake hakiwezi kuwa tofauti na mifumo miwili ya lugha inayochunguzwa.

Kwa ujumla, nadharia kidhi ya mawasiliano inatoa mtazamo muhimu wa jinsi watu wanavyopokea, kubadilisha, na kuimarisha mawasiliano yao kwenye mikutadha mbalimbali ili kuchangia katika uelewa wa mwingiliano wa kibinadamu. Mtafiti amechagua kutumia mfumo wa mtazamo wa kinadharia huu ambao unafaa kwa maeneo tofauti yanayokaribiana kwenye mawasiliano fulani. Jinsi ya vile huu utafiti unavyohusisha mawasiliano, nadharia hii inatoa mwanga wa kuelekeza. Aidha, nadharia hii inaelezea sababu za kubadilika kwa mtindo wa matamshi kwenye namna ya kuwasiliana kijamii na inachunguza vile inavyoathiri jamii. Mtafiti amebaini kwamba ni muhimu kutumia nadharia hii ili kufikia malengo kuhusu utafiti husika.

2.7 Namna ya kutumia Nadharia

Utafiti huu ulibebwa kwa kuelekezwa Nadharia mseto, ambazo zilikuwa mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kuchanganua makosa (UM), Mfumo wa mtazamo wa kinadharia wakuchanganua Linganuzi (UL), na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM). Mfumo wa kinadharia wa kuchanganua makosa ulianzishwa Mtaalam ajulikanaye kama Corder Stephen Pit mnamo mwaka 1967 na ikapata umaarufu katika miaka ya 1970. Nyakati hizo, Nadharia ya UM ilichukua nafasi ya mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa kuchanganua linganuzi (UL), ambayo ilianzishwa na Fries mnamo mwaka 1945 na kuendelezwa na Robert Lado mwaka 1957. Utafiti uliofuata, hudai kuwa mfumo huo wa UL ilionekana kuwa muhimu kwenye njia zinazotumika kufunzia lugha fuatizi (L2), lakini tangu miaka ya 1970, tafiti kadhaa zilionyesha udhaifu wake kwa kushindwa kuweza kuchunguza lugha za wanafunzi. Kwa kuzingatia mfumo wa

kinadharia huo wa UL, makosa yaliona kama matokeo ya mwingiliano kuhusisha lugha tangulizi (L1) ikilinganishwa na lugha fuatizi (L2) pekee, huku anayefundisha anazingatia umilisi wake kufikiri na kutabiri makosa ambayo wanafunzi wake huweza kuyafanya ikiwa sababu ya lengo lake lilikuwa kufundisha tofauti za kisarufi kulinganua lugha tangulizi na ile fuatizi. Hivyo, wakati Nadharia ya UL ilizingatia miundo sahihi kwa ile lugha tangulizi na ile fuatizi, Nadharia ya UM ilianza kuzingatia mbinu ya kuchunguza lugha za wanafunzi. Makosa sasa yalikuwa yanazingatiwa kwa kuangalia dalili kwamba mwanafunzi anajaribu kujifunza na kuelewa mfumo unaotumika kwa lugha fuatizi. Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ilisaidia kuelezea athari zilizomo chini ya lugha zinazojitokeza wakati lugha mbili zinaposhirikiana, kwa sababu inabainisha vipengele vilivyo katika lugha fuatizi ambavyo vinatofautiana na vya lugha ya kwanza na pia vile vinavyofanana. Ufanisi wa Nadharia ya UM umeonekana zaidi pale ambapo mwanafunzi anapewa fursa za kipekee kujifunza kwa kuchambua makosa anayofanya na pia makosa ambayo yalijitokeza wakati wanafunzi waliwasiliana na wengine. Mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa UM pia ulitumika kudhibitisha makosa yaliyoonekana kwenye lugha iliyotumiwa na mwanafunzi wa Kinyankore anayejifunza Swahili ikiwa kwake ni lugha fuatizi. Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) ilimsaidia mtafiti kubaini sababu za athari za lugha ya Kinyankore zinazotokea kutokana na watu kuiga mazungumzo katika mtindo wa matamshi na msamiati kutoka kwa watazamaji wao kwa lengo la kufanikisha mawasiliano, pia kuonyesha ufanano wa matamshi na tabia kwenye mawasiliano hayo.

Nadharia hizi zilimsaidia mtafiti kuchanganua data na kudhihirisha yaliyotokea kwenye utafiti. Mtafiti alitabaini athari mbalimbali za kifonolojia, kisemantiki, na kimsamiati ambazo zilikuwa matokeo ya lugha tangulizi wakati wa masomo shuleni, kutokana na

kwamba mtindo wa matamshi yanayohusu maneno yenye uhusisano katika lugha tangulizi ambayo umeshajengeka kutokana na umilisi huo wa Kinyankore.

2.8 Pengo la Utafiti

Hapo awali ilielezwa kwamba kumekuwa na tafiti nyingi kuhusu kuathiriwa kwa lugha za kiasili wakati wa mafunzo ya Swahili. Ingawa kuna juhudi za kuboresha hiyo lugha fuatizi, tafiti nyingi zaonyesha kuwa wanafunzi wajifunzao Kiswahili wanafanya makosa kwa mazungumzo na maandiko yao. Makosa hayo yanajumuisha kasoro za kimaumbo, kisintaksia, kisemantiki, na kifonolojia. Tukiendeleza utafiti huo, mtafiti aligundua athari za Kinyankore wakati wanafunzi wanapojifunza lugha fuatizi ya Swahili na wanaozungumza Kinyankore kama L1 yao. Aidha, mapendekezo ya utafiti huu yaliibua mbinu mbalimbali zinazoweza kuwasaidia wanafunzi walioathiriwa na Kinyankore wanapojifunza Kiswahili. Wanaisimu wamekuwa wakifanya kazi ili kutambua ni wapi kasoro hizi zinapoanzia, halafu namna bora za kusuluhisha shida hizo. Hivyo, katika mtazamo wa mtafiti, hakuna mtafiti aliyewahi kufanya utafiti kuhusu "Athari za L1 ikiwa kinyankore kwa wasomaji wa Swahili Kiswahili kama L2." Kwa hivyo, mtafiti anakubali umuhimu wa kuendelea na utafiti kuhusu "Athari za L1 wakati wa mafunzo ya Kiswahili" ili kuziba pengo lililopo katika utafiti huu.

Mapitio ya msingi wa utafiti yameonyesha kwamba kazi zinazohusiana na kuathiriana kwa lugha zinaweza kugawanywa kwenye vikundi viwili; kikundi cha kazi ambazo hazijashughulikia kiutafiti suala la kuathiriana kwa lugha, halafu kikundi cha kazi ambazo zimezingatia kuathiriana kama suala kuu la tafiti. Ilibainika kwamba kuathiriana kwa lugha na kuwa jambo linalochukua muda mrefu, ambalo linatokana na maingiliano ya lugha mbili au zaidi, hasa pale zinapokutana kwenye mikutadha iliyo ya pamoja ili kukidhi mawasiliano. Kazi nyingi zilizokaguliwa zimechunguza kuathiriana kwa matumizi ya lugha kupitia mwelekeo mmoja; yaani, zikiwa zina

mwelekeo ulio na lugha yenye hadhi kuu ikihusishwa na lugha isiyo na hadhi. Hata hivyo, kazi hizi zote zimedhihirisha kwamba athari zinaweza kutoka pande zote za lugha zinazohusiana.

Zaidi, iligunduliwa kwamba wataalamu wengi wanatumia msamiati kwa namna inayohakikisha kuathiriana kwa lugha. Kutokana na mwelekeo huu, udhihirishaji wa dhima ya wataalamu kuangazia masuala ya kuathiriana kwa lugha na kuibua mifano inayothibitisha kwamba lugha zinaweza kuathiriana katika nyanja tofauti. Katika mazingira yaliyoko barani Afrika, tafiti nyingi za kuathiriana kwa lugha zimefanywa. Swahili imekuwa lugha teule kwenye zile nyingine zilizofanyiwa tafiti kama hizi. Kulingana na utafiti huo, ilionekana kwamba Swahili, kulingana na lugha nyingine duniani, imekuwa ikifanya na kupokea athari. Hata hivyo, kuathiriana huku kati Swahili halafu zile nyingine lugha zote hakujapata taarifa za kutosha, hivyo kunatokea mahitaji kuendeleza utafiti wenye namna hii. Kwa mfano, hata kama Swahili inaheshimika kuwa lugha iliyopanuka kimataifa inayohusiana na lugha kuu za dunia na lugha nyingi za Kiafrika, tafiti kuhusu kuathiriana kwa lugha hii kulinganishwa na zile za kwanza hazipo kwa wingi.

Limethibitishwa kinagaubaga kuwa nchini Uganda, suala la kutafitia athari za lugha zilizo za kiafrika na Kiswahili halijapewa umuhimu unaostahili, tofauti na nchi jirani kama Kenya na Tanzania ambapo utafiti kama huu umefanywa tangu mwongo wa saba wa miaka iliyopita. Kwa hivyo, utafiti wa sasa huwa hatua, ingawa ndogo, ya kuziba pengo hili. Inatarajiwa kwamba utafungua njia pana kuchunguza kisayansi kuhusu zile lugha kwa nyakati zijazo.

Hivyo, lugha zote zinazozungumzwa kwenye maeneo ya uganda zinaweza kuwa lengo la utafiti wa aina hii. Vilevile, lilidhihirishwa kwamba lugha zilizoathirika zinaweza

kutokea kwenye baadhi ya lugha zinazohusiana. Hata hivyo, njia za kuathiriana kwa hatua fulani na athari hizo hutofautiana. Kwa mfano, jinsi lugha inavyoathiri nyingine yenye hadhi zinaweza kuonekana haraka haraka kiurahisi kwa lugha isiyo na hadhi, hasa katika ngazi ya mofolojia, kwa sababu lugha hiyo ina msamiati mpana uliopatikana kwanamna ya kutumia lugha katika maeneo na muktadha mbalimbali. Aidha, lugha kama Kitigania, ambayo haijapewa hadhi, inaweza kuathiri lugha nyingine ikiwa ni sehemu kubwa ya mtindo ulio wa kiundani, hasa kifonolojia.

Wakati wa kuchunguza jinsi lugha inavyoathiri, mtafiti hapaswi kujihusisha na kiwango kimoja cha lugha pekee. Haya yote yanajitokeza kusababisha athari zinazotokea katika kiwango fulani zinaweza kusababisha mabadiliko katika viwango vingine (Massamba, 1986). Linadhihirika pia kwamba lugha yoyote inayotumika kwenye mikutadha ile ile inaweza kuathiriana. Kwa hivyo, lugha zote za Afrika zinazozungumzwa katika mazingira ya Kiswahili zinaweza kufanyiwa utafiti kwa kuzingatia hatua tofauti ili kubaini jinsi zinazohusiana kwa kuathiriana na Kiswahili. Wakati wa kufanya utafiti unaokuwa kama kategoria hiyo, ni muhimu kuzingatia viwango vya lugha kama matamshi ya sauti, maumbo ya neno, muundo wa tungo na maana yake. Aidha, athari zinapaswa kuchunguzwa kutoka mtazamo wa lugha asilia kwa ile yenye kupokea. Hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba tafiti hizi zinachangia katika ukuzaji wa lugha zote husika mwisho wake kuonyesha manufaa[48].

Katika hii sura, kazi zinazohusiana na mahusiano kati ya Kinyankore na swahili, huonyesha mafunzo ya Swahili yalivyoathiriwa, zilipitiwa. Mapitio hayo yameonyesha kwamba ingawa kuna mahusiano ya muda mrefu kuhusu lugha hizo, haimaanishi kuwa zimekuwa zikiathiriana kwa muda wote. Hii ilionyesha kwamba, pale wahusika wa

[48] Fulass, H. (1971). *Problems of Terminology*.

lugha mbili wanapokutana, si lazima kuwa lugha hizo zimeanzisha mchakato unaoziathiri.

Kwa utafiti huu, nadharia tatu zilitumika. Wa kwanza kabisa ulikuwa mfumo wa kinadharia wa Uchanganuzi-linganuzi, ambayo inaruhusu ulinganifu wa mifumo miwili inayohusu lugha halafu kuonyesha shida zilizopo wakati wa mafunzo ya lugha kutokana na kuathiriana kati ya hizo. Mfumo mwingine wa kinadharia ulikuwa UM, ambao ulitolewa ili kujaza mapengo yaliyokuwepo katika uchanganuzi linganuzi wa wanaisimu wa kuzilinganisha baina ya hizo lugha tangulizi na ya pili ya mwanafunzi na kutabiri makosa yanayotokea. Mfumo wa tatu,ni ule wa kimawasiliano ambao unasisitiza kwamba, pale ambapo lugha mbili zinakutana ili kutimiza mawasiliano, ni maneno katika lugha yenye ujumbe ndiyo yanayoleta athari hizo. Hivyo, kwa mikutadha ya lugha hizo imekuwa ikichanganyika kwa muda mrefu, kiwango cha kuathiriana kinazidi kuongezeka. Ni muhimu kutambua kwamba kuathiriana kwa lugha ni njia muhimu kuendeleza mawasiliano, na ili lugha iweze kuwasiliana kwa njia ya kisasa katika nyanja yoyote ya kitaaluma, inapaswa kuathiri na pia ikaathirirwa lugha husika, Nyanda (keshatajwa).

2.9 Hitimisho

Kwa muhtasari, tunataja na kujadili mapitio ya tafiti zilizopita na misingi ya nadharia iliyotumika katika kuchambua matokeo ya utafiti huu. Vitu muhimu vilivyojadiliwa katika tafiti zilizopita kudhihirisha vile lugha zinavyoingiliana. Aidha, nadharia mseto zimeelezwa, zikiwemo Nadharia ya Uchanganuzi-Linganuzi, ambayo inaruhusu ulinganishi wa mifumo miwili au kadhaa inayotumika kuelezea shida ambazo zinapatikana katika mafunzo ya lugha ya lugha mbili tofauti na zinazosababishwa na kuathiriana kwa lugha hizo. Pia, kuna mfumo wa mtazamo wa kinadharia wa UM ambao unasaidia kutambua kasoro zinazopatikana kwenye lugha za wanafunzi, halafu

mfumo wa kinadharia wa kimawasiliano, ambayo inaonyesha kuwa, pale ambapo lugha mbili zinapokutana kwa mawasiliano, ni maneno yanayoleta athari hizo. Kwa hivyo, kuathiriana kwa lugha huongezeka kwenye mikutadha ya lugha hizo zimekuwa zikichanganyika kwa muda mrefu. Ni muhimu kutambua kwamba kuathiriana kwa lugha ni njia kueneza ukuzaji wa lugha, na ili lugha iweze kufanikiwa katika mawasiliano ya kisasa katika nyanja zote za kitaaluma, inahitaji kuathiriana na namna inavyoweza kuathiriwa.

Kwa hivyo, sehemu hii imedhihirisha mifumo yote ya mitazamo ya kinadharia yote iliyoelezwa pamoja na jinsi zinavyofanya kazi. Mapitio kuhusu kiini cha utafiti yameonyesha kwamba tafiti zinazoangazia kuathiriana kwa lugha zinaweza kugawanywa kwenye kategoria mbili; ya kwanza ni ile isiyoshughulikia kuathiriana kwa lugha kwenye mfumo ulio wa kiutafiti, na ya pili ni yale yanayochunguza kuathiriana kama kipengele muhimu cha utafiti. Umebainika kuwa kuathiriana kwa lugha kumejikita katika maingiliano ya lugha zaidi ya mbili, hasa wanapokutana kwenye mikutadha iliyo ya pamoja kwa mawasiliano. Tafiti nyingi zilizopitiwa zimeangazia kuathiriana katika mwelekeo mmoja, zikizingatia lugha yenye hadhi juu ya lugha isiyo na hadhi. Hata hivyo, tafiti hizi zote zinaonyesha kwamba athari zinaweza kutokea kutoka pande husika zinazohusiana katika lugha. Aidha, inabainika kwamba wataalamu wengi hutumia msamiati ili kuweza kubainisha kuathiriana kwa lugha. Kutokana na hili, kuna haja ya wataalamu kuangazia zaidi masuala ya kuathiriana na kutoa mifano inayodhibitisha kuwa lugha zinaweza kuathiriana kwenye hatua tofauti.

Katika mazingira kwenye bara la Afrika, kumekuwepo na tafiti nyingi zinazohusiana na kuathiriana kwa lugha. Kiswahili huwa mojawapo ya lugha zilizopewa uzito katika tafiti kama hizi. Kutokana na tafiti hizi, kimeonekana kwamba Swahili, ukiilinganisha

na lugha nyingine, kinathiri na kinaathiriwa. Hata hivyo, utafiti wa kuathiriana kutofautisha Swahili na baadhi ya lugha tofauti haujapata umakini wa kutosha; hivyo, kuna umuhimu wa kuendeleza utafiti wenye mwelekeo kama huu. Kwa mfano, Hata kama Swahili huwa lugha ya kimataifa na inahusiana na lugha kubwa za ulimwengu na mamia ya lugha za Kiafrika, tafiti zinazohusiana na kuathiriana kwake huwa huajakuwa wa kutosha sana.

Nchini Uganda, mchango wa kuathiriana kati ya lugha za kienyeji na Kiswahili haujapewa uzito unaotakiwa, tofauti na Tanzania ambapo tafiti kama hizi zimefanyika tangu enzi za kale mno. Utafiti huu ni hatua ndogo ya kufungua njia ya kujaza pengo hili, na tunatarajia utaongeza fursa ya utafiti kwa wasomi wa lugha siku zijazo.

Kwa kuwa, lugha hizo zote zinazotumiwa katika mazingira ya lugha zilizomo nchini Uganda huwenda zikafanyiwa kazi kwa njia hiyo hiyo. Pia, ni wazi kwamba athari za lugha zinaweza kutokea pande zote ambazo zinazohusiana. Hata hivyo, jinsi ya kuathiriana huleta athari hizo hutofautiana. Kwa mfano, kuathiriana kwenye hadhi kunatokea kwa urahisi kwenye lugha isiyo na hadhi ya vigezo vya kisarufi, kwa sababu lugha hiyo ina msamiati mpana kutokana na matumizi yake katika muktadha tofauti. Hata hivyo, lugha kama Kinyankore, isiyo na hadhi, inaweza kuathiri lugha zingine na kuingilia miundo yake ya ndani, hasa kisarufi.

Katika sura inayofuata, tutajadili utafiti wa awali halafu ukusanyaji wa data na uchambuzi wake. Tutatoa ufafanuzi wa ndani sana kuhusu jinsi njia ya ukusanyaji data zilitumika katika utafiti na vile zilivyowezesha kufanyika utafiti kamili. Pia tutatoa ufafanuzi wa ndani kuhusu jinsi utafiti wa awali ulivyosaidia kuelekeza utafiti kamili, pamoja na uchanganuzi wa data, muundo wa utafiti, uthabiti wa matokeao na ufafanuzi wa kimaadili kwa undani.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia vile utafiti ulivyofanywa kwa kuonyesha mbinu zilizotumika kukusanya data, sehemu data ilikokusanyiwa, kundi lengwa, sampuli ya wahojiwa, mbinu zilizotumika kukusanya data, na hasa aina ya utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, uadilifu wa matokeo, na hayo yote yaliyofanyika kuunda utafiti kamili. Hivyo basi, sura hii inatoa ufafanuzi wa kina kuhusu jinsi utafiti huu ulivyofanywa na vile mtafiti alivyotumia mbinu ili kutekeleza wajibu wake kiutafiti. Maelezo kuhusu njia alizozitumia kukusanya, kuchambua na kuchanganua data kukamilisha utafiti mzima yanazingatiwa kwa kina.

3.1 Sehemu ya Utafiti

Kwa kurejelea utafiti huu, sehemu iliyofanyiwa utafiti ilikuwa mahali ambapo data na taarifa kuhusu utafiti mzima zilipatikana[49]. Wataalam hawa wanaeleza kuwa ni vizuri mtafiti anastahili kuchagua anapopendelea kufanyia utafiti wake na akapata data ifaayo utakayohitaji. Kwa hivyo, huo utafiti huenda ukawa wa nyanjani na ulikusanya data kuhusu wanafunzi waliochaguliwa kwenye asasi zinazojihusisha na masomo mkiwemo shule za juu na zile za msingi hata vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili jijini Mbarara nchini Uganda. Mtafiti alichagua vyuo vikuu na asasi zilizoteuliwa jijini Mbarara. Mtafiti alichagua asasi hizo kwa sababu ndizo zenye wazungumzaji wanaotumia Kinyankore. Kwa hivyo, alikabiliwa na urahisi katika kupata data juu ya jinsi vile lugha yenyewe tangulizi ilivyokuwa inaathiri kujifunza ile ya Swahili.

---

[49] "Research Methods: The Basics" ni kitabu kilichoandikwa na Polit na Hungler, kilichotolewa mwaka 1999 na Routledge Taylor and Francis Group. Kitabu hiki kinatoa mwanga juu ya mbinu mbalimbali za utafiti, kikiwemo uchambuzi wa data, ukusanyaji wa taarifa, na mbinu za kutathmini uhalali wa tafiti.



Kielelezo 3.1: Ramani ya Jiji la Mbarara kama sehemu utafiti ulikotokea

Kielelezo hapo juu kinaonyesha sehemu utafiti ulikofanyika jijini Mbarara ambako asasi za elimu mbalimbali zilichaguliwa. Jiji la Mbarara lilichaguliwa kwasababu kuna wenyeji wenye umilisi wa L1 ambayo ni Kinyankore, na tena kuna asasi nyingi za elimu zinazofundisha Kiswahili kama L2. Hali hii inalifanya jiji la Mbarara kuwa eneo lifaalo kuelewa muktadha wa wanafunzi wanaosoma Kiswahili na vile wanavyoathiriwa na

Kinyankore kama L1. Jijini Mbarara unajitokeza kuwa mji mkubwa nchini Uganda, ambao unajulikana wenye tamaduni na desturi za kipekee na kuwapatia mahali pa wanafunzi wengi wa vyuo vikuu na shule za upili.

Jiji hili lina jamii mbalimbali, wengi wao wakizungumza Kinyankore ikiwa ni L1 nyumbani, ambao wanadhaniwa kuwa na uhusiano wa karibu kutumia L2 iliyo Swahili, ambayo inafundishwa kwa wanafunzi kama lugha nyingine na ni ya muhimu kielimu.

Kinyankore, ikiwa ndiyo L1 katika sehemu za jiji la Mbarara ambako utafiti ulifanyika, pamoja na Kiswahili, ambayo hutumiwa katika mawasiliano ya kitaifa, huchangia katika mipango inayotumika kufunzia. Utafiti uliangazia mtagusano wa lugha mbili hizi unaojitokeza kudhihirisha yanayofundishwa kielimu. Asasi za elimu katika Mbarara zina ngazi za wanafunzi ambao wanajifunza L2 ikiwa Swahili, huku Kinyankore ikiwa L1 nyumbani au ya kwanza. Utafiti uliangazia athari za sarufi ya L1 kinyankore kwa wanfunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2 kwa kuzingatia njia bora zinazotumika kuwasomesha na changamoto zinazokabili wanafunzi katika kujifunza L2 kwa kurejelea uelewa waliwo nao juu ya Kinyankore.

Vyuo vikuu jijini Mbarara vinatoa mafunzo ya kisasa kwa kuhusisha wanafunzi waliohitimu wamehitimu kutoka asasi za sekondari, wengi wao wakizungumza Kinyankore. Hapa, utafiti ulichunguza mipango mbalimbali inayotumika kwenye ufundishaji wa wanafunzi na vile wanavyotumia maarifa yao ya Kinyankore katika kujifunza Kiswahili. Vyuo vikuu vinaweza kuwapa hali ifaayo kuwasaidia kidijitali ambayo yanaruhusu wanafunzi kuelewa L1 kwa kupitia mifumo ya mtandaoni, na hii ilikuwa kipengele muhimu katika utafiti.

Utafiti ulichunguza jinsi lugha ya Kinyankore inavyoweza kuleta sababu zinazoathiri mafunzo ya L2 kufanikiwa. Hasa wanafunzi wanaweza kuelezea jinsi wanaweza kuhusisha njia ya lugha wanayojua kuwasaidia kuelewa namna ya kusoma L2.

Utafiti uliangazia mifano halisi ya kutumia lugha kwa wanafunzi wanaozungumza Kinyankore na Kiswahili, kuchunguza jinsi wanavyotumia lugha hizo mbili pamoja kwenye mawasiliano yaliyo ya kawaida.

Sehemu ya utafiti jijini Mbarara ilikuwa muhimu kusaidia mtafiti kupima uelewa wa wanafunzi wenye L1 ya Kinyankore na shida zinazowakumba wakisoma L2 ya Swahili. Kutokana na mazingira ya kidemografia, kihistoria na kitamaduni, utafiti unatoa uelewa mzuri kuhusu jinsi L1huleta athari wakati wa mafunzo ya L2 iliyo Swahili, na mchango wa asasi zilizochaguliwa katika mchakato huu. Hapa inatoa mwangaza kwamba kuna maelezo yenye maana ambayo wanafunzi wanaweza kuwa nayo wakati wa mafunzo yao.

3.2 Taarifa kuhusu Wahojiwa

Habari zilizotangulia kwanza kutoka kwa waliohojiwa zinazozungumziwa kwenye utafiti huu zilihusu mambo ya kiumri, hadhi zao kielimu, kazi zao, na kabila la wahojiwa.

3.2.1 Taarifa kuhusu kabila la washiriki

Wakati wa kutekeleza utafiti husika, jamii inayochunguzwa ni ya Wanyankore, kwa sababu wao ndio wahusika wakuu walioshiriki kwenye utafiti husika. Shabaha iliyoelekeza utafiti huu ilikuwa kuchambua jinsi lugha ya Kinyankore inavyoathiri mafunzo ya L2 iliyokuwa Swahili. Kwa hivyo, huu utafiti ulilenga watu kutoka kwenye sehemu za wazungumzaji wa kinyankore pekee, wanaopatikana wilayani Mbarara. Kulingana na nafasi ya kupata wahojiwa wasiokuwa wa jamii ya Kinyankore, kama

walimu, mtafiti alijikuta akihitaji kuwashirikisha kwenye utafiti pale lilipokuwa muhimu kufanya hivyo.

3.2.2 Taarifa kuhusu jinsia ya wahojiwa

Wakati wa utafiti husika pia, jinsia ya wahojiwa iliangaliwa kiundani kwa sababu ya kuhakikisha kwamba jinsia zote mbili zilihusika kwa kiwango sawa.



Kielelezo 3.2: Kuhusu jinsia ya washiriki

Matokeo yaliyokuwa katika kielelezo namba 4 hapo juu yanadhihirisha kwamba jinsia zote mbili zilikuwa na uwakilishi sawa. Kulikuwa na angalau washiriki hamsini wa wasichana na washiriki kiasi cha hamsini cha wavulana walioshirikishwa na utafiti huu.

Matokeo ya kielelezo namba 4 hapo juu yanayoonyesha uwakilishi sawa wa jinsia mbili katika utafiti yana dhihirisha dhima mbalimbali kuhakikisha usawa na kutathmini jinsi jinsia zinavyoathiri mambo yaliyotokea kutoka kwa utafiti mzima. Kielelezo kinaonyesha kuwa kiasi cha hamsini cha washiriki walikuwa wasichana huku asilimia 50 wakiwa wavulana. Hii inaonyesha uwakilishi wa usawa wa jinsia katika utafiti, jambo lililokuwa lenye manufaa ili kufanya tathmini sahihi ya maoni yenye tajriba ya wanafunzi wote bila upendeleo wa jinsia. Uwakilishi sawa wa jinsia unahakikisha kwamba yaliyotokea kwenye utafiti yanaweza kutumika kiujumla kuwakilisha namna mambo yanavyokuwa kihalisia katika mazingira yao. Utafiti ambao unawabagua jinsia

moja unaweza kuathiri matokeo na kutoa picha iliyopotoka kuhusu mtazamo unaohusu jamii nyingine.

Ikumbukwe kwamba kila jinsia inaweza kuwa na njia mbalimbali zinazoweza kusaidia kujifunza na kutumia lugha. Kwa mfano, wasichana na wavulana wanaweza kuwa na mitazamo tofauti juu ya L2 iliyo Swahili, halafu na vile wanavyohusisha L1 iliyo Kinyankore.

Uwakilishi sawa unatoa fursa ya kutambua ikiwa kuna athari za kijinsia zinazoweza kujitokeza ili kujenga harakati za kuinua mtindo wa mafunzo ya L2. Hii inaweza kuhusisha uchambuzi unaozingatia uelewa wanafunzi walio nao, hali zao zinazohusu mazingira yao, umri wao, walimu wao, hata wanavyofanya vizuri katika masomo yao ya lugha.

Utafiti uliofanywa ulidhamiria kuondoa ubaguzi kuhusu tofauti za kijinsia wakati L2 inafunzwa, jinsi wasichana na wavulana wakipambana kuepukana ugumu wa kusoma Swahili, halafu kueleza njia za kuvunjia mbali njia za kawaida za kujifunza.

Kwa hivyo, matokeo katika kielelezo namba 3.2 yanayoonyesha uwiano sawa wa jinsia katika utafiti ambao unathibitisha uwezo wa kuelewa jinsi jinsia inavyoweza kuathiri njia ya kusoma L2. Kwa kuhakikisha kuwa washiriki wa jinsia zote mbili wanawakilishwa, utafiti unakuwa na uhalali na usawa, unaowezesha kutolewa kwa matokeo na mapendekezo ambayo yatasaidia kuboresha usomaji wa L2 na wanafunzi wote.

3.2.3 Kuhusu Umri wa wahojiwa

Huu utafiti ulilenga kuwashirikisha wahusika wenye umri kati ya miaka 16 kama watoto katika asasi za elimu hadi 60 kama wanaofundisha kielimu umri ambao ndio mwisho wa wafanyakazi wa serikali. Kwa vile utafiti ulilenga wanafunzi wanaokuwa

shuleni kwenye asasi za elimu ndio washiriki wanaofaa kuhusika tathmini jinsi L1 ya Kinyankore inavyoathiri L2 ya Swahili. Walimu walihusishwa kwenye huu utafiti kwani wanaweza kuelezea na kuchambua jinsi maneno yanavyotamkwa kwa usahihi katika jamii ya Kinyankore, pamoja na kuelewa mbinu mbalimbali zinazotumika kufundisha L2 ya Swahili kwa wanafunzi wa Kinyankore. Vilevile, maafisa wa elimu walihusishwa kwa sababu wana uwezo wa kuelekeza sera za elimu na yale mapendekezo kuhusu namna ya kuboresha ufunzaji na kuwezesha wanajamii wasomao wa Kinyankore kusoma L2 iliyo Swahili. Watu hawa waliohusika hupatikana kwenye kategoria ya rika ya walio na miaka kumi na sita (16) mpaka miaka sitini (60).

Jedwali 3.1 Umri wa Wahojiwa

Kundi la umri	Idadi	Asilimia
Miaka 15- 18	60	30
Miaka 19- 21	45	22.5
Miaka 22 – 25	75	37.5
Miaka 26-50	15	0.75
Miaka 51-60	5	0.25
Jumla	**200**	**100**

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)



Kielelezo 3.3: Umri wa Wahojiwa
Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Kielelezo 3.3 kinaonyesha umri wa washiriki katika utafiti. Kinadhibitisha kipengele muhimu kilichoweza kuathiri matokeo na mazingira ya kiutafiti. Kundi hili linajumuisha wanafunzi wanaoshiriki kwenye shule zinazofundisha watoto, walimu na maafisa wengine wenye asasi hizo jijini Mbarara na wote wanaohusika kwenye ngazi za kielimu kusoma L2 ya Swahili, washiriki wa umri tofauti walikuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu lugha ili kuelewa na kuchanganua kwa urahisi mitindo inayosaidia kusoma L2. Vilevile, kundi hili liliwakilisha wanafunzi wanaofanya maamuzi juu ya mitazamo yao ya kielimu kujiunga na mahusiano kiteknolojia na kidijitali.

Kundi la washiriki kati ya miaka 26-40 lilihusisha watu wa kati ya umri wa vijana na watu wazima, ambapo washiriki wanapewa uzoefu wa kitaaluma na maisha kabla ya kuhusisha mafunzo yanayogusa elimu ya lugha. Washiriki katika kundi hili walikuwa na mtazamo mchanganyiko, wakileta uzoefu unaohusu elimu ya kijamii kwenye mikakati ya kufunza. Wanajihusisha na masuala mbalimbali yanayoshughulikia kazi, jamii na majukumu ya kifamilia, ambavyo vinaweza kuathiri jinsi wanavyojifunza Kiswahili. Washiriki katika kundi la watu wazima miaka 41-60 wanaweza kuwa na uzoefu mkubwa katika kazi na maisha, na wengi wao wanaweza kuwa wanajifunza lugha ili kukamilisha shabaha ya kurahisisha uelewa wa mawasiliano waweze kujihusisha na jamii. Washiriki wa umri huu walileta mtazamo wa kitamaduni na kijamii kuhusiana na lugha. Wanafunzi hao wanaweza kupata shida katika kujifunza, haswa kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia yanayopatikana katika harakati za masomo ya lugha husika. Kuwa na washiriki kutoka makundi mbalimbali ya umri kulisaidia katika kuelewa tofauti zinazojitokeza katika jamii na kitaaluma na jinsi zinavyoathiri mchakato wa ujifunzaji. Utafiti huu uliweza kutoa mwanga kuhusu haja mahsusi yenye makundi tofauti ya umri na mikakati bora ya kufundisha.

Kwa hivyo, Umri wa washiriki katika utafiti kutoka miaka 17 hadi miaka 60 unatoa fursa nzuri inayotumika kufunzia kuchanganua jinsi tofauti za umri na uzoefu vinaweza kuathiri kujifunza lugha. Utafiti huu ulibaini mikakati bora inayolenga kusomesha, hivyo kusaidia katika kuifanya bora hali ya elimu za mashule na vyuo vikuu. Hii inatoa picha kamili ya hali halisi ya changamoto na fursa zinazojitokeza kuhusu hali ya kufunzia lugha shuleni.

3.2.4 Elimu ya wahojiwa

Katika utafiti, washiriki waliohusika walikuwa wale ambao wanachaguliwa ili kufanyiwa utafiti huo. Kila kundi la washiriki linaweza kuwa na sifa na kiwango tofauti, na hii inatoa mtazamo wa jinsi utafiti unavyoweza kuathiriwa na tofauti hizi.

Mtafiti alilengakutafuta habari kuhusu washiriki waliohitimu katika mfumo rasmi wa elimu. Uhusiano huo ulisaidia mtafiti kugundua data zilizolenga kuboresha mpango rasmi unaotumika katika elimu ya kisasa. Wahusika wengi wao walichangia pakubwa kuhusu mambo kadhaa yanayohusu ufundishaji unaofanyika wakati wa hali yanayohusu L1 iliyo Kinyankore ambayo yalihitajika kukusanya taarifa nyanjani. Kama inavyoonyeshwa katika jedwali 3.2 iliyo hapo chini inaonyesha ngazi za kielimu za wahusika.

Jedwali 3.2 Elimu ya washiriki

Wanafunzi walio katika “O’level”	Wanafunzi wa ngazi ya “A’ level”	Wanafunzi vyuo vikuu	Walimu wenye Kiwango cha stashahada	Walimu wenye shahada ya Juu(digri)	Walimu wenye cheti cha Uzamili
60	45	75	05	07	04

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Tukirejelea kwa kina jedwali iliyo hapo juu 3.2 wanafunzi sitini (60) wanasoma katika kiwango cha asasi za upili. Hawa walichaguliwa kwa sababu wanatarajiwa kuwa na hadhi ndogo ya uelewa kuhusu matumizi ya lugha ya msingi. Wanaweza kupata shida

zisizoepukiki wanaposoma L2 mpya, ikijumuisha uelewa wa sarufi, msamiati, namna inavyotumika wakati wa mazingira ya kijamii.

Wanafunzi waliosoma katika ngazi za juu walikuwa arobaini na watano (45) ambao ni wanafunzi waliomaliza elimu ya ngazi ya shule ya sekondari ya juu kabla ya kuingia vyuo vikuu. Wanafunzi hao wana uwezo wa juu kidogo zaidi wanaposoma lugha wakilinganishwa kwa wenzao walio na ngazi ya msingi, na wanaweza kuwa tayari wanajifunza lugha za kigeni au kujiboresha katika lugha wanazozijua.

Wanafunzi walio katika vyuo vikuu walikuwa sabini na watano (75). Hawa ni wanafunzi wanaosoma katika vyuo vikuu na wana ngazi ya juu zaidi ya uelewa wa lugha husika. Hao wanafunzi wanajifunza kwa kina katika masomo yao, na wanaweza kupata umilisi mzuri unaoweza kuwatia moyo kutumia L2 kwenye hali ya kitaaluma na hata kwingine katika mazingira ya jamii isiyo rasmi. Walimu wenye Kiwango cha stashahada /12 walikuwa watano (05). Walimu hawa wana elimu ya ngazi isiyo ya juu, wanaweza kupata tajriba ya kufundisha lakini hawana ngazi ya juu ya elimu. Umilisi wanaoutumia katika kufundisha na kuelewa lugha huweza kuleta mipaka, lakini wanaweza kuwa na maarifa yenye nguvu za lugha. Walimu wenye shahada ya Juu(digri) /12 walikuwa saba (07). Hawa ni walimu wenye digrii, na wana uwezo mzuri kusaidia Watoto kusoma hata kuelewa lugha kutokana na elimu na mafunzo yao rasmi. Wanatarajiwa kutoa mwongozo bora kwa wanafunzi wasomao L2.

Wanaofundisha wenye digri katika uzamili /07 walikuwa wanne (04). Hawa ni walimu waliokuwa katika kuendeleza elimu ya ngazi ya juu zaidi, wakiwa na maarifa ya kina kwenye sehemu zao za kitaaluma. Wanatarajiwa kupata umilisi mzuri unaozingatia lugha hata uwezo wa kufundisha wakitumia namna bora kukamilisha uwezo wa kutumia lugha kwa kurejelea namna bora ya kisasa ya ufundishaji.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Cohen (2007) anaeleza jinsi utafiti unaweza kusanifishwa kwa kuzingatia mchakato wa kupanga, kutoa maelezo, kuchambua matokeo kulingana na vile yanavyotolewa na wahusika wa utafiti. Mtafiti alipanga taarifa kutegemea mafunzo na maswala yenye uhusiano. Mtafiti alikuwa mwangalifu katika kudhihirisha, kupambanua, kugundua, kuelezea, kujaribisha, hata kufasiri taarifa ambazo alizipata kupitia muundo wenyewe wa huu utafiti.

Usanifu katika utafiti huwa jambo linalohitajika ambalo linahusisha kupanga na kuandaa mchakato mzima wa utafiti, kutoka hatua za awali za upangwa mpaka wakati wa kukusanya habari na kuchanganua matokeo. Usanifu ulitambua jinsi matokeo yatakavyowakilishwa katika ripoti nzima ya utafiti

Usanifishaji pia hueleza maswali ya msingi ambayo utafiti unajaribu kujibu na malengo ambayo unataka kufikia. Hii inajumuisha kueleza sababu za kuendelea na utafiti ulio na umuhimu wake katika nyanja husika. Usanifu unaeleza kategoria ya utafiti unayofanya – kama ni wa kiasili, wa takwimu na mambo yote mawili. Usanifu ulieleza mbinu zilizotumika kukusanya data, kama vile, dodoso mahojiano, uchambuzi wa vifaa, kufanya utafiti wa mfululizo. Usanifu pia ulitambua washiriki amabo wanataka kufanya utafiti nao, ikihusisha vipengele kadhaa vya umri, jinsia, mazingira ya kijamii, na kitaaluma. Ulieleza jinsi washiriki watakavyoteuliwa. Hii inaweza kuwa kutumia namna iliyo usampulishaji wa nasibu au usampulishaji lengwa, nyingine zikiwa washiriki na jinsia zao, umri, na vigezo vingine muhimu. Usanifu ulieleza jinsi mtafiti alivyochambua data iliyokusanyika, halafu matumizi ya takwimu, programu za uchambuzi, au mbinu za kiasili za uchambuzi kama mkakati wa kufanya utafiti.

Kwa ujumla, kusanifisha utafiti huwa mchakato muhimu wa kutenga mbinu na rasilimali zinazohitajika ili kufanikisha utafiti. Kujenga mpango mwafaka kiutafiti kulisaidia kuwakilisha matokeo sahihi inayoaminika, na kutoa mchango wa maana kwa uwanja wa masomo husika.

3.4 Sampuli

Sampuli huwa istilahi inayotumika katika utafiti kumaanisha washiriki wachache kutoka kundi kubwa ambalo hupewa nafasi na mtafiti ili kutoa taarifa zinazolengwa kuchunguzwa (Kothari, 1990). Cooper (1989) anasema kwamba kundi linalolengwa na mtafiti linajumuisha jamii kubwa, yenye kuhusisha watu au vitu vile vingine ambavyo mtafiti anavitumia wakati anapokuwa anaanza kuchagua habari ya utafiti. Enon (1998) anaeleza kwamba kundi lengwa linahusu washiriki au mambo ambayo mtafiti anatarajia kupata data kutoka kwao. Hivyo, mtafiti aliufanya utafiti ili kudhihirisha taathira zilizohusu L1 Kinyankore wakati wanaposoma L2 ya Swahili.

Wakati wa kutekeleza utafiti huu, sampuli ilihusisha uchaguzi wa washiriki wachache wa wahusika kutoka katika jamii pana ili kuitumia kuchanganua kazi ya utafiti. Kuzingatia sampuli ni kufuatia kigezo kilicho muhimu sana kwenye kazi ya utafiti kinachohitaji umakini na upangaji. Kichaguo sahihi cha sampuli huenda kikasaidia katika harakati zinazohakikishia yale yaliyotokea kuthibitisha kuwa yako sahihi, yaliyo halali, na yenye manufaa kwa jamii kubwa. Kuelewa vyema aina gani ya sampuli inastahili kuchaguliwa na kutumika katika utafiti, na vile sampuli inavyoweza kutumika vizuri ili kuhakikisha italeta mafanikio kwa utafiti.

3.4.1 Sampuli ya wahojiwa

Cohen na Manion (2003) wanaeleza kuwa usampulishaji huelezwa kama kiwakilishi cha kundi kubwa. Vivyo hivyo, Creswell (2005) anafafanua kwamba usampuli ni kile

kiasi kinachowakilisha kundi kubwa ambalo mtafiti anapanga kulichunguza ili kujumuisha sehemu yote nzima. Aidha, Mligo (2012) anasema kwamba sampuli ni sehemu ndogo ya watu kuwakilisha kundi zima la watu ambao mtafiti anaamini lina taarifa zinazomwezesha mhojiwa atapata majibu ya kile anachokitafitia. Kundi lengwa linajumuisha watu wote wanaohusishwa na utafiti, kulingana na wataalam kama Kothari, Bryman, Kombo na Trump (keshatajwa).

Jedwali 3.3: Sampuli ya wahojiwa

Walengwa	Jumla	Washiriki	Asilimia	Wasioshiriki	Asilimia
Wanafunzi wa Vyuo Vikuu	75	75	100%	0	0%
Wasomao katika sekondali ya juu	45	39	96%	4	0.4%
Wasomao katika sekondali ya chini	60	60	100%	0	0%
Wafunzao Kiswahili vyuoni	13	10	80%	02	20%
Walimu wakuu	05	05	100%	0	0
Maofisa wa Elimu	02	02	100%	0	0
Jumla	200	195	98.3%	05	1.7%

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Katika muktadha wa utafiti, sampuli ya wahojiwa inapaswa kuwa ya kutosha kwa kulinganishia na kile mtafiti anachokusudia kuchunguza, ambapo sampuli hiyo itawakilisha eneo lenyewe ambako utafiti unafanyika. Sababu hiyo inamaanisha kwamba, kulingana na maelezo hayo, sampuli ya utafiti huu ilijumuisha wahojiwa mia mbili (200). Mtafiti alilenga kutumia idadi hii ya wahojiwa ili kupata maoni yanayowakilisha wengine wote mkoani.

Jedwali hapo juu linaonyesha jinsi wanafunzi walio katika vyuo vikuu walikuwa sabini na watano (75). Hawa ni wanafunzi waliomaliza masomo ya sekondari na sasa wanaendelea kusoma katika mafunzo ya Chuo Kikuu. Wanaelewa vizuri misingi yenyewe namna wanaweza kutoa mtazamo wa kina kuhusu njia ya ujifunzaji wa L2, hata vile pia wanaweza kulinganisha uzoefu wanaotumia kwa L2. Wanafunzi katika

asasi za elimu za juu walikuwa arobaine na watano (45). Hawa ni wanafunzi ambao wana uwezo mzuri wanaoutumia kukuza L2 halafu wanaweza kutolewa mawazo kuhusu jinsi lugha ya Kinyankore inavyoweza kuathiri kawaida yao ya kisarufi, msamiati na ushirikiano wa unaotumika kueleza mafunzo ya L2. Wale wanafunzi waliopo kwenye asasi za elimu katika ngazi ya chini walikuwa sitini (60). Hawa ni wanafunzi ambao wanaweza kuwa na uelewa mdogo wa Kiswahili. Hili lilidhihirisha kuwa wanaweza kukumbana na changamoto kadhaa wanapojifunza L2, maoni yao yalionyesha jinsi Kinyankore inavyoathiri uelewa unaosaidia kuelewa L2 kimsingi.

Walimu na wahadhiri wa Kiswahili walikuwa kumi na watatu (13). Walimu hawa wanafanya kazi nzuri sana kwenye utafiti kwa kuwa wao ni wale wanaofundisha Kiswahili. Wanatoa mawazo kuhusu njia za kufundisha na changamoto wanazokabiliana nazo kutokana na athari za Kinyankore kwa wanafunzi wao.

Walimu wakuu walikuwa watano (05) kwa sababu asasi za elimu zilikuwa tano. Walimu hawa walihusika katika usimamizi wa shule na walitoa mtazamo juu ya sera za elimu na jinsi zinavyoathiri mafunzo ya L2, hata taathira za lugha mama kwa kurejelea mtindo wa shule.

Maofisa wa Elimu walikuwa wawili (02) kwa sababu ndio wanaosimamia mambo ya elimu jijini. Maofisa hawa ni muhimu katika kutoa mtazamo unaofaa kuhusu ngazi zote zinazoshughulikiwa na sera zinazohusiana na lugha. Wanatoa mtazamo wa kitaifa au kikanda juu ya shida za kufunzia L2, kwenye mazingira yanayoathiriwa na L1 Kinyankore.

Kwa ujumla, sampuli hii ya wahojiwa ilitoa mchanganyiko wa maoni ya wanafunzi kulingana na viwango tofauti na wataalamu wa elimu, ambayo itasaidia katika kufanya uchambuzi kiundani kabisa kuhusu taathira za Kinyankore wakati L2 inapofundishwa

ikisomwa kama lugha nyingine. Hii inaweza kusaidia kubaini namna iliyo nzuri ya kusomesha na kuifanya iwe bora.

3.5 Usampulishaji

Kulingana na Kothari (1990), usampulishaji ni hali ya kuchagua sehemu ya watu wa kuhojiambao si wengi kutoka katika kundi lingine kubwa lililotumika katika utafiti, ili kuwakilisha kundi zima. Sigh (2007) anaelezea usampulishaji kama mbinu ya kutumia kutoa kiwakilishi kidogo kutoka kwenye sehemu nzima ya wahojiwa kwa lengo la kufanya makisio kuhusu kundi lengwa. Kombo na Tromp (2006) wanabainisha kwamba muundo wa usampulishaji unakuwa kiini cha mkakati wa utafiti kwa sababu unayonyesha mambo yanayochaguliwa ili kufanikisha utafiti. Kwa kuzingatia utafiti huu, sampuli ya wahojiwa iliteuliwa kwa ufanisi kulingana na asasi za elimu kama vyuo vikuu vilivyoteuliwa jijini Mbarara ili kuwakilisha zile asasi nyingine zote katika jamii ya wazungumzaji wanaoelewa Kinyankore na wanaojifunza L2 ya Swahili.

3.5.1 Mbinu za Usampulishaji

Aina za usampulishaji zilizozingatiwa ni mbili: Usampulishaji lengwa, halafu usampuli wa unasibu. Kwa kurejelea utafiti huu, mtafiti alisaidiwa njia zile mbili za usampulishaji, ambazo zilikwishatajwa hapo juu kuwa, usampulishaji lengwa, halafu usampuli wa kinasibu.

3.5.1.1 Usampulishaji lengwa

Usampulishaji lengwa ni pale ambapo sehemu ya washiriki inachaguliwa kimaksudi kulingana na sifa zao maalum katika utafiti. Wahojiwa waliokuwa sehemu ya eneo hili walitambulika kuwa wanafunzi wanaosoma kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, wanafunzi waliwo katika vyuo vikuu, walimu wanaofundisha Kiswahili, wakuu wa asasi ambazo zilishughulikiwa, na wadhibiti ubora na maendeleo ya kielimu wilayani

husika. Walimu walimsaidia mtafiti kuelewa kwa nini taathira kama hizo zinatambulika kutoka kwa wenyeji wa L1 ya Kinyankore wanaojifunza L2 ya Swahili. Aidha, walimu walipendekeza maoni yao kuhusu njia zilizo bora ambazo wanazitumia kuepukana na shida zinazowasumbua wanafunzi wanyankore wanapojifunza Kiswahili. Wadhibiti ubora wa elimu na wakuu wa shule walilengwa moja kwa moja, kwani idadi yao haikukuwa kubwa, hata kutambua vyeo vyao vya kimadaraka viliwezesha mtafiti kupata maoni mbadala kuhusu jinsi wanavyoshughulikia changamoto ya kuwasaidia wanafunzi wa Kinyankore wanaojifunza Kiswahili.

3.5.1.2 Usampulishaji wa nasibu

Mbinu ya usampulishaji wa nasibu iliyotumiwa na mtafiti ni kupata idadi sahihi ya wahojiwa, kwa sababu wahusishwa wote huweza wakamiliki sifa na uwezo sawa. Ruane (2005) anaelezea usampulishaji nasibu kama njia ya kutafuta aina ya usampulishaji ambayo kila mtu kwenye sehemu hiyo ya utafiti ana nafasi kubwa ya kuchaguliwa. Aidha, usampulishaji nasibu unahusisha mchakato ambapo kila sampuli kutoka kwa wahojiwa ina fursa inayolingana kiusawa kuchaguliwa[50]. Koul (2009) anasema kwamba usampulishaji nasibu ni njia rahisi ambapo kila kitu au kikundi kinapewa fursa ile ile kwa wote waweze kuchaguliwa bila upendeleo wowote. Anasisitiza pia kwamba usampulishaji nasibu linganishi huwa ile namna ya usampuli inayoweza kutumika kwa kugawa wahojiwa kwa uwiano sawa. Aina hizi za usampulishaji inasaidia kuondoa upendeleo wakati tunapochagua usampulishaji wa wahojiwa. Kazi ya mtafiti hapa ilikuwa kutumia njia hiyo kupata wanafunzi wa asasi zote ambazo walishiriki kwenye utafiti, halafu walimu, maafisa, na wazazi.

---

[50] Kazi ya Kombo na Tromp (2006) inatoa mwangozo muhimu kuhusu uandishi wa mapendekezo ya utafiti (proposals) na tasisi za utafiti. Katika kitabu chao, wahakiki hawa wanasisitiza umuhimu wa kupanga na kuwasilisha mawazo ya utafiti kwa njia ya wazi na ya kitaalamu.

3.6 Mbinu za ukusanyaji wa data

Sehemu inayohusika hapa inashughulikia vile mtafiti alivyoeleza jinsi data ilivyokusanyika pamoja na mbinu na zana tofauti zilizoweza kutumika katika shughuli zilizotumika wakati wa ukusanyaji wa data hizo. Kothari (1990) anabainisha kwamba ukusanyaji wa data huwa kama hatua muhimu katika utafiti iliyomsaidia Mtafiti kutafuta data iliyofaa kwa sababu ya kutimiza shabaha zake kama ilivyohitakikana na utafiti. Kwa hivyo, kwa kutegemea utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu tatu: mbinu ya maktabani, matumizi ya majadiliano, na hoja. Mtafiti alikusudia kutumia mbinu hizi zote tatu ili kufanikisha namna ya kukusanya data kiurahisi kutoka kwa wahojiwa. Kulitokea miongoni mwa makundi ambapo mbinu moja haingekuwa rahisi kutumika ili kukusanya taarifa kwa kutumia mbinu kadhaa kama hojaji, lakini uwepo wa majadiliano ulisaidia kukusanya data kutoka kwao pia.

3.6.1 Njia za majadiliano katika utafiti

Kwa kurejelea TUKI (2013), majadiliano ni mawasiliano ya kimazungumzo yanayohusu washiriki wawili au zaidi wanaoshirikiana mawazo kuhusu mada maalum. Wataalam wengine kam Tromp na Kombo (keshatajwa) hudai kwamba mbinu hii inamwezesha mtafiti kupata taarifa nyingi na zinazofaa kwa haraka. Kwa hivyo, mbinu hii ilikuwa na manufaa makubwa kutimiza malengo ya utafiti huu. Mtafiti alikusudia kuitumia ili kupata taarifa nyingi kwa muda mfupi. Mbinu ya majadiliano ina faida nyingi, ambazo zinaweza kutajwa ifuatavyo; kwanza, mada ya kujadili inachaguliwa kabla, hivyo kuwapa wahojiwa nafasi ya kujiandaa vizuri ili kuweza kutoa mchango kuendeleza mjadala. Pili, maswali huandaliwa kabla ya majadiliano. Tatu, mwelekeo wa mjadala unategemea uzoefu wa washiriki kuhusu mada inayojadiliwa. Ingawa mbinu hii ina faida, huhitaji kujiandaa ipasavyo kuanzia kupanga michango ya kujadili, washiriki, hadi mahali pa kutekeleza mjadala. Kwa kurejelea utafiti huu, mtafiti

alitumia kategoria zifaazo ili kukamilisha majadiliano; majadiliano yenye mawazo yaliyokuwa yamefungwa, halafu yale yasiyo na maswali funge.

Mtafiti alitumia majadiliano ya vikundi kukusanya taarifa za utafiti. Aliwakusanya wanafunzi wanaofahamu L1 iliyo Kinyankore na Kiswahili katika makundi ya watu saba hadi kumi, wakakutana katika chumba kwa muda tofauti. Kila kundi lilihusisha muda wa kujadili wa dakika thelathini, ambapo lengo lilikuwa kupata maoni, mtazamo, na suluhisho za kukabiliana na athari zinazohusiana na Kinyankore.

Majadiliano yaliyokuwa na maswali funge yalifanyika kwa kufuatia hali teule, yakilenga kupata majibu mafupi, wakati majadiliano yasiyo na maswali funge yalitoa fursa kwa wahusika kueleza mawazo yao kiundani juu ya masuala yanayoulizwa. Kwa kuzingatia utafiti huu, mtafiti alifuatilia kategoria zote mbili za majadiliano ili kutoa nafasi kwa wahojiwa kujieleza kwa uhuru kuhusu taathira zinazosababishwa L1 iliyo Kinyankore wakati wa mafunzo ya L2 ambayo ni Swahili.

Majadiliano yalihusisha walimu wakuu, walimu, maafisa wa elimu, na wazazi. Hawa walichaguliwa kwa sababu kulitakiwa matokeo yaliyo ya kina kuhusiana na zile taathira za Kinyankore wanapokuwa katika harakati za kusoma L2 kati kati ya mazingira ya jamii ya Wanyankore. Mtafiti pia alilenga kugundua mbinu wanazotumia kuwasaidia wanafunzi wanaojifunza L2 ambayo ni Swahili. Mtafiti akitumia mbinu hiyo ya majadiliano, haikuwa ngumu kupata habari walizozitoa wa wenyewe. Wanafunzi waliohusika katika kuhojiwa waliwekwa katika chumba maalum ili kuwezesha mazingira ya kuhojiana bila kuingiliwa na mambo ya nje.

3.6.2 Matumizi ya dodoso

Kulingana na TUKI (2013), dodoso ni ile njia ya kutumia karatasi iliyo na maswali ya kufanyia utafiti. Kwa kutumia njia hii ya dodoso, dodoso hupelekwa kwa wahojiwa

ambao wanahitajika kujibu maswali yaliyoandikwa kwenye karatasi na kisha kurejeshwa kwa mtafiti. Dodoso lina maswali yaliyoandikwa kwa muonekano mzuri, na kwa ujumla linalenga kusaidia wakati wa kukusanya taarifa. Wahojiwa hujibu maswali yaliyopangwa kwenye karatasi hiyo, na njia hizo zilizomwelekeza mtafiti kufanikiwa na data muhimu za utafiti.

Dodoso ni moja ya njia maarufu za kukusanya data katika tafiti za kijamii, na linaweza kutumika kwa ufanisi kutafuta jinsi sarufi ya L1 Kinyankore inavyoathiri usomaji wa L2 Swahili. Kwa kuangalia utafiti huu, dodoso lilihusisha maswali mbalimbali, ikiwemo zile hoja funge nan a maswali yasiyo funge. Maswali funge yalitoa chaguzi za majibu (kama "Ndio" au "Hapana") ambazo ziliwezesha ukusanyaji wa takwimu zinazoweza kupimika, wakati maswali yasiyo funge yalitoa nafasi kwa wahojiwa kujieleza kwa uhuru. Hii ilikuwa muhimu kwa kuelewa mtazamo unaochukuliwa na wanafunzi, hata walimu kuhusu athari za Kinyankore katika uelewa wa kanuni za L2 Swahili. Vilevile, dodoso lilijumuisha maswali ya kulinganisha namna ya kutumia kanuni sahili kati ya Kinyankore na Kiswahili, hali iliyosaidia kubaini maeneo ya uhusiano au tofauti.

Njia ya kutumia dodoso ina manufaa kadhaa wakati inapotumika na mtafiti. Kwanza, inahitaji gharama ndogo hata kwenye hatua za kutumia sampuli kubwa na maeneo mengi.[51]. Pili, njia hii haipendelea majibu yoyote, kwani wahusika wanatoa majibu kwa maneno yao wenyewe. Tatu, wahojiwa wanapata wakati unaowatosha kutoa majibu. Nne, inawawezesha wahusika walio mbali kujibu kwa wakati maalum. Tano, mbinu ya dodoso ina uwezo kutumika katika ukusanyaji wa taarifa likizingatia sampuli kubwa,

[51] Kazi ya C.R. Kothari iliyochapishwa mwaka 1990, "Research Methodology: Methods and Techniques," ni kitabu kinachojulikana kwa kutoa maelezo wazi na yanaeleweka kuhusu hatua na mbinu za kisayansi katika kufanya utafiti.

na hivyo kufanya matokeo kuwa halisi na yanayojiwakilisha. Kwa kuongeza faida hizo, dodoso pia huokoa muda na kuimarisha usiri unaohitaka kutoka kwa wahusika. Hata inavyokuwa, njia hiyo ya dodoso ina mapungufu; kama isiposimamiwa vema, inaweza kuleta data zisizo sahihi, kwani mhojiwa anapewa uhuru wa kujibu leegale, na inaelekeza tu kwa wahusika wanaoweza kutambua yaliyoandikwa na kuyasoma, hivyo kuacha wengine nyuma, ambao huenda wakawa na upungufu wa stadi hizo za usomaji.

Ili kuhakikisha mbinu hii inatoa data sahihi, mtafiti alijiandaa maswali ya dodoso yaliyoajulikana katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ilikuwa utambulisho unaofafanua lengo la dodoso, hata ufafanuzi wa jumla kwa washiriki walio na utambulisho wa mtafiti. Upande mwingine wa dodoso ulijumuisha taarifa binafsi za wahojiwa kama vile umri, wajibu, kiwango cha washiriki kielimu, kabila; majina na mawasiliano hayakuwekwa ili kuwapa uhuru mhojiwa. Wakati wa sehemu hii, mhojiwa alitakiwa kuweka alama ya (√) kwenye chaguo analofikiri ni sahihi. Upande mwingine unaofuata ulikuwa na maswali ambayo yalihitaji mhojiwa kujieleza kwa kina kuhusu maarifa yake yanayohusiana na swali husika, yakiwemo namna ya kutumia ya kanuni za sarufi ya ujumla na athari yakewakati wa kusoma Swahili. Maswali mengine pia yalihusu matamshi yenye mawazo tofauti katika Kinyankore.

Maswali yaliyomo katika dodoso yalikuwa yanahusu kategoria kadhaa, yanayojumuisha funge na yasiyo funge. Mtafiti alikusudia kuchanganya mifumo yote ya hoja kwa sababu ya kupunguza mapungufu ya njia hizo zote, ukizingatia kwamba kuna changamoto za kila mbinu. Kwa hivyo, hizi mbinu mbili zilitumika kwa pamoja ili moja ikamilishe upungufu wa nyingine. Alipofika kwenye sehemu ya utafiti mtafiti alijieleza kueleweka na wanaoongoza asasi teule na kuwaomba ashirikishe wanaofundisha na wanafunzi waweze kuhusika kwenye utafiti. Halafu, mtafiti alieleza

kwa undani kabisa kuhusu njia za kujaza dodoso, hasa wanaofundisha, kufundishwa walioweza kuyatambua na kuyasoma yaliyoandikwa.

Kwa sababu wahusika kama maofisa wa elimu na walimu wakuu hawakuwa na muda wa kujisomea au kujaza hojaji, na mahojiano yalitumika na mtafiti ili kukusanya taarifa zao. Lengo lake lilikuwa ni kufanya zoezi la kutafutaa taarifa kuwa rahisi halafu data iweze kupatikana iliyo sahihi na kukamilisha utafiti. Mtafiti aliwapa wanafunzi dodoso ili wajaze katika darasa lililoratibiwa na walimu. Watoto waliokuwa wanatoa taarifa za utafiti walisimamiwa na mtafiti hata walimu waliojitoakwa hivyo kila mwanafunzi aliyekihitaji msaada alikua na nafasi ya kuupata mara moja.

Kwa kuzingatia utafiti huu, dodoso lililotumika kukusanya data kutoka kwa wahusika waliokuwa tofauti, na hawa walikuwa kina wanafunzi, walimu, na maofisa wa elimu, kuhusu uzoefu wao ambao ungewawezesha kusoma L2 ya Swahili, halafu sarufi ya Kinyankore. Kwa maswali maalum, dodoso linaweza kusaidia kubaini wazi jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoathiri uelewa walionao wanafunzi wa Swahili, hasa katika vipengele kama vile sintaksia, matumizi ya viambatisho, hata upatanisho wa kisarufi.

Kwa hivyo, dodoso lilitumika kukusanya maoni tofauti kutoka kwa wadau mbalimbali, kuwasaidia watafiti kuelewa vichochezi na vizuizi wanapokuwa wanasomeshwa L2 ya Swahili. Kwa ujumla, dodoso ni chombo muhimu kinachotumika kukusanya taarifa kutoka kwa washiriki katika utafiti na kudhihirisha athari za sarufi ya Kinyankore katika mafunzo ya L2 ya Swahili. Katika harakati za kutekeleza shabaha ya utafiti, ni muhimu kubuni dodoso lenye maswali ya maana na lililo rahisi kueleweka, halafu kufuatilia maafikiano kuhusu muktadha wa lugha. Hii itasaidia kufanikisha shughuli za ukusanyaji wa taarifa bora ambazo zinaweza kutoa mwanga wa kina kuhusu mahusiano kati ya sarufi ya Kinyankore kuilinganisha na usomaji wa L2 ya Kiswahili.

Dodoso zote zilipojazwa kikamilifu, zilikusanywa na mtafiti ili zilchambuliwe. Walimu walipewa dodoso walipatiwa muda wa ziada kutokana na majukumu yao mengi ambayo mtafiti aliona wakitekeleza. Mtafiti alikusudia kuzingatia matumizi ya dodoso kama njia bora ya kukusanyia data kutoka kwa kundi kubwa la watu kwa wakati mfupi, hususan dodoso za papo kwa papo. Njia hiyo tena inarahisisha mchakato wa kukusanyia data na kuichanganua baadaye. Zaidi, ikiwa itasimamiwa ipasavyo, data nyingi huenda zikatolewa zikiwa sahihi sana kwa kutegemea uwezo alionaomhojiwa hasa katika hali ya kupata taarifa.

3.6.3 Mbinu ya mahojiano

Mahojiano huwa na mbinu zinazohusisha kumuuliza mtu maswali, ambapo mwitikio wa kisauti hutolewa wakati ambapo mtafiti anarekodi majibu hayo katika daftari. Kulingana na Mdee (2010), usaili hutumika kama njia ya kumhoji mtu ili kubaini uwezo wake katika shughuli fulani. Kothari (1990) anasema kuwa njia hii ni muhimu katika upataji wa taarifa kwa kuzingatia mawasiliano ya mdomo washiriki wahojiwa wakionana na mtafiti. Hivyo basi, ilimbidi mtafiti kutumia haya mahojiano yaliyo wazi aweze kuitumia kupata taarifa ya utafiti. Maswali yaliyo funge yalitumika pale ambapo kunahitajika taarifa maalum, wakati maswali yasiyo fungwa yalitoa mtafiti nafasi ya kujieleza kuhusu hoja zinazohusiana kupata matokeo katika utafiti.

Katika shughuli za huu utafiti, mahojiano yaliyofanyika yakihusisha mtafiti na wahusika, yalitumia mbinu zilizosaidia katika kukusanya taarifa nyingi. Kothari (1990) alifafanua juu ya njia hiyo ya mahojiano kwamba inaboresha mahusiano katika jamii, hivyo kuwawezesha watoa habari kutoa taarifa kwa urahisi. Kwa hivyo, hii mbinu inatumika kwa minajili ya kukusanyia taarifa zinazohusiana na ulinganifu wa taathira ya L2 ya Kinyankore kwa wanafunzi wanpojaribu kufundishwa L2 ya Swahili. Mtafiti aliwezeshwa mbinu ya kuwahoji washiriki aweze kufanikiwa kugundua habari

zilizowahusu wahadhiri, wanafunzi, maafisa wa elimu, na wazazi. Washiriki katika huu utafiti walipewa uhuru wa kujieleza, na kwa hiyo waliweza kumtolea ufafanuzi wa kiundani mtafiti.

3.7 Data za Utafiti

Neno data limefasiriwa kwa kufuatia mitazamo ya wataalamu wengi walio tofauti: TUKI (2013) wanaelezea data kama jumla ya taarifa zilizokusanywa ambazo zitatumika kama msingi wa uchambuzi. Mdee na wenzake (2011) wanasema taarifa za utafiti huwa ni zile data zinazoakisi hali halisi na zinaweza kuonekana katika maelezo au takwimu. TUKI (2013) inasema taarifa inakuwa zile habari au takwimu zinazotumiwa kuelezea au kuthibitisha swala husika. Kwa ujumla, huenda tukasema kuwa hizi habari ni taarifa zilizokusanywa kutoka kwa washiriki walioteuliwa ili kufanya uchambuzi katika utafiti. Mtafiti alikusanya na kurekodi taarifa ambazo zinajulikana kama habari ghafi. Kawaida, haya ni zile habari zinazotolewa na wahojiwa au watoa habari wakati mtafiti anapofanya mahojiano, usaili, au kutumia mbinu nyingine za utafiti. Kwa kurejelea tafiti zote zile, data ina umuhimu mkubwa. Data ilikusanywa kwa sababu nyingi muhimu, na sababu hizo zinatajwa vifuatavyo: kwanza, kusaidia kuchochea mawazo mapya, kwani taarifa husaidia kubaini sehemu ya kufanyia utafiti ambalo linahitaji kuboreshwa na kutathiminiwa. Pili, data inajenga utayari na ugumu katika utafiti. Tatu, data inashawishi sera na sheria za usajili. Nne, data inatoa uthibitisho wa kuwepo kwa dhana mpya katika eneo husika linaloshughulikiwa na utafiti. Basi hayo yote, tunahitimisha kwamba data ina mchango wake wenye thamani sana kwa utafiti, hasa wakati wa kuandika ripoti.

Ili kutoa ripoti bora, mtafiti lazima aelewe vizuri kile alichosikia kutoka kwa watoa habari na aweze kukieleza kwa wazi kwa wasomaji wake.[52] Hivyo, ili wasomaji waelewe kile ambacho mtafiti amekipata kutoka kwenye utafiti, matumizi ya data na taarifa ni muhimu. Wataalamu wengi wa utafiti wana eleza kategoria zinazoeleza data. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), Pons (1992), wanajadili kategoria ya taarifa za utafiti ambazo zinajulikana kama data zilizo za msingi na data ya pili.

3.7.1 Data za msingi

Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuhusu taarifa zinazojulikana kama za msingi kuwa taarifa zinazokusanywa mfululizo kutoka kwa wahojiwa. Kulingana na Mligo (2012), hizo taarifa zilizo za msingi hukusanywa mfululizo kutoka kwenye sehemu ambapo utafiti ulitokea. Hivyo, Mligo anaonyesha kuwa neno data linaweza kueleweka kama "habari" zinazohusiana na utafiti. Kwa ujumla, mbinu zinazotumika kupata taarifa hizo za kimsingi ambao huwa majadiliano, usaili, hoji na ushuhudiaji. Kwenye utafiti huu, mtafiti alifanikiwa kwa kutekeleza habari hizo za kimsingi zilizopatikana kupitia mbinu za hoji na majadiliano ambayo yalionyesha athari za utamkaji wa maneno kwa L2 ya Swahili.

Katika sura hii, utafiti kamili ulifanyika katika mazingira ya nyumbani na maktabani, hasa kwenye sehemu hizo Jijini la Mbarara. Njia nyingi zilizomwezesha mtafiti kukusanya taarifa nyanjani zilijumuisha uwezo wa kuandika Makala, kazi za kutafsiri. Data iliyopatikana kutoka kwa utafiti huu ilichambuliwa kwa maelezo, kujaza hojaji, kuchunguza maneno, kubainisha maneno mapya kwenye makundi, kulinganisha maana za istilahi hasa kuzipanga kwenye takwimu.

---

[52] Mligo E .S. (2012). *Jifunze utafiti mwongozo kuhusu utafiti na utamaduni wa ripoti yenye Mantiki.* Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGY)

Kwa kufuatia utafiti huu, taarifa hizo za kimsingi ziligawanywa katika makundi mbalimbali. Mtafiti alikusanya taarifa za kimsingi mkiwemo data za demografia ya wahojiwa. Mtafiti alikusanya taarifa kuhusu umri, jinsia, hali ya kimasomo na uelewa juu ya lugha wa wahusika. Utafiti huu tena ulikusanya data zilizohusu usomaji wa L2 iliyo Swahili juu ya muda wa kujifunzia, maelezo kuhusu mtalaa wa Kiswahili, data kuhusu muundo wa sarufi ya kinyankore, pamoja na uelewa kwa wanaofundisha na wale wanaosoma kuhusu usomaji wa L2 ya Swahili, pamoja na maelezo juu ya jinsi vigezo vya sarufi ya Kinyankore na vile vya ile ya Swahili vinavyovweza kutofautishwa hata na maeneo ambako wanafunzi wanapatwa na changamoto. Taarifa za kimsingi pia nyingine zilihusu mawasiliano ya walimu juu ya mbinu zenyewe wanazozitumia wakiwa wanafundisha L2 ya Swahili darasani. Walimu waliweza kueleza jinsi wanafunzi wanavyoshughulika utofauti uliopo wa kisarufi. Taarifa kuhusu mkutadha wa kijamii na kiuchumi, halafu jinsi yalivyoathiri ujifunzaji pia ilishughulikiwa.

Data hizi za msingi zilitoa mwanga wa ndani sana juu taathira ya sarufi ya Kinyankore wakati ambapo mafunzo ya L2 Kiswahili yanaendelea. Kupitia uchanganuzi wa taarifa hii, utafiti ulibaini vikwazo na kwa nini wanafunzi wanaweza kupata ugumu au urahisi katika masomo ya L2 ya Swahili halafu pia uligundua maeneo yanayohitaji kuimarishwa kwenye njia zinazotumika kufunzia.

3.7.2 Data za upili

Data za upili ni habari zilizokusanywa na kuchapishwa na wengine, Kothari (1990). Katika utafiti huu, data za upili zilipatikana kutoka Fasihi na Machapisho ya Kiisimu kama Kamusi za Kinyankore na Kiswahili. Hizi zilisaidia mtafiti kulinganisha muundo wa maneno, sarufi, na kupata mifano ya maneno yaliyokopwa tayari. Sarufi za Kinyankore na Kiswahili na marejeleo ya sarufi yalitumika pia kutoa sheria za lugha

hizo, na hivyo yalimfaa sana mtafiti kubainisha mabadiliko ya kimuundo yaliyoweza kusababishwa na mwingiliano. Pia, makala za utafiti na tasnifu yalihusishwa ili kuonyesha kazi za kitaaluma zilizofanywa awali kuhusu kwa mfano ukopaji wa maneno kati ya Kiswahili na lugha za Kibantu, au hasa Kinyankore, ubadilishaji msimbo na kuchanganya lugha kati ya lugha hizo, hasa katika maeneo yanayozungumzwa Kinyankore.

3.8 Vifaa vya data

Vifaa vinavyotumika katika utafiti huwa vile vifaa vinavyotumika katika utafiti zikiwa zimepangwa kukusanyia taarifa ya utafiti. Mulokozi (1983) katika Komunte (2001) amezitaja zana hizo za utafiti zinazoweza kutumiwa kukusanyia taarifa. Hizi huenda zikahusisha tepurekoda, kamera ya video, kamera ya picha, kalamu ya kuandikia kwenye karatasi, hata mashine zilizo na uwezo wa kutafsiri matamshi na maandishi kwa kuwezeshwa na tarakilishi.

3.8.1 Unakilishaji wa data

Kwa kurejelea utafiti huu, mtafiti aliweza kufanikiwa kwa kutumia zana kadhaa ili kuweza kupata rikodi ya data kwa njia ya maandiko.

Mtafiti alipokuwa uwanjani akikusanya data kupitia hojaji, aliwatolea washiriki kifaa cha kuandikisha kwa ajili ya kujaza hilo hojaji kiurahisi. Katika wakati mwingine, mtafiti pia alitumia kitabu na kalamu ya wino kuhifadhi kumbukumbu, kama vile kuangalia idadi ya watu waliokamilisha hojaji, kupanga kazi za kila siku za utafiti, na kuchanganua data zilizokusanywa katika sehemu alikofanyia utafiti. Vifaa hivi pia vilitumika kurekodi maeneo na kuna mambo tofauti yaliyotokea. Mtafiti alichagua vifaa hivyo kwani vilikuwa rahisi kubeba na hazina gharama kubwa.

Matumizi ya kitabu na kalamu ya wino katika utafiti yanajumuisha mbinu mbalimbali za kukusanya, kuhifadhi, na kuchambua data. Kwa kurejelea utafiti wenyewe huu, kitabu na kalamu ya wino ni vifaa vilivyotumika kwa kiwango kikubwa. Washiriki walitumia karatasi kuonyesha matokeo ya kiutafiti kwenye dodoso na namna walivyojaza maelezo yao, kujibu hoja katika utafiti na kutoa majibu ambayo walitumia kalamu. Mtafiti pia alitumia karatasi na kalamu kurekodi mazungumzo, mahojiano, au matukio muhimu wakati wa kutafuta taarifa. Aidha, alitunga muhtasari wa taarifa zilizokusanywa kwa kutumia kalamu na karatasi ili kupata muonekano wa jumla wa matokeo badala ya kuendeleza uchanganuzi kiundani. Mtafiti pia alitumia vifaa hivi kuandaa orodha ya mambo muhimu au maswali yanayotakiwa kuzingatiwa akifanya kutafiti

Matumizi ya kalamu na karatasi kwenye utafiti huwa mbinu rahisi, ambazo zilitoa uhuru ili kuweza kurekodi mawazo, data, hata kuchanganua awali. Hata hivyo, ilimbidi mtafiti kuzingatia njia za kielektroniki na teknolojia za kisasa zilizoweza kuongeza ufanisi wa kutafuta na kuchanganua taarifa.

3.8.2 Tarakilishi

Tarakilishi inajulikana sana kama Kompyuta. Matumizi ya tarakilishi katika utafiti yamefanya kazi nyingi kugeuka sana kuhusu njia ambayo watafiti wanakusanya, kuchambua, na kuwasilisha data. Kwa kuzingatia utafiti huu, kompyuta ilitumika kuunda hojaji, dodoso za kutoa taarifa kwa washiriki. Pia program za kuchora kama *"Excel*" zilitumika kuunda michoro na grafu zinazosaidia kuwasilisha matokeoili iweze kuleta maana kamili ya kazi ya utafiti. Kompyuta pia ilitumika kuhifadhi data nyingi kwa njia salama na ya haraka ya kutumia kama hifadhi ya "*cloud"* au *diski*. Kompyuta ilimruhusu mtafiti kufanya tafiti kupitia vyanzo vya mtandaoni, kama vile maktaba za mtandaoni, machapisho ya kisayansi, na majarida. Kompyuta ilisaidia pia katika

programu za uandishi kama *Microsoft Word* na *Google Docs* zilizotumika kuandika ripoti zinazoonyesha matokeo ya utafiti, halafu makala kwa urahisi. Matumizi ya kompyuta katika utafiti yalikuwa muhimu katika kuifanya bora njia ya kupata taarifa, kuichanganua na kuiwasilisha katika ripoti ya mwisho. Ilimpa mtafiti fursa ya kipekee kutekeleza wajibu wake kwa haraka sana, kuongeza ubora wa matokeo, na kumsaidia kuwasilisha matokeo yake kwa njia ya kisasa na yenye mvuto.

3.8.3 Rununu

Rununu mara nyingi inajulikana sana kama simu ya mikononi. Rununu ni chombo cha kidigitali kinachotumika kuwezesha ukamilishaji wa kimawasiliano. Matumizi ya Rununu katika utafiti yamekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mchakato wa ukusanyaji, uchambuzi, na usambazaji wa data. Kwa kurejelea yaliyopatikana kwenye utafiti huu, Rununu yenyewe ilitumika sana katika mawasiliano yote yaliyohusu utafiti. Mtafiti aliamua kuwezeshwa na Rununu husika kuzungumza na washiriki ili kwa sababu aliifikiria kuwa njia rahisi ya kuwafikia washiriki wa utafiti waweze kuamua kwa pamoja nyakati za kukutana zinazofaa bila kuathiri ratiba ya washiriki na mtafiti. Mtafiti alijaribu sana kuwasiliana na wahadhiri washiriki wa hadhi ya juu, hasa walimu waliokuwa wanashiriki ili kuona kwamba utafiti umefanikiwa. Simu ya mkononi licha tu ya kuwa chombo cha kuwasiliana kwa mtu na mtu lakini pia kimeboreshwa sana ili kufanikisha haja ya kisayansi ya teknolojia inayotumika siku hizi za leo. Simu hii inayoitwa Rununu ilitumika kupiga picha, hata kunasa video, ikatumika kurekodi vituko na kuhifadhi taarifa kikompyuta, na hata kurekodi sauti za washiriki kama rekoda. Kwani rununu hii ilisaidia pakubwa kuwezesha ukusanyaji wa taarifa wakati wa kuchagua taarifa za utafiti.

Kwa kuzingatia taarifa hizi, mtafiti aliweza kutumia program za simu kushughulikia mahojiano ya macho kwa macho na kukusanya taarifa kutoka kwa washiriki katika

maeneo tofauti. Simu ya mkononi iliwezesha mtafiti kufuatilia mitindo na mitazamo kupitia mitandao kuruhusu namna ya kupata taarifa kuanzia vyanzo tofauti.

Simu ilitumika kuhifadhi na kufuatilia mipango na shughuli zinazoletwa urahisi. Pia mtafiti alitumia simu kuwasiliana na washiriki kupitia ujumbe wa maandiko au mazungumzo yaliyo na sauti na video kwasababu ya kurundi nyumbani ili kuweza kupata maoni na mrejesho. Simu ilirahisisha kuwa na mawasiliano ya haraka na washiriki au wadau wa utafiti kwa kutumia programu za ujumbe kama *WhatsApp*. Simu ya mkononi ilitoa uwezekano wa haraka katika maeneo mbalimbali na kwenye hali mbalimbali. Simu ya mkononi pia ilirahisisha mawasiliano ya utafiti washiriki katika tafiti na kufuatilia hojaji na dodoso. Rununu ilimwezesha mtafiti kufanya kazi yake bila kujali mahali walipo, hivyo kuruhusu utafiti wa uwanjani na wa haraka.

Matumizi ya Rununu kwenye utafiti ni chombo muhimu cha kuboresha hatua zote zilizotumika kukusanya taarifa, na kuzichambua, hata usambazaji wa taarifa za utafiti. Pia, matumizi ya rununu ilitoa fursa mpya za ufikivu, ushiriki, na usahihi katika tafiti nyingi, na hivyo kuongeza ubora wa matokeo.

3.9 Uchanganuzi wa Data

Katika harakati za kuchanganua taarifa za utafiti unategemea mbinu mbili: kiidadi na zisizo za kiidadi, ambazo ni za kimaelezo. Kulingana na Mligo, mbinu ya kiidadi inahusisha matumizi ya namba au takwimu katika kuchambua data, wakati mbinu zisizo za kiidadi zinahusisha kueleza hasa kujadili taarifa kupitia maandiko ya maelezo.

Mkabala huu unatoa bayana kuhusu sababu na njia zinazohusiana na matukio yaliyotokea[53]. Kwa jinsi mbinu zilivyo na dhima yake, mtafiti alikusudia kuchambua

---

[53] Kazi ya Kress, S. D. na Tracy, D. T. kuhusu "The Natural Approach: Language Acquisition in the Classroom" inatoa mwandishi wa kina kuhusu mbinu ya "Natural Approach" katika ufundishaji wa lugha. Mbinu hii, ambayo inajulikana kwa kuzingatia mazingira ya kutoa lugha, inataja mambo

taarifa za utafiti akitumia zote mbili. Mtafiti alihusisha njia iliyo ya kiidadi kusanya data za kitakwimu kutoka kwa wahojiwa, wakati mbinu zisizo za kiidadi zilitumika katika uchanganuzi wa majibu yaliyoelezwa, hata kama ni maoni na mapendekezo ya wahojiwa.

Data iliyokusanywa ilikuwa inaelekeza kuchanganua kiundani kwa kina, hasa kutoka utafiti uliofanywa kwenye asasi za elimu kama shule ya sekondari na vyuo vikuu. Hapa, mwanafunzi anatakiwa kuwa Kinyankore zilianishwa tofauti kwa wanafunzi wengine pamoja wakihusisha walimu na maofisa wa elimu. Mtafiti alifanya uchambuzi wa kazi hizo mwenyewe, akizingatia mambo kadhaa kuhusu mchango unaowashirikisha L1 ya Kinyankore na L2 ya Kiswahili, kama vile:

i) Kutathmini maendeleo ya wanafunzi, hasa pale makosa yanapohusishwa na L1, Kinyankore.

ii) Kuchunguza msamiati, ambapo maneno ya Kinyankore yaliyotumika yalirekodiwa na kupitiwa.

iii) Uchambuzi wa sarufi, ambapo vipengele vyote vya sarufi, kama vile ngeli, vionyeshi, na vitenzi, vilichunguzwa ili kubaini jinsi namna sarufi ya L2 inavyoathirika.

iv) Matarajio kutoka kwenye wale maofisa kushughulikia njia zinazoleta kuboresha mafunzo ya L2.

v) Kuchunguza kama athari za sarufi ya Kinyankore zilijitokeza kwenye kujifunza Swahili iliyo L2 ili pia kurekodi athari hizi katika muktadha maalum.

---

muhimu yanayoathiri mchakato wa kujifunza lugha na ina lengo la kusaidia wanafunzi kujifunza lugha mpya kwa njia ya asili na isiyokuwa na shinikizo.

Baada ya hayo, mtafiti alifanya uchambuzi wa msamiati wote wa utafiti, akijitahidi kuelewa kwa undani na kupanga data hizo kwa makundi mbalimbali, akizingatia vipengele vya mikakati inayoshirikisha lugha kwenye Nyanja ambazo ni wa kimatmshi, kimaumbo, kimuundo, na kisemantiki. Pia alilinganisha yale maneno yalivyoakisiwa ile zile za asili ili kubaini zikiwa zilikuwa na mabadiliko ya kimaana

Kulingana na hivyo, Kiswahili na Kinyankore ni mojawapo ya, nomino zilizowakilisha sehemu za ngeli ziliwekwa ipasavyo. Aidha, maneno yaliyokopwa na yanayoweza kuingia katika makundi ya ngeli yalichunguzwa ili kuona jinsi yalivyoweza kuathiriwa na lugha ya Kiswahili. Mtafiti alikusudia kutumia njia hii kwa kuwa zilizobabishwa Kinyankore wanaojifunza L2 iliyo Kiswahili, sambamba na kukusanya maoni na mapendekezo kutoka kwa watu waliokuwa wakisaidia wanafunzi hao.

3.10 Uthabiti na Kuaminika kwa Mbinu za Utafiti

Utafiti wa sasa pia ulizingatia uthabiti wa namna ya kupata taarifa ili kukubalika kwa data. Hii inafanyika kwa uthabiti na kuaminika kwa utafiti. Kuthibitishwa kwa uthabiti na kuaminika ni hatua muhimu katika kutekeleza mahitaji ya utafiti, kwani huzungumzia juu ya ubora unaozingatia kanuni za kisheria kuthibitisha matokeo yanayopatikana. Wakati wa kutekeleza utafiti, mtafiti anapaswa kuchukua hatua ya kudhihirisha kwamba kazi ya utafiti imetimiza hali ya juu ya uthabiti na kuaminika, kama vile kutumia zana za utafiti zilizothibitishwa, kwa sababu ya kuleta njia ya kuonyesha kujaribu kwa kipindi tofauti, na kutathmini matokeo kupitia vyanzo mbalimbali. Hii inasaidia kuhakikisha kuwa muhtasari wa kuhitimisha kazi hii ya utafiti inaweza kuaminiwa na hutumika kwa madhumuni tofauti katika utafiti au maamuzi ya kisayansi.

3.10.1 Uthabiti wa mbinu za kukusanya data

Tukirejelea zile sifa muhimu za taarifa za utafiti ni kuzingatia ule uthabiti wa data zilizokusanywa. Kulingana na mtaalam Kothari (keshatajwa) huonyesha uthabiti kwa kusisitiza hali ya taarifa ambayo mbinu za utafiti zinapima kile kilichokusudiwa kupimwa. Inasisitizwa kwamba mbinu zote zilizoundwa zililenga tafiti zinazopaswa kupimwa ili kuthibitisha kama zinafaa kufanyika kwenye mikutadha halisi iliyokusudiwa[54]. Mtafiti alikusudia kupima maswali kwa watu ambao sio walengwa, lakini kimsingi wanafanana kulingana na sehemu zinazohusu elimu kabla taarifa hazijakusanyika. Lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha maswali yanaweza kutumika vizuri. Aidha, ilikuwa muhimu kuangalia kama mtafiti angeweza kupata taarifa au data anazotarajia kulingana na utafiti wake. Kwa kuzingatia utafiti wa sasa, maswali yalijaribiwa kwa kuwahoji wazungumzaji asilia wanaohusika kutumia L1 ambayo ni Kinyankore.

3.10.2 Uaminifu wa data

Mligo (2012) anasema kuwa taarifa za utafiti huwa zinaaminika kwa kutegemea uwezo wa njia za kufanyia utafiti kuzalisha matokeo sawa ambayo yalikusudiwa kupatikana njia hizo zikitumika vizuri. Kuaminika hujumuisha ushirikiano kuhusu taarifa zinazotolewa na wenyeji waliohusika katika nyakati tofauti. Kwa kufuatia utafiti wa sasa, uaminifu wa taarifa za utafiti ulithibitishwa kupitia mbinu nne ambazo mtafiti alitumia kukusanya taarifa za utafiti. Kwa kuangalia sehemu hiyo hapa, taarifa ziliwasilishwa mtafiti akitumia michoro, majedwali, vielelezo na hata maelezo ambayo ilisaidia katika uwasilishaji ili taarifa zote za utafiti ziweze kueleweka kwa urahisi.

[54] Kazi ya Sigh K. (2007) inatoa mwangaza kuhusu mbinu za utafiti na inajikita katika kuelezea mchakato wa utafiti wa kisayansi. Kwa ujumla, Sigh K. (2007) ni chanzo muhimu kwa wanafunzi, watafiti, na wataalamu wanaotaka kuelewa vyema mchakato wa utafiti wa kisayansi na mbinu zinazohusiana na ukusanyaji na uchambuzi wa data.

Utafiti wa sasa ulitegemea mtindo wa maelezo katika kuwasilisha data. Kuwasilisha taarifa ya utafiti wa sasa ilithibitisha ya kwamba mbinu hii ilikuwa njia ya kibinafsi ambayo haikuhitaji matumizi ya kanuni nyingi za kihesabu na majedwali. Kwa hivyo, Utafiti wa sasa ulitegemea mtindo wa maelezo na takwimu kwa ajili ya kubainisha taarifa zile muhimu kutoka kwa wahojiwa.

3.11 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha malengo ya utafiti huu, mtafiti aliwapa wahojiwa maelezo kuhusu mikakati ya kimaadili yanayotawala tafiti za kitaaluma ili waweze kutoa data zilizo kamili za kuaminika. Kulingana na Aaker (2002) kama alivyotajwa na Adamm (2008), uadilifu wa kiutafiti unajumuisha haki ya mhojiwa kutekeleza mikakati ya kuheshimu taarifa za watu kisiri, ambayo inamaanisha kuwa mtafiti hataruhusiwi kufichua taarifa za siri za mshiriki wa utafiti. Yeye Mligo katika kazi yake ya mwaka 2012 anabainisha kwamba maadili ni sheria zinazoongoza wanajamii ambazo zinaongoza tabia na mwenendo unaoangalia jinsi wanajamii wanavyoishi. Pia, anasisitiza kwamba mhojiwa anapaswa kuelezwa jinsi atakavyokuwa na amani kiusalama, kuwa na uwezo wa kufahamu malengo yanayoongoza utafiti, uwezo wa kupokea yaliyotokea kwenye utafiti hasa kupata majibu ya maswali atakayoulizwa, hata mshiriki akiamua kutohusika katika utafiti hastahili kuzuiliwa. Kwa hivyo, kwa kuangalia utafiti huu, mtafiti alihakikishia wahojiwa usiri wa mazungumzo yao. Aidha, mtafiti alihifadhi siri za wahojiwa wake, na hasa taarifa na mahojiano yaliyofanyika wakiendeleza utafiti huu. Usiri huo ulidumishwa, kwani mtafiti alizingatia umuhimu wa kukadiria maadili ya kiutafiti.

3.12 Mpango wa Ushiriki wa Jamii

Mpango wa ushiriki wa jamii ni sehemu muhimu sana, ambayo hujitokeza katika kazi ya utafiti kwa njia mbalimbali, hasa katika masomo yanayohusisha moja kwa moja watu, jamii, au mabadiliko ya sera, Kothari (1990).

Madhumuni makuu ya mpango wa ushiriki wa jamii yalikuwa kuhakikisha kwamba utafiti unafanyika kwa maadili, Jamii ya washiriki ilijua, na kukubali, na kushiriki katika maamuzi yaliyoathiri utafiti na matokeo yake. Mpango wa ushiriki wa jamii pia uliendelezwa kudhihirisha kwamba matokeo ya utafiti yanatumiwa na jamii kunufaika baada ya utafiti kukamilika.

Utafiti huu ulihusisha mijadala ya vikundi lengwa katika hatua ya kupata taarifa iliyokuwa inalengwa na baadaye kusambaza hizo taarifa zilikusanyika. Usambazaji unakuwa na lengo la kueneza matokeo ya utafiti kwa kupitia warsha, kongamano, mitandao ya kijamii, na hata uchapishaji wa makala. Uchapishaji wa matokeo na usambazaji wa nakala za matokeo kwa jumuiya zinazoshiriki ulisisitizwa.

3.13 Muhtasari

Kwa kuzingatia sura ya mbinu hii, mambo mengi yamejadiliwa kama eneo pamoja na njia zote ambazo mtafiti alizizitumia kupata taarifa, kuwasilisha, kuchanganua taarifa zilizokusanyika za utafiti. Tumeanza kwa kuelezea sehemu utafiti ulikofanyika ambalo ni asasi za elimu katika jiji la Mbarara, na kisha tumeendelea kuangazia vipengele vingine mbalimbali. Vipengele hivi vilihusisha usanifu wa utafiti, washiriki waliochaguliwa kuhojiwa, sampuli zilizolengwa, njia ambazo mtafiti alizozifuata kupata taarifa kwa mfano mahojiano, dodoso, hojaji, namna ya majadiliano. Njia ya hojaji imetumika kama mbinu kuu ili iweze kusaidia kupata taarifa tangulizi ya utafiti wa sasa. Aidha, mbinu ya maelezo imekuwa muhimu kwa kutekeleza uchanganuzi wa

taarifa zilizokusanywa. Mwisho, sehemu hii tunaonyesha na kujadili vipengele vilivyodhihirisha taarifa za utafiti, uthabiti na ukubalifu wa data, vifaa vilivyotumika, halafu mambo yanayozingatiwa katka utafiti wowote.

Katika sura inayofuata, tunaangalia mtagusano unaojitokeza ukuhusisha L1 Kinyankore na L2 Kiswahili. Tutakagua pia chanzo cha athari hizo na namna zinavyoonekana za lugha hiyo hiyo.

SURA YA NNE

ATHARI ZA SARUFI YA KINYANKORE NA MAFUNZO YA KISWAHILI KAMA L2

4.0 Utangulizi

Kwa kuzingatia hii sura hapa, tunaangazia Uwasilishaji wa kuchanganua taarifa zilizokusanywa unalenga kujadili lengo maalum la kwanza, ambalo lilikuwa ni kutathmini jinsi lugha ya Kinyankore inavyoathiri masomo ya L2 ya Swahili. Katika surah hii, vigezo vilivyojadiliwa vinahusu mchango wa mwingiliano wa L1 Kinyankore ikiathiari masomo ya L2 ambayo ni Swahili kwa ngazi zote za kimatamshi, kimiundo, kimsamiati, na kimaana. Ili kutimiza lengo hili, utafiti huu umezingatia vile lugha hizi mbili huenza kuathiriana kwenye vigezo vya kimatamshi, kimaumbo, kimuundo, na kisemantiki.

4.1 Aina za Fonimu za Kinyankore

Kulingana na wataalam kama Karanja na Habwe (keshatajwa) wanazungumzia jedwali hilo la kiabjadi la kimataifa la IPA kuwa linaainisha silabi zinazotumika katika L1 kwenye makundi tofauti kulingana na sifa zao. Tukijaribu kueleza jinsi sauti zinavyotamkwa, sauti hizi zinagawanywa kwa kufuatia kategoria mbili kuu: konsonanti na vokali. Kwa mujibu wa magwiji wa kiisimu, sauti za nusu irabu zimeainishwa kama konsonanti. Hivyo, tunaweza kusema kuwa hiyo L1 Kinyankore huwa na konsonanti 22, ikiwa na nusu irabu 02. Aidha, kuna sifa zinazotumika kufafanua kategoria za irabu, kama urefu wa vokali na mkondohewa. Vokali ikivutwa ili kuwezesha utamkaji wa neno, na ikiwa haikuvutwa, neno linaweza kubadilika maana, huitwa vokali ndefu.

Vokali ndefu huwakilishwa kwa kurudia hiyo vokali kiothografia. Kwa mfano, maneno **<bana> na <baana>** yanatofautishwa kimaana, ambapo vokali **[α]** ni fupi kwenye lileneno lililotangulia kwanza, na ndefu kuzingatia lile lililofuata la pili. Vokali ndefu

huonyeshwa kifonetiki kwa diakritiki [:], hivyo maneno haya yanaweza kuwakilishwa kifonetiki kama **[b ɑ n ɑ] na [ba:na].**

Maganga na Schadeberg (1992) wamesema kwamba kuna lugha nyingi zinazofanana na Kinyankore zilizo na mfumo wa irabu saba. Hata hivyo, mtafiti alipofanya utafiti wa kimaeneo aligundua kuwa Kinyankore kina irabu tano fupi.

4.1.1 Vokali fupi za Kinyankore

Irabu katika Kinyankore kama ilivyo tukiangalia mifumo ya sauti zote inachangia pakubwa kujenga muundo wa sarufi. Kinyankore hutumia muundo wenye irabu ambazo zinachangia kujenga mpangilio wa kutunga neno na kuonyesha muktadha wa kisarufi.

Lugha ya Kinyankore ina irabu tano kuu, ambazo ni, **-a-, - e-, - i-, - o-, na - u-.** Irabu hizi zinaweza kuunganishwa na konsonanti ili kuunda silabi tofauti halafu baadaye kukaundwa neno. Lugha hiyo ya Kinyankore ina irabu ambazo zinaweza kubadilika kidogo kufuatilia jinsi muundo wa matamshi ulivyo.

Jedwali 4.1: Namna ya kutumia vokali tano fupi

Irabu	Neno (Kinyankore)	Maana yake kwa Kiswahili
/ **a** /	[βara]	hesabu (kuhesabu vitu au pesa na kadhalika).
/ **ɛ** /	[hɛnda]	Vunja
/ **i** /	[imuka]	Amka
/ **ɔ** /	[kora]	Fanya
/ **u** /	[βura]	Potea

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)



Kielelezo 4.1: Sauti za Vokali Fupi za Kinyankore

Kila irabu inaweza kutoa maelezo yasiyofanana ikitegemea namna inavyotumika katika maneno. Mabadiliko ya irabu yanaweza kuathiri jinsi maneno yanavyoeleweka na kutumiwa, kwa sababu ni bora kuzingatia kila badiliko dogo la irabu linaloweza kubadilisha maana kabisa.

Utafiti wa sasa huu hapa uligundua kwamba ingawa Kiswahili pia kina irabu, mifumo ya sarufi na matumizi yao ni tofauti. Kinyankore inajulikana kuwa na sarufi yenye utata zaidi na ina muktadha mzuri wa utamaduni wake. Kwa hivyo, ingawa Kinyankore na Kiswahili zina irabu zinazofanana, jinsi zinavyotumika na athari zao katika kujenga maneno kimaumbo na kisintaksia ni tofauti.

4.1.2 Irabu ndefu

Wataalam wengine kama Massamba (keshatajwa), wanabainisha kwamba vokali ndefu ni irabu inayotumia muda mrefu zaidi katika kutamkwa. Mtafiti pia alitambua kwamba Kinyankore kina irabu tano ndefu. Kama vile inavyoonyeshwa katika maneno yanayofuata kama inavyoonyeshwa chini:

Jedwali 4.2: Namna ya kutumia vokali ndefu

Irabu	Neno (Kinyankore)	Maana yake kwa Kiswahili
/ **a** /	[βa:sa]	Weza
/ **ɛ** /	[rɛ:ta]	leta
/ **i** /	[handi:ka]	Andika
/ **ɔ** /	[β ɔ:na]	wote
/ **u** /	[ɛhu:ma]	uma

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Katika Kinyankore, irabu ndefu ni irabu ambazo zinachukuliwa kuwa na muda mrefu kadri zinavyotamkwa. Mara nyingi, irabu hizi zina umuhimu katika kugeuza kusudi la neno au sauti. Ijapokuwa irabu za Kinyankore zinajulikana kuwa na urefu tofauti, hakuna mfumo rasmi wa kuonyesha irabu ndefu kama inavyopatikana kwenye mifumo ya sarufi nyingine.

Irabu ndefu zinatamkwa zikirefushwa zaidi kuliko irabu fupi. Hii inaweza kuwa na athari kwenye kusudi la sauti. Irabu ndefu zinaweza kuwa na matumizi maalum katika vifungu vya kisarufi, kama vile kategoria ya Nomino na kitenzi.

Mabadiliko ya irabu kutoka iliyo fupi hadi kwenye ile iliyo ndefu yanaweza kubadilisha sababu ya neno. Mabadiliko haya yanaifanya kuwa muhimu kurahisisha mafunzo ya L2 kuelewa tofauti hizo. Katika kusoma L2, tuzingatie ubora wa kuelewa umuhimu wa irabu ndefu za Kinyankore na jinsi zinavyoathiri maana kwa kuzingatia mazingira ya maneno. Ingawa hakukuwa na angalizo maalum la irabu ndefu katika sarufi ya Kinyankore, maarifa haya huwa ya lazima kufuatiliwa na wasomaji wote wasomao somo hilo la L2 hiyo.

Jedwali 4.3: Kiolezo cha vokali za Kinyankore

Vokali	/a/	/aa/	/ ɛ/	/ ɛ:/	/i/	/ii/	/ ɔ/	/ ɔ:/	/u/	/uu/
Juu	-	-	-	-	+	+	-	-	+	+
Chini	+	+	-	-	-	-	-	-	-	-
Nyuma	-	-	-	-	-	-	+	+	+	+
Mbele	-	-	+	+	+	+	-	-	-	-
Mviringo	-	-	-	-	-	-	+	+	+	+
Urefu	-	+	-	+	-	+	-	+	-	+

Jedwali 4.3 linaonyesha Matriki ya irabu za Kinyankore inayohusisha namna vokali zinavyoainishwa na jinsi wanavyojenga maneno na silabi katika lugha hii. Matriki hii inasaidia kuelewa jinsi sauti zinavyoungana zikaunda umbo la neno halafu zikajumuisha vipengele mbalimbali kama vile, silabi, vifungu na kuunda silabi zenye mfumo unaoleta maana.

Kinyankore ina sheria anuwai zinazohusiana na uratibu unaounganisha konsonati na vokali kuunda silabi, kama vile sauti zinazoweza kuunganishwa na zile zisizo na kuunda maneno. Hii inapaswa kuzingatiwa katika kujifunza au kuandika Kinyankore. Kwa hiyo, matriki ya irabu za Kinyankore ni nyenzo muhimu katika kuelewa namna

silabi na maneno na lugha vinavyoundwa vyote, halafu jinsi maneno yanavyoundwa, pamoja na kuelewa muktadha wa kisarufi na kiutamaduni. Matamshi ya irabu yanaweza kubadilika kwa kutegemea mkutadha uliopo. Hivyo, muktadha wa kisarufi huwa wa manufaa ili kupata maana sahihi. Jambo hili linasababisha jinsi sauti zinavyoweza kubadilika kutegemeana mikutadha inayosababisha matumizi ya sentensi.

4.1.3 Konsonanti za Kinyankore na Kiswahili

Konsonanti za Kinyankore na Kiswahili zinafanana kwa kiwango fulani, lakini pia kuna tofauti muhimu kati ya lugha hizo. Kinyankore, ikilinganishwa na lugha nyingine za Kibantu, ina konsonanti nyingi, ambazo zinajumuisha:

Vipasuo /p/, /t/, /k/, /b/, /d/, /g/

Vikwamizwa: /f/, /s/, /h/, /v/, /z/, /β/

Vizuia kwamizwa: / ɟ /, / ʧ /

Nazali: /m/, /n/, /ŋ/

Kitambaza: /l/

Kimadende: /r/

Viyeyusho /w/, /j/

Konsonanti za Kinyankore zinaelezwa katika jedwali 4.4 lifuatalo chini hapa.

Jedwali 4.4: Konsonanti na Nusu Irabu za Kinyankore

Jinsi ya kutaja sauti	**Sehemu ya kutajia**								**Hali ya Glota**
VIPASUO	Midomo	Midomo meno	Meno	Ufizi	Kaaka gumu na ufizi	Kaaka gumu	Kaaka laini	Koromeo	
	b			d			g		Ghuna
	p			t			k		Hafifu
VIZUIWA						/ ɟ /			Ghuna
						/ ʧ /			Hafifu
VIKWAMIZWA	β	v		z				H	Ghuna
		f		s	ʃ				Hafifu
NAZALI	m	ɱ		n		ɲ	ŋ		Ghuna
KITAMBAZA				l					Ghuna
KIMADENDE				r					Ghuna
VIYEYUSHO	w					y			Ghuna

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Tofauti na Kiswahili, kulingana na vile inavyodhihirishwa kwa jedwali hilo juu, inavyoonekana Kinyankore hakina sauti /r/, /x/, / **ð/, / ɣ /, /Ɵ /.** Sauti ya /b/ inapatikana hapo maneno yanapokuwa ni ya mkopo na asili yake si Kinyankore, ambayo yalitoholewa kuwa ya kinyankore kama vile **[ɛbakuri], [ɛba:fu], [baibuli].**

Pia, Kazi ya utafiti huu inakubaliana na mtaalam Dimendaal (2011) aliyewanukuu mabingwa wa lugha kina Maganga akiwa na Schadeberg (1992) wakisema kwamba sauti huenda ikabadilika kimatamshi kutoka lugha moja kwenda nyingine. Ndiposa, Utafiti huu ukabainisha ya kwamba sauti /b/ inayopatikana katika Kiswahili inaonyeshwa katika Kinyankore kama sauti /β/, na hivi ndivyo lugha nyingi zenye asili ya kibantu zinavyokuwa. Mifano inaweza kutolewa katika Kinyankore kama neno ‘abaabo’, linaweza kuandikwa kama **/aβa:βo/** badala ya **‘aba:bo’.** Mfano mwingine ni neno ‘ebiintu” ambalo linatamkwa kama **/eβi:ntu/** badala ya **/ebi:ntu/**

4.2 Jinsi Kiswahili kinavyoathiriwa na L1 ya Kinyankore

Imekwishaonyeshwa hapo mwanzoni kwamba shabaha ya utafiti huu ni kubaini athari za sarufi za Kinyankore wakati masomo ya L2 iliyo ya Kiswahili yanaendelea. Takwimu ambazo zilikusanywa kwa matumizi ya njia ya hojaji, majadiliano, na mahojiano katika utafiti na zinadhihirisha taathira hizo za L1 Katika masomo ya L2. Mtafiti alikusanya taarifa kutoka kwa washiriki akiwahoji na kunakiri maoni yao yaliyohusiana na lengo hili. Kwa kurejelea kazi hii, tulitambua kwamba kunajitokeza zile taathira nne zilizo kuu ambazo zinaonyesha watoto wa Kinyankore wakijifunza L2 ya Swahili. Athari hizi hudhihirika kwa kupoteza maana ya maneno yaliyotumika, athari za kimsamiati kubadilisha maneno yenyewe, ziliathiri pia namna ya matamshi kwa vile maneno yalivyotamkwa tofauti, halafu kuathiri kisintaksia jinsi muundo wa sentensi unavyojengwa.

4.2.1 Athari za kisemantiki (maana)

Wataalam kama Lusesa (keshatajwa) wanasisitiza kuwa tawi la kisemantiki hudhihirisha ujuzi wa maana, na linajihusisha na kutambua vile maneno yanavyoeleweka kutimiza kusudi la mawasiliano ya binadamu kwa mkutadha wake. Uwanja wa kisemantiki nu ule uwanja wa kiisimu unaoshughulikia uchambuzi wa maana ya maneno katika lugha na inazingatia maana iliyo wazi pamoja na ile iliyofichika. Aidha, semantiki inashughulikia uchambuzi wa maumbo yanayotumika kutunga sentensi zinazobeba maana zinazotumiwa kueleweka kukamilisha matumizi ya lugha husika. Kulingana na kazi ya sasa, ilibainika kuwa wazungumzaji wa Kinyankore walikuwa wakifanya makosa ya kisemantiki katika matumizi yao ya maneno. Kielelezo kinachofaa ni vile msemaji anayezungumza Kinyankore anaweza kusema **"Wanazina mziki"** badala ya **"wanacheza mziki,"** ambalo ni kosa la kisemantiki linalojitokeza mara nyingi kwa wanyankore wajifunzao L2 ya Swahili. Semantiki, kama fani ya isimu,

inashughulikia utafiti unaolenga kuchanganua maana za maneno au sentensi katika lugha. Taaluma hii inachunguza maelezo yanayapatikana kutoka matamko fulani ya mambo halisi na hisia kwa namna inayoeleweka. Semantiki inatoa makini kwenye maana za mofimu, fonimu, neno, na tasifa. Kwa hivyo, mtafiti alikazia athari zote za kisemantiki zinazotokea kutoka kwa L1 ya Kinyankore na wanafunzi wanaosoma Swahili kama L2 kuzingatia maana za maneno yaliyotumika.

Data za uwanjani zinaonyesha kwamba kuna Watoto wa Kinyankore wanaosoma L2 kwa Kiswahili wanatafsiri maneno au sentensi wakifanya makosa; hali hii inasababisha athari za kimaana katika Kiswahili. Katika mahojiano yanayohusisha Watoto wa Kinyankore, mara nyingi walipendelea kusema "wanafunzi walizina pamoja" badala ya **"walicheza pamoja"** na **"napigwa kichwa"** badala ya **"naumwa kichwa".** Makosa haya yanaweza kufanya iwe vigumu kwa wasikilizaji wa Kiswahili kuelewa maana halisi ya sentensi hizo. Maneno mengine yanayoonekana yakitoa maelezo yenye yasiyo sahihi kwa Kinyankore kwenda L2 ya Swahili ni neno kama **"kaka",** ambalo kwa Kinyankore lina maana ya **nyanya/bibi**, na kumbe kwa Swahili huwa linamaanisha ndugu wa kiume. Matokeo ya utafiti huu yanathibitishwa na Rocha (2011), ambaye alifafanua kwamba taathira zinazohusu maelezo ya maneno zinazojitokeza katika Kiswahili zinaweza kuchochewa ujuzi wa L1 iliyotangulia. Ingawa makosa haya ya kimaana yanakubalika na kuonekana kuwa yanajulikana na kueleweka na watumiaji wa Kiswahili, yanatia doa yakitumika bila maelezo zaidi ya kutosha kufanikisha mawasiliano. Wakati mwingine, makosa haya yanaweza kuathiri mawasiliano, hasa pale neno linapopata melezo yasiyo sahihi kama ikiwa mzungumzaji wa Kinyankore anaposema "kuzina" badala ya "kucheza" na **"napigwa"** badala ya **"naumwa."**

Mifano ya taathira ya Kisemantiki inaonyeshwa katika jedwali namba 4.5 hapo chini zinazotokana na makosa yanayofanywa na watoto wa Kinyankore wakati kufunza Kiswahili.

Jedwali 4.5: Jinsi L2 inavyoathirika Kisemantiki

Kosa	Neno lengwa
Napigwa Kichwa	Naumwa kichwa
Walizina pamoja	Walicheza pamoja
Aliingiza chaja	Alichomeka chaja
Walitoa msumari	Walichomoa msumari
Nimepigwa Mvua	Nimenyeshewa
Alienda paka chini	Alishuka/aliteremka hadi/mpaka chini
Nasikia Njaa	Nahisi njaa

Neno	Maana kwa Kiswahili	Maana kwa Kinyankore
Kaka	Ndugu wa kiume	Mama anayemzaa Mzazi wako (Nyanya/Bibi)
Kiti	Mahali pa kukalia	Kijiti kama kuni
Paka	Mnyama afugwaye nyumbani	Kujivunia na kuhisi kiburi
Mpaka	Mahali ambapo majirani wanapotengana	Hadi
Ita	Kumwambia mtu aje	Kuua
Enda	Kutoka	Tumbo/ mimba
Ndiyo	Kukubali / "Naam"	Niko
Zina	Kitendo cha ngono	Kucheza

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Katika jedwali 4.5, inadhihirika kwamba wanafunzi hutumia maneno yanayofanana au yanayokaribiana kudhihirisha mfumo wa L2 ya Kiswahili sanifu wakiamini kwamba maelezo yake yatakuwa sawa. Mfano mmoja ni pale mwanafunzi anaposema, **"Napigwa kichwa,"** ambapo kitenzi **"kupigwa"** linachanganya na kuondoa maana halisi, kwani inabakia kuwa ni swali la jinsi kichwa kinavyoweza kumpiga mtu; je, kichwa kinatumia fimbo kumchapa mtu au kinachapwa? Kuna maneno yaliyotumiwa na wanafunzi yakatoa maelezo ambayo hayakuwa sawa na maana lengwa. Mifano iliyotolewa hapo juu kwenye jedwali inaelezwa hapa chini ifuatavyo; kauli ya **"Walizini pamoja,"** matumizi ya neno **"kuzini"** lenye maana ya" kucheza" kwa

kinyankore na maana ya “ngono” kwa Kiswahili. Neno “walizini” kwa hivyo badala ya kukamilisha maana ya kucheza, linaleta mkanganyiko wa maana.

Hali kadhalika, sentensi **“nasikia njaa”** badala ya **“nahisi njaa”** inatoa maana ya kwamba masikio yana uwezo wa kusikia njaa, jambo ambalo linakuwa na maelezo tofauti na linapotosha maana halisi ya **“kuhisi”.** Kikawaida, Wanyankore huwa wanasema “nimpurira enjara” kauli inayomaanisha kwamba “nina njaa”, lakini wakitafsiri neno “nimpurira” kwa Kiswahili linakuwa “ninasikia”. Kwa hivyo linapotumika katika mkutadha wa njaa, huwa linapotosha maana.

Matokeo haya yanatoa picha ya kile ambacho kimeelezwa kwenye Nadharia ya Giles, ambayo inaeleza kwamba makutano au mawasiliano ya kiisimu huwa yanatumika kwa watu wengine ili kupokea kukubalika katika jamii hiyo. Vilevile, katika jedwali 4.5, mahojiano yanayohusu Watoto wa Kinyankore yanaonyesha mara nyingi walipendelea kusema **"wanafunzi walizina pamoja"** badala ya "walicheza pamoja". Na tayari tumeonyesha hapo juu vile maana ya “walizini” inapochukuliwa kuwa kwa Kiswahili. Wengine walitumia **"Alileta ekiti"** badala ya **"Alileta kiti"**. Neno “ekiti” kwa kinyankore linamaanisha “kijiti” katika Swahili. Kwa akisema “alileta ekiti” inakuwa na maana ya kuleta kijiti na siyo Kiti ambacho msemaji alilenga kumaanisha.

Kauli ya **"Walimwita"** badala ya **"Walimuua"** pia ilijitokeza ambapo msemaji alilenga kumaanisha “walimuua” na akatumia “walimwita” kwa sababu “kuita” katika kinyankore ni kuua, kumbe katika Kiswahili ni kumwita mtu akaja kwako. Makosa haya yanawafanya wasikilizaji wa Kiswahili kutofahamu maana halisi ya sentensi hizo.

Aidha, kulijitokeza maneno kadhaa yaliyodhihirisha yana maana zisizo sawa na maana lengwa kutoka Kinyankore na kwenda Kiswahili. Kwa mfano, neno **“kaka”** katika

Kinyankore linamaanisha **Nyanya/bibi,** wakati katika Kiswahili linamaanisha ndugu wa kiume.

4.2.2 Athari za kimsamiati

Pia, Mtaalam aitwaye Massamba (keshatajwa) alifafanua ya kwamba Msamiati huwa ni istilahi zinazojitokeza kutumika katika mazingira yanayohusika. Hii inaashiria kuwa maumbo hayo yanaweza kuleta maana inayotofautiana na maana inayoeleweka na inayotarajiwa. Vilevile utafiti huu unatafiti jinsi maana ya msamiati mpya ilivyoibuka kwenye mazingira ya leo, hata ufafanuzi huo unaotoa mwanga muhimu wa kitaaluma. Takwimu zilizokusanyika katika utafiti huu zimeonyesha kuwa Watoto asilimia 65% waliohusishwa katika mahojiano walikabiliwa na ugumu katika kutamka kwa ufasaha maneno yenye asili ya L2 iliyo swahili vizuri. Sababu ya hili jambo ni kwamba wazungumzaji wa Kinyankore wanakosa msamiati unaofaa wa L2, hivyo wanatumia maneno ya Kinyankore kama mbadala unaotakikana kutumia maneno yafaayo ya Kiswahili. Mtafiti aligundua kwamba katika jamii ya Kinyankore, hili halitukani tatizo kwani wanajielewa vizuri. Hata hivyo, changamoto inajitokeza kwa mwanafunzi asiye wa jamii hiyo, kwani anashindwa kabisa kuelewa maana halisi iliyokusudiwa. Mifano mizuri inayoweza kutolewa inaonyeshwa katika jedwali 4.6.

Jedwali 4.6 Makosa ya Kileksika

Kinyankore	Kiswahili	Waliotumia neno kamili	waliokosea
Tonto	Pombe za kienyeji	18 [18%]	82 [82%]
Enkeiga	Maharage mateke	12 [5%]	88 [88%]
Obwitizo	Funeli	0[0%]	100 [100%]
Obwato	Mtumbwi	5 [5%]	95 [95%]
Ebikanja	Machicha ya Mtama	0[0%]	100 [100%]
Okwevuga	Majigambo	15 [15%]	85 [85%]
Okwecura	Mtaratibu/Mzito kusutuka	0[0%]	100 [100%]
Okutsya	Mvua kukatika	20 [20%]	80 [80%]
Empuruturiro	Fundo la Mtego	0[0%]	100 [100%]
Okukona	Kufuba/Kutoiva vizuri	0[0%]	100 [100%]

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Takwimu za utafiti huu zinaonyesha kuwa Watoto wa asili ya Kinyankore wanapotumia L2 ya Kiswahili, mara nyingi wanachanganya maneno ya Kinyankore kuwenda L2 husika. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kusema **"leo nimekunywa Tonto,"** akijaribu kumaanisha **"leo nimekunywa pombe,"** ambapo neno **"Tonto"** linatumika kumaanisha **"pombe."** Kwa kuzingatia mfano huu, kuna madai manne yanayojitokeza. Kwanza, namna ya kutumia neno la Kinyankore inapendwa ili kurahisisha mawasiliano katika jamii, hasa kwa maneno yanayotumiwa kwa kawaida kama vile vyakula, matunda, na mengineyo.

Pili, inaonekana kuwa wanafunzi hutumia maneno ya Kinyankore wanaposhindwa kupata msamiati sahihi unaofaa kwa L2 ya Swahili. Jambo hili linajitokeza mara nyingi wakiwa wameathirika kwa uelewa wao wa L1 ya Kinyankore. Tatu, ni tabia ambayo wanafunzi wanyankore wameizoea kulazimisha kutumia Kinyankore katika mazungumzo yao kikawaida. Nne, ni kawaida kwa lugha kuathiriana pale ambapo lugha mbili zinapoelekezwa kutumika mfululizo zote kwa jamii moja. Katika jamii ya Kinyankore, Kiswahili na Kinyankore hutumika sambamba. Hivyo, kubadilishana maneno na kutumia msamiati wa pamoja si jambo la kushangaza.

Kwa kuzingatia mtaalam Giles mwasisi wa nadharia ya kimawasiliano, makutano au mawasiliano ya kiisimu yanajitokeza watu wanapowasiliana ili kukubaliana katika jamii hiyo. Hivyo, ikiwa jamii imeshikilia na inaelewana ikitumia maneno Fulani yanayokubalika, basi inaweza kuendelea kutumia hata yakiwa yana makosa katika Kiswahili sanifu.

4.2.3 Athari za Kifonolojia

Huu utafiti umebaini kwamba wanaotumia L2 Kiswahili kutoka jamii ya Kinyankore wanafanya kasoro nyingi kimatamshi. Data za utafiti zilionyesha taaathira za

kifonolojia katika kubadilishana kwa fonimu kama /l/ na /r/, /sh/ na /s/, pamoja na /th/ na /dh/, hata /γ/, kulingana na maelezo katika sehemu zinazofuata.

4.2.3.1 Kubadilisha fonimu

Utafiti ulitambua ya kuwa Watoto wenye asili ya Kinyankore ambao wanajifunza Kiswahili mara nyingi hufanya makosa yanayohusiana na fonimu, ambapo fonimu fulani inatumika badala ya nyingine sahihi. Katika maandiko yaliyoangaliwa ya Watoto wanyankore, sauti ambazo zilibadilishana zilikuwa /r/ badala ya /l/ na mifano yake inaonyeshwa kwenye jedwali namba 4.7.

Utafiti umebaini kwamba wanafunzi wengine hutumia herufi /r/ badala ya /l/ katikati ya mazungumzo yao na hata maandishi. Jambo hili linadhihirisha kuwa L1 ya Kinyankore haina /l/ katika abjadi yake, na hivyo popote palipo /l/ katika neno la Kiswahili itabadilishwa na kuweka /r/. Hivyo, wanafunzi wengi wa Kinyankore wanashindwa kutofautisha namna ya kutumia sauti hizi mbili ipasavyo, na huweza kutumia /l/ mahali panapohitajika /r/ au kinyume chake. Wanafunzi wanyankore wanaposoma L2 Kiswahili, inawalazimu kujifunza fonimu /l/ ambayo haipo katika uelewa wake wa awali. Wengi wanashindwa kutofautisha hizi fonimu mbili, jambo linalosababishwa mwingiliano wa ujuzi wa lugha iliyotangulia, hasa katika hatua za mwanzo wanafunzi hao kusomeshwa L2 ya Swahili. Matatizo yanajitokeza wakati sauti alizozizoea mwanafunzi katika Kinyankore hazipatikani kwenye L2 anayojifunza, hivyo anajaribu kutamka kulingana na vile anavyojua kivyake. Katika mifano iliyotolewa, mwanafunzi ametumia sauti hiyo /r/ ambapo angekuwa anatumia /l/, na pale ambapo inahitajika kutumia /r/ ametumia /l/.

Jedwali 4.7 Jinsi fonimu zinavyobadilishana

Kinyankore	Kiswahili
Ria	Lia
Mrango	Mlango
Reta	Leta
Serikari	Serikali
Turienda	Tulienda

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Tukirejelea hiyo mifano katika jedwali hilo juu, inadhihirika wazi kuwa wanafunzi wanachanganya sauti /l/ na /r/ kwa sababu kadhaa. Kwanza, fonimu hizi zimekaribiana kabisa kwenye mpangilio wa kutamkia fonimu za swahili, kwa hivyo wanafunzi wanaweza kuzikosea, jambo ambalo linaweza kuzua mkanganyiko wa kiufafanuzi. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuandika "ria" badala ya "lia." Pili, matokeo ya taarifa za utafiti zimeonyesha kwamba kosa hili la kuchanganya sauti ni mkakati wa mawasiliano yanayotokea kwa watumiaji wa Kinyankore peke yao. Hii inadhihirisha kuwa mawasiliano yao haya kawazwa. Data zinaonyesha kwamba Wanyankore wanapowasiliana kati yao, wanaelewana vizuri.

Tatu, data zinaonesha kwamba makosa haya yanasababishwa matumizi ya mifumo ya L1 Kinyankore kupita kiasi wakati wa kujifunza Kiswahili. Hapa, mwanafunzi anajua kwamba L2 ya Swahili huwa na sauti hizi mbili /r/ halafu /l/, lakini anazitumia bila kuelewa vizuri wapi zinapaswa kutumika kwa usahihi. Kama anavyoeleza Giles katika nadharia ya mawasiliano, hapa lengo ni mawasiliano tu.

Kwa kurejelea utafiti huu, iligunduliwa pia kuwa L1 ya Kinyankore haina sauti /l/ katika abjadi yake, lakini taarifa za utafiti huu zinaonyesha kuna sauti /l/ iliyotumika badala ya /r/ kwenye masomo ya L2. Jambo linalofikiriwa kusababishwa mazingira na ufundishaji usiofaa maana hakuna namna yoyote nyingine ambayo lingekuwa linajitokeza kuingilia Kiswahili. Makosa yafuatayo yalibainika:

Jedwali 4.8: Ubadilishanaji wa Fonimu za /r/ kwa /l/

Kosa	Kiswahili sahihi
Jalibu	Jaribu
Sufulia	Sufuria
Mpila	Mpira
Ledio	Redio
Sukali	Sukari

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Katika Jedwali nambari 4.8 lililoonyeshwa hapo juu linadhihirika kwamba matumizi yasiyo sahihi ya fonimu yanaweza kusababisha maumbo fulani kupoteza maana yake yaliyokusudiwa. Kwa mfano, kuandika "serikari" badala ya "serikali".

Lililogunduliwa wazi ni kwamba, katika mfumo wa Kinyankore hakuna sauti /l/ katika abjadi yake, lakini data za utafiti huu zinaonyesha kuna sauti /l/ ilivyotumika badala ya /r/ katika Swahili, mfano mzuri ulikuwa neno "Sufuria" ikaitwa "Sufulia" au "Mpila" badala ya "mpira", jambo linalofikiriwa kusababishwa na mikutadha mingine ya kukosea. Pia, makosa haya yanaweza kuwa matokeo ya ufundishaji usio sahihi, ambapo wanafunzi wamejifunza makosa, labda kutoka kwa mwalimu au wenzao hadi wakajifunza tahajia yenye makosa.

Jedwali 4.9: Ubadilishanaji wa /ki/ na /chi/

Kosa	Kiswahili
Chishwahiri	Kiswahili
Chitabu	Kitabu
Chitanda	Kitanda
Chintu	Kitu
Chijiko	Kijiko
Chisu	Kisu

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Kulingana na mifano kwenye jedwali 4.9, inadhihirika wazi kuwa wanafunzi wanachanganya sauti /ki/ na /chi/ kwa sababu kadhaa. Kwanza, fonimu hizo huwa na sifa zinazofanana kwa karibu katika mfumo wa fonimu wa Swahili, ndiposa wanafunzi

wanatumia sauti hizi kiholela, jambo ambalo linaweza kusababisha mkanganyiko wa kiufafanuzi. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuandika "chitabu" badala ya "kitabu".

Jambo linguine lililojitokeza lilikuwa utafiti ulivyoonyesha kwamba kosa hili la kuchanganya sauti ni mkakati wa mawasiliano unaonekana zaidi katika jamii ya Kinyankore, na katika maandiko, kosa hili halijitokezi kila wakati. Hii inathibitishwa katika takwimu zilizonyesha kuwa wanafunzi hawa wanapowasiliana, wanapata kuelewana bila shida. Data zinaonyesha kwamba Wanyankore wanapokuwa pamoja, wanajenga uelewano mzuri.

Tatu, data zinaonesha kwamba kosa hili linajitokeza kutokana na kuhusishwa kupita kiasi na kanuni zinazotawala matumizi ya Kinyankore katika masomo ya L2 ya swahili. Jambo kama hili likitambulika, mwanafunzi anapojua kwamba Kiswahili kina fonimu /ch/ na /k/, lakini anazitumia bila kuelewa mahali sahihi ambapo zinapaswa kutumika. Kama anavyoeleza Giles kuhusu mfumo wa mawasiliano, lengo hapa ni mawasiliano peke yake.

4.2.3.2 Athari ya matumizi ya /θ/

Sauti hii inakwamiza na ni fonimu inayotamkwa na meno ambapo wakati sehemu ya ulimi iliyoko mbele inapoingia katikati ya meno hapo juu na pale chini, sauti hiyo inatamkwa. Mtu akiwa anatamka maneno fulani, analenga kutoa hewa au pumzi bila kuzingatia mpangilio mwafaka, bali anairuhusu kupita huku ikigusa ala sogezi na ala tuli ziweze kutoa sauti lengwa, na hilo ndilo jambo ambalo linaweza kusababisha sauti kutolewa kwa njia ya kukwama.

Utafiti umebaini kwamba baadhi ya wanaotumia L1 ya Kinyankore wanaojifunza L2 ya Swahili wakifanya makosa ya kimatamshi bila kusisitiza usanifu wa lugha husika. Mifano hasa iliyodhihirika katika utafiti huu ilikuwa kama sauti /θ/ huwa inabadilishwa

kuwa /s/, ambapo silabi kama tha, the, thi, tho, thu hubadilishwa na kuwa sa, se, si, so, su. Sauti /s/ na /θ/ zote ni vikwamizi, hivyo zina sifa zinazofanana kwani zote zinatamka wakati sehemu zinapotamkiwa zinakaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti, jambo ambaloo husababisha hewa ipite kwa shida na hivyo kuleta mkwaruzo. Jedwali nambari 4.10 linadhihirisha baadhi ya taathira hizi.

Jedwali 4.10: Uchanganuzi wa makosa ya /Ө/

Neno lililo sahihi	Kosa	Waliolitamka vyema	Walioshindwa kutamka vyema
Thawabu	Sawabu	6.3%	93.7%
Theluthi	Selusi	9.9%	90.1%
Thelathini	Selasini	9.7%	90.3%
Theluji	Seluji	2.3%	97.7%
Thamani	Samani	4.8%	95.2%
Wastani		4.0%	96%

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Katika jedwali hili, kuna washiriki waliolitamka vizuri na walioshindwa kutamka vizuri. Hapa, hakuna wanafunzi wowote waliofanikiwa kutamka neno vizuri, bali pia wale ambao walishindwa. Mtafiti alionyesha kipimo cha ufanisi wa wanafunzi kwa kujaribu kutamka fonimo hizo.

Kuhusu maneno “Thawabu na Sawabu”, Wanafunzi 6.3% walitamka vyema "thawabu," wakati 93.7% walikosea na kusema "sawabu."

Kuhusu maneno “Theluthi na Selusi”, Washiriki waliolitamka vyema "theluthi" ni 9.9%, huku 90.1% wakikosea kwa kusema "selusi."

Kuhusu maneno “Thelathini na Selasini”, Hapa, 9.7% walikamilisha matamshi sahihi ya "thelathini," wakati 90.3% walikosea kwa kusema "selasini."

Kuhusu maneno “Theluji na Seluji”, Wanafunzi 2.3% waliweza kutamka "theluji," lakini 97.7% walitumia neno "seluji," ambayo ni makosa.

Kuhusu maneno “Thamani na Samani”, washiriki waliotamka vyema "thamani" ni 4.8%, ambapo 95.2% walitumia "samani."

Takwimu za utafiti zinaonyesha pia wastani kuwa matamshi sahihi ni 4.0%, huku asilimia 96% wakiwakilisha wale ambao walikosea.

Matokeo haya yanaonyesha changamoto kubwa katika matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili kati ya wanafunzi. Wengi wao wa hawa wanafunzi hawakufanikiwa kutamka maneno haya kwa usahihi, na inamaanisha kwamba kunahitajika kuimarisha namna ya kufundisha somo hili la L2 kwenye ujuzi wa matamshi. Hii inaweza kuwa kiashiria cha hitaji kubwa la kujifunza lugha kwa kuzingatia mikabala ya kutumia mitindo sahihi ya maneno.

Kulingana na jedwali nambari 4.10, kazi ya utafiti ilidhihirisha wazi kuwa wanafunzi wametumia /s/ badala ya /Ɵ/. Hii Kasoro inaonyesha kuwa madai ya kwamba kasoro yenyewe imesababishwa na kutokuwepo kwa fonimu /Ɵ/ katika jamii ya Kinyankore yana mchango mkubwa katika jambo hili kutokea. Jambo hilo linasababisha mtafiti kupata nafuu kwa vile sauti /s/ inavyotumika na vile inavyojitokeza katika matumizi ya L1; hivyo kusababisha namna maneno yalistahili kutumika kukosa nafasi katika L2. Kwa hiyo, maneno kama "theluji" yanatamkwa kama "seluji," na "thawabu" inatamkwa kama "sawabu," pamoja na mengineyo kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali nambari 4.10.

Katika jamii ya Kinyankore, hali hii inakidhi kile kilichosemwa katika mfumo wa mawasiliano kulingana na Giles ambapo watu huwasilisha historia ya uzoefu wao wa mawasiliano kupitia matamshi na tabia zao. Hivyo, mwanafunzi wa Kinyankore anaposema “semanini” badala ya “themanini,” anaonyesha uhusiano wa matamshikwa

kuangalia zile fonimu zilizopo kwenye mfumo mmoja wa L1 na zile zinazopatikana katika lugha anayoijifunza.

4.2.3.3 Athari katika matumizi ya /ð/

Kwa kurejelea takwimu za utafiti huu, zinadhihirisha kwamba kuna wanafunzi wa asili ya Kinyankore ambao wanajifunza Kiswahili wakikosea kimatamshi kwa sauti fulani. Sauti /z/ na /ð/ zote huwa vikwaruzo na hutamkwa wakati ala za sauti zinakaribiana, hivyo kupunguza upenyo wa bomba la sauti na kufanya hewa ipite kwa ugumu, hali ambayo husababisha mkwaruzo. Hii ni fonimu inayokwamiza ambayo inatamkwa kwa kutumia meno, ambapo mwanafunzi akiwa anatamka, anaruhusu pumzi kupitia chemba cha hewa bila kukiweka chini kabisa, bali unaachwa kupita kwa kukwama kati ya meno ya juu na chini. Katika hayo yote, hii hewa inaruhusiwa kupita, ingawa kwa kugusanisha ala sogezi na ala tuli kiasi, hivyo kuleta sauti kwa kukwama. Sauti /ð/ hupotoshwa kuwa /z/, ambapo fonimu inayostahili kutamkwa kama /dha/ ama /dhe/ ama /dhi/ ama /dho/ au /dhu/ zinabadilishwa kuwa /za/ badala ya /dha/, /ze/ kwa /dhe/, /zi/ kwa /dhi/, /zo/ kwa /dho/, na /zu/ kwa /dhu/ kama inavyoonyeshwa katika jedwali nambari 4.11.

Jedwali 4.11 Matumizi ya /ð/

Kiswahili sanifu	Kosa	Waliotamka vizuri	Waliokosea kutamka
Fedha	Feza	9.6%	90.4%
Aidha	Aiza	9.9%	90.1%
Dhiki	Ziki	4.8%	95.2%
Dhana	Zana	7.6%	92.4%
Dhahabu	Zahabu	6.3%	93.7%
Afadhali	Afazali	7.2%	92.8%
Dharau	Zarau	5.6%	94.4%

Chanzo: Takwimu ya Uwanjani (2023)

Utafiti umebaini kwamba kasoro za wasomi yanayohusu kuchanganya fonimu ni kwa sababu ya kuingiliwa na L1 ya Kinyankore kwa njia mbili. Kwanza, sauti /ð/ haipo katika abjadi ya Kinyankore. Pili, sauti /z/, ambayo ipo kwenye alfabeti, ndiyo

inayotumika kimaandishi. Kwa hivyo, hakuna hitilafu kwenye mpangilio wake kifonolojia kwa Kinyankore kwa ujumla.

Aidha, kasoro hizi zihuenda zikawa zinatokana na ufundishaji usiofaa, ambapo wanafunzi wamerithi makosa ambayo ni vigumu kwelina vyaeleweka. Hii inasababisha mkanganyiko katika kutambua sauti ipi inayopaswa kutumika, hali ambayo inachangia mchanganyiko huo. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa sauti hizi zina sifa zinazofanana za kifonetiki kwani hutamkwa kwenye sehemu sawa na namna inayowezesha kutamka vikwamizwa, isipokuwa tu kwamba /ð/ ni ghuna na /z/ si ghuna.

Kwa hiyo, mwanafunzi akitumia fonimu moja kuliko kutumia iliyo ya pili, mtengano wa kanuni zinazotawala namna ya kutamka hauonekani vyema. Hali hii inatofautiana tukiangalia mfumo wa matamshi kwa Kinyankore, kwa sababu ilionyeshwa kulingana na takwimu za utafiti, ambapo wazungumzaji hutumia sauti /z/ badala ya /ð/, mfano ikiwa ni kusema /zambi/ badala ya /dhambi/. Sauti /ð/ hutamkwa msemaji akitumia ulimi wake kugusana na meno, lakini Kinyankore hakina sauti kama hiyo, hivyo sauti /z/, ambayo ni ghuna kama /ð/, inatumika kama mbadala. Sauti /z/ hutamkwa wakati sehemu ya juu ya ulimi inakaribiana na kaakaa gumu, huku hewa ikipitishwa kwa kukwamizwa kuzunguka ulimi, hali ambayo husababisha mkwaruzo. Ala hizo husika ni za karibu na za kutamka sauti /ð/, na hivyo mzungumzaji wa Kinyankore hutumia /z/ kutokana na inakosa fonimu ya /ð/ kwenye mfumo wa abjadi yake.

4.2.3.4 Athari za matumizi ya / γ/

Hii fonimu ya /γ/ inakwaruza na inahusiana na sauti ya kaakaa laini (kaakaa la nyuma). Kutamkwa kwake kunategemea bapa la juu kwenye ulimi, ambalo huwa sehemu inayosogeasogea wakati wa utamkaji, na inayoigusa kaakaa laini ambayo kwake ni sehemu iliyo tuli. Sauti hii hutokea wakati ala za sauti zikiwa zinakuwa karibu kwa

zinaweza kugusana halafu zikazuia hewa kupitia kwenye sehemu hizo, hivyo zikaleta kukwaruzana na kuizuiwa hewa kutoka ikizuiliwa na ikawa ngumu kwake kupita. Fonimu hiyo ya /γ/ inaweza kubadilishwa kuwa /g/, ambapo sauti za /gha/ au /ghe au /ghi/ au /gho/ au /ghu/ zinakuwa [ga] badala ya /gha/, au [ge] badala ya /ghe, au [gi] badala ya /ghi/, au [go] badala ya /gho/ na [gu] badala ya /ghu/.

Jedwali 4.12 Mifano ya athari katika matumizi ya /γ/

Kosa katika Kiswahili	Umbo sahihi katika Kiswahili
Garama	Gharama
Luga	Lugha
Agalabu	Aghalabu
Gorofa	Ghorofa

Chanzo: Takwimu ya Uwanjani 2023

Sauti /g/ na /γ/ huwa zinajulikana kutamkiwa kwenye sehemu ya Kaakaa laini, na kutamkwa kwake kunahusishwa kwa mkwaruzo wa hilo bapa la juu la ulimi kugusa kaakaa laini. Kwa kurejelea mfumo wa abjadi ya Kinyankore, kama vile inavyoonyeshwa na tafiti, wazungumzaji hutumia sauti /g/ badala ya /γ/, kwa mfano kusema /luga/ badala ya /lugha/. Fonimu /γ/ hutamkwa kwa kaakaa laini, lakini Kinyankore haina fonimu hiyo inayotamkwa kwenye kaakaa ya nyuma hiyo /γ/, hivyo sauti /g/, ambayo ni ghuna kama /γ/, inachukuliwa kama mbadala.

4.2.3.5 Uchopekaji

Wanafonolojia kama Massamba (keshatajwa) wanasisitiza kuwa uchopekaji unahusisha namna ya kupanga irabu, kiyeyusho, au konsonanti ndani ya neno. Uchopekaji unarejelea mbinu iliyo ya kifonetiki ambapo kipashio kinaongezwa katika neno, na kupelekea kujaza neno hilo na sauti za ziada ambazo hazikuwepo kwenye mfumo wa silabi ya asili. Wazungumzaji wa Kinyankore wanachopeka silabi fulani hasa hapo neno linapotangulia. Kwa kufuatilia data zilizotokea kwenye utafiti huu, mtafiti alibaini wanafunzi ambao walikumbwa na ugumu wa kutamka baadhi ya

maneno ya L2 kwa usahihi. Utafiti huo uligundua ya kwamba wanafunzi wasomao Kinyankore katika kujifunza Kiswahili wanajumuisha viambishi visivyohitajika kwenye sehemu zinazotangulia za maumbo hayo, mfano kusema "saati" badala ya "sati," "ikumi" badala ya "kumi," na "shukari" badala ya "sukari."

Jedwali 4.13 Namna ya kuchopeka /i/ na /e/

Kiswahili	Kinyankore	Waliotamka vizuri	Waliokosea
Sati	*Esaati*	8.6%	91.4%
Kumi	*Ikumi*	7.9%	92.1%
Duka	*Eduuka*	5.8%	94.2%
Bati	*Ibaati*	8.6%	91.4%
Sukari	*Shukari*	4.3%	95.7%
Dirisha	*Edirisa*	8.2%	91.8%

Chanzo: Takwimu ya uwanjani, (2023)

Utafiti ulitambua kwamba mzungumzaji wa Kinyankore mara nyingi anafanya hivyo ili aweze kukamilisha haja ya kuwasiliana na wenzake wakati wa mazungumzo kati yake na mwasilianaji. Ilitambulika katika utafiti huu ya kwamba, mzungumzaji haweki mkazo sana kuhusu usahihi unaofaa wa yale anayoyatamka, bali lengo lake ni kufikisha ujumbe, na kwa kuwa mawasiliano yanapatikana, huwa anajiona kwamba amefanikiwa. Wazungumzaji wa Kiswahili ambao wameathiriwa na Kinyankore wana tabia ya kuongeza viambishi visivyohitajika wakati wakizungumza Kiswahili, huku shabaha yao ilikuwa inalenga kurahisisha mazungumzo kwa muda wa hapo hapo.

Data hii ilipatikana ikiletwa na wanaofundisha L2 ya Kiswahili ambao walijibu dodoso lililouliza kuhusu athari zinazojitokeza hasa kutoka wasomao wenye asili ya Kinyankore katika kujifunza Kiswahili. Mifano kadhaa ilitolewa na waliohusika katika utafiti. Katika hayo yote, utafiti wa sasa, ulibaini kwamba wengi wa Wanyankore hujumuisha utamkaji usio wa lazima katika maneno ya L2, na hili lilibainishwa katika jedwali namba 4.13 tukirejelea takwimu za utafiti wa sasa.

Wakati mzungumzaji wa Kiswahili sanifu anaposikia njia hiyo inayowezesha kutamka maneno, mara moja anagundua kwamba anayezungumza si mzoefu wa L2. Inakuwa rahisi kwake kutambua na kubashiri kwamba mtu anayeongea ameathiriwa kwa matumizi yanayoegemea sana L1 Kinyankore. Mtaalamu wa Kiswahili anaweza kugundua hili kwa sababu tayari anafahamu vile fonimu za lugha zinavyostahili kutamkwa hasa sehemu zinapotamkiwa pia. Wazungumzaji wa Kinyankore hufanya jitihada kubwa katika kutamka maneno, hivyo wakati wanapozungumza Kiswahili, wanatumia nguvu ile ile, na kusababisha kuweka mkazo hata mahali pasipohitajika.

Utafiti wa sasa unaonyesha mabadiliko yaliyotokea kwenye matamshi yenye makosa ya L2 iliyo Swahili ambayo yalisababishwa ujuzi wa wanafunzi uliotangulia wa L1 ya Kinyankore kwa wazungumzaji. Mtu anayeweza kutambua utofauti huu inabidi kuwa na uelewa unaotosha kuhusu L2 kwa usanifu. Athari moja ni kuongezwa kwa viambishi vinavyotokea katika sentensi zisizo sahihi, pamoja na makosa ya matamshi. Utafiti huu umeonyesha kwamba wengi wa wale walioathiriwa na Kinyankore walikuwa wanafunzi wanaoanza kujifunza Kiswahili upya kama L2.

Jedwali 4.14: Uchopekaji wa /e/ ikitangulia maneno

Kinyankore	Kiswahili	Waliotamka Vizuri	Waliokosea
Entwiga	Twiga	9.2%	90.8%
Embwa	Mbwa	6.9%	93.1%
Esaati	Shati	7.5%	92.5%
Emotoka	Motokaa	7.9%	92.1%
Emeeza	Meza	8.6%	91.4%
Esimu	Simu	4.3%	95.7%
Eduuka	Duka	5.8%	94.2%
Edirisa	Dirisha	6.5%	93.5%
Enyama	Nyama	5.4%	94.6%
Etaara	Taa	6.6%	93.4%
Ecupa	Chupa	7.2%	92.8%
Ekiganja	Kiganja	8.1%	91.9%
Ekitanda	Kitanda	5.3%	94.7%
Ebakuri	Bakuli	9.6%	90.4%

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Katika uchambuzi wa namna ya kuchopeka hiyo vokali "e" kutoka Kinyankore hadi Kiswahili, tunaweza kuona jinsi irabu hii inavyobadilishwa au kuondolewa wakati wa matamshi na tafsiri ya maneno. Utafiti huu unatoa mwanga juu ya changamoto zinazowakabili wanafunzi wanapojaribu kujieleza na matamko yenye maumbo ya Kinyankore kwa usahihi. Maneno yafuatayo yalichambuliwa. Maneno “Entwiga na Twiga”, wanafunzi 9.2% walitamka Twiga na wengine 90.8% walichopeka “e”. Maneno “Embwa na Mbwa”, wanafunzi 93.1% walichopeka “e”, halafu wanafunzi 6.9% walitamka “mbwa”. Maneno “Esaati na Sati”, wanafunzi waliochopeka “e” walikuwa 92.5% na wanafunzi wengine 7.5% walitamka “sati”. Kuhusu maneno “Emotoka na Motokaa”, wanafunzi 92.1% walichopeka “e”, na wengine 7.9% walitamka motokaa. Kuhusu maneno “Emeeza na Meza”, wanafunzi 91.4% walichopeka “e”, halafu Wanafunzi 8.6% walitamka “meza”.

Kwa hivyo, uchambuzi huu unaonyesha wazi kuwa irabu "e" inachopekwa kwenye maneno sahihi ya Kiswahili, kuondolewa au kutokuwepo katika tafsiri inayofaa katika L2 iliyo Swahili ikitolewa kwa Kinyankore. Wanafunzi wengi wanaonekana kuwa na changamoto kubwa katika kutamka kulingana na muktadha wa mtagusano wa lugha husika zote, ambako uelewa na mafunzo bora yanahitajika kisayansi. Kulingana na vile vokali "e" inachopekwa, ni kati ya vichocheo vya ufanisi na kuna hitaji la mabadiliko ya mtaala na mafunzo bora ili kusaidia kuboresha matamshi na uelewa wa wanafunzi.

Jedwali 4.15 Uchopekaji wa /i/

Kinyankore	Kiswahili	Waliotamka vizuri	Waliokosea
Ikumi	Kumi	6.9%	93.1%
Ibaati	Bati	9.2%	90.8%
Ipapari	Papai	7.5%	92.5%
Itaano	Tano	7.9%	92.1%

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)



Kielelezo 4.2: Jinsi Uchopekaji wa /i/ unavyojitokeza
Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Kwa kurejelea kielelezo kilicho hapo juu, kuna uchambuzi wa jinsi vokali 'e' inavyochopekwa kwenye maumbo ya L1 Kinyankore na Kiswahili. Kila neno linaleta picha ya jinsi wanafunzi wanavyotamka maneno haya yanatolewa kwenye mfumo wa lugha husika kwenda lugha inayofuata, pamoja na ufanisi wao katika kutamka maneno hayo. Mifano iliyoko kwenye jedwali inaonyesha mifano ya Maneno kama "Ikumi na Kumi", wanafunzi 6.9% walichopeka "i" kwenye "kumi' ikawa "ikumi," wakati 93.1% badala ya kusema "kumi." Hii inaashiria kwamba wengi hawaelewi au hawawezi kutamka umbo hilo la Swahili ifaavyo vizuri. Maneno "Ibaati na Bati", wanafunzi 9.2% walichopeka "i" na kutamka "ibaati", lakini 90.8% walisema "bati." Kuna hitaji la kuimarisha mafunzo ya matamshi kwenye maneno kama hayo pia. Maneno "Ipapari na Papai", wanafunzi 7.5% walitamka "ipapari" kwa kuchopeka "i", wakati 92.5% walisema "papai." Hii inaonyesha kwamba wanafunzi wengi kwa idadi kubwa walichopeka "i" katika kutamka neno hili. Maneno "Itaano na Tano", wanafunzi 7.9% walichopeka "i" na kutamka "itaano," huku 92.1% walitamka "tano." Kama ilivyo

tukiangalia maumbo tofauti, hii inaashiria changamoto katika uelewa na matamshi sahihi.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha makosa katika matamshi yenye asili ya Kinyankore kwa kuangalia hao wasomi wanaosoma L2 ya Kiswahili. Watoto wengi wa Kinyankore wanaosoma Swahili hawakufanikiwa kuhifadhi na kutamka maneno haya vizuri, kwenye hali inayoonyesha hitaji la kujenga uwezo L1 iliyo Kinyankore. Kuwepo kwa hali zinazotofautisha matamshi kati ya Kinyankore na Kiswahili kunatoa changamoto ambayo inahitaji ufundishaji zaidi ili kuboresha matamshi sahihi na jinsi wanavyojua L2. Hii inaweza kuhusishwa kwa kutokuwepo kwa mazingira mazuri kufunzia stadi za lugha ifaavyo hasa uelewa wa tamaduni zinazohusiana.

Jedwali 4.16 Matumizi ya /o/ na /u

Kinyankore	**Kiswahili**
Omuti	Mti
Omuntu	Mtu
Omugongo	Mgongo
Omwana	Mwana
Okunywa	Kunywa

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Kwa kurejelea takwimu za utafiti wa sasa zilizowasilishwa katika jedwali 4.14, 4.15, na 4.16, uchopekaji mwingi ulibaini kuhusiana na sauti /i/, /o/, na /e/ zikijitokeza zikitangulia maumbo husika. Maneno mengi yanayoonyeshwa kuwa yaliathirika kifonetiki yanaonyesha jinsi irabu hizo zilivyochepeka mwanzoni. Uchopekaji huu ulilenga kufanya maneno hayo yatekeleze kanuni za Kinyankore, jambo lililosababisha makossa kudhihirika kwenye mpangilio unaoathiri L2 kifonolojia. Data za utafiti zilionyesha kwamba vokali kadhaa hasa /i/, /o/, na /e/ huwa zina chopekwa kimazoea zikitangulizwa mbele ya maumbo hayo. Watafitiwa walizungumza kwa kudhihirisha

jinsi mpangilio wa L1 wa kifonolojia unavyoweza kusababisha kasoro kufanyika katika muundo wa kifonolojia katika L2 ya Swahili, wakianzisha silabi zenye fonimu ambazo hazifai kuchopekwa kwa sababu zina uambatano ambao hauziruhusu kufuatana. Jambo hili lilileta usahihishaji mkubwa ambapo mwanafunzi hakujua zinapostahili kutumika sauti hizo kwa pale ambapo hazikufaa. Kwa mfano, kuchopeka vokali ya /e/, /i/, na /o/, kwenye mwanzo wa neno umesababishwa na desturi ya wazungumzaji wa Kinyankore kuanzisha maneno, hasa majina na vokali. Ni nadra kukutana na maneno ya Kinyankore yanayoanza kwa konsonanti, hali ambayo pia imehamishwakuunda maumbo ya L2 ya Swahili. Watumiaji wa Kinyankore hufanya hivyo waweze kutamka maumbo ya L2 kwa urahisi.

Pamoja na hayo, kuchopeka fonimu kama /h/ pia ulijitokeza kwa kiwango kikubwa. Makosa haya yalifanywa na Watoto hao wenye asili ya Kinyankore, hasa yalitokea kwa yale maumbo yanayotangulia na vokali, kama vile "huzi" badala ya "uzi." Mara nyingi pia sauti /h/ huongezwa inapofuatana na /s/. Mtafiti aligundua kasoro hii alipowaagiza wanafunzi kuhusika katika zoezi la kutoa mifano ya maumbo ya L2 swahili, hata katika utamkaji wao wa maneno hayo, sauti /h/ iliweza kusikika ikitamkwa na washiriki.

Mifano ya aina hii ilijitokeza katika maneno kadhaa, ambayo inajadiliwa ifuatavyo;

Jedwali 4.17: Maneno kadhaa ya uchopekaji

Eshaaha badala ya Saa
Shukari badala ya Sukari
Eshuura badala ya Sura
Orubaho badala ya ubao
Ebaruha badala ya barua

Uchopekaji huu pia ulijitokeza ukihusisha hasa yale maneno katikati ya neno bila ufahamu wa watafitiwa. Utafiti ulionyesha kuwa uchopekaji unaojitokeza unasababishwa ukosefu wa ustadi kuhus L2 ya Swahili kwa baadhi ya washiriki. Inaweza kuwa watafitiwa walipachika sauti /h/ mahali ambapo haikuwa inahitajika.

Uchopekaji huo umepelekea kuwepo kwa fonimu zinazoambatana na zilitumika katika sehemu zisizostahili. Hali hii ilihusishwa na changamoto zilizowakumba Watoto wanyankore wanaotumia L1 ya Kinyankore katika kutumia sauti hizo kwa usahihi.

Tatizo hili ni la muda mrefu kwa wazungumzaji wa L1 ya Kinyankore, na linajidhihirisha kupitia makosa wanayoyafanya wakati wa kuchopeka fonimu husika. Mifano hiyo inaonyesha jinsi kuchopeka fonimu /h/ kunajitokeza kwa silabi nyingi. Kutokana na mazingira ambapo irabu pekee ingekuwa inatumika, utafiti ulibaini kwamba haya ni makosa ya kimazoea kwa wazungumzaji wa Kinyankore, kwani vokali inapotumika bila kuiambatanisha na nyingine, hapo kuchopeka /h/ kunajitokeza hasa bila kujua.

Katika maneno kama "shura" badala ya "sura," "Orubaho" badala ya "ubao," na "Ebaruha" badala ya "barua," kuna uwepo wa kuchopeka fonimu /h/ mara mbili ambapo inatokea kwenye sehemu ya kati kati ya neno halafu na mwisho mwisho wake. Kuchopeka fonimu hapo awali ulitokea kabla ya /a/, wakati wa pili ulitokea kwenye sehemu inayotangulia /u/, mwingine kabla ya /o/, na wa mwisho kabla ya /a/. Changamoto inayodhihirika kwa sababu ya kuchopeka fonimu bila kujali inayofaa au isiyofaa ilijitokeza tena kwenye maandishi yaliyoandikwa na washiriki wanafunzi wanyankore. Uchopekaji huo ulikuwa unadhihirika sana sana hapo kutangulia maumbo, halafu kidgo kidogo kati kati ya maneno, kama inavyooneshwa kwenye jedwali namba 4.14, 4.15, na 4.16.

Kulingana na msimamo wa nadharia ya NKM kama iliyoanzishwa na Giles (1973), anaeleza kuwa sababu kuu ya kubadilisha matamshi ni kuonyesha makubaliano na uhusiano baina ya watu.

4.2.3.6 Kudondosha fonimu

Kulingana na wataalam kama Massamba (keshatajwa), wanasisistiza kuwa kudondoa kunahusisha kutoa kwa kimakusudi fonimu kutoka kwenye mfumo wa neno lililo kamili. Kwa ujumla, kudondosha kwa fonimu kunaweza kuwa kwa aina tatu: mwanzoni, katikati, au mwishoni mwa neno. Utafiti huu ulibainisha ya kwamba Watoto wanaotumia L1 ya Kinyankore mara nyingi wanapokuwa wakitumia Kiswahili, huathiriwa na lugha yao na kuweza kudondosha maneno Takwimu za utafiti zinaonyesha kuwa kuna wanaozungumza L1 ya Kinyankore wanaojifunza Kiswahili hufanya kasoro za kifonolojia kwa kudondosha sauti fulani.

Jedwali 4.18: Athari inayosababishwa kudondosha fonimu /h/

Kiswahili	**Kosa**
Shule	Sule
Hapana	Apana
Asubuhi	Asubui
Shitakiwa	Sitakiwa
Hasara	Asara
Gharama	Garama

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Data kutoka jedwali namba 4.18 zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya watoto wa Kinyankore waliondoa baadhi ya vipashio katika maneno kwa njia inayokiuka mbinu zinazotawala matumizi ya L2 ya Swahili. Mifano ilikuwa kama, neno "sitakiwa" linaonyesha uondoaji wa fonimu ya /h/, halafu inapaswa kuwekwa nyuma ya fonimu /s/ kwa ajili ya kupata fonimu ya /ʃ/. Vilevile, sauti /ɤ/ inahitajika katika neno "garama," lakini inakuwa changamoto ikisumbua Watoto wa Kinyankore kwani tofauti kati ya matamshi yao na jinsi wanavyoandika kwa kutumia lugha wanayomiliki kama L1. Uchanganuzi unaohusu maumbo yanayotamkwa na wanafunzi wanyankore umebaini kwamba sauti nazali /h/ imedondoshwa zaidi kuliko sauti zingine katika matamshi ya washiriki, hivyo kuathiri ubora unaotakikana kwa maumbo hayo yanayotamkwa.

Udondoshaji huu umetokea kwenye mkutadha unaoonyesha irabu mbili zimekuwepo na inahitaji sauti kujitokeza kati kati ya irabu hizo. Vielelezo vya kudondosha fonimu hizi vinaonekana kwenye jedwali namba 4.18, ambapo maneno kama "asubui," "sule," na "asara" yanaonesha sauti /h/ iliyondolewa. Utafiti umebaini kwamba kasoro hizi zinafanyika mara kwa mara kwa sababu sauti /h/ inatamkwa kwa njia tofauti kwenye L1 iliyo Kinyankore. Kukosekana kwa sauti hii kunawafanya Watoto wenye umilisi wa L1 ya Kinyankore wasitumie pale inapohitajika.

Tukirejelea msimamo wa nadharia ya NKM (keshatajwa) watu huwa wanajaribu kuzungumza lugha au kuiga mitindo fulani ya matamshi na msamiati mpya kutoka kwa wasikilizaji wao ili kufanikisha mawasiliano. Hufanya hivyo kwa ufahamu au bila ufahamu, kwa kutafakari au bila kutafakari, lakini lengo kuu ni daima kufikia makutano ya mawasiliano.

4.3 Athari za Kimofolojia

Kuna wataalamu wengi ambao wamejaribu kutafiti na kushughulikia uwanja wa kimofolojia kwa undani Zaidi. Mathew (1974) anasema kwamba sarufi maumbo huweza kufasiliwa kama uwanja wa kitaaluma unaojishughulisha na kuchunguza maumbo ya maneno hasa kwenye ngazi ya mofimu. Mtaalam mwingine aitwaye Hartman (1972) alisema kwamba mofolojia huwakilisha uwanja wa sarufi unaojishughulisha na kuchambua maumbo ya maneno na aina zake pamoja na etimolojia zao. Yeye mtaalam mwingine aitwaye Richard na wenzake (1985) walieleza kwamba uwanja wa mofolojia unatumika kutoa maelezo Zaidi kuhusu maana muhimu mbili ili kueleweka vizuri;

i. Tawi la mofolojia unatumika kuchunguza yale maumbo yanayojenga mofimu na alomofu, n ahata vile zinavyowekwa kwa pamoja ili kujenga maumbo tofauti yanayoeleweka katika lugha husika.

ii. Mofolojia ni mfumo kamili wa mofimu unaojitokeza kwenye lugha husika. Kwa kuzingatia maelezo haya huenda tukafasili mofolojia ya lugha ya Kingereza ama mofolojia ya Kirusi.

Kulingana na wachapishaji wa TUKI (keshatajwa), wanaifasili dhana hiyo ya mofolojia kuwa uwanja wa kiisimu unaochambua maumbo ya maelezo halafu na kategoria zinazohusika. Wataalam hawa wanafafanua kwamba, tukiyaangalia vilivyo yale maelezo yaliyotolewa na wataalam hao, inadhihirika kwamba mofolojia ni uwanja mpana sana, na huenda ikawa taaluma ya sarufi iliyo na uwezo wa kuchanganua maumbo kwa ajili ya kuyafafanua Zaidi kwa watu kwamba maumbo ya maneno kama kimojawapo cha kila lugha. Uwanja wa kimofolojia unaotofautiana na Nyanja nyingine ambazo zinashughulikia matamshi, muundo, au kileksika. Kwa upande wa pili, wataalam wanaunganisha matawi haya mawili na kile cha sintaksia.

4.3.1 Namna ya kuchambua vivumishi vya sifa

Kwa mujibu wa Massamba (2006), vivumishi ambavyo ni vile vya sifa na vinaweza kutumiwa kuwa changamoto kwa watu, kwa sababu muundo sahihi wa vivumishi hivi unategemea jinsi vinavyohusishwa na nomino. Jedwali linalofuata linaonyesha matatizo halisi wanayokutana nayo wanafunzi Wanyankore wanapojifunza Kiswahili.

Jedwali 4.19: Vivumishi vya sifa

Kivumishi	**Aina ya Ngeli**	**Jawabu sahihi**	**Wanafunzi waliokosea**					
			Katika shule ya upili	%	Katika Vyuo vikuu	%	Jumla /180	%
Sifa	u/i	Mguu safi	88	73	55	53	143	80
	i/zi	Kazi nzuri	79	66	39	59	118	65
	u/zi	Uma mrefu	92	76	54	81	146	81
	li/ya	Gari zuri	103	86	53	80	156	86

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Matokeo yanayoonyeshwa kwenye jedwali na.4.19 yanaonyesha kinagaubaga kuwa upatanishi unaodhihirisha matumizi ya majina na vivumishi vyake kama vya sifa vinatokea kwenye ngeli kama ya {li/ya} umekuwa changamoto kwa wengi wa wanafunzi. Kundi hili linajumuisha majina yenye viambishi awali {ji/Ø-ma}, hasa vile yanavyotumika kwa ajili ya umoja pamoja na vivumishi vya sifa huchangia matatizo katika muundo wa vivumishi hivyo. Utafiti umebaini kwamba 86% ya wanafunzi walishindwa kuunganishia jina gari na kivumishi zuri, na wengi walitoa majibu kama gari nzuri au gari lizuri.

Aidha, nomino mguu kutoka kundi la {u/i} iliwatatiza 80% kwa Watoto wanyankore tunaoweza kusema kwamba hawakuweza kuunganishia jina hili na kivumishi safi, badala yake waliita msafi. Kwa njia hiyo hiyo 81% walikumbwa na matatizo katika kuunganisha jina uma na kivumishi refu, ambapo baadhi ya miundo isiyo sahihi waliyotoa ni kama mguu msafi na mguu usafi. Pia, namna mfumo wa majina unavyokuwa za kundi la {i/zi} kama kazi ulikuwa changamoto kwa wanafunzi 65% walioshindwa kutumia viambishi vya kufaa katika kuunganisha jina hili na kivumishi nzuri. Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa hao Watoto wako dala la sita walionyesha udhaifu katika miundo mibovu, ambapo 86% walishindwa kuunganishia jina gari na kivumishi zuri, na 80% walikosa kuunganisha nomino mwili na kivumishi safi.

4.3.2 Vivumishi vimilikishi

Walipokabidhiwa sentensi tano za kukamilisha kwa kutumia viambishi vya kupatanisha majina ya nomino hasa vivumishi vinavyoweza kuwepo na kimilikishi, wanafunzi walifanya makosa kwa viwango mbalimbali kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali lililo hapa chini:

Jedwali 4.20: Matumizi ya vivumishi vimilikishi

Vivumishi	Ngeli	JawabuSahihi	Washiriki waliofanya makosa			
			Makosa	Sekondari Asilimia %	Vyuo vikuu Asilimia %	Jumla 100%
Kimilikishi	U/i	Mti wangu	Mti gwangu	28	10	38
	a/wa	Baba yako	Baba wako	35	30	65
		Mbuzi wao	Mbuzi yao	34	29	63
		Kipofu wetu	Kipofu chetu	30	20	50
	Ki/vi	Kitu changu	Kitu changye	10	4	14

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Katika Jedwali na. 4.20 matokeo huonyesha maswali yaliyoulizwa kuhusu upatanishi unaohusisha majina ya vitu na maneno yanayokuwa vivumishi vimilikishi yakionyesha kwamba kundi la ngeli za {a/wa} lilikuwa na changamoto kubwa kwa wanafunzi wengi. Asilimia 65 hawakuweza kubainisha vimilikishi kutambua kilicho sahihi cha jina **"mbuzi",** ambacho ni **"-ao."** Majibu mengi yalikuwa kwenye mfumo unaokuwa na maneno kama **"mbuzi"** yao. Katika kundi hili, wanafunzi 63% walikumbwa na ugumu wa kuunganisha jina **baba** na kimilikishi **"-ako,"** wakati 38% walishindwa kuhusisha jina **mti** na kimilikishi **"-angu,"** ambalo kulikuwa na kikundi cha ngeli za {u/i}. Miongoni mwa matokeo ya wanafunzi kwani wanafunzi hao ni kama Baba wako, mti gwangu, na kipofu chetu. Ngeli iliyoonekana kuwa rahisi zaidi inahusu zile nomino inayokuwa katika kundi la {ki/vi}, ambapo 14% pekee walishindwa kutumia kimilikishi sahihi cha jina kitu, ambacho ni **"-angu."**

4.3.3 Vivumishi vya idadi

Wanafunzi pia walipatiwa maswali ili kuchambua jinsi wanavyoweza kuunganisha hayo majina na vivumishi vya idadi. Makosa yao yandhirisha Viwango ambavyo vimeelezwa kwenye Jedwali lifuatalo.

Jedwali 4.21: Matumizi ya vivumishi vya Idadi

Vivumishi	Ngeli	Jawabu yafaayo	Washiriki waliokosea	Shule za upili Asilimia %	Vyuo vikuu Asilimia %	Jumla 100%
Idadi	li/ya	Jino moja	Jino limoja	35	15	50
	a/wa	Baba mmoja	Baba moja	20	10	30
		Ng'ombe watano	Ng'ombe itano	28	19	47
		Kiziwi Mmoja	Kiziwi kimoja	31	30	61
	Ki/vi	Kitabu Kimoja	(Chi)tabu (Chi)moja	05	4	09

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Matokeo kwenye Jedwali Na. 4.21, yanaonyesha kwamba idadi kubwa ya Watoto wasomao walishindwa kutoa majibu sahihi kuhusiana na upatanishi wa jina kiziwi na kivumishi cha idadi moja. Jina kiziwi linatanguliwa kwa kuweka {ki} kwenye umoja, lakini linakiuka kanuni ya kawaida ya upatanishi, ambapo {ki} inayotumika kwa umoja na {vi} katika wingi. Badala ya kutumia viambishi hivi, jina hili linaendelezwa kwa namna sawa na majina mengine yanayoweza kuwekwa chini ya ngeli ya {a/wa}. Asilimia 61% ya wanafunzi walishindwa kuunganisha jina Kiziwi na kivumishi cha idadi moja. Hivyo basi, asilimia kubwa ya wanafunzi walitoa majibu yaliyojumuisha muundo wa **kiziwi kimoja** badala ya **kiziwi mmoja**. Majibu yaliyotolewa kuhusu upatanishi wa jino na kivumishi cha moja yalikuwa jino limoja na jino jimoja. Aidha, upatanishi wa jina **"ng'ombe"** na kivumishi cha idadi tano pia ulionekana kuwaletea ugumu Fulani wanafunzi waliposhindwa kvyaunganisha ipasavyo, ambapo asilimia 47 walikabiliwa na makosa. Wengi walitumia muundo kama **ng'ombe itano** au **ng'ombe zitano** badala ya **ng'ombe watano**. Kwingineko, asilimia 9% ya wanafunzi walifanikiwa kupatanisha jina Kitabu katika ngeli ya ki/vi na kivumishi cha idadi moja, ingawa walitaja matamshi mabaya ya "chi-" badala ya "ki."

4.3.4 Vivumishi vionyeshi

Kulingana na matokeo yaliyowekwa wazi kwenye Jedwali Na. 4.22, inadhihirika kuwa ngeli za watu na wanyama {a/wa} zilikuwa na utata kwa wanafunzi kutaja hasa kufuatilia upatanishi huo na kivumishi kionyeshi. Asilimia 58% ya wanafunzi walishindwa kutoa majibu sahihi kwa kutumia viambishi sahihi. Pia, asilimia 40% walikosa kuunganisha jina **kondoo** na kivumishi hawa. Miongoni mwa majibu waliyoyatoa, kuna matamshi kama **kondoo hizi, kondoo hiyo**, na kadhalika ambayo ni makossa yakisababishwa vile wanavyosema kwa Kinyankore kumanisha Wanyama. Kwani katika kinyankore wanawaita “entaama ezi” siyo hawa bali hizo badala ya **kondoo hawa**. Kuna mtazamo kuwa wanafunzi wengi kutumia miundo kama **askofu huu** na **Askofu hiyo** badala ya **Askofu huyu**. Aidha, upatanishi wa jina Mahali na kivumishi hapa pia uliwatatiza wanafunzi asilimia 49, huku neno **uzi** likiwatatiza asilimia 16 inayoonyesha kwamba Watoto hawa walishindwa kutumia kiambishi sahihi kwa kuunganisha jina hilo na kionyeshi ule. Jina **kitanda** kutoka kundi la {ki/vi} halikuonyesha matatizo yoyote, kwani hakuna mwanafunzi (00%) aliyeshindwa kutumia viambishi sahihi katika kionyeshi.

Jedwali 4:22: Matumizi ya vivumishi vionyeshi

Kivumishi	Ngeli	Mawazo yafaayo	Washiriki waliokosea			
				Sekondari Asilimia %	Vyuo vikuu Asilimia %	Jumla 100%
Kionyeshi	li/ya	Maziwa haya	Maziwa hiyo	10	05	15
	a/wa	Mkulima huyu	Mkulima huu	15	11	26
		Kondoo hawa	Kondoo hizi	32	18	40
		Askofu huyu	Askofu huu	35	23	58
	Ki/vi	Kitanda hiki	-	00	00	00
	u/zi	Uzi ule	Uzi hii	11	05	16
	u/i	Mkate huu	Mkate huyo	9	05	14
		Mahali hapa	Mahali haya	39	10	49

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Kulingana na matokeo yaliyobainishwa katika Jedwali Na. 4.22, inajidhihirisha kuwa ngeli za watu na wanyama {a/wa} ndizo ziliwatatiza wanafunzi kwa ngazi iliyo juu

sana kwa upatanishi wake na kivumishi kionyeshi. Wanafunzi 58% walishindwa kutoa majibu sahihi kwa kutumia kiambishi kinachofaa. Nao wanafunzi 40% walishindwa kupatanisha k***ondoo* na *hawa*.** Miongoni mwa majibu wanafunzi waliyotoa yalikuwa na makosa kama ***kondoo hizi*, *Kondoo hiyo,*** nakadhalika badala ya ***kondoo hawa***. Pengine, miundo kama ***Askofu huu*, *Askofu hiyo*** ilipendelewa na wanafunzi wengi badala ya Askofu huyu. Pengine, kupatanisha jina ***mahali*** na kivumsihi ***hapa*** kuliwasumbua wasomao kiasi chao 49% wakati ambapo neno ***Uzi*** liliwasumbua wasomaji 16% ambao hawakuweza kutumia viambishi vilivyo sahihi kwa kupatanisha nomino hiyo na kionyeshi *ule*. Jina ***kitanda*** la kundi la {ki/vi} ndilo halikubainisha matatizo yoyote pale tunapokuta hakuna wanafunzi wowote (00%) ambao hawakuweza kuunganisha viambishi sahihi kuambatana na majina ya vionyeshi vyake.

4.4 Athari za Kisintaksia (Kimuundo)

Kwa kurejelea wataalamu wa TUKI (2013), wanaeleza kwamba sintaksia ni uwanja wa sarufi unaoshughulikia uchambuzi wa mpangilio unaohusu vipashio vinavyodhihirisha muundo wa tungo. Wataalam wa isimu kama Massamba (keshatajwa), wanafafanua kwamba sintaksia huelezwa kama uwanja wa kiisimu unaoangazia jinsi miundo ya tungo inavyojengwa katika lugha, ikijikita katika kanuni zinazotawala mfumo wa vipashio vya lugha. Sarufi muundo husika inahusu ile mipangilio ya kuunganisha maneno kadhaa ili kujenga miundo sahihi ya tungo na kuunda maudhui yenye maana. Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba isimu muundo huwa kiwango fulani cha sarufi kinachohusu kuchambua mfumo wa maumbo na jinsi yanavyopangwa kutunga tungo sahihi zenye vipashio vyake ili kutengeneza maudhui yaliyokamilika. Katika sintaksia, mambo muhimu yanayoangaziwa ni sheria na kanuni zinazotumika kupanga maneno katika muafaka unaokubalika na wenye maelezo yanayofaa. Kwa kurejelea kazi nyingi za tafiti ambazo zinakubaliana na takwimu za utafiti huu, iligunduliwa kwamba mfumo

wa lugha unakuwa na mpangilio wa kipekee wa kupanga vipashio kujenga sentensi sahihi au zinazoeleweka.

Mbali na isimu muundo, uwanja wa sintaksia unachunguza jinsi maneno yanavyohusiana katika tungo, inaeleza namna maneno huweza kumiliki na kuyatawala mengine.

Taarifa za utafiti zilibaini makosa ya kimuundo kwa wanafunzi kutoka jamii ya Kinyankore ambao wanasoma L2 ya Swahili. Mifano yake imetolewa ifuatavyo:

i. **Kabungo keitu ni kazuri,** wakati inapostahili kuwa **Mlima wetu ni mzuri.**
ii. **Bakuru ba Idara bamekwenda nyumbani**, wakati inapostahili kuwa **Wakuu wa idara wamekwenda nyumbani.**

Taathira zilizojitokeza kwa masomo ya L2 swahili yalitambulika kuwa yanasababishwa ujuzi wa L1 Kinyankore hasa katika muundo wa tungo. Athari hizi zinatokana na jinsi mpangilio wa tungo za Kinyankore zinavyokuwa, ambapo wanafunzi mara nyingi hujikuta wakizungumza lugha potofu wanapojaribu kutafsiri sentensi bila kuzingatia muundo sahihi wa Kiswahili.

Jedwali 4.23: Jinsi sarufi ya Kinyankore inaathiri tungo za Swahili

Umbo lisilo sahihi	**Umbo sahihi**
Abari za iwe Mwalimu	Habari zako mwalimu
Asante mingi sana kwako	Shukrani sana kwako
Bakuru ba Idara bamekwenda nyumbani.	Wakuu wa idara wamekwenda nyumbani
Hakuna yenyini kabisa	Hakuna yenyewe kabisa
Jicho limezimba sana	Jicho limevimba sana
Kabungo keitu ni kazuri,	Mlima huo ni mzuri
Kamata makofi gake	Upigiwe makofi wewe
Mpira gwangye gumepotea	Mpira wangu umepotea
Ngombe zangye zimeibwa	Ng’ombe wangu wameibwa

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Tukiangalia hiyo jedwali namba 4.23 linadhihirisha mifano ya tungo zilizoundwa kisentensi kwa Swahili hasa vile zinavyopindishwa kwa wasomaji wanyankore. Hali kadhalika, Jedwali namba 4.19 linaeleza vile lugha ya Kinyankore inavyoathiri namna ya kutumia L2 ya Swahili. Katika jamii husika ya Kinyankore, imezoeleka kuwakuta wanafunzi wakisema **"Ngombe zangu zimeibwa"** badala ya **"Ng'ombe wangu wameibwa,"** au **"Abari za iwe mwalimu"** badala ya **"Habari zako, mwalimu."**

Mtafiti aligundua kwamba wanafunzi wa Kinyankore mara nyingi wana lengo la kuwasilisha ujumbe tu bila kuzingatia usahihi wa sarufi. Haya matokeo ya utafiti yanakubaliana na utafiti wa (Giles, 1973), muasisi wa msimamo wa NKM (keshatajwa) ambaye alionyesha kwamba binadamu hujaribu kuzungumza kwenye mpangilio unaoelekza kuunda lugha au kuiga lafudhi halafu kutoa maneno mapya kutoka kwa wasikilizaji wao ili kutimiza namna ya kuwasiliana. Hii inafanywa kwa ufahamu au bila ya ufahamu, kwa kuzingatia au bila kuzingatia mikakati maalum.

4.5 Muhtasari

Kwa kuangalia sehemu ya nne, tumewasilisha na kuchanganua matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyofanyiwa kazi vimekuwa vingi hasa kubainisha athari za Kinyankore na vile zinavyochangia katika kuathiri masomo ya L2 ya Kiswahili. Athari zenyewe zimabainishwa zikidhihirisha zile za kileksika, kifonolojia, kisemantiki, na kimiundo ya sentensi. Katika sura inayofuata, zitajadiliwa sababu zinazochangia kasoro za watumiaji wenye asili ya Kinyankore wakijifunza L2 iliyo Swahili.

SURA YA TANO

ASILI YA ATHARI ZA SARUFI YA L1 KATIKA MAFUNZO YA L2

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti na mjadala wa sababu zinazohusu taathira kutoka kwa L1 ya Kinyankore zinabainishwa katika mafunzo ya L2 iliyo swahili. Lengo maalum la pili ndilo linalolengwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa sababu zinazoleta kutokea kwa taathira hizo. Shabaha iliyofuata ya pili yenyewe ililenga kutambua chanzo cha athari hizo. Utafiti ulibainisha kwamba huenda kukawa na sababu tofauti zinazoathiri Watoto walio na L1 ya Kinyankore wanapojifunza Kiswahili.

5.1 Sababu za Kutokea kwa Taathira za L1 Iliyo Kinyankore katika Kujifunza L2 iliyo Swahili

Kwa kurejelea utafiti wa sasa, shabaha iliyofuatia ilishughulikia sababu zinazoletea kuwepo kwa taaathira za L1 iliyo Kinyankore kuingilia usomaji wa L2 iliyo Kiswahili. Lengo hilo limezingatiwa mtafiti akisaidiwa matumizi ya njia ya majadiliano na hojaji, ambapo majibu ya washiriki yalidhihirisha ufanano kwenye vikundi viwili mkiwemo kikundi cha walimu wanaofundisha Swahili, halafu wazazi wanaozungumza Kinyankore. Miongoni mwa sababu zilizotajwa na Watoto wanyankore wasomao Swahili kulikuwa hiyo ya taathira yakuingiliwa na L1, matumizi ya sauti za kaakaa, kutokuwepo kwa fonimu /th/ na /dh/ katika Kinyankore, ufundishaji usioridhisha wa matakwa ya hali na hadhi ya swahili, hata sababu nyingine kama zitakavyoonyeshwa na kujadiliwa hapa chini.

5.1.1 Mwingiliano wa L1

Kwanza kabisa athari za Kinyankore kwenye mafunzo ya L2 iliyo Swahili zinasababishwa na ala za matamshi zinazoathiriwa na Kinyankore.

Jedwali 5.1: Wanavyotumia lugha nyumbani

Washiriki	Kiswahili	Kinyankore
180	09	171

Chanzo: Data za nyanjani 2023

Katika jedwali linaloonyeshwa katika 5.1 linadhihirisha kuwa wanafunzi 9 (tisa) walio sawa na asilimia (5.1%) walijibu kuwa hutumia Kiswahili zaidi wakiwa nyumbani, wakati wanafunzi 171 (94.9%) walionyesha kuwa wanatumia Kinyankore zaidi katika mawasiliano yao nyumbani.

Wanyankore waliojifunza Kiswahili lakini bado wanatumia Kinyankore nyumbani kwa sababu kadhaa, Kinyankore inatumika kama kielelezo cha utambulisho wa desturi za Wanyankore. Watu wengi wanajivunia lugha yao na wanafanya juhudi kuthibitisha kwamba lugha yao inatambulika kitaifa na kiutamaduni. Kutumia Kinyankore nyumbani huimarisha urithi wao wa lugha. Kwa kuangalia mikutadha inayokuwa nyumbani, watu mara nyingi wanazungumza kuhusu mada za kila siku, hisia, haja zao, na hata mengi ambayo yanaweza kuwasilishwa kwa ufanisi zaidi kwa kutumia L1 iliyo Kinyankore. Hii ni hasa wakati wanapokuwa wanazungumza kwa kina na familia.

Wanafunzi wengi hujifunza Kiswahili katika mazingira rasmi kama shuleni na wanapofika nyumbani, wanatumia Kinyankore kufafanua dhana au maneno ambayo ni magumu kwa Kiswahili. Wakati mwingine, baadhi ya maneno au dhana katika Kinyankore huenda yakatoa maana zaidi au kuwasilishwa kiurahisi bila usumbufu wowote kushinda wanapotumia Kiswahili. Hii inawawezesha kuwa na mawasiliano bora na kuelewana kwa urahisi.

Utafiti huu ulitambua pia kuwa watu au vijana wanaweza kupata uwezo kuzungumza Swahili bila shida yoyote kuliko watu wazima ambao wanaweza kuchukua muda kusoma na kupata umilisi wa haraka wa L2. Kutumia Kinyankore nyumbani

kunawezesha kizazi kilichokuza Kiswahili kuvutana na Kinyankore katika mazungumzo wanayotumia kwa kawaida.

Kinyankore, kikitumika kwa kuzingatia uasili wake, mara nyingi hujenga hisia za faraja na urahisi, hata wanaokitumia wanaweza kujisikia kuwa na ushindi zaidi wakati wanazungumza kwa lugha wanayoijua vizuri. Kwa hivyo, kutumia Kinyankore nyumbani kuendeleza mawasiliano kwa wananyankore wanaojifunza Kiswahili ni mwenendo wa kawaida ambao umejengwa kwa msingi wa kukuza utamaduni, mazingira yanayotawala mawasiliano hasa uhusiano wa kijamii.

Kwa kurejelea utafiti huu, iligunduliwa kuwa hiyo ndiyo sababu kuu inayochangia taaathira ya Kinyankore wakati wa kujifunza Kiswahili.Ilijitokeza pia kwamba waafunzi wanatumia Kiswahili wakati wanapokuwa shuleni peke yake. Na walipoendelea kuulizwa kuhusu lugha inayotumiwa zaidi wakiwa hawapo nyumbani na shule, majibu yalikuwa yafuatayo:

Jedwali 5.2: Watafitiwa - Walioshiriki

Wanafunzi	Kinyankore	Kiswahili
180	54	126

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, wanafunzi 126 wa vyuo vikuu, sawa na 53%, walieleza kuwa wanatumia Kiswahili zaidi kwa mawasiliano wanapokuwa vyuoni. Tukiangalia matokeo mengine, wanafunzi 54, walio sawa na 46%, walisema kwamba wao wanatumia Kinyankore zaidi wakiwa wanawasiliana kivyao vyuoni.

Halafu wakaulizwa ikiwa Kinyankore kina athari kwenye mafunzo ya L2 kimsamiati, na wakajibu hivi: wanafunzi 102, sawa na 56.6%, walijibu NDIYO, wakati wanafunzi 78 (43%) walijibu HAPANA. Wale ambao waliokiri kutumia kiswahili waliweza kutamka maumbo ya Swahili na ikadhihirika wazi vile yanayoathiriwa na Kinyankore.

Jedwali 5.3: Watafitiwa

Washiriki	Naam	La
180	102	78

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Kulingana na jedwali lililotolewa katika 5.3, wanafunzi 102, sawa na asilimia 56.6, walijibu NDIYO. Washiriki 78, wakilinganishwa na asilimia 43, walijibu HAPANA. Na wale ambao walijibu NDIYO walitaja maumbo katika L2 iliyo Swahili yenye uhusiano wa karibu sana na yale maumbo ya Kinyankore. Kuna mifano inayoonyeshwa ifuatavyo kama;

Jedwali 5.4: Athari za kimsamiati

Kinyankore	Kiswahili
Omuntu	Mtu
Omuti	Mti
Embuzi	Mbuzi
Esimu	Simu
Emeza	Meza
Enjoka	Nyoka
Omwana	Mwana
Enyama	Nyama
Ebinyasi	Nyasi
Mpaka	Mpaka
Ebyokurya	Vyakula
Ekyokurya	Chakula
Embwa	Mbwa
Esaati	Shati
Sikati	Sketi
Ekaramu	Kalamu
Esihani	Sahani
Enanasi	Nanasi
Esafuria	Sufuria
Ekitabo	Kitabu
Embaata	Bata
Enkoko	Kuku
Amaguru	Miguu
Omupiira	Mpira
Ameino	Meno
Ekanisa	Kanisa
Mama	Mama
Rediyo	Redio
Omukono	Mkono
Orurimi	Ulimi
Eiziina	Jina
Omukyeka	Mkeka
Amaizi	Maji
Ebaruha	Barua
Orubaho	Ubao
Emyaka	Miaka
Eshaaha	Saa
Okunywa	kunywa
Gyenda	Enda
Omugati	mkate
Ekijiko	Kijiko
Amaisho	macho
Okutetema	tetemeka
Omuzeeyi	Mzee
Emotoka	motokaa
Amakara	Makaa
Embarasi	Farasi
Naaba	nawa
Ina	Nne
Apana	hapana
Reeta	leta
Amakara	makaa
Dureiva	Dereva
Omusitari	mstari
Imuka	Amka
Amashita	mafuta
Kuzara	kuzaa
Shukari	sukari
omusingi	Msingi

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Jedwali lililo hapo juu linadhihirisha kwamba Kinyankore kikilinganishwa na Swahili huonyesha lugha mbili ambazo zina uhusiano wa karibu, hasa kutokana na mwingiliano wa kisiasa na kijamii uliotawala mambo mengi yanayowahusu wanaAfrika mashariki.

Kulingana na wale wanajamii wanaozungumza Kinyankore na Kiswahili, mara nyingi hujifunza na kutumia maneno haya wakati wa mawasiliano, hasa wakiwa mijini. Lugha huweza zikawa zinatumia maneno sawa, lakini matumizi yao yanaweza kutofautiana kulingana na muktadha. Sauti au matamshi katika lugha moja yanaweza kuwa tofauti na nyingine, hata kama maneno ni sawa.

Watu wanaozungumza Kinyankore na Kiswahili wanaweza kuwasiliana kwa urahisi kupitia maneno mengi yanayofanana. Hii huonyesha jinsi lugha zinavyoweza kuathiriana na zikaendelea zikitumika kukamilisha shabaha ya mawasiliano kwa wanajamii husika.

5.1.2 Matumizi ya ala sauti za kaakaa

Aidha, katika utafiti wake, mtafiti alikuja kugundua kwamba waulizwaji wanatumia sana yale matamshi yanayotamkwa kwenye sehemu za ukaakaaishaji wanapozungumza lugha yao ya asili (Kinyankore), hali ambayo inaathiri lafudhi ya wale wanaojifunza Kiswahili.

Iligunduliwa pia kwamba maneno ya Kinyankore yakitamkwa kwenye kaakaa laini yanasababisha mabadiliko katiko lafudhi. Lafudhi hiyo inakuwa na athari pale ambapo matamshi yanayojitokeza yametokana kwenye L1 anayoitumia msemaji hata kwenye mazingira aliyojifunzia lugha. Kwa nyakati tofauti, watu huweza kugundua kutoka kwa matamshi kama anayezungumza akiwa mgeni kutoka nchi fulani au kama ni mzaliwa wa mji fulani kwa kuzingatia vile anavyotamka baadhi ya maneno.

Jedwali 5.5: Fonimu za kaakaa laini

Na	KINYANKORE	KISWAHILI
1	Omugongo	Mgongo
2	Omukono	Mkono
3	Emigati	Mkate
4	Amakara	Makaa
5	Gaba	Gawa
6	Imuka	Amka
7	Muhogo	Mhogo
8	Okuguma	Ugumu
9	Okutu	Sikio
10	Ngaaha	Hapana/la
11	Okugura	Kununua
12	Ngambira	Niambie

Chanzo: Data za uwanjani (2023).

Jedwali na. 5.5 linaonyesha kwamba wazungumzaji watumiapo Kinyankore, fonimu zinazotamkwa kwenye sehemu ya ukaakaaishaji zinajulikana kama konsonanti ngumu na konsonanti laini. Hizi ni muhimu katika kubainisha maelezo yanayotolewa na maumbo hayo na zinachangia tofauti katika matamshi na sarufi. Fonimu hizo zinazotamkwa kwenye sehemu za kaakaa gumu hutamkwa kwa urahisi, na mara nyingi zina nguvu zaidi. Mifano ya fonimu kama hizo kwa Kinyankore ni /k/ na /g/. Kaakaa hizi mara nyingi zinawakilisha sauti zenye nguvu na zinahitaji nguvu zaidi katika kutamkwa.

Pengine, fonimu zinazotamkwa kwenye sehemu ya kaakaa laini zinatamkwa kwa urahisi zaidi na zinaweza kuwa na sauti nyororo. Mifano inayoonyesha matamshi hayo ya kaakaa laini katika Kinyankore ni /j/ na /ch/. Konsonanti hizi zinaweza kuathiri muktadha unazunguka matumizi ya neno husika. Kuelewa zile fonimu zinazotamkiwa kwenye sehemu hiyo ya ukaakaaishaji ni muhimu katika kujifunza Kinyankore na Kiswahili, kwani zinachangia katika maana na uelewa wa lugha.

5.1.3 Fonimu za /θ/ na / ð / hazipo katika Kinyankore

Takwimu za utafiti zilionyesha kwamba lugha ya Kinyankore ina upungufu wa miongoni wa fonimu, jambo linalomfanya ajifunzaye Kiswahili kutotamka vizuri maneno fulani. Utafiti umegundua kwamba fonimu /θ/ na / ð/ zinakosekana kwenye L1 iliyo Kinyankore. Ndiyo sababu washiriki walikosea kutaja maneno mengine kama ipasavyo. Kwa mfano, "**Thelathini",** ambayo hutamkwa kama **"Selasini",** na **"Adhabu",** ambayo hutamkwa kama **"Azabu",** kufuatilia maelezo yanayoonyeshwa kwenye jedwali namba 5.6.

Jedwali 5.6 Uchopekaji wa /θ/, /ð/

Kosa	**Kiswahili**
Serasini	*Thelathini*
Samani	*Thamani*
Azabu	*Adhabu*
Zawabu	*Dhahabu*

Chanzo: Takwimu za Uwanjani (2023)

Jedwali na.5.6 linadhihirisha kwamba katika Kinyankore, matamshi ya th (/θ/, /ð/) hazipo kama zilivyo kwenye miundo ya tungo zinazopatikana katika Kiswahili au Kiingereza. Hata hivyo, Kinyankore kina fonimu zinazofanana na matamshi hayo, ila zinaweza kutolewa kwa njia tofauti. Kinyankore haina sauti hii kama inavyopatikana kwenye tungo za Swahili. Badala yake, sauti hii inaweza kubadilishwa na sauti zenye karibiana zinazopatikana katika Kinyankore, kama vile /s/ kwa /th/ au /z/ kwa /dh/.

5.2 Mafundisho Yasiyofaa ya Kiswahili

Ufundishaji usiozingatia haja za wasomao huleta sababu nyingine iliyotambuliwa katika utafiti. Mtafiti aligundua sababu hii kutoka kwa majibu ya washiriki. Utafiti ulibaini kuwa ufundishaji usiofaa kuhusu matumizi ya Swahili ilikuwa sababu moja wapo inayochangia athari za kisarufi. Pia, ilionekana kwamba waliokuwa wanafundisha L2 wenyewe walikuwa wana upungufu fulani kuhusu lugha waliyokuwa

wanajaribu kufundisha wanafunzi hata kutokuwa na umilisi unaofaa kuwafafanulia ifaavyo.

Jedwali 5.7: Makosa ya walimu

Kosa	Neno sahihi
Jumapiri	Jumapili
Lara	Lala
Sarama	Salama
Sule	Shule
Gholofa	Ghorofa

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Kama inavyoelezwa katika jedwali 5.7, ilijitokeza kuwa kuna walimu waliokuwa wanafundisha ambao wao wenyewe huathiriwa na lugha zao zinazokuwa L1 kwao, halafu wanafunzi wanajifunza lugha kwa kuiga matamshi ya walimu wao. Hivyo, washiriki walishindwa kutambua matamshi yaliyo sahihi iwapo walimu wao wanafanya makosa, mfano, walimu wanapokuwa wanatamka "r" badala ya "l" na "s" badala ya "th-"kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Jedwali 5.8: Ubadilishanaji wa /r/ kwa /l/; /th/ na /s/

Makosa ya Walimu	Neno sahihi
Mbari mbari	Mbali mbali
Semanini	Themanini
Murango	Mlango
Chiswahiri	Kiswahili
Selusi	Theluthi
Serasini	Thelathini

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Jedwali 5.8 hilo juu linadhihirisha kwamba kufundisha Kiswahili kinapofunzwa Watoto wenye asili ya Kinyankore kunakabiliwa kikionyesha shida mbali mbali kutokana na ufundishaji mbaya. Kinyankore na Kiswahili vina sauti tofauti, na walimu wanaweza kuwa na ugumu katika kuzitaja zile fonimu kwa swahili. Hii inaweza kusababisha matatizo katika kueleweka na kufikiri kwa wanafunzi. Ikiwa walimu wenyewe wanaweza kuwa na ukosefu wa uelewa unaofaa kutosha katika kusomesha

Swahili inayostahili kutumika na Watoto wanyankore, basi wanaweza kupata matatizo wanapokuwa wanatoa maelekezo yaliyofaa na kuunda mazingira mazuri ya kufunza.

Njia mahsusi zinazotumika kufunzia ambazo hazijazingatia mahitaji ya yale mazingira ya wanafunzi zinawapelekea kukosa uhusiano ambao ungeliwasaidia kutekeleza wajibu wao wa kufundisha L2. Kwa mfano, kutumia mfumo wa kufunzia unaojikita zaidi katika sarufi kuliko kwenye namna watumiaji wa lugha wanavyoweza kuitumia kutekeleza shabaha ya kuwasiliana wao kwa wao kikawaida. Walimu wanaoshindwa kuleta vifaa vya kufunzia katika kutimiza kazi yao yao ya kufunza, kama vitabu, kamusi, na vipaza sauti, kunaweza kupunguza ufanisi wa ufundishaji. Walimu pia, huweza kupata hofu ya kufanya makosa wanapojaribu kufundisha Kiswahili, na hii inaweza kuathiri motisha ya wanafunzi darasani. Walimu wanaokosa kuelewa muktadha wa kihistoria na kitamaduni wa Kiswahili wanaweza kukosa ujuzi unaofaa kufundisha lugha kulinga na muktadha mpana. Walimu wengine ambao hawana tajriba ya kuzoea matumizi ya Swahili kwenye mawasiliano ya kawaida, wanaweza kuwa na upungufu fulani kutokana na kukosekana kwa fursa za kuzungumza lugha hiyo kikawaida.

Kushughulikia changamoto zinastahili kuzingatiwa ili kuboresha mafundisho ya Swahili kuwezesha Watoto wanyankore kupata urahisi wa kuelewa L2 kiswahili. Mbinu bora zinaweza kujumuisha namna ya kuhusisha njia zinazovutia, vifaa vifaavyo, na kusistiza mtazamo wao kuhusu Swahili ili waweze kujisaidia kujifunza, na kuwezesha mazingira ya mawasiliano.

Hivyo basi, mafundisho yasiyosisitiza viwango vya ufaulu kuhusu ujifunzaji unasabaisha walimu wanaofundisha bila kujali jinsi wanavyotumia zana za kufunzia na mtindo wa lugha, leksika na maana yanayojitokeza kwenye mfumo wake huo.

Ilibainika pia kwamba kuna wanaofundisha wa Swahili ambao wakati mwingine hawatumii mbinu zifaazo wakiwa wanafundisha halafu zinazowawezesha mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika somo. Pia, Kuna njia zinazozistahili kutumika katika kufundishia Kiswahili ni kuhusisha Watoto kwenye matendo kama vile midahalo, mijadala ya uzungumzaji inayoweza kusaidia mwanafunzi kuendeleza uelewa wao wa L2 inayofunzwa.

5.3 Kiswahili Haipewi Kipaumbele

Takwimu za utafiti zilionyesha kwamba jamii ya Kinyankore haijali kuipa kipaumbele L2. Wanafunzi wa Kinyankore walikiri kwamba wanapendelea kutumia Kinyankore nyumbani na wakiwa kwenye shughuli za kijamii kama harusi, misiba, na mikutano ya ukoo. Hii inamaanisha kwamba Kiswahili hakina umuhimu wa kutumika sana kwa wanyankore, hali inayokwamisha juhudi za wanafunzi kujifunza lugha hiyo kwa ufanisi zaidi.

Jedwali 5.9: Wanaopendelea Kinyankore kuliko Kiswahili

Washiriki	Kiswahili	Kinyankore
180	05	95

Chanzo: Data za nyanjani 2023

Takwimu kutoka jedwali 5.9 zinaonyesha kwamba Kiswahili hakitumiki katika shughuli rasmi za serikali, vituo vya afya, shule, mahakamani, ofisi za kata, wala katika maeneo mengine ya umma. Aidha, isipokuwa maeneo ya kijeshi, wanaotumia Swahili kwa ajili ya mawasiliano ya kawaida ni wachache sana, hata idadi ya wanahabari na wanabiashara au waingilisti wa kidiini na shughuli nyingine zilizo rasmi za kiserikali huwa ni ya chini sana. Matokeo haya yanathibitishwa tukiangalia matokeo ya utafiti yaliyotafitiwa na mwanaisimu Barton (1980), ambaye aligundua kuwa Kiswahili kinafanya vyema katika mazingira rasmi kama shuleni, na kongamano za waswahili. Polome (1980) alieleza kwamba vile namna Swahili inavyotumika kienyeji, huwa

inatumika kwenye mazingira mbalimbali. Utafiti ulionyesha kwamba Kiswahili hakitumiki sana kwenye sherehe zilizo rasmi za serikali, huku kuna wakati ambapo lugha za kienyeji zinadumu katika matumizi yasiyo rasmi, hasa nyumbani.

Hiyo L2 ya Swahili inayoelezwa inakosa kipaumbele tukizingatia Watoto wanyankore wanaoitumia kwa sababu kadhaa ambapo idadi kubwa ya Watoto wanyankore wanalenga kujifunza na kutumia Kinyankore kama njia iliyo ya kiasili ya mawasiliano. Hivyo, Kiswahili kinaweza kukosa umuhimu kwao katika mazungumzo wakiwasiliana kikawaida. Watu wa Kinyankore wanaona Kiswahili kama lugha isiyo na umuhimu mkubwa isiyo na uwezo wa kuendeleza sekta za jamii yao hata kiuchumi. Wanapokutana na lugha kama Kingereza au Kinyankore, Kiswahili kinaweza kuonekana kama si chaguo linalostahili kutangulia kuendeleza mazungumzo ili kufanikisha mawasiliano yao.

Kwa kurejelea sehemu nyinginezo, historia inayojulikana kuhusu siasa za nchi hata za jamii iliweza kuathiri mtazamo wa wananchi kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, mfumo wa kisera juu ya mawasiliano katika elimu na uhusiano wa kisiasa zinaweza kuathiri jinsi lugha hii inavyotumika. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba kuna baadhi ya shule ambako somo la Kiswahili halikuchukuliwa kuwa somo muhimu kwa wanafunzi hata kwa uongozi wa shule. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi wanaweza kuhimizwa kutopendelea kufundishwa Swahili au kuchagua masomo mengine isipokuwa Kiswahili.

Wazazi na familia wanaweza pia kutoshawishi watoto wao kujifunza Kiswahili, wakishikilia zaidi kudumisha matumizi ya L1 ya Kinyankore. Hii inasababisha watoto wenye mtazamo chanya zaidi kwa Kinyankore kuliko Kiswahili.

Ili kuboresha kipaumbele cha Kiswahili kwa wanafunzi wenye umilisi juu ya Kinyankore, ni muhimu kudumisha mafunzo ya kusomesha L2 vizuri, kuboresha mkutadha na hali ya kufunzia hata kuhamasisha dhima ya L2 hiyo Swahili kwenye shughuli za kisasa wa kijamii na kiuchumi.

5.4 Mtagusano wa Kinyankore na Kiswahili

Athari za sarufi ya kinyankore zilijitokeza katika masomo ya L2 swahili kwa unasaba. Mgullu (2004) anabainisha kuwa wanaisimu wamegawanya lugha katika makundi tofauti kwa kuzingatia vigezo fulani. Moja ya vigezo hivi ni kile cha unasaba, ambapo maelezo kuhusu tungo za kienyeji ziliwekwa kwenye vikundi hata Kiswahili ikiwa inahesabika kama mfano wa lugha hizo.

Kipengele hicho cha unasaba kinachangia kwa kiwango kikubwa katika kuathiri kujifunza kwa L2 hata kwenye wale wanaokitambua kuwa njia nyingine ya mawasiliano inayoweza kusaidia taifa Uganda. Mwingiliano ukijitokeza baina ya mifumo hiyo ya Kinyankore na Kiswahili ni wa kipekee na unajitokeza kwenye sehemu mbalimbali. Kunajitokeza pia vigezo bora vinavyodhihirisha mwingiliano huu:

Kuna maneno mengi katika Kiswahili na Kinyankore yanayofanana au yanayoweza kutumika kwa njia sawa. Hii inakuwa kwa sababu ya kuona Swahili kama lugha inayobeba sifa za kibantu ambayo ina mchakato wa kutoa maumbo yanayofanana na mengine yanayotambulika katika lugha nyinginezo. Kwa kurejelea maumbo tofauti, Kiswahili kimeingilia Kinyankore kwa kuleta maneno mapya, hususani kwenye mambo yanayoshughulikia biashara, teknolojia, hasa sesturi za jamii husika ya kisasa. Wanafunzi wa Kinyankore wanawajibika kujifunza L2 swahili kwa kuwa ni lugha inayotumika katika elimu, biashara, na mtandao wa kijamii. Hii inaongeza mwingiliano unaopatikana uhusiano wa mifumo ya lugha zinazoingiliana. Kiswahili na Kinyankore

zinaathirana katika nyanja za utamaduni na sanaa. Wanafunzi na wasanii wa Kinyankore mara nyingi hutumia Kiswahili kudhihirisha mambo yao kwa hadhira kubwa.

Ingawa Kinyankore na Kiswahili zina maneno tofauti kimsamiati, baadhi ya kanuni za mtindo kwenye tungo ambazo zinaweza kueleweka kirahisi kwa sababu ya muktadha unaohusisha tungo hizo.

Mwingiliano kati ya Kinyankore na Kiswahili husaidia kwenye mfumo wa kuimarisha mazungumzo yanayoendelezwa na wanajamii tofauti. Hii inachangia utamaduni wa kisasa wa waafrika wa mikoa ya upande wa mashariki na kufungua fursa za kuendeleza manufaa ya wananchi.

5.5 Thamani ya desturi za Wanyankore

Utafiti huu ulionyesha kwamba washiriki wanaotumia Kinyankore (71%) nyumbani wanaendelea kudumisha na kurithisha Kinyankore kwa familia zao. Kulingana na Tabouret-Keller (1989) na Giles (1979), jamii zinazosisitiza namna ya kutumia L1 zinaonyesha kuthamini lugha hiyo. Matokeo haya yakielezwa na wahusika wa utafiti yanaweza kuashiria kwamba wanasababisha kudumisha utambulisho wa wanyankore katika jamii zao wakiwahimiza wanyankore kuendelea kutumia Kinyankore majumbani, hususan kwa washiriki wa rika la vijana. Hivyo, matokeo haya yanadhihirisha kauli ya Coulmas (2005) anaposema kuwa lugha huwa njia ya kutambulisha jamii, hutumika kama ishara inayounganisha wanajamii hata kuashiria jamii inayotumia lugha hiyo.

Katika mawasilisho yaliyotangulia mwanzoni, kuna yale maeneo, historia ya desturi, tamaduni na mila ya kijamii inaweza kuathiri mtazamo wa wananchi kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, tukirelea mifumo ya kisera luhusu lugha katika elimu ya nchi na uhusiano

wa kisiasa zinaweza kuathiri jinsi lugha hii inavyotumika. Pia kuna asasi za elimu ambapo Kiswahili inaweza kuwa si somo muhimu katika mfumo wa elimu. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi wanaweza kutengwa na kufundishwa mada ambazo hazihusiani usomaji wa mfululizo wa Kiswahili.

Wazazi na familia wanaweza pia kutoshawishi watoto wao kujifunza Kiswahili, wakishikilia zaidi utamaduni wa Kinyankore. Hii inasababisha watoto wenye mtazamo chanya zaidi kwa Kinyankore kuliko Kiswahili.

5.6 Ukosefu wa Mazingira Rafiki ya Kufunzia Kiswahili

Kwa kuangalia utafiti huu, mtafiti mwenyewe aligundua kwamba moja ya sababu zinazochangia wanafunzi wengi wa Kinyankore kuwa na matatizo katika masomo ya L2 ya Swahili kama kukosa mazingira mazuri ya kujifunzia. Utafiti ulibaini kwamba wanafunzi wanapokuwa nyumbani, sokoni, kwenye misiba au harusi, wanazungumza Kinyankore. Mazingira haya yanawapa ugumu wanafunzi kupata fursa kujieleza na kutumia Kiswahili.

Sehemu pekee ambapo wanafunzi wanapata nafasi inayowapa kujieleza katika L2 ya swahili shuleni, na mazingira haya hayawezeshi wanafunzi kulitumia Kiswahili kwa ufanisi. Hivyo, mwanafunzi ambaye amezoea kuishi katika jamii inayozungumza L1 iliyo Kinyankore atapata changamoto katika mawasiliano. Shida hii itajitokeza wazi iwapo mwanafunzi atahamia eneo ambapo tungo hizo za asili haziruhusiwi, hali itakayomfanya apate ugumu wa kuwasiliana na wengine kwa kipindi fulani.

Jedwali 5.10: Wanaoathiriwa na mazingira

Washiriki	La	Ndiyo
100	15	85

Chanzo: Data za nyanjani 2023

Kulingana na Jedwali 5.10 hilo juu, ni dhahiri kwamba mazingira yanaathiri Watoto wengi sana wanapojifunza L2, kwani wanaheshimu sana uelewa wa L1 inayotambulishwa kuwa ndio ya kiasili, na hivyo kujifunza na kutumia L2 iliyo Kiswahili huwa hakufai kwao. Lugha ya Kinyankore inawafanya Watoto wanyankore kukumbwa na shida wanapotamka na kuwasiliana kwa Kiswahili. Kwa hiyo, inaweza kutambulika kinagaubaga kwamba taathira za jamii au za mikutadha hudhihirisha zile sababu zinazoathiri wanafunzi wa Kinyankore wanapokuwa wanasoma L2 ya Swahili. Aidha, jamii ya Wanyankore haina desturi ya kuwahimiza watoto wao kuzungumza Kiswahili muda baada ya muda kutokana na mazingira wanayokabiliana nayo.

5.7 Kinyankore kuwa Kitambulisho cha Jamii

Kama inavyoelezwa katika utafiti wa sasa kurejelea wale wanaisimu kama Bourhis na Sachdev (1984), kuna lugha zaidi ya 6500 duniani, na takriban zile lugha nyingi hizo ziko katika hatari ya kuangamia au kutoweka kutokana na kupoteza utambulisho wao. Giles (1979 na 1982) anaeleza kuwa ule ushirikiano baina ya tungo husika unakuwa utambulisho. Mfumo wa kinadharia ya wataalam hao kina Giles zinatoa maelezo kwamba kutambua wanajamii wana mchakato unaoendelea unaohusisha vibainishi vingi vinavyoshikiliwa na jamii ya watu wanaoshiriki lugha inayounda kiini cha kutambua mifumo hiyo.

Giles (keshatajwa) anasisitiza kwamba jamii ya lugha inajumuisha watu wanaojitambulisha kuwa wanajamii fulani ambao wanatofautiana na wengine. Fasili hii ya wanajamii hawa kuhusu lugha ndio msingi unaotegemewa na mfumo wa kinadharia ya Giles kujumuisha na kutoa maana halisi ya utambulisho.

Uhusiano unaojitokeza pia unaoeleza jinsi lugha inavyoingiliana na utambulisho umeelezwa katika nadharia hiyo inayozingatia mahusiano ya kimawasiliano kama

ilivyoelzwa na Giles (1982), ambapo anasema kwamba utambulisho wa jamii unategemea sana watu wazungumzao lugha yenyewe ya asili. Nadharia hii inabainisha kwamba wanajamii wanaohusika katika kundi fulani wanaposhindwa kujieleza kwa lugha yao mahsusi na kuamua kuzungumza lugha ya kundi linguine la jamii tofauti ili kufaidika kijamii na kiuchumi, kuna makutano kati ya jamii hizo mbili.

Makutano hayo huenda yakajitokeza na taathira hafifu zinazoathiri jamii hiyo, kwani lugha yao yenyewe inaweza kupotea na kukosa wazungumzaji. Wakati lugha yao hiyo inaposhindwa kudumisha utambulisho, utambulisho wa jamii ile iliyo tofauti pia hupotea kwani wazungumzaji wake wenyewe walipotea na hawapo tena

Kulingana na takwimu za utafiti wa sasa, wanaofundisha Watoto wanyankore walipoulizwa kwa nini wanapendelea kuzungumza L1 yao iliyo Kinyankore kila wakiwa kwa mazingira yao, wengi wao walijibu kwamba wanalenga kutunza na kulinda lugha yao kutoathirika na kukubadilika na mwisho wake ikapotea kabisa. Walimu hawa wanaamini kuwa, ikiwa wasipozungumza L1 ya watoto wao hawataweza kuzungumza lugha yao ya asili na hivyo itakufa. Wazo hili pia linakubaliwa na kuaminiwa vijana wa Kinyankore ambao 56% hupenda kuzungumza lugha wa Kinyankore popote pale walipo.

5.8 Upungufu wa Wataalam wa Swahili

Tukirejelea takwimu za utafiti wa sasa, imegunduliwa kuwa asasi nyingi za elimu utafiti ulikofanyika hazina wataalam walio na wajibu wa kufundisha Swahili ipasavyo. Utafiti huu ulifanyika kwa asasi hizi ukilinganishwa na mahitaji ya mafunzo shuleni. Kila shule ilikuwa na wastani wa wanaofundisha Swahili kutoka kidato cha kwanza hadi cha sita mfululizo. Jambo hili linawaletea walimu hawa kuhisi mzigo mkubwa kutokana na

wingi wa vipindi. Utafiti umeonyesha kwamba somo la Swahili hupewa vipindi viwili vyenye dakika themanini kila wiki kwa madarasa mengi.

Hivyo basi, walimu wengine wanaweza kukwepa kufundisha kipindi cha Swahili wakihisi kuchoka kutokana na uwingi wa vipindi darasani. Aidha, idadi ya walimu hao waliohitimu kufundisha somo hili ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi.

Jedwali 5.11 Washiriki wanaofundisha Swahili

Asasi	Idadi ya Washiriki	Idadi ya Walimu/Wahadhiri wa Kiswahili
Shule A	93	3
Shule B	88	3
Shule C	65	2
Shule D	85	2
Shule E	62	2
Chuo Kikuu A	24 (Idarani)	3
Chuo Kikuu B	12 (Idarani)	2

Chanzo: Data za Uwanjani 2023

Kwa kurejelea data za uwanjani, kutokuwa na walimu wa kutosha wanaoelewa vizuri Swahili kulikuwa moja wapo ya sababu zinazochangia wanafunzi kukumbwa shida zinazosababisha L1 kuingilia L2 na ikaizuia kueleweka kwa urahisi na kwa haraka.

5.9 Mafunzo Yasiyokidhi Kiwango Sanifu

Utafiti umebaini kwamba, ikiwa Watoto watakaposoma L2 na wakaweza kujifunza kwa ufanisi, inabidi wanaoifundisha kusistiza umuhimu wa kuhakikisha kuunda mazingira yafaayo ya kufundishia na kufunzia yanayokidhi haja za wasomaji. Kufanya hivyo kutawasaidia kuelewa matumizi ya zana zinazotumika kusomesha msamiati na vipengele vingine katika L2 kama vinavyopaswa kujumuishwa ili kufanikisha na kutekeleza ujifunzaji.

Ili kufanikisha uelewa mzuri na matumizi yafaayo ya L2 inayofundishwa, ni sharti walimu wabuni mbinu bora zinazotumika kufundishia, halafu zinapaswa kuzingatia

njia mwafaka za kuzitumia hasa zile zana na vitu halisi ili kurahisisha ufunzaji na uelewaji wa msamiati na mambo mengine yanayofunzwa.

Taarifa za uwanjani zilionyesha kwamba walimu wanapaswa kufanya juhudi kuwa mfano mzuri kama vielelezo bora mbele ya wasomaji wakati wa kujua na kujifunza Kiswahili, hasa wanapokuwa nao shuleni. Wanapaswa kulithamini somo wanalolifundisha kwa kuwasiliana nao na kuwasaidia wakiwa wanafanya kazi za miradi yao wakati wanapokuwa shuleni. Hali hii itawasaidia wanafunzi kujenga msingi mzuri na kujiamini wanapozungumza Kiswahili wakiwa mbele ya umati au umma. Aidha, walimu wanapaswa kuwahimiza wanafunzi wao kuendeleza upendo na kuwahimiza kuhusika katika masimulizi ya hadithi vilivyoandikwa kwa Kiswahili, ili kukuza uwezo wao wa msamiati unaopatikana upya wakisoma Makala na hadithi hizo.

5.10 Ujuzi na Tajriba ya Wafundishao Swahili

Utafiti wa sasa ulionyesha kwamba wafundishao L2 wenye uelewa unaofaa kuhusu matumizi na ufundishaji wake wa jumla si wengi. Pia, kuna wale walimu wanaofundisha katika asasi Fulani bila kuwa na uzoefu na tajriba inayotakikana kufanya kazi hiyo. Ujuzi ukikosekana wa kufunza Watoto hao unaweza kuleta madhara mabaya kwa wasomao na hata kuharibu uelewa wa msomaji wote. Inajulikana kuwa mwanafunzi anajifunza vizuri kutokana na vile mwalimu wake anavyomfundisha, na hivyo basi, ikiwa mwalimu hawezi kujiamini kitaaluma yeye mwenyewe, mwanafunzi atachukua muda mrefu kujifunza lugha hiyo. Jambo hilo linasababishwa na msimamo wa kuwa mwalimu pia hupendelea L1 yake mwenyewe inayomwathiri pia akiwa anajaribu kufunza L2 kwa wasomaji wake.

Jedwali 5.12: Tajriba ya wafundishao Kiswahili

Walimu wenye Kiwango cha stashahada /12	Walimu wenye shahada ya Juu(digri) /12	Walimu waliohitimu Uzamili /07
05	07	04

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Data za utafiti huu zilionyesha kwamba umilisi usiofaa wa L2 inayotumika kufundishia unaathiri vibaya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwanafunzi hukariri matamshi yanayotajwa na anayemfundisha, hata anamwigiza mwalimu huyo kuonyesha amemwelewa vizuri. Watoto wanapenda kuigiza vile mwalimu wao anavyosema na wakimsikia mwalimu anatamka maneno vibaya, anakuwa na uwezekano wa kufanya kasoro za kimatamshi asipojihadhari na kuchunga. Pia, ufundishaji mbovu wa walimu wengi wa Kiswahili unachangia tatizo hili. Mkakati duni unaoweza kuongoza ufunzaji wa L2, unaotokana na uelewa hafifu wa walimu, unakuwa kikwazo, kwani walimu wengi hawawezi kuchagua njia zinazofaa kutumika kufunzia hata kuzitumia inavyotakikana. Aidha, mara nyingi hawatumii zana halisi za kutumia katika mafunzo na hawazitumii ipasavyo kuona kwamba zimewasaidia kutekeleza shabaha yao ya kuwafunza Watoto na wakaelewa ifaavyo. Hali hii inaweza kupelekea walimu wasitambue kwamba wao ndio kiini cha changamoto, halafu mwishowe wanadhani kuwa wanafunzi ndio hawawezi kuelewa na kuzungumza vizuri Kiswahili. Mtazamo huu unaweza kuwa kikwazo kikubwa kuwaletea waspmaji utata wa kitaaluma kuwajengea hofu kuwazuia kuelewa L2 mpya (Kress & Tracy, 2008).

5.11 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili

Utafiti wa sasa pia ulitambua ya kwamba ni muhimu kuwepo na mambo mbalimbali yatakayomsaidia kuwa na umilisi wa L2 ili mwanafunzi ajifunze kwa ufanisi. Haya yanajumuisha matumizi ya njia zifaazo za ujifunzaji. Wapenzi na wakereketwa wa elimu wanapaswa kuhakikisha kuna uwiano mzuri kwa wasomao na wanaowafunza

kwenye kila darasa. Hii itawasaidia wanafunzi kujifunza mapema na kiurahisi wanapohitaji msaada.

Utafiti umebaini kwamba mwanafunzi anapopata msaada wa kimasomo kwa wakati, anajifunza kwa ufanisi na haraka zaidi. Wanafunzi wanapopata msaada wa haraka wakiwa wanasoma darasani, wanapata motisha ya kutumia uwezo wao na kuendelea haraka wakiwashinda wenzao wanaokosa msaada. Hata hivyo, kama mwanafunzi hana muda unaomtosha kuzungumza na kujifunza somo la L2 ya Kiswahili nje ya shule, hiyo itakuwa changamoto kubwa kwake.

Pia, Walimu wanatakiwa kuunda mazingira ambayo yatawezesha Watoto haokutumia L2 ya Swahili sana wakichukua wakati mrefu wa kujizoeza, kwa kuweka sheria rahisi shuleni zinazokataza kutumia L1 ya Kinyankore. Wazazi, walimu, na watu wote wanajamii husika wanahitaji kujitahidi kuunda mazingira mazuri yanayomsaidia mwanafunzi kusomeshwa L2 akawa na ufanisi unaostahili. Hivyo, jamii ya Kinyankore inapaswa kujitahidi kuimarisha masomo yanayolenga kusawazisha uelewa wa L2 ya swahili, hasa wanapokuwa nyumbani. Wazazi wanapaswa kuithamini L2 kwa wakiwasiliana na wale wasomaji hata kuwawezesha kuelewa maumbo ya tungo wanaposoma L2 hiyo wakiwa makwao nyumbani.

5.12 Wazazi Kutoheshimu Kiswahili

Utafiti unaonyesha kwamba jamii ya Kinyankore inatoa kipaumbele zaidi kwa L1 ya Kinyankore kuliko kwa Kiswahili. Upeo huu wa jamii ya Kinyankore unawafanya wanafunzi wasioneshe umuhimu unaosabisha usomaji wa L2. Kwa kurejelea mfumo wa kisera unaotawala lugha za kielimu nchini Uganda, Kiswahili kiliteuliwa kama moja wapo inayotakiwa kuwa somo la lazima kwenye mtalaa wa elimu na inastahili kufunzwa kwa asasi zote za elimu kuanzia zile za kimsingi, shule zote za upili, hata

kuna vyuo vikuu. Pia, lugha hii hutahiniwa na baraza linalojishughulisha na kutahini wanafunzi kwa viwango mbali mbali. Hiyo swahili inatambuliwa kwenye kiwango cha kimataifa kwa sababu inatumika katika kanda la Afrika ya mashariki na nchi nyingi za Afrika kwa ujumla. Hivyo, jamii ya Kinyankore inapaswa kuzingatia muhimu wa unaohusiana na kusoma L2 ya Swahili kwani hivi sasa kinafundishwa katika vyuo vingi barani Afrika, Ulaya, Asia, na Marekani. Vituo vingi vya redio pia vinatoa matangazo yao kwa Kiswahili. Swahili yenyewe huwa lugha inayofanyiwa utafiti halafu imeandikwa kwa vitabu vingi na kamusi. Kuna machapisho chungu nzima yaliyochapishwa na yakasambazwa ikiwa ni pamoja na ngano za hadithi fupi, diwani za mashairi, michezo ya kidrama na tamthilia za kuigiza, riwaya za waandishi mashuhuri, vitabu vya sarufi, nakadhalika. Idadi ya watu wenye umilisi wa kusikia na kusema swahili duniani inakadiriwa kuwa imefika miliyoni 200 (Chimerah, 1998).

Kinyume na nafasi hii kuhusu swahili na heshima iliyo nayo kulingana na vile inavyoheshimika, pengine wanajamii wa wanyankore ambao hawajali kuwepo na manufaa Zaidi kama L2 ya swahili na wanaona haifai kupewa umuhimu unaofaa.

Mazingira kama haya ambapo L2 swahili haitathaminiwa na kupewa umuhimu wake yanaweza kukwamisha usomaji wake, kwani wazazi wa wanafunzi wanaposhindwa kuithamini wanaweza kutoweza kuwapa watoto wao motisha kupenda, kufuatia, ktia moyo katika kutumia lugha ianyofunzwa. Jambo hili hupelekea wanafunzi kukosa nafasi za mazoezi yanayokuza L2 kwenye maisha yao, hivyo kuathiri maendeleo yao na kushindwa kuikuza L2 hiyo.

Kutoithamini L2 ya Swahili kunawaletea wanafunzi kutoona manufaa yake na ina maana kwamba Watoto watakosa kuelewa umuhimu, heshima, na sifa yake katika maisha yao kikawaida wakiendelea kukua. Hii inaweza kujidhihirisha katika mambo

kama kukosa mwelekeo wa kupenda L2 halafu wazazi wakasifu au kuhamasisha watoto wao kutumia zile nyinginezo, kama Kiingerezana kuachilia Swahili. Pengine, wanafunzi wanapokosa motisha ya wazazi wanaostahili kuwaelekeza kuwapatia nafasi kuelewa Swahili nyumbani, wanashindwa kuizungumza au kuiandika kwa ufanisi na mwishowe kunaweza kusababisha ukosefu wa uelewa wa tamaduni na mila zinazohusiana na lugha hiyo.

5.13 Mbinu Zisizofaa za Ufundishaji

Sababu nyingine inayosababisha athari za sarufi inayotawala Kinyankore ni mbinu duni za ufundishaji. Hii inatokea ambapo mwalimu hana ujuzi wa kiisimu unaohitaji mikakati ya kufunzia L2. Mwanafunzi anajifunza lugha kwa kusikiliza jinsi mwalimu anavyotoa matamshi, hivyo anaposhuhudia kwamba mwalimu mwenyewe amekosea kimatamshi akizungumza, huwa anafanya makosa kama asipofuatia kanuni za lugha hiyo vizuri. Hii inatokea kufuatia hali ya kwamba mwalimu mwenyewe anazungumza L1 (Kinyankore) na anashawishiwa na L1 yake hiyo kuingilia L2 kimatumizi na kimuundo, na hivyo anapofundisha hutoa makosa ambayo mwanafunzi huchukulia kama sahihi.

Makosa haya yanapoingia, mwanafunzi huhamasishwa kuyatumia kwenye kujifunza kwa kujaribu kuendana na sarufi ili kufanikisha uelewa. Athari hizi hufanyika wakati mwanafunzi anapohamisha desturi zinazojitokeza katika L1 zikaletwa kwenye L2 wakati wa mawasiliano. Haya yanajitokeza katika ngazi mbalimbali, ikiwemo ngazi ya sauti, ambapo sauti alizozoea mwanafunzi katika Kinyankore hazipatikani kwa L2 ya Swahili.

Kwa kurejelea hayo yote, imedhihirishwa kuwa L1 Kinyankore inaathiri pakubwa masomo ya L2 kwa Watoto waisomapo. Wanafunzi wanapata matatizo katika L2 kwani

matamshi ya sauti waliyoyaelewa kwenye L1 hayafanani na yale yanavyotumika kwenye L2. Athari hizi zinasababishwa jinsi matamshi ya sauti zinazopatikana baina yake zote mbili inavyotofautiana. Kutokuwepo kwa ulinganifu wa matamshi na muundo kwenye yale maneno, pamoja na makosa kutoka kwa mfundisha akiwa anafunza, kunachangia matatizo haya.

Utafiti umepata kuwa madhara yanapotokea wakati mwalimu hawezi kufikisha ujumbe aliokusudia, kuna uwezekano wa kutokuelewana anapofundisha Watoto hata kuwapotosha kitaaluma. Hii inaweza kuletwa shida za kitaaluma alizo nazo mwalimu mwenyewe au mwanafunzi. Watoto wanyankore wengi hukabiliwa utata wa kiisimu unaosababisha kutokuwa na umilisi wa lugha zao wa muda mrefu. Kwa hiyo, mwalimu anahitaji kutumia mbinu bora kuwasaidia wanafunzi.

Rocha (2011)[55] anafafanua kwamba watu wengi waliathiriwa kiisimu mwingiliano wa L1 wakiwa wanashughulikia L2 kwani lugha hiyo L1 inajitokeza zaidi katika mawasiliano. Hoja hiyo inalingana na ytafiti wa sasa, ambao umebaini kuwa wanafunzi wengi wameathiriwa na Kinyankore kama L1 inayotangulia, hivyo njia zinazofaa kutumika kufunzia ndizo zitakazowasaidia.

Takwimu za utafiti wa sasa zinaonyesha kuwa matumizi mabaya ya njia za kufunzia, ambapo mwalimu anapewa jukumu pekee la kufundisha halafu mtoto akawa anasubiri kupokea elimu, yanakwamisha Watoto hasa wakashindwa kuelewa L2 kiurahisi.

---

[55] Rocha (2011) katika kitabu chenye kichwa "Error Analysis and Second Language Strategies," kilichohaririwa na J. H. Schumann na N. Stenson, anajadili kwa kina jinsi uchambuzi wa makosa unavyoweza kusaidia katika mchakato wa kujifunza lugha ya pili. Katika kazi hii, Rocha anachunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili, akitoa mwangaza juu ya sababu zinazoweza kusababisha makosa hayo na mbinu zinazoweza kutumika ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha.

5.14 Muhtasari

Tukiangalia takwimu za utafiti mzima zilizokusanyika kupitia mbinu za hojaji, mahojiano, majadiliano, na maktabani ziliwasilishwa na kuchambuliwa. Hapa, uchanganuzi wa takwimu za utafiti unajadili lengo maalum la pili, ambalo lililenga kubaini sababu za athari za kisarufi zinawasumbua Watoto wanyankore katika kujifunza Kiswahili. Data zenyewe zilichambuliwa kwa kuzingatia malengo maalum yanayotawala kanuni za utafiti halafu zikafuata mtazamo wa kimaelezo. Kwenye sehemu hii ya utafiti tumedhihirisha kwamba kuna sababu nyingi zinazoathiri wanafunzi wa Kinyankore wakati wakijifunza L2 ya Swahili. Katika Sura inayofuata, tutachambua lengo la tatu na mbinu zinazoweza kuwasaidia wasomao L2 wakiwa wanaisoma darasani.

SURA YA SITA

MBINU ZA KUFUNZA KISWAHILI KAMA L2

6.0 Utangulizi

Sehemu hii inajadili lengo maalum la tatu katika utafiti wa sasa, lililokusudia kuchunguza mbinu tofauti zinazoweza kutumika kurahisishia namna usomaji wa L2 ya Swahili inavyowezekana hasa ikilenga wasomi wenye asili ya Kinyankore ili waweze kuepuka zile shida zinazowazuia kuielewa L2 kwa sababu ya kuingiliwa na L1.

6.1 Namna ya Kukabili Changamoto Zinazokumba Usomaji wa L2

Washiriki katika utafiti wa sasa waliokuwa wanafunzi pamoja na wataalam waliowafundisha waliulizwa juu ya mbinu zinazofaa kutumika kufundishia wanafunzi wa Kinyankore wanapojifunza Kiswahili, na walitaja mbinu kadhaa kama zinavyoelezwa hapa chini.

6.1.1 Haja ya Kiswahili kufundishwa tangu Utotoni

Data za utafiti zilidhihirisha kwamba kuna manufaa ya kipekee kwa sababu ya kusomeshwa L2 kuanzia utotoni, kwenye umri ambapo unawapa watoto uwezo wa kujenga msamiati mzuri wa L2 pamoja na kuelewa muundo wa lugha na fonolojia sahihi.

Inabainika pia kuwa L1 ambayo mtoto huanza kuizungumza inakuwa na uwezo mkubwa wa kumsaidia mtoto katika uelewa wa lugha nyingine zinazofunzwa baadaye. Kwa kuzingatia msimamo huo, inakuwa kazi ama jukumu la wazazi au walezi kuhimizwa watie bidii za kuondoa dhana potofu kwamba kujifunza Kiswahili kunasababisha kupoteza utamaduni wa kabila lao. Hili likitokea na wanazaa wanafunzi hao wakaungana na kuongeza juhudi, watoto wao wataweza kuwa wazungumzaji wazuri wa Kiswahili.

Jedwali 6.1: Wahusika walipoulizwa kuhusu usomaji wa L2 tangu utotoni

Wahusika	Waliounga mkono	Wengine
Walimu	98%	02%
Wanafunzi	100%	00%

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Kwa kurejelea takwimu za utafiti wa sasa hapo juu, matokeo yanadhihirisha kwamba msingi mzuri wa kufunzia L2 huanzia utotoni, na hii itawasaidia watoto katika mawasiliano katika siku zijazo. Umuhimu wa kufundisha Kiswahili kuanzia utotoni ni mkubwa sana na unaenea katika nyanja mbalimbali za maisha ya mtoto, familia, jamii, na hata uchumi wa nchi. Kufundisha Kiswahili, hasa kwa watoto wanaoishi katika mazingira ya lugha nyingi (mtoto anajifunza lugha mbili au zaidi, mfano Kiswahili na lugha ya mama/Kinyankore/Kiingereza), kuna faida za moja kwa moja kiakili. Watoto wanaojifunza lugha mbili mapema huonyesha uwezo mkubwa wa kubadili fikra zao haraka kati ya kazi mbalimbali na kuwa na umakini bora. Kujifunza lugha tangu utotoni huongeza uwezo wa mtoto kutazama tatizo moja kwa mitazamo tofauti, hivyo huongeza ubunifu na uwezo wa kufikiri katika viwango vya juu zaidi.

Aidha, wazazi au walezi wanapaswa kuhamasishwa kutumia Kiswahili na kuondoa wasiwasi wa kupoteza utamaduni wao. Kwa kuongeza jitihada katika eneo hili, itawawezesha watoto kuwa wazungumzaji bora wenye umilisi kamili wa L2. Walimu walihusishwa kukamilisha utafiti wa sasa, na hatua hizi zitatoa fursa kwa watoto kuwa wajuzi wa Kiswahili.

6.1.2 Haja ya Mijadala ya L2 ipewe Kipaumbele

Kwa kuzingatia utafiti wa sasa, data zilidhihirisha kuwa iwapo wanafunzi watapata fursa ya kufanya mazoezi ya kutosha ili kuwaletea kupata uzoefu wa kuzungumza na kujadili katika L2, halafu watakuwa na uwezo mzuri wa kumudu lugha hiyo.

Mijadala ni mojawapo ya mbinu bora zaidi za kufundishia na kujifunzia lugha yoyote, ikiwemo Kiswahili. Kinachoifanya mijadala kuwa na ufanisi wa hali ya juu ni kwamba inawahamisha wanafunzi kutoka katika hali ya "kupokea" maarifa tu na kuwa katika hali ya "kushiriki" na "kutumia" lugha kikamilifu. Katika mjadala, mwanafunzi anapaswa kutoa mawazo yake kwa haraka na kwa ufasaha mbele ya hadhira. Hili hulazimisha ubongo kufikiria kwa Kiswahili na kuunda sentensi papo hapo, badala ya kutafsiri kutoka lugha nyingine. Pia, mwanafunzi hulazimika kutumia maneno magumu, misemo ya kitaaluma, na msamiati mpana ili kuimarisha hoja zake. Hii hufanya msamiati mpya ujikite akilini. Kwa kupitia mijadala pia, mwalimu anaweza kusahihisha matamshi au sarufi papo hapo, na hivyo kutoa marekebisho ya haraka ambayo huimarisha matumizi sahihi ya lugha.

Jedwali 6.2: Wahusika walipoulizwa Kuhusu nafasi za kuzungumza Kiswahili

Wahusika	**Waliounga mkono**	**Wengine**
Walimu	100%	00%
Wanafunzi	100%	00%

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Utafiti umeonesha umuhimu wa kupatia watoto wanyankore wanastahili kupewa fursa za kuhusika katika mazoezi ya kutosha kutumia L2, hiyo inatokea katika kutunga sentensi, kujifunza msamiati, kuandika insha, kutaja maelezo, hata tungo zenye changamoto. Pia, ni muhimu kufanyika midahalo shuleni kwa L2 ili wanafunzi wapate fursa ya kushindana, ambapo washindi watapaswa kupewa motisha na uzoefu wa kuielewa L2.

6.2 Haja ya Uhamasishaji wa L2

Vilevile, utafiti umebaini kwamba ili mwanafunzi asome L2, anatakiwa sharti kwanza aelewe dhima ya usomaji unaomfanya kuisoma L2 hiyo. Hivyo, Watoto wanyankore

wanaojifunza Kiswahili wanahitaji kueleweshwa uzito wa kusoma lugha hii ili waweze kuipa umuhimu unaostahili. Mjadala si tu kuhusu kuzungumza bali ni kuhusu kusikiliza mpinzani wako. Mwanafunzi anapaswa kusikiliza kwa makini ili kuelewa hoja kamili ya upande wa pili. Kwa kutumia mijadala pia, mwanafunzi husikiliza ili kupata mapengo katika hoja za upande wa pili na kuandaa majibu yenye nguvu. Hii inaboresha stadi za utambuzi wa lugha.

Jedwali 6.3: Wahusika walipoulizwa sababu za kujifunza Kiswahili

Wahusika	Walio na umilisi	Wengine
Walimu	58%	42%
Wanafunzi	75%	25%

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 33.5 ya watu wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu hawajui umuhimu unaosababisha kusoma L2 maishani mwao, hata wengi wanaikadiria kama lugha isiyo na manufaa zaidi nje ya maeneo ya shuleni.

Mtafiti aligundua wanafunzi wachache wenye uelewa kwamba Kiswahili kinaweza kuwasaidia kutekeleza haja za kimawasiliano kwa wanajamii wengine. Ikumbukwe kwamba Kiswahili kinatumika sana katika mikutadha na mazingira mbalimbali nchini, licha ya kuwa na hadhi iliyo rasmi katika nchi nyingi, hasa za Upande wa mashariki wa Afrika (EAC) na ilitarajiwa kuwa wanafunzi wanapojifunza Kiswahili wanaelimishwa pia kuhusu umuhimu wake katika mawasiliano mapana.

Tukirejelea mtazamo huo, inakuwa bora kwa jamii, koo, na wazazi kuelimishwa kuhusu manufaa yanayolazimisha watu kujifunza na wakatumia L2 ya swahili katika ngazi mbalimbali kama ni mtu binafsi, kama ni ukoo, iwe jamii, taifa, na kimataifa. Wanafunzi wahamasishwe na wapate kujua pia umuhimu wake L2 kwenye ngazi za kitaifa na kimataifa. Wanafunzi wanapaswa kuhimiza ujenzi wa mikakati ya

kuzungumza Kiswahili wanafunzi wakiwa shuleni, nyumbani, na maeneo mbalimbali. Kuwapa vijitabu vyenye ngano na hadithi zinazoweza kuwafunzo na kuwapatia mawaidha wakiwa nje ya shule kutasaidia kuongeza uelewa na uwezo wao wa kusema L2 iliyo Swahili.

Ferdinard de Saussure (1916) anasema kwamba utendaji unaohusisha L2 ni ule unaoitumia ukifanywa na mtu mmoja akiwa peke yake. Haya ni matendo ya kibinafsi ambapo mtu anajitahidi kuzingatia mikakati ya L2 kwa ajili ya kuzungumza kwa usahihi. Hivyo, iwapo jamii itaongozwa kutumia Kiswahili kwa wakati wowote, kila mwanajamii ataweza kuzungumza L2 kiufanisi na kwa haraka.

6.3 Haja ya Ajira ya wanaofundisha L2

Takwimu za utafiti zilionyesha kwamba mwanafunzi anahitaji walimu wengi wenye sifa zinazofaa ili afanye vizuri katika masomo yake. Hata hivyo, sio kila mwalimu ana ujuzi unaofaa kuweza kuwafunza Watoto wanyankore L2. Kufuatia sababu hiyo, inakuwa bora kuchukua hatua za kuajiri walimu wengi Zaidi wenye weledi wa kutosha katika kufundisha Kiswahili shuleni na vyuoni ili kuhakikisha shule zinapata wataalam wanaofaa wenye uzoefu na tajriba vya kutosha.

Jedwali 6.4: Walipoulizwa kuhusu Kuajiri Walimu wengi wa Kiswahili

Waliounga mkono	**Waliopinga**
78%	22%

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Tukizingatia takwimu za utafiti wa sasa, tunagundua ya kwamba wanaofunza L2 wana uwezo wa kushawishi wanafunzi kujiunga na somo la L2. Jambo hili lilidhihirishwa na walimu wenye uelewa wa kuboresha ufunzaji wa L2 kwa wanafunzi waliopata hamu ya kuendelea nayo kitaaluma na kijamii. Walimu wakiwa wengi wanaboresha na kurahisisha ufahamishaji wa taaluma. Kuwa na walimu wengi wenye ujuzi na taaluma

tofauti kutatoa muktadha mpana na kiundani katika ufundishaji, ambao unaweza kusaidia wanafunzi kuelewa lugha hiyo kiurahisi na kwa haraka. Wataalam wa L2 wanapokuwa wengi wanaweza kusaidia katika kukuza na kuhifadhi desturi na historia zinazohusiana na hiyo L2, na kuwafundisha wanafunzi umuhimu wake wakiwa na wanajamii wengine. Kuajiri walimu wengi kutasaidia wanafunzi kuboresha jinsi wanavyotumia umilisi wao kuwasiliana na wenzao kwa Kiswahili, kwani wataweza kupata mazungumzo zaidi na mazoezi yanayohusiana na lugha hiyo. Wanafunzi wataweza kuhamasika zaidi katika kufanya utafiti na kutoa michango mbalimbali inayohusisha kanuni za sarufi na mtindo wa L2, hata mazingira bora ya kujifunza yanayowezeshwa na walimu wengi. Kuajiri walimu zaidi kutasaidia katika kuratibu programu za masomo ya L2 kwa viwango mbalimbali, kuimarisha elimu inayolenga kukuza L2 kuanzia asasi za elimu zilizo chini hadi vyuo vikuu.

Kwa hivyo, takwimu za utafiti zilidhihirisha kuwa kuajiri walimu wengi wanaojua L2 ifaavyo huwa jambo la maana sana ili kuboresha elimu ya lugha hii, kuhifadhi urithi wa tamaduni, na kukuza mawasiliano bora baina ya wazungumzaji walio na lugha mbalimbali.

6.3.1 Mchango wa tamaduni za Kinyankore

Kwa kurejelea data za utafiti, Mchango wa mila desturi za Kinyankore ulijitokeza kuwa moja wapo ya sabau zinazoathiri namna ya kufunza L2 kwani tamaduni zinazobebwa na wanyankore zinasisitiza kutumia L1 iliyo Kinyankore kuliko kutumia L2 isiyo ya asili yao. Mawasiliano ya nyumbani yanajikita kwenye lugha ya Kinyankore, na takwimu za utafiti wa sasa unadhihirisha kuwa wanafunzi wengi wanaporudi nyumbani kutoka shule hutumia Kinyankore kuwasiliana. Mazungumzo ndani ya familia na ukoo yanathaminiwa kwa kutumia lugha ya Kinyankore, kwani inachukuliwa kuwa ni

tamaduni bora, na mtu ambaye anajitahidi kwa uaminifu kujionyesha akiheshimu tamaduni zake.

Watu ambao hawaongei Kinyankore hujulikana kama **“wakoko”**, neno lenye maana ya “Wanyama” au wasio binadamu, watu wasio wa kabila la Kinyankore. Wanyankore wanapenda kutumia lugha yao, na jambo hili linasababisha sana kuwajenga watoto wao katika utamaduni wa kuzungumza lugha yao mama. Hali hii inawanyima watoto muda wa kutosha kujifunza au kuzungumza Kiswahili wakiwa peke yao na kwenye mikutadha ambayo ingewasaidia kukuza L2.

Jedwali 6.5: Wahusika kuhusu L2 kupewa kipaumbele

Wahusika	**Waliounga mkono**	**Wengine**
Walimu	100%	00%
Wanafunzi	100%	00%

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Kulingana na Dixon (1992), anasema kwamba ushirikiano uanojitokeza katika L1 na L2 unategemea jamii husika, wazazi, watoto, na jamaa katika ukoo. Lugha huweza kuendelea, kuharibika, au kuathiriwa kwani L2 inatumika katika jamii hiyo. Ili wasemaji wa Kinyankore waweze kuchukua muda kusoma L2 kiurahisi, ni muhimu kubadilisha hizo tamaduni za wanyankore kuwalazimisha kutumia Kinyankore ili kuwawezesha Watoto kupata nafasi ya kujizoeza na L2 iliyo Swahili kiufanisi. Pia, mila ya kuwabagua na kuwaita wale wasiozungumza Kinyankore “Wakoko” inahitaji kubadilishwa.

Mila na desturi za Kinyankore zinaweza kuunganishwa na kutumika kuwezesha mafunzo ya L2 kusaidia wanafunzi kuelewa jinsi kuingiliana kwa mifumo miwili ya kanuni za sarufi zinavyohusiana, na kuwapa mtazamo mpana wa tamaduni zinazohusiana na mawasiliano yanayojitokeza. Wakati wa kusomesha L2, milango ya

desturi za Kinyankore inaweza kutumika kama mifano halisi inayohusu kuzungumza katika L2 ili kusaidia watoto kuielewa wakati huo, hivyo kufanya ujifunzaji uwe wa karibu zaidi na wa vitendo. Wanafunzi wanaweza kujifunza maneno, misemo, na nahau za Kiswahili zinazofanana zikilinganishwa na L1 ya wanafunzi iliyo Kinyankore, ambayo inawasaidia kukumbuka na kuelewa vizuri lugha wanayojifunza. Wakati wanafunzi wanapojifunza Kiswahili huku wakitumia desturi za Kinyankore, wanapata ujasiri wa kuzungumza L2 hasa uzoefu wa umilisi ufaao, kwani wanajua wanaweza kutumia vigezo vyao vya tamaduni zao kufanya mazungumzo ya maana. Wanafunzi wanapojifunza kuhusu mila na desturi za Kinyankore, wanajifunza pia kuhusu njia za kiutamaduni zinazosaidia kwenye mawasiliano ya kuelewa hisia na fikra kwa wanajamii wanaotumia Kiswahili, hivyo kuimarisha uwezo wao wa kuelewa L2 husika. Kushiriki katika matukio ya kijamii ya Kinyankore, kama vile harusi, sherehe au sherehe za jadi, kunaweza kuwa fursa nzuri kwa wanafunzi kutumia Kiswahili katika mazingira halisi, hivyo kuwezesha mafunzo yao kupata maelezo yanayolengwa. Kwa kuzingatia mafunzo ya L2 inayozungumziwa, kujumuisha tamaduni zinazosisitizwa na wanyankore kunaweza kusaidia kuunda mazingira mazuri ya kujifunza, ambapo mwanafunzi anaweza kupata mtazamo wa mambo yanayohusiana na uhusiano uliopo kati ya mitazamo ya kidesturi ikiangaliwa kwa upande wa lugha yenyewe. Kwa hivyo, mitazamo ya kitamaduni inayosisitiza matumizi ya L1 inaweza kuwa rasilimali kubwa kuimarisha mafunzo ya L2 kwani inatoa muunganiko wa kiutamaduni na kisaikolojia ambao unachochea hamasa na uelewa unaosabaisha kufahamu L2 inayofunzwa.

6.4 Haja ya Umahiri wa Walimu

Kwa kuzingatia takwimu za utafiti wa sasa, mtafiti alibaini kwamba walimu wanastahili kumiliki uelewa unaofaa kudhihirisha umilisi wa somo wanalolifundisha hasa ikiwa L2 kwa wasomaji. Hatua hiyo ingewawezesha kupata nafasi kutumia tajriba yao wakitaka

kuwasaidia wanafunzi wa jamii ya Kinyankore kufanikiwa katika usomaji wa L2 ya Swahili. Hii itachangia pakubwa katika kufundisha L2 na kuwezesha wanaoisoma kufanikiwa kuielewa vilivyo.

Utafiti umeonyesha kuwa kuna walimu, hasa wanaofundisha madarasa ya msingi (kama kuanzia darasa linalotangulia kwenda lile la tatu), mara nyingi wanakosa elimu ya kutosha katika kufundisha Kiswahili. Sababu hiyo inaletea wanaofundisha, hasahasa wale wanaojua Kinyankore kuwasiliana wakitumia mchanganyiko wa L2 na L1 ili kukamilisha mafunzo kuelewesha wanafunzi ipasavyo. Jambo hili likifanyika kwa muda mrefu, linawaletea wanafunzi kupata uhuru wa kutumia Kinyankore hata wakiwa shuleni. Mtafiti aliwaona wanafunzi wakizungumza kwa Kinyankore kati yao darasani, na alipouliza mwalimu kuhusu hali hiyo, alijibiwa kwamba wanafunzi walipohojiwa, mmoja wa wasomao aliyekuwa katika darasa la sita alieleza kwa nini walikuwa wakizungumza Kinyankore wakati wakiwa darasani, na akasema;

> *Hakuna kitu ninapata nacho shida nikisikia wanafunzi wanaongea kilugha darasani. Kwa hapa Mbarara sijui ni kwa vile tuko kijijini, wanafunzi wao huona kawaida tu kuzungumza L1 darasani, kuna kipindi wanajisahau wanaongea hata mbele ya mwalimu.*

Mmoja wa wanafunzi wahojiwa aliulizwa kwa nini anatumia kinyankore wakati somo la Swahili likiwa linaendelea, halafu alijibu;

> *Kwa kweli mimi huwa naongea lugha ya Kinyankore kila siku hata nikiwa shule. Ni mara chache sana naongea Kiswahili nikiwa na wenzangu. Huku kwetu, ukimsemesha mnyankore mwenzako L2 ya Swahili, utaonekana wewe ni mswahili na wenzako wataanza kukutenga. Haya mazoea ndiyo hunipelekea mimi na wengine kujikuta tunaongea Kinyankore hata tukiwa darasani.*

Jedwali 6.6: Wahusika kuhusu Walimu wenye umahiri unaohitajika kufunza L2

Wahusika	Waliounga mkono	Wengine
Walimu	100%	00%
Wanafunzi	100%	00%

Chanzo: Data za Uwanjani (2023)

Tukiangalia wataalam wanaoajiriwa kufundisha L2, wao wenyewe wanatarajiwa kumiliki umahiri wa lugha wa hali ya juu ili waweze kuwajibika kufunza Watoto kwa uzoefu ufaao. Pia walimu wanaofundisha L2 wanapaswa kujitolea kuwasaidia Watoto wasomao L2 kujifunza Kiswahili kufuatia umilisi unaostahili uelewa wake. Kwa hivyo, mtafiti alisisitiza kwamba wanafunzi waweze kufundishwa matamshi sahihi katika L2 iliyo swahili darasani ili kupunguza athari zinazotokana na L1. Vilevile, miongoni mwa walimu wanakosa ujuzi unaofaa katika lugha hii, halafu upande unaofuata baadhi yao wanatumia mbinu zisizofaa, kama vile ujumlishaji wa kiholela na matumizi mabovu ya mikakati ya L2 hiyo.

6.5 Haja ya Mazingira Yafaayo ya Kufundishia Kiswahili

Mazingira yanajumuisha mambo yote yanayowazunguka wanajamii. Kila msemaji wa lugha anakuwa katika mazingira yanayomhusisha katika ulimwengu anamoishi. Hili linajitokeza katika mifano ya wale Watoto wanaozungukwa na watu wasiozungumza Kiswahili wanaweza kugundua kwamba ni vigumu sana kuzungumza Kiswahili sanifu. Walimu wengi wanakubaliana kwamba mazingira haya yanaathiri wanafunzi wa Kinyankore wakiwa wanasoma L2 ya Swahili.

Jedwali 6.7: Wahusika walipoulizwa juu ya mkutadha wa mafunzo ya L2

Wahusika	Waliounga mkono	wengine
Walimu	98%	02%
Wanafunzi	100%	00%

Chanzo: Data za uwanjani (2023).

Kutokana na jedwali hapo juu, Mazingira yanayofaa ya kufundishia yanajumuisha nyumbani, shule, njiani, na sehemu nyinginezo ambapo mtu anapoweza kupata mafunzo ya namna yoyote. Kwa mfano, mwanafunzi aliyezoea kuishi katika mandhari ya watu wanaojua kusema L1 kwa ufasaha, huenda wasipate athari yoyote katika

mawasiliano yao. Aidha, hata ingawa atahamia sehemu ambapo watu hawazungumzi lugha hiyo, ataweza kukutana na changamoto za kimawasiliano hadi atakapozoea mazingira mapya.

Utafiti pia uligundua kwamba taathira zilizosababishwa kutumia sana L1 iliyo Kinyankore katika kujifunza L2 ya Swahili zilienezwa kutokuwepo mazingira yanayofaa ili kufunzia L2 kwa haraka na kiurahisi. Wahojiwa wengi wanazungumza Kiswahili wakati wanapokuwa darasani pekee, lakini nje ya shule, kama nyumbani, sokoni, na kwenye sehemu za ibada, wanapendelea kutumia Kinyankore. Hali hii imesababisha wanafunzi wengi kujiweka kwenye sehemu inayokuwa ya wabobezi katika Kinyankore kuliko Kiswahili.

Lugha ya Kinyankore inatoa athari kubwa kwa wanafunzi wanapojaribu kuwasiliana kwa Kiswahili. Hivyo, inakuwa dhahiri kuwa mazingira na jamii ni mojawapo ya sababu zinazochangia athari kuwaingilia watoto wanyankore kuwazuia kufahamu masomo ya L2. Aidha, jamii ya Wanyankore haitahimiza watoto wao kuzungumza Kiswahili kila muda waupatao kutokana na muktadha waliomo.

6.6 Uhamasishaji wa Wazazi na Watoto kuhusu L2

Kwa kurejelea takwimu za utafiti wa sasa, tunatambua kwamba takwimu zinaonyesha kwamba zaidi ya 90% ya wanafunzi wanaoshindwa kufahamu somo la L2 kiurahisi huwa ni hao wanaoisoma ikiwa L2 kwao. Utafiti umeonyesha kwamba lugha anayojifunza mtoto tangu utoto ina ushawishi mkubwa katika maeneo yote ya lugha, ikiwa inahusu maana, matamshi, maumbo, halafu miundo.

Walezi wote mkiwemo hata waliowazaa watoto wanahitaji kuhamasishwa ili watumie L2 ya Swahili kutekeleza haja za kuwasiliana ili waweze kuondoa imani potofu kwamba kujifunza Kiswahili kutasababisha watoto wao kupoteza utamaduni wa kabila

lao au jamii yao. Iwapo wazazi na walezi watafanya jukumu hilo wakishirikiana, watoto wao wataweza kuwa wazungumzaji wazuri wa Kiswahili. Jitihada zaidi zinapaswa kufanywa ili kufanikisha hili. Takriban asilimia 87 ya washiriki walitaja kuwa kutumia L2 kunapunguza athari za Kinyankore kwa Watoto wakiwa wanaendelea na mafunzo ya L2. Mwishowe, inabidi ieleweke kwamba utafiti wa sasa unasisitiza kwamba msingi mzuri wa ustadi katika lugha huanzia utotoni na kwamba lugha inapaswa kufundishwa mapema ili kusaidia katika mawasiliano ya baadaye.

Aidha, wazazi au walezi wanapaswa kuhamasishwa kuzoea namna ya kuzungumza L2 wakitekeleza haja za kuwasilisha ujumbe kwa watoto wao, na waondoe dhana potofu kwamba uelewa wa L2 ni chanzo cha kupoteza tamaduni zao. Hii itawasaidia watoto kuwa wazungumzaji bora wa Kiswahili.

6.7 Muhtasari wa Sura

Sehemu hii inayowasilisha sura ya sita, tumejikita kuchambua na kuelezea shabaha ya tatu ya utafiti, ambalo linazingatia mbinu za kuwasaidia wanafunzi wanapojifunza L2 ya Swahili. Data zilizokusanywa kupitia namna tofauti hasa hojaji, mahojiano, majadiliano, na maktaba zinaelezwa na kuchambuliwa. Kulingana na sehemu iliyoshughulikiwa, Utafiti huu umebaini mbinu tofauti ambazo zinaweza kutumika kusaidia wanafunzi wanaojifunza Kiswahili.

Sura hii imezingatia mikakati mbalimbali ya kusaidia wasomaji wanyankore wanaoshiriki mafunzo ya L2 ili kujiepusha na taathira za kisarufi wanapojifunza L2. Katika sura inayofuata, tunajadili vipengele muhimu vya utafiti huu vya hitimisho, mapendekezo na muhtasari wa utafiti mzima.

SURA YA SABA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi

Sura hii ya mwisho imetoa muhtasari wa utafiti. Aidha, imetoa takwimu na mjadala wa kutosha kwa ufupi kisha mahitimisho ya utafiti. Mapendekezo ya utafiti yametolewa pia kuelekeza kile kinachostahili kufanywa kwa kurejelea malengo na data za utafiti.

7.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti wa sasa ulizingatia kusudi la kuangazia kuathiriana kwa Kinyankore na Kiswahili. Utafiti ulishughulikia kutathmini jinsi kuingiliwa na L1 kwenye usomaji wa L2 kunavyoweza kusababisha taathira kati ya Kinyankore na Kiswahili, ili kuchambua uhusiano wa kisarufi. Kiini cha utafiti huu kilikuwa kubaini tatizo la matumizi mwafaka yanayopatikana katika masomo ya sarufi kwa watoto wanaosoma L2. Ikumbukwe kuwa utafiti wa sasa ulifanyiwa jijini Mbarara. Kuathiriana kwa lugha kulichunguzwa kwa kuzingatia mfumo wa kufundisha katika asasi za elimu kama shule kwenye kiwango cha sekondari na vyuo vikuu. Changamoto kuu ya matumizi sahihi kujifunza kanuni zinazotawala mifumo ya sarufi ya lugha hiyo ndiyo ilikuwa msingi unaohitajika kwa L2, ambapo utafiti ulifanyika katika Jiji la Mbarara. Utafiti huo ulilenga kuchunguza kama kuna kuathiriana kisarufi kati ya Kinyankore na Kiswahili, huku kutoa maelezo ya kiisimu kuhusu athari hizo. Nadharia kuu iliyotumika ilikuwa kwamba Swahili na Kinyankore ni mifumo miwili ya lugha inayoshirikiana katika maumbo yanayojengwa kutunga tungo za nje. Tafiti nyingi zimefanywa lakini hakuna utafiti wowote ambao umeshughulikia kuathiriana kwa sarufi za L1 ikiwa Kinyankore kwenye usomaji wa L2 ikiwa Swahili.

Yaliyoangaliwa katika sura iliyotangulia mwanzoni iliweka msingi wa utafiti kuangazia mambo yanayobainisha nadharia zilizosawiriwa na kuwasilishwa. Masuala

yaliyowasilishwa ni ya utangulizi na habari kuhusu usuli ambako utafiti unaegemea, tatizo la utafiti, halafu msingi wa nadharia, upeo na mipaka iliyozingatiwa katika utafiti, mantiki na sababu za utafiti pia zimefafanuliwa.

Sura ya pili imewasilisha mapitio ya maandishi kuhusu vile lugha hizi lugha mbili zinavyoathiriana. Mapitio haya yamegawanywa katika makundi matatu: jopo la mapitio ya jumla kuhusu kuathiriana kwa lugha, jopo linalotusheheni masuala ya kitaaluma kupitia tafiti, na jopo linalohusisha njia zinazofaa kufunzia L2 kwa Watoto wenye asili ya Kinyankore. Kila jopo lilionyesha kuwa kuathiriana kwa lugha kunaendelea, ila kunaanzia kwenye mwingiliano wa lugha mbili au zaidi katika mazingira yanayotumika kwa mawasiliano. L2 ikiwa ya swahili, inaathiriwa na kutoa athari kwa lugha nyingine, lakini utafiti wa kuathiriana huku hakujafanywa kwa ukamilifu.

Mapitio yote yalibainisha kwamba tangu zamani sana jambo la lugha zinazotagusana kuingiliana na taathira zinazojikeza limepamba moto nyakati hizi. Chanzo chake kimekuwa ni maingiliano ya lugha zinazotumika kwa wakati mmoja, hasa zinapokutana katika mazingira ambapo zinatumika mfululizo ili kufanikisha haja za kimawasiliano. Upekuzi wa mapitio yaliyoandikwa awali ulitubainishia kwamba lugha zote zinazotumika katika jamii-lugha ya Uganda zinaweza kufanyiwa utafiti tukirejelea njia zilizotumika katika utafiti wa sasa, ukijikita katika viwango mbali mbali vya lugha. Taathira zinazotokana na L1 kwa L2 hujikita kwenye sehemu za lugha husika zote zinazoingiliana kwa njia mbalimbali. Isitoshe, hali ambapo lugha inakuja kuathiriwa na myingine inajitokeza kwenye ngazi za utumiaji wa lugha unaotofautiana kimkutadha. Mfano mzuri ni zile taathira zinazoathiri L2 iliyo maarufu kama Swahili, zitajitokeza kinagaubaga kutagusana na lugha ambayo haijakuwa na umarufu, kama Kinyankore, kufuatia mfumo wa kanuni za kisarufi. Hii inasababishwa lugha imepanuka kimsamiati kuletwa vile wanavyotumia L2 katika sekta na miktadha mbali mbali. Hali kadhalika,

lugha mfano wa L1 ya Kinyankore inaathiri L2 ya Swahili kwa kiwango kikubwa katika miundo inayotawala kanuni zinazohitajika kuelewa sarufi, ikiwemo: fonolojia, mofolojia, semantiki pamoja na kimuundo. Ni wazi kuwa tukiwa tunashughulikia maumbo yanayosababisha taathira kutoka lugha kwenda kwa nyingine, mtafiti hawezi kujifunga katika kipengele kimoja cha lugha bali hujifunga kwa vipengele vingine. Hili linaletea taathira zinazopatikana kwenye kiwango kimoja cha lugha kinachoweza kuletea taathira katika viwango vingine. Nadharia tatu zilitumika katika utafiti huu; hizi zilihusisha mifumo ya kinadharia inayochanganua kasoro za maumbo, halafu ile mifumo inayochanganua na kulinganua maneno na hata Nadharia Kidhi ya Mawasiliano.

Katika sehemu iliyofuata kwenye sura iliyokuwa ya tatu, utafiti ulijadili mbinu zilizotumika kukusanyia data na kuonyesha mahali ambapo utafiti ulifanyiwa katika jiji la Mbarara ukitumia mipango mikakati mbalimbali za ukusanyaji data, kama vile hojaji, dodoso, na mazungumzo. Mbinu hizi zilionyesha uwezo wa kuzalisha data ya kisemantiki, kimuundo, kifonolojia, na kimofolojia. Hata hivyo, mbinu hizi zilifanikiwa kuwaruhusu washiriki, hasa wanafunzi, kujieleza kutoa habari za kutoa kuelezea masuala tofauti. Hii iliwezesha mkusanyiko mkubwa wa data ikilinganishwa na mbinu nyingine zisizo na ubunifu. Sehemu ya sura hiyo pia ilijadili mbinu za kuchanganua takwimu za matokeo zilizotambuliwa na kufafanuliwa kwa kina.

Sura iliyofuata ilikuwa ya nne, uchanganuzi wa matokeo ulifanyika. Matokeo haya yalionyesha kuwa maingiliano ya lugha yanafanyika pale tunapoona mtagusano wa L1 na L2 ukitokea mfululizo katika mawasiliano. Kinyankore na Kiswahili zimeathiriana katika umbo la ndani na la nje, ambapo L1 ya Kinyankore imechangia pakubwa kuathiri L2 iliyo Kiswahili na kuletea mabadiliko ya miundo ya kujenga tungo kimakosa. Aidha, athari za Kiswahili kuelekea Kinyankore zinadhihirika kwenye ngazi ya kileksika, hasa

kwa maneno ya mkopo. Kinyankore pia kimeathiri Kiswahili katika maana za mofu na katika mifumo inayotawala sarufi ya L2 kisintaksia na kisemantiki.

7.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti wa sasa uligundua kwamba L1 iliyo Kinyankore imeathiri mafunzo ya L2 iliyo swahili katika viwango vyote va sarufi. Jambo linguini ni kwamba kumebainishwa mambo mbalimbali yaliyoonekana kuwa sababu za kuathiriana kwa L1 na L2. Kwanza ni kukopa kwa maneno, ambako unaweza kusababishwa kuwepo kwa kutagusana kwa mifumo inayofananisha muktadha wa kimawasiliano. Pia, mielekeo ya wazungumzaji huenda ikasababisha ukopaji. Kiujumla, kukopa husababisha lugha inayopokea kuingiza sifa za mfumo wa lugha iliyo tofauti inayokopeshwa kubadilisha ngazi ya sauti, muundo, na tungo. Lugha yoyote inayoathirika ina njia yake ya kushughulikia athari hizo ili ziweze kuendana na mfumo wake.

Utafiti huu ulibaini kuwa, mifumo yote ya kisarufi, Kinyankore kinachangia maneno yaliyo ya mkopo, baadhi yao yakitumiwa bila mabadiliko, wakati mwingine, kama ya nomino, yanapata ngeli mbalimbali. Kulingana na utafiti wa sasa, vifungu vya maneno huhusika, vna huweza kukatizwa ili kuunda neno moja bila kupoteza maana; na pale ambapo neno linakosa kisawe, linaweza kutafsirika. Miongoni mwa mofu zilizo za kigeni zinaweza kuhusishwa na mizizi ya leksia na hivyo kusababisha sifa za mfumo wa sarufi kupotea.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa maneno kutoka Kinyankore yanayoathiri Kiswahili yamepokelewa bila kubadilika. Utafiti ulitambua kuwa Kinyankore kinapoathiri uzalishaji wa Kiswahili, mifumo ya kimofolojia kama vile uambishaji, ukatizaji, na uunganishaji huibuka. Mifumo hii iliweza kueleweka ikifuatia vipengele vya kiisimu na inasaidia kuwasilisha athari za mkopo.

Lugha ya Kinyankore imekuwa na athari kubwa ikiingilia watoto wakisoma L2 ya Swahili na kuwaletea kufanya kasoro za kilugha, hasa kwenye viwango vya fonolojia, mofolojia, semantiki, na kimuundo. Kwa mfano, Kinyankore kimeathiri miundo ya kisarufi ya Kiswahili, kusaidia katika uwasilishaji na kupanua dhana za msamiati wa mkopo, na kubadilisha mizizi ya maneno mkopo kutoka kiwango kimoja cha kisarufi hadi kingine. Kinyankore kimeathiri misingi inayotumika kwa kategoria ya kitenzi cha L2 halafu kuunda maneno ya nomino kutokana na mizizi hiyo. Hali hii inaonyesha kwamba athari za msamiati wa Kiswahili kupitia Kinyankore zinapanua muundo unaofuatia maumbo ya L2 hadi kuongeza zaidi athari za Kinyankore.

Jambo lingine lililogunduliwa ni kwamba mbinu za uundaji wa maneno huwa na dhima inayosababisha maingiliano ya lugha. Msamiati ukishakopwa na kuwekwa kwenye lugha inayopokea inabadilisha muundo wa kimofolojia kama vile utohozi, uambishaji, hata ufupishaji zinaweza kusaidia lugha ya kupokea kuwasilisha maneno ya mkopo, kupanua dhana, na kubadilisha maumbo yanayoweza kugeuka kutoka kundi moja la sarufi kwenda kundi lingine.

Pia, ilibainika kwamba watoto hao walio na asili ya Kinyankore wanakumbana na shida zinazodhihirika wakiwa wanasoma L2 ya swahili, ikiwemo matatizo ya kitahajia, kisarufi, kuchanganya ndimi, na kutafsiri dhana na istilahi zikiwa kwa L2 za kimsingi zikilinganishwa na zile za Kinyankore. Utafiti ulionyesha kuwa shida hizi zinachimbuka kwenye tofauti katika mtindo wa kimatamshi, kimofolojia, kimuundo, na kisemantiki kwenye lugha husika zote zikitagusana. Hata hivyo, matatizo haya hayana muunganisho unaofululiza kuathiriana kwa L2 kutoka kwa L1 ya Kinyankore; baadhi ya matatizo yanatokana na ukosefu wa ustadi unaojitokeza kwenye L2 hiyo. Kuathiriana kwa lugha unakubalika kuwa halisi duniani nzima bila shaka na hakuna lugha isiyokuwa na athari kutoka kwa nyingine. Athari hizi zinaweza kutokea kutokana

na ukosefu wa muundo fulani ikihusisha L2 inayopokea, ambayo husababisha "pengo" linalohitaji kufungwa, hasa pale tunapokuwa na L1 inayokuwa na utamaduni wenye nguvu na vitu ambavyo havipo katika L2 nyingine.

Vilevile, vipengele vingine vya lugha huweza kuingia katika lugha inayopokea, sio kusema kuwa L2 hiyo haina vipengele hivyo, bali ikijitokeza kukamilisha yale mambo yanayohusu kijamii yasiyo na uhusiano na masuala ya kiisimu. Kwa mfano, ukiangalia hadhi inayoonyesha desturi za lugha asilia, tofauti za kiuchumi, kisiasa, na kijamii zinaweza kuathiri sana lugha inayopokea. Kwa mfano, kufunza L2 kumepata athari kubwa kutoka Kinyankore, hasa katika msamiati, kutokana na juhudi za Wanyankore kujifunza Kiswahili, ambayo imeenea kukuza ngazi za kielimu, jeshi, muziki, na siasa za maendeleo ya bala la Afrika nzima.

Hivyo, Kiswahili kinakuwa rahisi kufundisha, na ndiyo sababu Kinyankore hakikuzuia L2 katika kiwango cha msamiati. Kiswahili pia kimeweza kuimarika sana, kikiwa njia ya limawasiliano ya kitaifa, somo la lazima shuleni hata vyuoni na vyuo vikuu, lugha ya usambazaji wa habari, licha ya kuanzia asasi na vituo vinavyokuza matumizi yake. Mambo haya pamoja na umoja wa kitaifa yameweza kusababisha wanafunzi na wadau wote wazima wengi kupendelea kuhimizwa kuongeza uelewa wao wa L2 ya Swahili.

Aidha, wanaotumia L2 huweza kujiona huru kutumia vigezo vya lugha kwani yale anayozungumza yanaeleweka kwa wasikilizaji (ujozi-lugha) (Mochiwa, 1979). Lugha kuathiri nyingine kunatokea pale ambapo jamii zenye lugha mbalimbali zinapokutana. Sababu mbalimbali zinaweza kusababisha hali hii, kama vile shughuli za vita, siasa, biashara, dini, uongozi, ujirani, michezo na kadhalika.

Aidha, lugha kuathiriana huenda kukatokana wakipata uwezo wa kutumia L2 iliyo na changamoto fulani. Athari hizi zinaweza kuonyesha mabadiliko ambayo hayana

uhusiano wa mfululizo kueleza maumbo kiisimu na mifumo ya kifonolojia, hasa inapokuwa L2 haina ulinganifu. Kwa lugha kuathiriana si jambo rahisi kufahamika katika mkondo wake. Jambo hili linadhihirisha kwamba lugha zinazofanyiwa utafiti huweza kuwa zimeathirika moja kwa moja kutoka L1, au moja ikaathiriwa na nyingine katika msamiati uliokopwa.

Kwa kurejelea hayo yaliyojadiliwa hapo juu, swala linaloshughulikia kuchunguza mwathiriano wa lugha hizi linafaakuangaliwa kisinkronia, kwani, kuelewa vile lugha zinavyoingiliana kwa nyakati tofauti maalum za kihistoria na kupuuza matukio ya kihistoria. Maelezo yanayohusu etimolojia yanapaswa kujikita kwenye ushirikiano wenye historia ya jinsi lugha zinavyoathiriana.

Katika shughuli za masomo yanayohusu athari za lugha, ni muhimu kutambua kuwa suala hili ni pana, na ni ngumu kulitekeleza katika utafiti mmoja ndani ya kipindi kifupi. Utafiti unaokuwa na mwenendo kama huu unastahili wakati mrefu ili kufanikisha matokeo mazuri. Ingawa L1 ya Kinyankore imeonekana kuwa iliathiri L2 iliyo Swahili kwenye ngazi ya majina na kileksika, kwenye kiwango cha mumbo, fonolojia na kimuundo, utafiti huu haukutambua athari kubwa zinazoathiri mafunzo ya L2 ikiwa Swahili. Aidha, Kinyankore kimeathiri vitenzi vya Kiswahili vikijitokeza vikiathiri maneno binafsi kama leksika. Kinyume na hayo, Kinyankore kimeathiri makundi haya ya maneno yakibadilisha matumizi ya maumbo hayo katika L2. Sarufi za Kinyankore na Kiswahili zinategemea mtindo wa uambishaji wa kimofolojia ili kukamilishwa. Hivyo, nomino za mkopo huwasilishwa katika uundaji wa mfumo wa sentesi kwa kuambisha maumbo yanayotangulia kwenye ngeli kukamilisha usanifishaji wake.

Athari nyingine za kifonolojia zinaweza kuonekana kwenye kiwango cha tungo, kwa sababu usanifu wa maneno ya nomino yanategemea uhusiano wa kisarufi unaotokana

na viambishi vya nomino. Mfano ni kama vile athari za matumizi yasiyofaa ya {mu} kama kiambishi awali katika maneno ya vivumishi, kama 'mzuri' katika ngeli ya Ki – Vi, zinaweza kubainika kwa kusaidiwa uchanganuzi kwenye sentensi zinazovumisha nomino hizo. Katika ngazi ya kimatamshi, kuna uwezekano wa lafudhi ya msemaji kuleta athari. Lafudhi ni jinsi msemaji anavyotamka maumbo kwenye L2 husika (Kihore 2001). Kwa kawaida, jinsi watu wanavyoshiriki mazungumzo ndiyo inavyoakisi jinsi wanavyoandika. Matamshi yao mara nyingi yanaonyesha kwamba yameingiliwa na kuathirika na L1, hata hizi zinaweza kuonekana katika maandiko yao.

Kwa kuzingatia upande wa kimatamshi, utafiti huu haukuonyesha athari zozote zinahusu irabu za Kinyankore wakati wanaposoma L2 iliyo Swahili. Mwisho, huku kuathiriana hakupaswi kuonekana kama hali ambayo haifai, kwani pale ambapo mifumo ya kisarufi ya lugha haidhuriwi, athari hizi zinaweza kujitokeza na manufaa ya kusaidia wanaisimu kutafiti etimolojia ya maneno tofauti badala ya kuzififisha, na hivyo kukuza usomaji wa L2 ya Swahili kwa wanafunzi wenye L1 iliyo Kinyankore.

7.2.1 Jinsi umilisi L1 unavyoathiri usomaji wa L2

Kifungu hiki kinatoa muonekano wa matokeo ya shabaha iliyotangulia ya utafiti. Katika lengo hili, utafiti ulifanywa kuhusu athari za sarufi ya Kinyankore katika kujifunza L2 inayokuwa Swahili. Utafiti wa sasa uligundua athari mbalimbali katika viwango vya leksika, sentensi, semantiki, fonolojia, na maumbo.

7.2.1.1 Kimsamiati

Kuhusu msamiati, tafiti zilionyesha kwamba kuna wale watoto Wanyankore wanaojifunza Swahili wakifanya kasoro kwa kuingiza maneno ya Kinyankore. Kwa kurejelea utafiti wa sasa, iligunduliwa kuwa Watoto waliokuwa wakisoma L2 wanaweza kutumia msamiati wa L1 yao ya Kinyankore kama njia inayoweza

kuwasaidia kutambua na kusoma yale maumbo katika L2 hasa wale ambao tayari wanajua kutumia lugha zote mbili. Pengine, uelewa unaohusisha leksika za Kinyankore unaweza kusaidia katika kukumbuka na kuelewa maana inayofafanua maumbo ya L2.

Utafiti unaonyesha pia kuwa Watoto wenye asili ya Kinyankore wakiwa wansoma L2 ya Swahili, baadhi yao wanategemea msamiati wa L1 ya asili kama Kinyankore kwa ufafanuzi unaohitajika wa maumbo yanayotakikana hasa kukidhi haja za mawasiliano katika mazingira yao.

Kwa hivyo, mwingiliano huu wa msamiati huchangia katika uelewano unaojitokeza kulingana na utamaduni, na kusaidia masomo ya L2 iliyo Swahili kwa wanafunzi wa L1 iliyo Kinyankore.

7.2.1.2 Kifonolojia

Katika eneo la matamshi, ilionekana kwamba kuna Wanyankore wajifunzao L2 iliyo swahili wanaobadilisha matamshi sahihi ya sauti wakitamka maumbo fulani, halafu, wanatumia matamshi yasiyo sahihi. Hali hii husababisha usumbufu katika mawasiliano kwani ujumbe haupokelewi ukiwa na ujumbe uiolengwa kuwasilisha kwa wasikilizaji. Wengine wanaojifunza Kiswahili huchanganya silabi na pia hukosa sauti kadhaa wanapozungumza lugha hii, hasa katika sentensi za Kiswahili.

Sababu nyingine za kasoro za kifonolojia ni ukosefu wa baadhi ya sauti katika Kiswahili. Kwa mfano, namna maumbo yanavyotamkwa ya Kinyankore yanaweza kuathiri Kiswahili, hasa yakitoka kwa kutumia hizo sauti za kipekee kwenye maumbo, mifano ilifafanuliwa katika sura ya nne.

7.2.1.3 Kisemantiki

Makosa mengine yaliyogundulika kwenye utafiti wa sasa yanahusiana na maana. Imeonekana kuwa baadhi ya wazungumzaji wa Kinyankore wanaojifunza Kiswahili hutafsiri maneno na maana kutoka Kinyankore halafu wanayabadilisha kama yalivyo kwa Kiswahili. Takwimu za utafiti zilionyesha kwamba wanafunzi wa Kinyankore wanaojifunza Kiswahili mara nyingi huunganisha maneno na maana za Kinyankore bila kujali yanamaanisha nini na jambo hilo linalosababisha athari za kimaana katika Kiswahili.

Kwa mfano, kama ilivyoainishwa katika jedwali 4.5, mahojiano yaliyohusisha watoto wenye asili ya Kinyankore yalionyesha kuwa walipenda kusema "wanafunzi walizina pamoja" badala ya "walicheza pamoja." Pia, waliposema "Alileta ekiti," walitaka kusema "Alileta kiti," na "Walimwita" badala ya "Walimuua." Makosa haya yanapelekea wasikilizaji kutokupata maana halisi ya sentensi.

Maneno mengine yaliyojitokeza ni hayo yanatoa maana tofauti kwa kinyankore yakitumika kwa L2 iliyo Swahili. Kama vile, "*Kaka* yangu alimzaa Mama". Kwa Kinyankore, neno *kaka* humaanisha *Nyanya/bibi*, bali likibadilishwa kwenda L2 ya swahili humaanisha ndugu wa kiume.

Haya matokeo yanathibitishwa na Rocha (2011), ambaye alisisitiza kwamba taathira ya kimaana zinaweza kujitokeza kwa L2 zikiwa zina uhusiano wa karibu wa L1. Ingawa makosa haya yanaweza kupatikana katika matumizi na mazungumzo ya watu wa kawaida wanaotumia L2 ya swahili, hivyo ujumbe huweza kueleweka, hali hii bado inaathiri lugha ya Kiswahili. Katika mandhari mengine, inaweza kuathiri mawasiliano, hasa pale ambapo neno huchukua maana tofauti, kama vile ilivyoelezwa katika sura ya nne.

7.2.1.4 Athari za kisintaksia (kimuundo)

Kwa kurejelea utafiti wa sasa, takwimu za utafiti zilionesha makosa ya kisintaksia kwa mwanafunzi wa jamii ya Kinyankore anayejifunza L2 ya Swahili, mifano inaonyeshwa hapa katika sura ya nne.

Uwezo wa L1 ya Kinyankore kuingilia masomo ya L2 iliyo Swahili ulipatikana katika tungo wanafunzi walizotunga zikidhihirisha kasoro za kimuundo wa tungo hizo. Taathira hizo zinatokana na mfumo wa kisintaksia wa Kinyankore ambapo wanafunzi hujipata wanazungumza lugha potofu pale wakitafsiri tungo bila kujali mfumo wa kisintaksia wa Swahili. Takwimu za utafiti zilibainisha kuwa L2 ya Kiswahili inaathiriwa na L1 Kinyankore kutokana na viwango vilivyoorodheshwa hapo juu vya kiisimu.

7.2.2 Sababu zinazosababisha athari za Kisarufi

Sehemu hii inaangazia matokeo ya shabaha ya pili ya utafiti. Pia, takwimu za huu utafiti zilibainisha sababu zinazochangia athari za Kinyankore katika kujifunza Kiswahili.

7.2.2.1 Mchango wa L1

Utafiti ulionyesha kuwa sababu iliyo kuu ambayo inasababisha taathira hizi kutambulika katika mafunzo ya L2 ya Swahili yakitoka kwenye uelewa wa mfumo wa L1 ya Kinyankore. Kwa kuzingatia utafiti wa sasa, ilitambulika kuwa wanafunzi wanatafsiri maneno na maana zake kutoka Kinyankore na yakatumika tena kwa Kiswahili wakiamini kuwa yatatoa maelezo kamili kama katika L1. Kielelezo kizuri ni pale Watoto wanaposema "Napigwa kichwa," kitenzi "kupigwa" kinazua mkanganyiko, kwani maana iliyokusudiwa inaweza kupotea, na kusababisha maswali kama: kichwa kinampiga vipi? Je, kichwa kina fimbo ya kuchapa mtu au ndicho kinachapwa? Mwanafunzi akisema “anasikia Njaa” ni kama anaisikia na masikio yake!

7.2.2.2 Kutumia L2 shuleni tu

Utafiti ulibaini kuwa Kiswahili kinatumika zaidi katika mikutadha inayokuwa shuleni pekee. Kulingana na data iliyooneshwa kwenye sura iliyotangulia hapo nyuma ya tano, wanafunzi 35 wa vyuo vikuu, sawa na 53%, walikiri kwamba wanapokuwa vyuoni, wanatumia Kiswahili zaidi katika mawasiliano. Hali kadhalika, wanafunzi 30, sawa na 46%, walieleza kuwa wanatumia zaidi Kinyankore katika mawasiliano yao. Hii inaonyesha kwamba jinsi L2 ya Swahili inavyotumika ni njia isiyo mazoea.

7.2.2.3 Ukosefu wa sauti /θ/ na /ð/ katika Kinyankore

Data za utafiti pia zilionyesha kuwa Kinyankore haina baadhi ya fonimu ambazo zinamfanya mwanafunzi kushindwa kutamka vizuri maumbo mengi ya L2 iliyo swahili. Utafiti ulionyesha kuwa fonimu /θ/ na /ð/ hazipo katika Kinyankore, na hii inasababisha mwanafunzi ashindwe kutamka maneno kama “Thelathini,” akilitamka kama “Selasini,” na “Adhabu,” akilitamka kama “Azabu”.

7.2.2.4 Ufundishaji usiofaa wa Kiswahili

Pia, takwimu za utafiti zilionyesha kuwa ufundishaji haukidhi nini Watoto wanachokihitaji, kulingana na vile wahojiwa walivyojibu hata vile takwimu za utafiti zilivyochambuliwa. Mtafiti aligundua kuwa ufundishaji usiofaa unaokosa L2 ndiyo sababu mojawapo ya athari hizi. Kuna wafunzao wanaofundisha Kiswahili ambao wasio na uzoefu na tajriba inayotakikana juu ya L2 hiyo. Wakati mwingine, walimu hawa wameathiriwa kutokana na L1 ya kimama, hivyo mtoto anayesoma L2 akisikiliza matamshi ya mwalimu yanavyokuwa. Hii inawafanya wanashindwa kutofautisha matamshi sahihi wakati mwalimu anapofanya makosa, kama vile kutamka “r” badala ya “l,” au “s” badala ya “thi.”

Aidha, kufundisha ambako hakukidhi viwango vya kusomesha na mafunzo yenyewe kunajumuisha pia matumizi yasiyofaa ya zana za kufundishia, hasa kuleta mitazamo ya msamiati na vigezo vinginevyo vya lugha.

7.2.2.5 L2 kutothaminiwa kama lugha muhimu

Takwimu za uwanjani zinadhihirisha kwamba jamii ya Kinyankore haipewi kipaumbele cha kutosha kinachofaa kusomeka kwa wanafunzi wanaosoma L2. Kuna wanaofundisha waliohojiwa walikiri kuwa wanapendelea zaidi kuzungumza Kinyankore nyumbani na katika maeneo mengine ya kijamii kama harusi, misiba, na mikutano ya ukoo. Hali tunayoizungumza ikdhihirisha kuwa Kiswahili hakina nafasi muhimu kwenye uwezo wa kijamii wanamoishi wasemaji wa Kinyankore, na hivyo inazuia juhudi za wanafunzi kujifunza Kiswahili kwa ufanisi zaidi.

7.2.2.6 Kuimarisha desturi za wanyankore

Utafiti ulionyesha kuwa washiriki wanaotumia Kinyankore nyumbani wanaendelea kuimarisha na kurithisha lugha hiyo kwa wale wanaoishi wao. Matokeo haya yanathibitisha maelezo ya Coulmas (2005) kwamba lugha inakuwa alama ya utambulisho wa jamii, ikitumika kama ishara ya umoja, na kuonesha kategoria ya wanafunzi wanaotumia lugha hiyo ikiwa L1 ya msingi.

7.2.2.7 Mazingira duni ya kufundishia Kiswahili

Utafiti wa sasa ulibainisha kwamba mwanafunzi akiwa nyumbani anatumia L1 iliyo Kinyankore, hata akiwa katika mazingira mengine yasiyo rasmi kama kwenye msiba, kwenye harusi, na mahali pengine wanakoelewa Kinyankore hajali kutumia L2 ya Swahili. Jambo hili la kimazingira linamletea msomi huyu kutopata nafasi kukuza L2 ya Swahili.

Mahali pekee ambapo mwanafunzi anaweza kupata muda anaoutumia kusema L2 huwa pale awapo shuleni tu. Huko ndiko mwanafunzi anaweza kupata mazingira ya darasani ambayo yanampa mwanafunzi fursa ya kukitumia vizuri L2. Tena, kwa mwanafunzi au mtu aliyezoea kukaa katika jamii yenye wasemaji wa L1 (Kinyankore) kama lugha yake hawezi kupata shida za kimawasiliano. Taathira hizo ataziona dhahiri pale zikitokea akilazimika kuhama kwenda mahali pengine ambako watu hawazungumzi lugha hiyo tangulizi kama yake, kijamii atapata athari kwa kuwa anaweza kushindwa kuwatolea habari wenzake hadi muda wa kipindi fulani upite.

Hata hivyo, jamii ya Wanyankore haiwahimizi watoto wao kuongea L2 wakati wote, hii huwa kwa sababu ya muktadha waliomo.

7.2.2.8 Lugha ya Kinyankore hutumika kama utambulisho

Wanafunzi wanaozungumza Kinyankore wanatumia tajriba waliyo nayo kuhusu L2 kama njia ya kuelezea utamaduni wao na kuleta muktadha wa kihistoria na kijamii yakiendeleza mafunzo ya L2. Takwimu za utafiti zinadhihirisha kuwa, wakati wanafunzi walipoulizwa sababu zinazowaletea kupendelea L1 iliyo Kinyankore katika maeneo yao, wengi walisema kwamba wanataka kuhifadhi lugha yao. Wanafunzi wahojiwa walidai kuwa kama wasipotumia lugha ya Kinyankore, kizazi chao hakiwezi kuendelea kuzungumza L1 iliyo ya kiasili na hivyo itakufa. Mawazo yao hayo pia yalithibitishwa na vijana wanyankore, ambapo 56% yao wanapendelea kuzungumza L1 wakati wote.

7.2.2.9 Vipindi vinavyotumika kufundisha L2.

Tukizingatia takwimu nyingi za utafiti, kuna asasi ambapo L2 haipewi kipaumbele katika ratiba za masomo, hivyo kusababisha Kiswahili kutopatiwa nafasi ya kutosha. Takwimu zinazotokana kwa utafiti huu zilionyesha kwamba, shule nyingine zinasisitiza

sana masomo ya sayansi, ile lugha iliyo tofauti ikiwa Kiingereza au lugha za kigeni, hivyo kufanya Kiswahili isionekane kuwa L2 inayotiliwa mkazo sana katika masomo. Kwa mfano utafiti huu ulionyesha kwamba kuzingatia zile asasi ambako utafiti ulifanyika, mtafiti alikuta kwamba wakati unaoratibiwa kufunza L2 huwa unapewa vipindi viwili vya dakika themanini kila wiiki kwa madarasa yote. Hii inamaanisha kwamba Wanafunzi hawatapewa wakati ufaao kujifunza Kiswahili kama wanavyojifunza masomo mengine, ambayo yanapewa vipindi zaidi ya vinne kwa wiki.

Ili kuboresha hali hii, ni muhimu kuimarisha mipango ya elimu, kuwazidishia masomo wahadhiri wanaofunza swahili, kuhamasisha walimu wakuu, maofisa wadhibiti masomo, na kuhakikisha rasilimali zinazofaa zinapatikana ili kuwezesha mafunzo ya L2. Hii itasaidia kuzidisha wakati ufaao unaohitajika kwa wanafunzi kutafakari na kuizoea L2 ya Swahili halafu kuongeza ufanisi wa elimu hii.

7.2.2.10 Mafundisho yasiyofaa kwa wanafunzi

Takwimu za utafiti zinaonyesha kwamba ikiwa wanafunzi watajifunza kwa ufanisi, walimu wanalo jukumu kubwa la kuunda mazingira mazuri yanayofaa kufundishia yaliyokusudia kutimiza malengo yanayotarajiwa kufanikisha usomaji wa watoto.

Mwanafunzi anajifunza lugha kwa kumsikia jinsi mwalimu wake anavyotumia lugha; jambo hili humfanya mwalimu amwathiri mwanafunzi anapofanya kasoro yoyote akisema swahili, mwanafunzi humwiga na kufanya kasoro hiyo hata asipokuwa na lengo lolote kukosa. Hali hii inatokana na mwalimu kuwa mzungumzaji asili wa L1 iliyo Kinyankore, na hivyo anaathirika vibaya akiitumia L1 hiyo wakati anapowafunza L2. Mwanafunzi anaiga makosa haya kama ni sahihi, akijaribu kurahisisha sarufi ili kufikia ufanisi.

Takwimu za utafiti zilidhihirisha kwamba walimu wanahitaji kufanya kila juhudi ili kuwa mifano bora wanapokuwa wanafunza L2 kuwasaidia Watoto wao, hasa wakiwa shuleni. Wanapaswa kutoa kipaumbele kusomeshwa L2 iliyo Swahili wakiwasiliana kuinua uelewa wa wanafunzi na kuwasaidia katika mazoezi yao. Hii itasaidia wanafunzi kujenga msingi mzuri na kujiamini wanapozungumza Kiswahili mbele ya watu wengine. Aidha, walimu wanapaswa kuwahimiza wanafunzi wao kuwa na ari ya kufunza machapisho kadha wa kadha ya hadithi vilivyoandikwa kwa Kiswahili, lengo likiwa ni kudumisha namna wanawyokuwa na umilisijuu ya istilahi na matumizi ya L2.

7.2.2.11 Tajriba ya wahadhiri kuhusu Swahili

Utafiti wa sasa uligundua kwamba inaposhindikana kwa mwalimu kuwasilisha ujumbe ulio kusudiwa kwa wanafunzi, inasababisha kutokuelewana kwa wanafunzi wakikosana na wahadhiri wao katika vipindi vya masomo. Hali hii inaweza kusababishwa mchango wa mwalimu mwenyewe au mwanafunzi. Wanyankore wengi wameathiriwa kwa kuegemea L1 sana. kutokana na matumizi yake kwa muda mrefu, ndiyo sababu mwalimu anajitoa kutumia njia nzuri zinazowasaidia kuwasaidia wanafunzi wake.

Kwa kuzingatia takwimu za utafiti wa sasa nchini Uganda, walimu wanaotosha wenye kuelewa L2 kikamilifu mara nyingi huwa ni wachache. Aidha, kuna wale wafundishao wanaofundisha L2 hata wasipokuwa na tajriba ifaayo kutosha kuwawezesha kufanikisha somo hilo.

Takwimu za utafiti zinaonyesha kuwa ujuzi duni juu ya L2 inayotumika kufunzia unaathiri kwa njia mbaya mchakato wa kufundisha na kusoma. Mwanafunzi hupata elimu inayohusu somo la L2 na jinsi mwalimu wake anavyozungumza. Kwa mfano, mwanafunzi anaposhuhudia kasoro za kifonolojia zinazotolewa na mwalimu, mara

nyingi yeye pia huzifanya kasoro hizo hata bila kutarajia na kuelewa. Hali hii inatokea wakati ikiwa mhadhiri anakuwa anatumia L1 yake kama Kinyankore. Aidha, ufundishaji usioridhisha wa wale wahadhiri ambao L2 iliyo Swahili wanachangia kusababisha matokeo kama hayo. Mkakati mbaya ukitumiwa kufunzia L2 unatokana na kukosa uelewa wa walimu, ambao wengi wao hawachagui njia zifaazo za kufunzia hata kuzitumia ipasavyo.

7.2.2.12 Matumizi yasiyofaa ya Stadi za kufunzia

Takwimu za utafiti zinadhihirisha kwamba njia zinazotumika kufunzia zikitumika vibaya zinamwonyesha mwalimu kama chanzo cha maarifa pekee yake na kumletea mwanafunzi kumtegemea mwalimu na kuwa katika hali ya kusubiri kupokea elimu. Matumizi mabaya ya njia zinazotumika kusomesha wanafunzi yanachangia katika kutokuwezesha wasomao kuwawia vigumu bila urahisi wowote. Hili ni mojawapo ya mambo mengine yaliyogunduliwa kuchangia kuwepo kwa taathira ambazo hutokana na mifumo inayoletwa mafundisho yasiyo mazuri kwa upande wa mwalimu kukosa umilisi (ujuzi) ufaao wa kilugha hasa stadi zenyewe anazozitumia kueneza L2. Mchango huu hutokea wakati mwanafunzi anapohamisha kanuni na mifumo ya L1 akiitumia kufunzia L2 iliyo swahili. Mambo kama haya hutokea katika ngazi ya kimatamshi kwa kuathiri namna sauti inavyotolewa, athari hizi hutokea wakati sauti aliyozoea mwanafunzi katika L1 iliyo Kinyankore haipatikani kwenye L2 iliyo Kiswahili. Hivyo basi, iligunduliwa kwamba jinsi vifaa vinavyotumika pamoja na zana nyingine za kufundishia msamiati na vigezo vingine kuhusu usomaji wa L2 huwa wa maana Zaidi wakati wa kufunza L2. Aidha, iwapo L2 iweze itaeleweka bara bara, walimu wanapaswa kuunda stadi zifaazo za kufunzia, ambapo ufundishaji huo unapaswa kuandamana kuonyesha uhusiano uliopo kati ya zana hizo na matumizi yake ili kusaidia katika uelewa wa maana ya msamiati.

Kwa kurejelea takwimu za utafiti, inaweza kubainishwa kuwa lugha ya Kinyankore inaathiri kwa kiwango kikubwa cha usomaji wa Watoto wakijifunza L2 iliyo Swahili, hata wanafunzi huenda wakapata ugumu kutokana na matamshi ya sauti wanayoyajua kwenye L1 iliyo Kinyankore halafu hayapatikani kwenye L2 iliyo Swahili. Madhaifu haya yanatokana na tofauti za kifonolojia hasa sauti na muundo katika maumbo yanayosemwa kutoka kwa walimu wakati wanapofundisha wanafunzi wa Kinyankore.

Kama anavyosema Rocha (2011), watu wengi wameathiriwa kwa kurejelea L1 yao ambayo hutumika zaidi katika mawasiliano, hii inaungwa mkono na utafiti huu ambao umebaini kwamba wengi wa wanafunzi wameathiriwa na Kinyankore ikiwa L1. Njia pekee ya kusaidia wanafunzi ni kwa kutumia njia nzuri zifaazo kufunzia.

7.2.2.13 Ukosefu wa baadhi ya msamiati wa Kiswahili

Ufundishaji usiofaa ambao walimu na wafunzaji wa L2 ya swahili walio nao unawafanya wanafunzi wasipate muda wa kutosha kujifunza lugha hiyo, hasa wanapokuwa mbali kutoka kwa mkutadha unaofaa wa shule. Aidha, wazazi na watoto wao hawana matamanio yanayofaa kutia motisha ya kuunga mkono ufunzaji wa L2 hiyo ya Swahili.

Ukosefu wa baadhi ya msamiati wakati wa vipindi vya kufunzia L2 unaweza kuwa na athari mbalimbali kwenye mchakato wa kujifunza na kuelewa lugha hiyo. Ukosefu wa msamiati unaweza kupelekea wanafunzi kukosa uelewa sahihi wa maudhui wanayojifunza. Hivyo, wanafunzi wana uwezo mdogo wa kuelewa andiko, mazungumzo, au mada zilizo tofauti kuhusu hiyo lugha inayozingatiwa. Wakati mwingine, bila msamiati mzuri, wanafunzi wanakuwa na wakati mgumu kuwasiliana mawazo yao kwa uwazi. Jambo linaloweza kusababisha mkanganyiko na kutokuelewana wakiwa wanawasiliana wao kwa wao au hata wenzao na walimu.

Ukosefu wa msamiati unaweza kuathiri mahusiano ambayo yangekuwa na athari iyanayofanywa na wanafunzi. Wanafunzi wanaposhindwa kuelezea hisia zao au mawazo yao, wanaweza kujihisi kutengwa na wenzao. Wanafunzi wa Kinyankore wanaposikia hawana maneno yanayofaa na wanaweza kujihisi wakiwa chini ya kiwango au kukosa kujiamini katika kujieleza au kushiriki katika majadiliano. Wanafunzi wanaokosa msamiati wanakuwa na shida za kusoma na kuwasiliana kama vile lugha za kigeni, kwa sababu wanakutana matatizo mengi sana wakati wa kujenga msingi mzuri wa kiswahili. Basi huenda ikawawia vigumu wadau wa elimu kujitahidi kuboresha ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili ili kusaidia wanafunzi kufikia uelewa mzuri unaohitajika wa L2 kwa kujiandaa ili kurahisisha maisha na masomo yao ya baadaye.

Tukizingatia sehemu hiyo, tumeangalia uchanganuzi juu ya shabaha mahsusi ya pili umejadiliwa. Shabaha nyingine ya pili ilinuia kubaini sababu za athari zinazowakabili wanafunzi wa Kinyankore wanapojifunza L2 ya Swahili.

7.2.3 Mbinu bora za kufunzia L2 ya Swahili

Sehemu hii inaangazia matokeo ya lengo la tatu la utafiti. Utafiti umeonyesha njia kadhaa zinazotumiwa kusaidia wanafunzi wa Kinyankore wajifunze L2 ya Swahili, ikiwemo kuanzisha mafunzo ya swahili tangu utotoni. Hii itawasaidia watoto kujenga msamiati unaotosha kupata miundo na matamshi sahihi ya Swahili.

Data za utafiti zimebainisha kuwa wanafunzi wanapopewa nafasi ya kufanya mazoezi ya kutoshakusema L2 ya swahili, inasaidia kuwa na uwezo wa kufanikiwa wakati wa kufunza L2 iliyo Swahili. Wanafunzi wanapaswa kupata fursa za kujizoeza kuunda miundo ya swahili, kujifunza msamiati, muundo wa kutunga habari halafu kutaja matamshi ya tungo zenye changamoto. Pia, midahalo kuhusu Kiswahili shuleni

inaweza kuleta mafanikio, ambapo wanafunzi wanaoshindana wapate motisha inayofaa.

Licha ya hatua hizo, ili mwanafunzi ajifunze lugha mpya, ni muhimu kwanza kuona dhima inayosababisha masomo ya L2 hiyo. Hivyo basi, mwanafunzi wa jamii ya Kinyankore anahitaji kueleweshwa umuhimu unaosababisha kwa nini L2 isomwe ikiwa ni swahili. Utafiti umeonyesha kuwa asilimia 44% ya walengwa walionyesha kutofahamu jinsi usomaji wa L2 ya Swahili unawasaidia baada ya kumaliza shuleni na huko mbeleni maishani, huku wengi wao wakiiona kama lugha isiyo na manufaa zaidi ya matumizi shuleni.

Hivyo, jamii, familia, na wazazi wanahitaji kuelimishwa juu ya manufaa ya L2 ya Swahili hata namna ya kuitumia kwenye kiwango cha kimataifa, nchi nzima, jamii inayuzunguka na hata matumizi ya kibinafsi. Walimu wanapaswa kuhamasishwa kuhusu manufaa ya mafunzo ya L2 ya Swahili katika mataifa yote. Wanafunzi wanapaswa pia kuonyeshwa kwamba wana uwezo wa stadi za kuzungumza Kiswahili shule na nyumbani. Wanapaswa kupatiwa vitabu vya hadithi na mafunzo mengine ili kuongezea maarifa yao kuwezesha namna ya kuzungumza Kiswahili.

Pia, utafiti umeonesha kuwa mwanafunzi anahitaji walimu na wahadhiri wengi wenye sifa zinazofaa ili kufanya vizuri katika masomo yake. Iligunduliwa kuwa si ukweli kwamba mwalimu yeyote huwa na uelewa ufaao kuwafunza wasomao Swahili, ndiposa inakuwa yafaa kuchukua hatua za kuhakikisha walimu wenye ujuzi wa kutosha wanapatikana shuleni na vyuoni.

Zaidi, watoto wanasoma L2 ya swahili vyema kwa kusikia matamshi bora wakiongozwa na utamkaji wa kiongozi wao mwalimu. Hivyo, mwanafunzi anaposhuhudia mwalimu wake akikosea kimatamshi, mara nyingi anaathirika kukosea

pia hata bila kukusudia. Jambo hili linaletwa na hali ya kuwa mwalimu huwa mtumiaji anayewaelekeza wasomaji kujifunza lugha kutoka kwake, hivyo inakuwa na uwezekano kwamba mwanafunzi kurekebisha makosa yake yanayotokana na matamshi mabaya.

Vilevile, utamaduni wa Kinyankore unapendelea kueneza utumiaji wa L1 iliyo Kinyankore badala ya Kiswahili. Mazungumzo yoyote ambayo yanafanyika nyumbani yanatumia Kinyankore, na utafiti ulionyesha kuwa wengi wa wanafunzi wanarudi nyumbani kutoka shule hutumia ile lugha inayoeleweka kwao. Mazungumzo kati ya wanafamilia na koo yanathaminiwa zaidi yanapofanywa kwa Kinyankore, kwani inachukuliwa kuwa ni ishara ya heshima na kujituma katika kazi, hata kutii uwepo wa tamaduni zao za kibinafsi.

Utafiti ulibainisha kwamba ni muhimu mwalimu kuwa mahiri na akawa anaelewa ipasavyo kiswahili ili kuwasaidia wanafunzi wa Kinyankore kusoma L2 ya Swahili wakafinikiwa vilivyo. Utafiti pia ulionyesha kwamba kulikuwa walimu, hasa wale wanaofundisha madarasa ya msingi (kuanzia darasa la awali hadi la tatu), mara nyingi hukosa elimu inayofaa katika kufundisha Kiswahili.

Waliokuwa wanafundisha L2 ya swahili wanapaswa kujitolea katika kuwasaidia wanafunzi kuelewa L2 ya swahili. Kwa jumla, mtafiti alipendekeza kwamba wanafunzi wahusishwe katika kufundishwa kwa umakini kuhusu matamshi sahihi kuhusu L2 iliyo swahili kwa ajili ya kupunguza vile L1 inavyoiathiri L2. Hata hivyo, kuna walimu ambao wanakosa uelewa unaofaa wa lugha kwasababu ya kutumia mbinu zisizofaa, kama vile kufuatilia kanuni zinazotawala utumiaji wa tungo husika.

Pia, mazingira yana ushawishi mkubwawa kufunza L2. Mwanafunzi anapozungukwa na watu wasiozungumza Kiswahili, anaweza kushindwa kuzungumza Kiswahili sanifu.

Walimu wengi walikubaliana kwamba mazingira yanayoathiri wanafunzi wa Kinyankore wakiwa wanasoma L2 yanahitaji kuzingatiwa.

Huu utafiti ulitoa matokeo pia yakionyesha umuhimu wa kuhamasisha wazazi au walezi wanaotumia L2 wakati wanapowasiliana na wasomi walio Watoto wa kwao, kwa ajili ya kuweza kuvunja dhana potofu kwamba kujifunza Kiswahili kunaweza kuathiri utamaduni wa kabila lao. Ikiwa wanaowazaa watoto hawa watashirikiana, wasomaji wao wataweza kuwa watumiaji wema wa L2 ya Swahili. Jitihada zinazohitajika kuongeza katika kutekeleza hili, ambapo takriban asilimia 87 ya washiriki waliona njia hii itasaidia kupunguza athari inayodhihirika kwa Kinyankore wanapokuwa wanaendelea na masomo ya L2 ya Swahili.

Msingi mzuri wa kuwa mjuzi wa lugha huanzia utotoni, na ni muhimu Kiswahili kifundishwe mapema ili kusaidia kuwezesha kuwasiliana kwa baadaye. Pia, wazazi wanapaswa kuhamasishwa kutumia Kiswahili na kuondoa imani potofu kuhusu kupoteza utamaduni wao. Utafiti ulibaini kwamba wanafunzi wanapaswa kupata wakati unaotosha kufanya mazoezi ya lugha. Walimu wanapaswa kuelimishwa na kuhamasishwa ili waweze kuwa na njia za kufundisha zinazofaa.

Mwisho, utafiti umependekeza maeneo mengine ya kuchunguzwa kwingine kunakoweza kushughulikia msamiati, maana, na matamshi, hata ikiangazia mikakati mingine ili kuweza kutambua maarifa mapya kuhusu athari hizi. Pia kutahitaji tafiti zaidi ili kugundua athari zinazohusiana na muundo wa maneno na sarufi kuelezea Zaidi tofauti zilizopo kutenganisha L1 na L2. Kufuatia mchango wa L2 kwenye jamii hiyohiyo, ni muhimu kufanyika tafiti kuhusu vile L1 inavyoingilia L2 katika usomaji wake, kama alivyosema Mvungi (2010) kuwa kutumia maumbo halisi ya matumizi ya viungo vyote vya sauti, ambao unazungumzwa kati ya watu hasa katika jamii

inayohusika. Hivyo, mifump inayojulikana inategemea lugha ambayo inatumika mara nyingi zaidi.

7.3 Hitimisho

Utafiti huu uliangazia jinsi sarufi ya Kinyankore inavyoingilia usomaji wa L2 katika kujifunza Kiswahili ulifanywa ukielekezwa mitazamo mbalimbali, hata ilizingatia nadharia ya Uchanganuzi Makosa, Nadharia ya Uchanganzi-linganuzi, na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano. Hatimaye, utafiti umeweza kubaini chanzo cha athari za sarufi ya Kinyankore zikiingilia ufunzaji wa L2 ya Swahili kwa watoto wanyankore. Aidha, utafiti umebaini mbinu zinazoweza kusaidia wanafunzi wanaokumbwa shida zinazohusiana na kanuni za L1 wanapojifunza Kiswahili. Hivyo basi, walimu wanaofundisha somo hili wanapaswa kuzingatia namna ya kutumia L2 ya swahili ili kutoa msamiati unaotosha kuwajumuisha wanafunzi katika midahalo shuleni ili kuimarisha stadi zao za kuzungumza. Kwa ujumla, ingawa Kinyankore kinavyoathiri L2 iliyo Swahili kwa sarufi, utafiti huu haukuonyesha kuwa kuna kikwazo chochote wakiwa wanafundishwa L2 ya Swahili.

7.4 Mapendekezo ya Utafiti

Baada ya juhudi kadhaa zinazohusiana na kumalizia utafiti wa sasa, mtafiti alipata jawabu la yale mambo aliyojiuliza kufikia shabaha zilizoongoza utafiti. Mtafiti pia alieleza mapendekezo kuhusu yale yaliyotokea kutoka kwa utafiti hata wito wa tafiti zijazo. Kwanza, walimu wanaofundisha L2 iliyo swahili wanapaswa kuonyesha uelewa unaotosha kwa ajili ya kujiwezesha kupata ufanisi ufaao. Walimu hawa wanapaswa kuchagua na kutumia njia zifaazo za kusomesha zinazomwanga ala zinazomwezesha kufundishia kuelewesha wasomaji. Matumizi sahihi ya zana hizo yatasaidia wanafunzi kuelewa haraka kupata msamiati mzuri wa Kiswahili.

La pili, jamii, koo, familia, wazazi na wanafunzi wanapaswa kuhamasishwa na kuelimishwa juu ya faida zinazoletwa usomaji wa L2 ya swahili hata umuhimu wake kwa mtu binafsi, koo, familia, jamii, taifa, na kimataifa, hasa kulingana na wakati huu ambapo Kiswahili kinapewa msukumo na mataifa tofauti kuendeleza Swahili kwenya bara kote. Serikali inapaswa kuandaa mikakati thabiti kuhakikisha kwamba wahadhiri wafundishao L2 ya swahili wanapata kufunzwa kila muda waweze kuongeza maarifa na ujuzi wao katika ufundishaji.

Tatu, serikali, walimu, wanaoongoza asasi mbalimbali za elimu, na wadau wengine ambao wanahusika kuendeleza L2 ya Swahili wanahimizwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuyafanya masomo ya L2 ya Swahili kuwa rahisi yaliyo bora Zaidi. Serikali ya Uganda imefanya vizuri kwa kuinua na kuendeleza kiwango cha Swahili hata kuifanya lugha iliyo rasmi sambamba na Kingereza. Hata hivyo, kama ilivyo katika kusomesha kwa Kingereza, inashauriwa kwamba Kiswahili kufundishwe ikihusisha asasi za msingi kama shule ya chekechekea na zile za chini kabisa. Katika hatua hii, watoto watajifunza miundo rahisi ya L2 wakiwa bado wachanga, na hivyo kuweza kushughulikia miundo changamano wanapofika kwenye asasi za elimu zilizo juu kidogo. Hii pia itasaidia kubadilisha jinsi watoto wengi wanavyoangalia mambo kuhusu Kiswahili, na kujiona kuwa maumbo wanayoyatumia huwa yenye hadhi kama nyingine zinazozungumzwa nchini Uganda.

Nne, tafiti zilizofanyika kuhusu walimu wa L2 zimeonyesha kwamba Watoto wanasumbuliwa na matatizo mengi yakiwemo kukosa muda wa kutosha kujifunza Kiswahili shuleni. Vipindi vinavyowekwa kwenye ratiba kufunzia Swahili havitoshi ikilinganishwa nay ale mafunzo yanayofundishwa. Kwa hivyo, idara inayosimamia masomo nchini inashauriwa kuweka maagizo ya kuongeza muda kuongezea muda wa kusoma Kiswahili.

Tano, kuna mapendekezo ya kueneza na kukuza uhusiano kati ya wakuza mitaala, watafiti, na asasi tofauti zinazojishughulisha na kusomesha L2 ya swahili, kama vile asasi zinazotumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) idara nyinginezo zinazohusika katika uendelezaji wa Swahili taifa zima. Ushirikiano huu ungesaidia kuendeleza misimamo inayohitajika kuinua Kiswahili kwa Watoto wasomao L2 ya Swahili katika asasi zao za elimu. Tena, shughuli hizi zingechangia katika kuanzishwa kwa klabu za Kiswahili shuleni na vyama vya somo hilo la pili kwenye viwango tofauti vya elimu.

Sita, mafunzo ya L2 iliyo swahili yanapaswa kuimarishwa kupitia asasi za TEHAMA, ambapo magazeti, na vyombo vingine vya kielektroniki vinavyosambaza habari vingepewa kipaumbele katika kubuni miradi hiyo. Kuanzishwa kwa magazeti kwa Kiswahili, pamoja na mashindano yanayohusisha kuongea hata kuandika, yanapaswa kufanywa kwa kushirikisha wahadhiri wa L2 ya Swahili hata wengine wanaohusika katika kufunza L2 hiyo nchini. Katika mashindano haya, wanafunzi wangeombwa kuandika na kuunda hadithi, na zawadi zingepewa kwa washindi, huku matokeo yakitangazwa kwenye zana zinazotumika kusambaza habari ili kuhamasisha watoto wengi kushiriki na kupendelea L2 hiyo.

Mwisho, walimu wanapaswa kuelewa umuhimu wa kasoro zilizofanywa na Wanafunzi wao ili waweze kuwa na uwezo wa kuzitambua na wakawakosoa hata kuzirekebisha. Matokeo yaliyotolewa kwa wahadhiri na wafundishao L2 katika asasi zilizoshiriki zimeonyesha kuwa baadhi yao hawaelewi jukumu la makosa katika ufundishaji. Inashauriwa kuzingatia nafasi inayomwezesha mwanafunzi kuelewa namna ya kuepukana na kukosea akiwa anatumia L2 ili aweze kujisahihisha. Walimu wanapaswa kushughulikia na kuelezea makosa ya wanafunzi kama namna nzuri inayoletea kupunguza makosa hayo.

Mwisho, inashauriwa kuwa na semina na makongamano katika shule nyingi ambapo Swahili inasomeshwa kama L2 ya lazima. Shughuli hizi zingewakusanya wahadhiri na wale wote wanaohusika katika kufunza Swahili kiisimu na kifasihi, na wadau wengine ili kubadilishana uzoefu kuhusiana na masuala yaliyo ya maana sana kuendeleza usomaji wa L2 ya Swahili nchini kote. Pia, makongamano hayo yanaweza kusaidia katika kuandaa michezo ya kuigiza, majadiliano, mahojiano na njia nyinginezo mbalimbali ili kuimarisha ujuzi wao wakitumia L2 yiliyo Swahili.

7.5 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatoa mwaliko kwa watafiti wengine wanaotaka kuangazia jinsi L1 inavyoweza kuingilia L2 wakiwa wanaisoma darasani wakirejelea somo la Swahili lililo somo pendwa katika jamii nyingi kwa wafrika. Kwa kuzingatia tafiti zilizofanywa na zimenukuliwa katika sura za awali, tunaweza kuona kwamba watumiaji wanaopendelea L2 iliyo swahili wanapambana na shida zinazowaletea kushindwa kuelewa lugha hii. Hivyo, utafiti huu unaleta mchango kwa wale wanaotumia L1 mbalimbali zilizo na chimbuko la ubantu ikiwemo Kinyankore, ambao wanatumia Kiswahili sanifu kama L2. Wao wanapatwa kusumbuliwa kutaja sauti zinazojitokeza katika L1 na katika vipengele vya kiisimu kama kisemantiki, kifonolojia, kimofolojia, na kisintaksia. Mtafiti akiendeleza utafiti wa sasa tayari amebaini kuwa huenda kukakosekana utafiti unaofaa uliofanyika kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili kati ya wazungumzaji wa Kinyankore. Hivyo, ukutafiti huku na matokeo yake huenda yakachangia sana watakaotafiti baadaye katika kuelewa mwingiliano wa L1 kwenye usomaji wa L2 ya Kiswahili.

Kwa hivyo, kujifunza Kiswahili kunakuwa na changamoto zinazowasumbua hawa Watoto wanyankore wakisoma maneno mengi ya mkopo kutoka kwenye lugha ya Kiarabu, ambayo yanaweza kuwafanya wahisi ugumu katika kujifunza. Hata hivyo, pia

kuna faida katika kujifunza L2 ya Swahili kwani imetambulika kuwa lingua franka, na jinsi inavyokaribiana na Kinyankore, wanafunzi hawa wanapata urahisi kuelewa vipengele vya sarufi hasa matumizi ya lugha inayolengwa kueleweka.

MAREJELEO

Aaker, D. (2002). *Qualitative Research methods for the social sciences* (6th ed) California

Aleidine, J. M., & Theresa, C. (2015). *Foreign language teaching and learning at University of Nebraska-Lincoln.* International Encyclopedia for Social and Behavioural Science 2nd Edition. 9, 327-332.

Candy, R.L., & Retting, M. (1996). *Teaching in the block: Strategies for engaging active learners.* Princeton, NJ: Eye on Education.

Carnine, D. (2000). Why Education Experts Resist Effective Practices (And what it would take to make education more like medicine). University of Oregon, January 2000.

Cohen, L. (2007). *Social Research Methods.* U.S.A: Allyn and Bacon, A Division of Simon and Schuster, *Inc.*

Collins, G. (2015). *Language to Motivate Learning: The Power of Inspirational Quotes. A Rising Tide*, *7*, 1-22.

Cooper, B. (1989). *Research methods, Techiniques and Procedures*, London University Press.

Corder, S. P. (1967). The Significance of Learners' Errors. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching,* 5, 161-170.

Cozy, P., & Bates, S.C. (2012). *Method in behavioral science. Research* (11th), New York. McGraw Hill.

Creswell, J.W. (2005). *Research methodology: methods and Techniques*. New York. McGraw Hill.

Curtain, F.L., & Martinez, L. S. (1990). Elementary school content-based foreign language instruction. In A. Padilla, H. Fairchild, C. Valadez (Eds), *Foreign language education: Issues and strategies.* (pp. 202-222). Newbury Park, CA. Sage.

Ellis, R. (1996). *The study of second language acquisition*. Oxford. Oxford University Press.

Enon, C. J. (1998), Education.Research and measurement Department of Distance Education, Makerere University, Uganda.

Fisher, D., & Frey, N, (2010). Identifying Instructional Moves during Guided Learning. October 2010. *The Reading Teacher* 64(2):84 – 95 DOI:10.1598/RT.64.2.1

Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2009). *An Introduction to Language* (8^{th} ed.). Boston, MA: Thomson Wadsworth.

Fulass, H. (1971). Problems of Terminology. In: Whiteley, W.H. (ed.); *Language and Social Change*; O.U.P., International African Institute, London (p. 309 – 317).

Gardner, R. C. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation.* London: Edward Arnold

Gleason, J. B. (1992). *The Development of Language* (2nd ed.). Needham Heights, MA: Allyn & Bacon.

Habwe, J. H., & Karanja, P. (2004). *Misingi Ya Sarufi Ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix publishers

Hagége, C. (1999). The child between Two languages, in M. Karra. *Second language acquisition Learners Error and Error correction in language teaching.* Retrieved July 22, 2023. from http:www.pro2/com/doc/633.

Iribe, M. (2010). *The Structure of Kiswahili: Sounds, Sound Changes and Words,* VDM Verlag, ISBN 978-3-639-27066-2.

James, C. (1980). *Contrastive Analysis.* London. Burnt Mill Harlow. Longman publishers.

Kariuki, M., & Duran, M. (2004). Using Anchored Instruction to Teach Preservice Teachers to Integrate Technology in the Curriculum.

Karoro, E.A. (2001). Development of Kiswahili in Uganda. Tanifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo cha Kitaifa cha Kakoba.

Kihore, Y. M., Masamba, D.P.B., & Masanjire, Y.P. (2009). *Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA). Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam.

Kisilu na wenzake (2006). *Desturi na Mila Zetu*. Arusha: East Africa Publication Limited.

Kombo, D.K., & Tromp, D.L.A (2006). *Proposal and Thesis writing: Introduction.* Nairobi, Paulines Publications Africa.

Komunte, B.S. (2001). The impact of Bantu languages in English Language learning processes in Tanzania. Secondary School, makala ya kongamano la Kimataifa Kiswahili, 2000, 287-296.

Kothari, S.K. (1990). *Research Methodology; Methods.* New Delhi New Age International Publishing Ltd Techniques.

Koul, B.N. (2009). *Research Methodology; Methods.* New York. McGraw Hill.

Krashen, S. D., & Terrell, T. D. (1983). *The natural approach: Language acquisition in the classroom.* California. Alemany Press.

Kress, S. D., & Tracy, D. T. (2008). *The Natural Approach Language Acquisition in The Classroom.* Oxford. Pergamon Press.

Ladefoged, P., & Johnson, K. (1972). *A phonetic study of West African languages: The Yoruba, the Igbo, and the Hausa*

Lado, R. (1957). *Linguistics across Cultures: Applied Linguistics and Language Teachers*. Ann Arbor. University of Michigan Press.

Lewis, M.P., na wenzake (2023). *Ethnologue: Languages of the World*. Dallas, TX: SIL International. Available Online at www.ethnologue.com/. *Retrieved September*, vol. 19, 2023, p. 2011.

Lusesa, J. (2013). The Use of Overgeneralization and Transfer Learning Strategies by Elementary and Intermediate Students of ESL. *Language Learning,* 25: 73-107. Retrieved in October 7th, 2023 from abisamra03.tripod.com/nada/languageacq-erroranalysis.html.

Mangwa, D.O. (2005). Athari za Kikisii katika Kiswahili na matokeo mabaya ya mtihani wa Taifa wa Kiswahili kwa wanafunzi wa kisii Wilayani kisii kusini. Tasnifu ya M.A Kiswahili (hat). Chuo kikuu cha Egerton, Kenya.

Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya lugha, Kiswahili 1. Kidato cha 5 na 6.* Nyambari Nyangwine Publisher. Dar es Salaam.

Masereka, L. K. (2020). Je, Kiswahili Nchini Uganda ni Lugha ya Kigeni au Lugha ya Pili? *Jarida La Chalufakita* 2020, Juz. Na. 2.

Mashaka, W. (2015). Athari za lugha ya Kijita katika ujifunzaji wa lugha Kiswahili. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D.P.B. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo,* Dar-es-Salaam, TUKI.

Massamba, D.P.B. (2004). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo,* Dar-es-Salaam, TUKI.

Massamba, D.P.B. (2006). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo,* Dar-es-Salaam, TUKI.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya lugha isimu na nadharia: kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu*. Serengeti Educational Publishers Limited.

Mdee J.S. (2010). *Nadharia na Historia ya leksikografia toleo la tatu,* DSM. Tuki.

Mligo, E.S. (2012). *Jifunze utafiti mwongozo kuhusu utafiti na utamaduni wa ripoti yenye Mantiki.* Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGY).

Mgullu, R.S. (2012). Acquisition of English Syntax by Keiyo L1 Speakers. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Morris, R., & Kirwan, M. (1972). *An introduction to the phonetics of English.*

Msanjila, Y. P., Kihore, Y.M., & Masamba, D.P.B. (2009). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Mudhune, D.R. (2008). Athari za Kifonolojia kwa wasomaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunziwa Kitigania, Kenya. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Munyua, J.G. (2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press.

Naik, H. S. (2013). *Content Cum Methodology of Teaching English*. Bangalore. Sapna Book House.

Ngugi, W. T. (2004). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Njoroge, K. (1987). The Acquisition of Six Morphosyntactic Structures of English by Kenyan Children. (Unpublished Ph.D Thesis) University of Edinburgh.

Nyanda, N. (2015). The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Ontieri, J. O. (2010). Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.

Otiende, M.A (2013). Athari za Kimofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama Lugha ya pili. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kenya.

Papert, S., & Harel, I. (1991). Situating constructionism. *Constructionism,* 36(2), 1- 11.

Poli, D., & Hungler, B. (1999). *Research Methods; The Basic.* London and New York, Routledge Taylor and Francis Group.

Rettig, M. D., & Canady, R. L. (1996). All Around the Block: The Benefits and Challenges of a Non-traditional School Schedule. *School Administrator*, 53(8), 8-14.

Rosenshine, B. (2007). Systematic Instructions. In T. L. Good (ed.). *21st century education: A reference handbook.* Sage Publications.

Ruane, J.M. (2005). *Research Methods; The Basic*. London and New York, Routledge Taylor and Francis Group.

Selinker, L. (1969). *Studies in Second Language Acquisition,* 3, (2), Spring 1981, pp.201-220

Sigh, K. (2007). *Research Methodology; Methods,* India, state SAGE Publication TATAKI.

Ssekamwa, J. C. (2000). *History and Development of Education in Uganda*. Kampala: Fountain Publishers.

Stern, H.H. (1983) *Fundamental Concepts of Language Teaching*. O.U.P, New York.

Taylor, I. (1985). *The development of phonetics in the 20th century.*

Thomason, S. G., & Kaufman, T. (2001). *Language Contact*. Citeseer.

Tsunoda, T. (2006). Language Endangerment and Language Maintenance: An Overview. 1(3), 335-352.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi.Oxford University Press.

Uganda Government White Paper, (1992) *Government White Paper on the Education Policy Review Commission Report*. UPPC Kampala, 1992.

Vigdis, S. (2003). Language and Gender: A New Approach. In The Cambridge *Handbook of Language and Gender* (pp. 1-46). Cambridge University Press.

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Hojaji lililojazwa na wanafunzi

Hujambo mhojiwa mpendwa, mimi ni **Kubakurungi Abraham Kyangungu,** ninasomea chuoni kikuu Moi, nchini Kenya. Kwa sasa ninaendeleza utafiti kuhusu "**Sarufi Ya Kinyankore na usomaji wa Swahili kama L2: Mfano Kutoka Asasi Teule Jijini Mbarara.**

Kwa hiyo, naombeni kwa heshima nyingi muda wako ili unisaidie kujaza hojaji hii. Ningependa kupata ushirikiano wako ili uweze kunisaidia kutoa majibu juu ya maswali yanayohusu utafiti, ambayo ni muhimu kwa kukamilisha utafiti wa sasa. Tafadhali toa taarifa zinazofaa na za kweli bila hofu yoyote; taarifa zote zitashughulikiwa kwa siri na zitatumika pekee kukamilisha utafiti wa sasa. Napenda kutoa shukrani kwako kwa kukubali kuhusika na ushirikiano wako.

SEHEMU 1: MAONI YA KIJUMLA

i. Huhitaji kuandika jina lako kwenye hojaji hili
ii. Majibu yanatarajiwa kulingana na maswali uliyoulizwa.
iii. Ikiwa utapata ugumu katika swali, tafadhali uliza mtafiti.

SEHEMU 2: HABARI KUHUSU MHOJIWA

Andika alama ya (√) kwenye chaguo unachokiona kuwa kinakufaa kwenye mabano [ ]

Maswali:

1. Umri wako

(a)8-10 (   )   (b)11-12 (   )   (c)13-14 (   )   (d)15 na zaidi (   )

2. Jinsia

(a) Kijana ( ) (b) Binti ( )

3. Darasa ulilopo

(a) IV ( ) (b) V ( ) (c) VI ( ) (d) VII ( )

SEHEMU 3: Tia alama ya (√) palipo herufi unayoona ni sahihi katika mabano [ ]

4. Je, wewe unatoka kabila la Kinyankore?

(a) Naam ( ) (b) La ( )

5. Je, unatumia Kinyankore kama L1 yako?

(a) Naam ( ) (b) La ( )

6. Je, Kiswahili ni L1 kwako?

(a) Naam ( ) (b) La ( )

7. Unapokuwa nyumbani, unatumia lugha gani zaidi?

(a) Kinyankore ( ) (b) Kiswahili ( )

8. Ukiwa uko kwenye sehemu za nje ya nyumbani na shuleni, unatumia lugha gani zaidi katika mawasiliano?

(a) Kinyankore ( ) (b) Kiswahili ( )

9. Je, umewahi kutambua kuwa Kinyankore kimeathiri ufunzaji wa L2 ya Swahili kwa matamshi?

(a) Naam ( ) (b) La ( )

SEHEMU 4: JAZA HABARI ZINAZOTAKIKANA KATIKA MAPENGO

10. Taja maneno angalau Kumi (10) katika Kinyankore yaliyo na maana sawa na maneno ya Kiswahili

i. --
ii. ---
iii. ---
iv. --
v. --
vi. ---
vii. ---
viii. --
ix. ---
x. ---

11. Taja maneno ya Kinyankore yanayofanana na ya Kiswahili

i. --
ii. ---
iii. ---
iv. --
v. --
vi. ---
vii. ---
viii. --
ix. ---
x. ---

12. Andika maneno kumi (10) ambayo mara unapoyatamka, mwalimu hukurekebisha.

i. --
ii. --
iii. --
iv. --
v. --
vi. --
vii. --
viii. --
ix. --
x. --

13. Je, unakuta shida yoyote wakati wa kujifunza masomo ya Kiswahili? Ikiwa ipo, tafadhali eleza,

----

----

14. Je, kuna unakuta urahisi wowote ukiwa uansomesha L2 ya Swahili? Ikiwa ipo, tafadhali eleza,

----

----

15. Je, mwalimu hutumia mbinu gani kurekebisha makossa yako unapokosea katika matamshi katika L2 ya swahili?

Shukrani sana

Kiambatisho 2: Hojaji lililojazwa na walimu

Hujambo mhojiwa mpendwa, mimi ni **Kubakurungi Abraham Kyangungu,** ninasomea chuoni kikuu Moi, nchini Kenya. Kwa sasa ninaendeleza utafiti kuhusu "**Sarufi Ya Kinyankore na usomaji wa Swahili kama L2: Mfano Kutoka Asasi Teule Jijini Mbarara.**

Kwa hiyo, naombeni kwa heshima nyingi muda wako ili unisaidie kujaza hojaji hii. Ningependa kupata ushirikiano wako ili uweze kunisaidia kutoa majibu juu ya maswali yanayohusu utafiti, ambayo ni muhimu kwa kukamilisha utafiti wa sasa. Tafadhali toa taarifa zinazofaa na za kweli bila hofu yoyote; taarifa zote zitashughulikiwa kwa siri na zitatumika pekee kukamilisha utafiti wa sasa. Napenda kutoa shukrani kwako kwa kukubali kuhusika na ushirikiano wako.

SEHEMU 1: MAONI YA KIJUMLA

i. Huhitaji kuandika jina lako kwenye hojaji hili
ii. Majibu yanatarajiwa kulingana na maswali uliyoulizwa.
iii. Ikiwa utapata ugumu katika swali, tafadhali uliza mtafiti.

SEHEMU 2: HABARI KUHUSU MHOJIWA

Andika alama ya (√) kwenye chaguo unachokiona kuwa kinakufaa kwenye mabano [ ]

Maswali:

1. Umri wako

(a)18-25 (   )   (b)26-30 (   )   (c)31-35 (   )   (d)36 – 40 (   )

e) 41-50 (   )   (f) 51 na zaidi   (   )

2.Jinsia

(a) Mume ( ) (b) Mke ( )

3. ngazi ya kielimu

(a) Cheti ( ) (b) Stashahada ( ) (c) Shahada ( ) (d) Shahada ya pili ( )

(e) Shahada ya Uzamifu ( )

SEHEMU 3: TOA MAONI YAKO KUHUSU YAFUATAYO;

1. Je, lugha ya kinyankore inaathiri mchakato wa kujifunza Kiswahili kimatamshi na kimaana?

(a) Naam ( ) (b) La ( )

2. Ikiwa unajibu "ndiyo," tafadhali toa mifano mitano kwa kila kigezo ili kuonyesha athari hizo: a) Athari za kimatamshi

i. ---

ii. --

iii. --

iv. ---

v. ---

b) Athari za kimaana

i. ---

ii. --

iii. --

iv. ---

v. ---

3. Je, ugumu unaowakumba wanafunzi wanyankore wanaposoma L2 ya Swahili unaletwa na sababu gani? Taja sababu tano.

i. --

ii. ---

iii. ---

iv. --

v. --

4. Ni mbinu zipi unazotumia kuwasaidia wanafunzi wa Kinyankore wanaojifunza L2 ya swahili? Taja mbinu tano.

i. --

ii. ---

iii. ---

iv. --

v. --

Nashukuru kwa muda na ushirikiano wako

Kiambatisho 3: Wamilisi wanaoelewa Kinyankore Wanavyozungumza L2 ya swahili

Hujambo mhojiwa mpendwa, mimi ni **Kubakurungi Abraham Kyangungu,** ninasomea chuoni kikuu Moi, nchini Kenya. Kwa sasa ninaendeleza utafiti kuhusu "**Sarufi Ya Kinyankore na usomaji wa Swahili kama L2: Mfano Kutoka Asasi Teule Jijini Mbarara.**

Kwa hiyo, naombeni kwa heshima nyingi muda wako ili unisaidie kujaza hojaji hii. Ningependa kupata ushirikiano wako ili uweze kunisaidia kutoa majibu juu ya maswali yanayohusu utafiti, ambayo ni muhimu kwa kukamilisha utafiti wa sasa. Tafadhali toa taarifa zinazofaa na za kweli bila hofu yoyote; taarifa zote zitashughulikiwa kwa siri na zitatumika pekee kukamilisha utafiti wa sasa. Napenda kutoa shukrani kwako kwa kukubali kuhusika na ushirikiano wako.

SEHEMU 1: MAONI YA KIJUMLA

i. Huhitaji kuandika jina lako kwenye hojaji hili
ii. Majibu yanatarajiwa kulingana na maswali uliyoulizwa.
iii. Ikiwa utapata ugumu katika swali, tafadhali uliza mtafiti.

SEHEMU 2: HABARI KUHUSU MHOJIWA

Andika alama ya (√) kwenye chaguo unachokiona kuwa kinakufaa kwenye mabano [ ]

Maswali:

1. Umri wako

(a)18-25 ( ) (b)26-30 ( ) (c)31-35 ( ) (d)36 – 40 ( )

e) 41-50 ( ) (f) 51 na zaidi ( )

2,Jinsia

(a) Mume (   )   (b) Mke (   )

3. Hadhi ya kielimu

(a) Cheti (   )   (b) Stashahada (   )   (c) Shahada (   ) (d) Digrii ya pili (   )

(e) Digri ya tatu (   )

SEHEMU 3: TOA MAONI YAKO KUHUSU YAFUATAYO;

7. Je, lugha yako asilia ni Kinyankore?

a) Naam [ ]   b) La [ ]

8. Ni lugha ipi unayotumia kwa wingi kuwasiliana mkiwa na familia yako unapokuwa nyumbani?

a) Kinyankore [ ]   b) Kiswahili [ ]

9. Je, wakati wanafunzi wa Kinyankore wanapojifunza Kiswahili wanatumia Kiswahili sanifu?

a) Naam [ ]   b) La [ ]

10. Ikiwa umejibu "la" hapo juu, tafadhali eleza matatizo yanayoibuka wanapozungumza, yanayohusiana na ujuzi wao wa lugha ya Kinyankore:

----

11. Kwa maoni yako, unafikiri ni kwa nini wanafunzi wa Kinyankore hukumbana na shida kutokwa kwa L1 ya Kinyankore wakiwa wanasoma L2 ya swahili? Tafadhali eleza kwa ufupi kwa kutumia mifano kisha orodhesha maneno matano (5) yanayoonesha athari inayoletwa L1 wakiwa wanasoma L2 ya swahili.

i. ……………………………………………………………….

ii. ……………………………………………………………….

iii. ………………………………………………………………..

iv. ………………………………………………………………

v. ………………………………………………………………..

Kiambatisho 4: Wanafunzi wa L1 ya Kinyankore katika Ngazi Tofauti wazungumzaji wa Kiswahili.

Hujambo mhojiwa mpendwa, mimi ni **Kubakurungi Abraham Kyangungu,** ninasomea chuoni kikuu Moi, nchini Kenya. Kwa sasa ninaendeleza utafiti kuhusu "**Sarufi Ya Kinyankore na usomaji wa Swahili kama L2: Mfano Kutoka Asasi Teule Jijini Mbarara.**

Kwa hiyo, naombeni kwa heshima nyingi muda wako ili unisaidie kujaza hojaji hii. Ningependa kupata ushirikiano wako ili uweze kunisaidia kutoa majibu juu ya maswali yanayohusu utafiti, ambayo ni muhimu kwa kukamilisha utafiti wa sasa. Tafadhali toa taarifa zinazofaa na za kweli bila hofu yoyote; taarifa zote zitashughulikiwa kwa siri na zitatumika pekee kukamilisha utafiti wa sasa. Napenda kutoa shukrani kwako kwa kukubali kuhusika na ushirikiano wako.

SEHEMU 1: MAONI YA KIJUMLA

i. Huhitaji kuandika jina lako kwenye hojaji hili

ii. Majibu yanatarajiwa kulingana na maswali uliyoulizwa.

iii. Ikiwa utapata ugumu katika swali, tafadhali uliza mtafiti.

SEHEMU 2: HABARI KUHUSU MHOJIWA

Andika alama ya (√) kwenye chaguo unachokiona kuwa kinakufaa kwenye mabano [ ]

Maswali:

1. Umri wako

(a)18-25 ( ) (b)26-30 ( ) (c)31-35 ( ) (d)36 – 40 ( )

e) 41-50 ( ) (f) 51 na zaidi ( )

2, Jinsia

(a) Mume ( ) (b) Mke ( )

3. Hadhi ya Kielimu

(a) Cheti ( ) (b) Stashahada ( ) (c) Shahada ( ) (d) digri ya pili ( )

(e) digri ya tatu ( )

SEHEMU 3: Maswali ya Kupima ujuzi wa lugha Kimaandishi, na Kimatamshi.

USTADI WA KUSOMA

1. Soma kifungu hiki cha kuelewa ambacho umeandikwa katika L1 iliyo Kinyankore na Kiswahili. (alama 20)

USTADI WA KUANDIKA NA KUSIKIA

2. unaombwa kusikiliza vizuri na kuandika vifungu vifuatavyo vya imla kama mtakavyoambiwa kwa L1 ya Kinyankore na Kiswahili. (alama 20)

USTADI WA KUONGEA

3. Wanafunzi watashiriki katika mijadala fupi kuhusu mada itakayochaguliwa na mtafiti ili kupima uwezo wao kuongea hasa kujieleza kwa L2 iliyo Swahili hata L1 iliyo Kinyankore. (alama 20)

Kiambatisho 5: Idhini ya REC

BISHOP STUART UNIVERSITY

P.O.BOX 9, MBARARA

Tel: 0772 512551

Website: www.bsu.ac.ug

E-mail: rec@bsu.ac.ug/info@bsu.ac.ug

RESEARCH ETHICS COMMITTEE

16/06/2023

To: ABRAHAM KUBAKURUNGI

BISHOP STUART UNIVERSITY
+256701858306

Type: Initial Review

Re: BSU-REC-2023-83: THE INFLUENCE OF RUNYANKORE GRAMMAR ON THE LEARNING OF KISWAHILI AS A SECOND LANGUAGE IN SELECTED SECONDARY SCHOOLS IN MBARARA DISTRICT

I am pleased to inform you that at the **12** convened meeting on **08/06/2023**, the Bishop Stuart University (BSU) REC meeting voted to approve the above referenced application.
Approval of the research is for the period of **16/06/2023** to **16/06/2024.**

As Principal Investigator of the research, you are responsible for fulfilling the following requirements of approval:

1. All co-investigators must be kept informed of the status of the research.
2. Changes, amendments, and addenda to the protocol or the consent form must be submitted to the REC for re-review and approval **prior** to the activation of the changes.
3. Reports of unanticipated problems involving risks to participants or any new information which could change the risk benefit: ratio must be submitted to the REC.
4. Only approved consent forms are to be used in the enrollment of participants. All consent forms signed by participants and/or witnesses should be retained on file. The REC may conduct audits of all study records, and consent documentation may be part of such audits.
5. Continuing review application must be submitted to the REC **eight weeks** prior to the expiration date of **16/06/2024** in order to continue the study beyond the approved period. Failure to submit a continuing review application in a timely fashion may result in suspension or termination of the study.
6. The REC application number assigned to the research should be cited in any correspondence with the REC of record.
7. You are required to register the research protocol with the Uganda National Council for Science and Technology (UNCST) for final clearance to undertake the study in Uganda.

The following is the list of all documents approved in this application by Bishop Stuart University (BSU) REC:

Kiambatisho 6: Matokeo kutoka uwanjani

Athari za kimsamiati

Kinyankore	Kiswahili
Amabega	Mabega
Amaguru	Miguu
Amaisho	Macho
Amaizi	Maji
Amakara	Makaa
Amashita	Mafuta
Ameino	Meno
Apana	Hapana
Chungwa	Omucungwa
Dureiva	Dereva
Ebaruha	Barua
Ebinyasi	Nyasi
Ebyokurya	Vyakula
Echupa	Chupa
Edirisa	Dirisha
Eduka	Duka
Efeeza	Fedha
Ehuuma	Uma
Eiziina	Jina
Ekanisa	Kanisa
Ekaramu	Kalamu
Ekengere	Kengere
Ekiganja	Kiganja
Ekijiko	Kijiko
Ekintu	Kitu
Ekitabo	Kitabu
Ekitanda	Kitanda
Ekyokurya	Chakula
Embaata	Bata
Embarasi	Farasi
Emboga	Mboga
Embuzi	Mbuzi
Embwa	Mbwa
Emeza	Meza
Emiyembe	Maembe
Emotoka	Motokaa
Emyaka	Miaka
Enanasi	Nanasi
Engiri	Ngiri
Engoma	Ngoma
Enjoka	Nyoka
Enjura	Mvua
Enkoko	Kuku
Entwiga	Twiga
Enyama	Nyama

Esaati	Sati
Esafuria	Sufuria
Eshaaha	Saa
Eshanduko	Sanduku
Esihani	Sahani
Esimu	Simu
Etaara	Taa
Gaba	Gawa
Gambira	Ambia
Gauni	Egauni
Gyenda	Enda
Handiika	Andika
Huzi	Uzi
Ibaati	Bati
Ichanuo	Chanuo
Ija	Kuja
Ikumi	Kumi
Imuka	Amka
Ina	Nne
Ipapari	Papai
Iua	Ua
Kache	Chache
Kuzara	Kuzaa
Kwoga	Kuoga
Mama	Mama
Masichini	Maskini
Mpaka	Mpaka
Muhogo	Mhogo
Muryango	Mlango
Naaba	Nawa
Obuso	Uso
Obwongo	Ubongo
Okufa	Kufa
Okuguma	Ugumu
Okunywa	Kunywa
Okutetema	Tetemeka
Omucheri	Mchele
Omucungwa	Chungwa
Omugati	Mkate
Omugongo	Mgongo
Omukono	Mkono
Omukwe	Mkwe
Omukyeka	Mkeka
Omuntu	Mtu
Omupira	Mpira
Omusharaba	Msalaba
Omusitari	Mstari
Omuti	Mti
Omuzeeyi	Mzee
Omuzigiti	Msikiti

Omwana	Mwana
Orubaho	Ubao
Orurimi	Ulimi
Rediyo	Redio
Reeta	Leta
Rira	Lia
Shoma	Soma
Shukari	Sukali
Shukari	Sukari
Sikati	Sketi
Sitayisahahu	Sitaisahau
Tara	Taa
Toroka	Toroka
Wule	Ule
Yoga	Oga

Semantiki

Kiti	*ekiti*
Kaka	
Paka	
Mpaka	
Ndiyo	
Enda	
Egaari	gari
Yita	Ita
Ebafu	bafu

Makosa

Chichwa	Kichwa
Jinthi	Jinsi
Kishwahiri	Kiswahili
Kurya	Kula
Muhazara	Mhadhala
Sheka	Cheka
Sibitisha	Thibitisha
Sukurani	Shukrani
Teremuka	Telemka

Maandishi

Abari	habari
Arobaini	Arobaine
Arobayine	arobaine
Asante	ahsante
Asate	
Chiti	kiti
Chuwo	chuo
Eshaara	Sala
Eshuura	Sura
Hesima	heshima
Ibiri	mbili
Ine	nne
Isirini	ishirini
Kaaka	kaka
Kalibu	karibu
Keri	Kheri
Keso	kesho
Kikopo	kikombe
Kimbiya	kimbia
Kyake	chake
Kyakunywa	chakunywa
Kyangu	changu
Kyeza	
Lehema	Rehema
Luga	Lugha
Maama	mama
Mama wako	
Matamsi	matamshi
Mayendelewo	Maendeleo
Mbarimbari	Mbalimbali
Miyoyo	
Mukali	mkali
Mulefu	mrefu
Muno	mno
Muntu	mtu
Murefu	mrefu
Musinji	Msingi
Mutoto	
Muzuri	mzuri
Mwarimu	Mwalimu
Mzeyi	mzee
Nakazarika	Nakadhalika

Nukuta	nukta
Rafichi	rafiki
Rayisi	rais
Selikali	serikari
Seruji	theluji
Teteya	tetea
Towa	toa
Ughali	
Viyatu	viatu
Wangye	wangu!
Zambi	Dhambi
Zowezi	Zoezi

Walivyokosea kwa kiwango cha muundo

Swahili yo tunajishoma
Kabungo keitu ni kazuri
Mwana wangye ni mubaya
Maishani yangu…. Mwangu
Waongozi//viongozi
Siku hilo…… siku hiyo
Kitabu moja
Masahani
Safari mrefu

Makosa ya Mpangilio wa Vipashio katika Sentensi

Kosa	**Usahihi**
Kiwanda mjini kitajengwa	Kiwanda kitajengwa mjini
Atakuja mtoto yule shuleni	Mtoto yule atakuja shuleni
Ile meza huonekana vizuri	Meza ile huonekana vizuri
Mama mtoto atazaa	Mama atajifungua mtoto
Lia usiku uta kila	Utalia kila siku
Tabia mzuri Brenda ana	Brenda ana tabia nzuri
Lala kitanda yeye	Yeye alilala kitandani
Kesho walikelele piga	Keshoye walipiga kelele

Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi

Kosa	Usahihi
Nimepoteza kalamu wangu	Nimepoteza kalamu yangu
Meza wangu ameanguka	Meza yangu imeanguka
Mtoto yangu kimekuja	Mtoto wangu amekuja
Kijiko wangu ni mkubwa	Kijiko changu ni kikubwa
Maji wangu mdogo	Maji yangu kidogo
Kitanda wake simzuri	Kitanda chake si kizuri
Wowote ni wanafunzi	Wao wote ni wanafunzi
Tulibeba mzigo letu	Tulibeba mizigo yetu
Mgonjwa kilienda	Mgonjwa alienda
Chakula yote pika	Pika chakula chote

Kabungo keitu ni kazuri

Mwana wangye ni mubaya

Wangye/wangu!

Muzuri/mzuri

Makosa ya Kuongeza Vitamkwa

Kosa	Usahihi
Ninasomeanga shule hii	Ninasomea shule hii
Mtoto geni amefikako	Mtoto mgeni amefika
Nipeko chakula	Nipe chakula
Aliwaambiao kuleta vitabu	Aliwaambia walete vitabu
Twambieo ukweli	Twambie ukweli
Msomeeko kitabu	Msomee kitabu
Alimwitako mama	Alimwita mama
Lalapo hapa	Lala hapa
Baba alikuweko shuleni	Baba alikuwa shuleni
Kulako kidogo	Kula kidogo

Makosa yaliyotokana na kutumia maumbo ambayo si Mwafaka

Kosa	Usahihi
Kondoo amenenepa	Kondoo amenona
Chunga mazingara	Tunza mazingira
Barabara inakwenda mjini	Barabara inaelekea mjini
Tutakuwa wazuri	Tutakuwa wanafunzi wazuri
Walipeza zao	Walipoteza pesa zao
Anapenda sisi	Anatupenda sisi
Mbuzi hupenda nyasi	Mbuzi hupenda kula nyasi
Mtoto anafungua macho	Mtoto anaona
Kosa hilo lisoluhisho	Kosa hilo lirekebishe

Walivyokosea Kifonolojia

Kosa	Usahihi
Mimi hura ugari	Mimi hula ugali
Huyu ni lafiki yangu	Huyu ni rafiki yangu
Tayarisa samba	Tayarisha shamba
Unasani ni mimi	Una dhani ni mimi
Kuhairisha	Kuahirisha
Kutekeresa	Kutekeleza
Kabuli	Kaburi
Terekamu	Teremka
Suhilusho	Suluhisho
Balidisha	Badilisha
Rekebisa	Rekebisha

Kukosea kitahajia

Kosa	Usahihi
Kwasababu	kwa sababu
Kwahiyo	kwa hivyo
Inamana	ina maana
Marakwamara	mara kwa mara
Vilevile	Vile vile
Kamavile	kama vile
Amakweli	ama kweli
Na kadhalika	nakadhalika

Kutenganisha Maneno

Kosa	Usahihi
Ali kuwa	Alikuwa
Wali enda	Walienda
Vilivyo vutia	Vilivyovutia
Tulipo wasili	Tulipowasili
Wana cheza	Wanacheza
Yo yote	Yoyote
Wali kimbia	Walikimbia
Pilika pilika	Pilikapilika
Po pote	Popote

Sentensi Tata

Kosa	Usahihi
Walivua nguo	Walifua nguo
Alikua akicheza na mamaye	Alikuwa akicheza na mamaye
Inchini kuna watoto wengi	Nchini kuna watoto wengi
Mambo aliendа gobo	Mambo yalienda kombo
Shombo chilizama	Chombo kilizama
Avya yake ni mbaya	Afya yake ni mbaya
Shanduku lilіletwa mjini	Sanduku lililetwa mjini
Walimchika mkono	Walimshika mkono

Kuchanganya Ngeli

Kosa	Usahihi
Vitabu zetu zimepotea	Vitabu vyetu vimepotea
Gari yangu ni mazuri	Gari langu ni zuri
Mwalimu yule kilikuwa mzuri	Mwalimu yule alikuwa mzuri
Jitu yale linatisha	Jitu lile linatisha
Masikini mirefu	Maskini mrefu
Kijiko mkubwa	Kijiko kikubwa
Chumba lidogo	Chumba kidogo
Mwalimu kizuri	Mwalimu mzuri
Wazee lile	Mzee yule

Kuongeza Herufi kwenye Neno

Kosa	Usahihi
Atatembeya	Atatembea
Chukuwa	Chukua
inje ya nyumba	Nje ya nyumba
inchini Uganda	Nchini Uganda

Utumiaji wa Herufi zisizofaa katika Neno

Kosa	Usahihi
Misichana	Msichana
Muti	Mti
Dakitari	Daktari
Dalasa	Darasa
Fuaua	Fuata
Mumeya	Mmea
Mulima	Mlima
Vinamaasi	Vinamasi
Maporoomoko	Maporomoko

Herufi kuachwa katika Neno

Kosa	Usahihi
Siku hio	Siku hiyo
Kueka vitu kichani	Kuweka vitu kichwani
Alisuka chini	Alishuka chini
Awezi kutembea	Hawezi kutembea
Awezi kusoma vitabu	Hawezi kusoma vitabu
Asubui	Asubuhi
Badae	Baadaye
Kusima	Kusimama
Samba langu	Shamba langu
Mandishi	Maandishi

Walivyotumia vibaya Vivumishi

Kosa	Usahihi
Mwanafunzi msafi	Mwanafunzi safi
Mtoto mbora	Mtoto bora
Alileta machungwa makumi	Alileta machungwa kumi
Wasichana kumi na wasita	Wasichana kumi na sita
Wanajeshi wa malidadi	Wanajeshi maridadi
Vitabu visita	Vitabu sita
Vifaa viharisi	Vifaa halisi
Mwimbaji mbora	Mwimbaji bora
Mvuvi mhodari	Mvuvi hodari

Makosa ya Muundo wa Sentensi

Kosa	Usahihi
Tumeona dunia katika mengi	Duniani kuna mengi
Alileta chakula badala ya kazi	Alileta chakula baada ya kazi
Usilete kuku na mchele	Usilete kuku kwa wali
Watoto yetu ni ndito mbili	Watoto wetu ni wasichana wawili
Meza yule amechafuka sana	Meza ile imechafuka sana
Kitabu wangu vina uchafu	Kitabu changu kina uchafu
Tulienda kumtafuta hatukukiona	Tulienda kumtafuta hatukumuona
Huyu ni jani la mti	Hili ni jani la mti
Nanasi zote alioza	Nanasi zote zilioza
Chakula yange ni kitamu	Chakula changu ni tamu sana
Nitawambia weije nyumbani	Nitawambia waje nyumbani
Twende field kulima	Twende shambani kulima

Stand twende sokono	Simama twende sokoni
Beba food twende shuleni	Beba chakula twende shuleni
Ente yangu ni ngonjwa	N'gombe wangu ni mgonjwa

Maswali	Mwalimu wa kwanza	Mwalimu wa pili
1	Miaka sita	Miaka kumi
2	Nam	Nam
3	➢ Kukosa vitabu ➢ Matamshi mabaya kilugha ➢ Mchanganyiko wa lugha mama hata L2	➢ Wanafunzi wadogo wanaosoma Kiswahili ➢ Nia mbaya ya lugha ya Kiswahili ➢ Mwingiliano wa lugha mama
4	Kukopa vitabu shuleni jirani kujitahidi kwa kusoma sarufi	• Kuwasawishi wanafunzi wengine • Kujaribu kutoa dhimay a L2 • Kufunzwa sana sarufi ya Kiswahili
5	Swahili, Kimombo hata L1	Kingereza na lugha mama
6	**Kukosea kifonolojia** **makosa sanifu** sheka cheka Tula tua Shoma soma **makosa ya maandishi** **makosa sanifu** ka kaa mela mea pat pata	**Makosa ya matamshi** **makosa sanifu** sheka cheka Genda enda batu watu **makosa ya maandishi** **makosa sanifu** ka kaa mchana msichana Mzi maji
7	Yanaathiri wanavyotumia maumbo hata wanafunzi kupewa alama chache katika Mitihani na gradi za chinindizo wanapata	Matokeo mabaya Kuanguka kwa mitihani
8	Kujitahidi kwa kusoma msamiati Kusikiliza vipindi vya Kiswahili kwa kupitia redio na runinga	Matumizi ya kamusi Kufanya midahalo na kutumia L2 Kuhudhuria midahalo katika L2

Walivyotumia vokali tano fupi

Irabu	Neno (Kinyankore)	Maana yake kwa Kiswahili
/ **a** /	[βara]	hesabu (kuhesabu vitu au pesa na kadhalika.
/ **ɛ** /	[hɛnda]	Vunja
/ **i** /	[imuka]	Amka
/ **ɔ** /	[kora]	Fanya
/ **u** /	[βura]	Potea

Walivyotumia vokali ndefu

Irabu	Neno (Kinyankore)	Maana yake kwa Kiswahili
/ **a** /	[βa:sa]	Weza
/ **ɛ** /	[rɛ:ta]	leta
/ **i** /	[handi:ka]	Andika
/ **ɔ** /	[β ɔ:na]	wote
/ **u** /	[ɛhu:ma]	uma

Makosa ya Kisemantiki

Kosa la kisemantiki	Maneno yaliyotarajiwa
Napigwa Kichwa	Naumwa kichwa
Walizina pamoja	Walicheza pamoja
Aliingiza chaja	Alichomeka chaja
Walitoa msumari	Walichomoa msumari
Nimepigwa Mvua	Nimenyeshewa
Alienda paka chini	Alishuka/aliteremka hadi/mpaka chini
Nasikia Njaa	Nahisi njaa

Neno	Maana kwa Kiswahili	Maana kwa Kinyankore
Kaka	Ndugu wa kiume	Mama anayemzaa Mzazi wako (Nyanya/Bibi)
Kiti	Mahali pa kukalia	Kijiti kama kuni
Paka	Mnyama afugwaye nyumbani	Kujivunia na kuhisi kiburi
Mpaka	Mahali ambapo panatenganisha majirani	Hadi
Ita	Kumwambia mtu aje	Kuua
Enda	Kutoka	Tumbo/ mimba
Ndiyo	Kukubali / “Naam”	Niko
Zina	Kitendo cha ngono	Kucheza

Athari za Kimsamiati

Kinyankore	Kiswahili
Tonto	Pombe za kienyeji
Enkeiga	Maharage mateke
Obwitizo	Funeli
Obwato	Mtumbwi
Ebikanja	Machicha ya Mtama
Okwevuga	Majigambo
Okwecura	Mtaratibu/Mzito kusutuka
Okutsya	Mvua kukatika
Empuruturiro	Fundo la Mtego
Okukona	Kufuba/Kutoiva vizuri

Ubadilishanaji wa Fonimu

Kinyankore	Kiswahili
Ria	lia
Mrango	mlango
Reta	leta
Serikari	Serikali
Turienda	Tulienda

Ubadilishanaji wa Fonimu za [L] kwa [r]

Kosa	Kiswahili sahihi
Jalibu	Jaribu
Sufulia	Sufuria
Mpila	Mpira
Ledio	Redio
Sukali	Sukari

Ubadilishanaji wa /ki/ na /chi/

Kosa	Kiswahili
Chishwahiri	Kiswahili
Chitabu	Kitabu
Chitanda	Kitanda
Chintu	Kitu
Chijiko	Kijiko
Chisu	Kisu

Chanzo: Data za uwanjani (2023)

Matokeo yaliyodhihirisha kutumia sauti [θ]

Neno lililo sahihi	Kosa	Waliolitamka vyema	Walioshindwa kutamka vyema
Thawabu	Sawabu	6.3%	93.7%
Theluthi	Selusi	9.9%	90.1%
Thelathini	Selasini	9.7%	90.3%
Theluji	Seluji	2.3%	97.7%
Thamani	Samani	4.8%	95.2%
Wastani		4.0%	96%

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Athari katika matumizi /ð/

Neno sahihi	Neno lisilo sahihi
Fedha	Feza
Aidha	Aiza
Dhiki	Ziki
Dhana	Zana
Dhahabu	Zahabu
Afadhali	Afazali
Dharau	Zarau

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Walivyoathiriwa na sauti ya /γ/

Kosa katika Kiswahili	Umbo sahihi katika Kiswahili
Garama	Gharama
Luga	lugha
Agalabu	aghalabu
Gorofa	ghorofa

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Mifano ya Uchopekaji wa Sauti nyingine kwenye umbo

Kiswahili	Kinyankore
Sati	*Esaati*
Kumi	*Ikumi*
Duka	*Eduuka*
Bati	*Ibaati*
Sukari	*Shukari*
Dirisha	*Edirisa*

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Mifano ya Uchopekaji wa /e/ kutangulia umbo

Kinyankore	Kiswahili
Entwiga	Twiga
Embwa	Mbwa
Esaati	Sati
Emotoka	Motokaa
Emeeza	Meza
Esimu	Simu
Eduuka	Duka
Edirisa	Dirisha
Enyama	Nyama
Etaara	Taa
Ecupa	Chupa
Ekiganja	Kiganja
Ekitanda	Kitanda
Ebakuri	Bakuli

Mifano ya Uchopekaji wa /i/ kutangulia umbo

Kinyankore	Kiswahili
Ikumi	Kumi
Ibaati	Bati
Ipapari	Papai
Itaano	Tano

Mifano ya Uchopekaji wa /o/ kutangulia umbo

Kiswahili	Kinyankore
Mti	**O**muti
Mtu	**O**muntu
Mgongo	**O**mugongo
Mwana	**O**mwana
Kunywa	**O**kunywa

Chanzo: Data ya Uwanjani (2023)

Jinsi kudondosha silabi katika neno kulivyotokea

Kiswahili	Kosa
Shule	Sule
Hapana	Pana
Asubuhi	subui
Shitakiwa	Stakiwa
Hasara	Asara
Gharama	Garama

Chanzo: Data ya uwanjani (2023)

Matumizi ya vivumishi vionyeshi

Kivumishi	Kundi la Ngeli	Majibu Sahihi	Makosa
Kionyeshi	li/ya	Maziwa haya	Maziwa hiyo
	a/wa	Mkulima huyu	Mkulima huu
		Kondoo hawa	Kondoo hizi
		Askofu huyu	Askofu huu
	Ki/vi	Kitanda hiki	-
	u/zi	Uzi ule	Uzi hii
	u/i	Mkate huu	Mkate huyo
		Mahali hapa	Mahali haya

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Mifano ya athari ya kinyankore katika tungo za Swahili

Umbo lisilo sahihi	**Umbo sahihi**
Abari za iwe Mwalimu	Habari zako mwalimu
Asante mingi sana kwako	Shukrani sana kwako
Bakuru ba Idara bamekwenda nyumbani.	Wakuu wa idara wamekwenda nyumbani
Hakuna yenyini kabisa	Hakuna yenyewe kabisa
Jicho limezimba sana	Jicho limevimba sana
Kabungo keitu ni kazuri,	Mlima huo ni mzuri
Kamata makofi gake	Upigiwe makofi wewe
Mpira gwangye gumepotea	Mpira wangu umepotea
Ngombe zangye zimeibwa	Ng'ombe wangu wameibwa

Chanzo: Takwimu ya uwanjani (2023)

Kiambatisho 7: Cheti cha Plagiarisim

SR1074

ISO 9001:2019 Certified Institution

THESIS WRITING COURSE

PLAGIARISM AWARENESS CERTIFICATE

This certificate is awarded to

KUBAKURUNGI KYANGUNGU ABRAHAM

PHD/KIS/6033/22

In recognition for passing the University's plagiarism

Awareness test for Thesis; **SARUFI YA KINYANKORE NA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI: MFANO KUTOKA TAASISI TEULE JIJINI MBARARA** with similarity index of 3% and striving to maintain academic integrity.

Word count:60087

Awarded by

Prof. Anne Syomwene Kisilu

CERM-ESA Project Leader   Date: 14/10/2025